28 OKTOBA, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Pili – Tarehe 28 Oktoba, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 20

Kumalizia Ujenzi wa Zahanati Vijiji vya Maswa – Magharibi

MHE. MASHIMBA M. NDAKI aliuliza:-

Je, lini fedha za kumalizia ujenzi wa zahanati za Vijiji vya Nyashimba, Funika, Mandela, Nhelela, Kidema na Igwata zitapelekwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Jafar, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi, ambaye pia ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2018/2019 hadi 2025/2026 Halmashauri ya Wilaya ya Maswa imekamilisha ujenzi wa maboma sita ya zahanati ya Isulilo, Jihu, Bukangilija, Nyabubinza, Mwang'anda na Mwabayanda *'S'*. Ukamilishaji wa maboma hayo umegharimu jumla ya shilingi milioni 410.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Maswa ina maboma sita. Aidha, maboma manne ya Nhelela, Kidema, Funika na Mandela yamepauliwa kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo na maboma mawili ya Nyashimba 'S' na Igwata yapo hatua ya lenta. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa zahanati ya Isanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma ya zahanati yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi kote nchini, yakiwemo maboma ya zahanati ya Vijiji vya Nhelela, Kidema, Funika, Mandela na Igwata katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, swali la nyongeza.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Maboma yaliyotajwa manne na mawili ambayo yametajwa kuwa kwenye ngazi ya lenta, kusema ukweli maboma yako saba na yote yameezekwa. Imechukua miaka saba kumaliziwa au kumaliziwa yale yaliyotajwa kumalizika mpaka 2026.

Je, ni lini maboma haya saba ambayo nayo tayari yamekwisha kuezekwa kwenye vijiji hivi, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuyamalizia?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba yale maboma yote aliyoyaainisha na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI tulishafanya tathmini jumla ya maboma 1,934 ya zahanati kote nchini ambayo yanahitaji jumla ya shilingi bilioni 115 ili kuweza kuyakamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele vya Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kwa sasa ni kamilisha vituo vya afya 111 ambavyo tumekwishaviombea fedha zaidi ya shilingi bilioni 23 zinatakiwa kukamilisha vituo ili vianze upasuaji. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI itaendelea kutenga fedha kuhakikisha maboma ya zahanati haya yanakamilishwa pamoja na vipaumbele ambavyo Mheshimiwa Ndaki amevitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Eng. Kija Ntemi, swali la nyongeza.

MHE. KIJA L. NTEMI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba niulize swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Majimbo mawili, mimi na wewe Katoro na Busanda lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekubali wananchi wake wapate vituo vya afya pamoja na zahanati ili aweze kuhudumia vizuri. Mheshimiwa Waziri ni Mbunge wa Jimbo la Busanda, kuna Kata ambayo iko katika Jimbo la Busanda inaitwa Bujula haina kituo cha afya wala haina zahanati: -

Je, Serikali na Mheshimiwa Naibu Waziri akitoka Busanda wana majibu gani ili kuwasaidia wananchi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ili waweze kupata huduma ya afya? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimpongeze Mbunge wa Jimbo la Katoro, huyu ndiye Mbunge kijana ambaye amefika Marekani kwa mara ya kwanza kupitia ziara za Kamati za mafunzo. Nimpongeze sana Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi kuhusu Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupeleka huduma za afya karibu na wananchi katika Kata ambayo ameitaja, Kata ya Bujula inayotoka Jimbo la Busanda. Tayari Kata hii tulianza ujenzi wa zahanati na zahanati ile ikawa na changamoto, kwa hiyo, kwenye umaliziaji ikabidi kuifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa; Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi pamoja na wanajimbo anaowaongoza katika Jimbo la Busanda, zahanati hii imetengewa fedha ambayo inakamilishwa na mpango *CSR*. Ni hoja ambayo pia hata Mheshimiwa Musukuma aliibeba, akasema kwamba ziko Kata ambazo hazina vituo vya afya lakini zina maombi ya zahanati, basi angalau wananchi wakamilishiwe zahanati hizi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kija na wanajimbo na Mheshimiwa Diwani wa Bujula, kwamba zahanati hii inakwenda kukamilika katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi muda huu mkandarasi yuko *site* kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, zahanati iliyopo Kijiji cha Dang'aida Kata ya Bassotu iko kwenye hatua ya ukamilishaji. Changamoto iliyopo ni umbali wa kutoka kituo cha afya kilipo, wananchi wanapata changamoto kubwa sana hasa ya umbali kulinga na jiografia: -

Je, Serikali ina kauli gani kuhusu ukamilishaji wa zahanati hii ili iweze kuwasaidia wananchi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Halamga na kwa mchango ambao aliutoa jana kwenye azimio la kumpongeza Rais. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa mchango ambao ulitugusa na vijana wengi walifuatilia mchango ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mbunge katika hili eneo la Dang'aida ukamilishaji wa zahanati hii unaenda sambamba na zile zahanati ambazo nimeziainisha. Nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha kuwa tunatenga fedha katika Halmashauri zetu kwa ajili ya kukamilisha zahanati hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maeneo ambayo Halmashauri zina uhaba au ufinyu wa bajeti, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI tunaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kama ambavyo

tumeona katika Jimbo la Sikonge na Jimbo la Uyui. Tulishirikiana na Jakaya Mrisho *Foundation* kukamilisha zahanati zile. Kwa hiyo, kwenye eneo lake Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI inalichukua hili kuhakikisha kwamba tutaendelea kutafuta maoteo ya fedha kuhakikisha tunakamilisha zahanati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kakoso swali la nyongeza.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika imejitahihdi sana kushirikiana na vijiji vya Kabanga, Mgansa, Isibangala kujenga zahanati zimebaki hatua ya mwisho ya kukamilisha: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweza kukamilisha majengo yao ambayo yalishaanzishwa na wananchi na ku-*support*-iwa na Halmashauri?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakoso kama ambavyo ameliuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimeainisha kwenye swali la msingi kwamba tumeendelea kuainisha maboma yote ambayo yanatakiwa ukamilishaji na tuko hatua za utafutaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie Wabunge wote kwamba katika mwaka wa fedha 2027/2028 tutahakikisha kuwa maboma yote ambayo yako kwenye hali nzuri ya ukamilisha tunatengea fedha na kufanya ukamilishaji. Kwa sasa kipaumbele ambacho kipo mezani kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ni kuhakikisha kuwa vituo vya afya vile 11 ambavyo tumeviombea

fedha, zaidi ya shilingi bilioni 23 tunahakikisha vinaanza kutoa huduma hasa zile huduma za upasuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba maboma yote ambayo tunaendelea kuyaainisha na kuyaombea fedha tutayakamilisha ili kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Temeke sasa aulize swali lake.

Na. 21

Ujenzi wa Bweni la Wavulana Shule ya Sekondari Kibasila

MHE. MARIAM N. KISANGI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Bweni la Wavulana katika Shule ya Sekondari Kibasila katika Halmashauri ya Temeke?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Jimbo la Temeke, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari ya Kibasila katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ilipelekewa shilingi milioni 240 katika mwaka wa fedha 2024/2025 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni

mawili. Aidha, kutokana na ufinyu wa eneo la ujenzi, kibali kilitolewa kwa Halmashauri ili kujenga mabweni ya ghorofa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kupitia mapato ya ndani imetenga shilingi bilioni 8.93 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule za sekondari, ikiwemo shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa bweni moja la ghorofa la wavulana 136 katika Shule ya Sekondari Kibasila.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule za sekondari, ikiwemo mabweni, kwa lengo la kukidhi ongezeko la idadi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali ya nyongeza. Kwanza niipongeze Serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya mabweni ya wasichana katika Shule hiyo ya Sekondari ya Kibasila tunawapongeza sana. Tunatambua hali iliyopo sasa hali imekuwa mbaya kwa watoto wa kiume wakiwa huko mitaani ambako wanafanyiwa ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, je Serikali sasa pamoja na kututengea hiyo shilingi bilioni 1.5 lakini ujenzi bado haujaanza na pale kuna nondo ambazo zinapata kutu, zilitengenezwa kwa ajili ya ghorofa kwenda juu.

Je, Serikali haioni haja sasa ya kuharakisha kwa hatua ile ya kwanza angalau jengo lile lifike kwenye *floor* ya kwanza na watoto waendelee kuishi wakati tukiendelea na ghorofa kwenda juu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nimpongeze sana Mama yangu Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Jimbo la Temeke kwa namna ambavyo anachapa kazi na anawasemea kwa dhati wananchi wa Jimbo la Temeke. Vilevile amekuwa mdau muhimu sana wa sekta ya elimu, katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Jimbo la Temeke pamoja na Watanzania kwa ujumla wanapata elimu bora. Kwa hiyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Temeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa mabweni. Kama alivyosema vizuri Mheshimiwa Mbunge, tunayo changamoto kubwa ambayo siku za hivi karibuni imeendelea kuongezeka ya watoto wetu wa kiume pia kuingia katika changamoto nyingi sana za ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali inatambua changamoto hiyo na ndio maana katika ujenzi wa mabweni tumeendelea kujenga mabweni kwa ajili ya watoto wa kike lakini tumeendelea kujenga mabweni pia kwa ajili ya watoto wa kiume. shilingi 1,500,000,000 hii iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa bweni la ghorofa katika Shule ya Sekondari Kibasila inajenga jengo la ghorofa kwa ajili ya watoto wa kiume.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika bajeti hii na niwapongeze Manispaa ya Temeke kwa kutenga shilingi 1,500,000,000 kwa ajili ya kujenga ghorofa ya kwanza kwa awamu ya kwanza mkandarasi amekwisha patikana, ujenzi umeanza na umefikia asilimia 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ujenzi ulisimama. Hivyo ninaomba nitoe wito kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, kwa bajeti hii ya mwaka huu iliyotengwa wapeleke fedha mapema iwezekanavyo ili ujenzi uendelee na kuhakikisha kwamba bweni hilo linakamilika mapema na kutoa huduma stahiki kwa wanafunzi wa Kibasila sekondari.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa *Engineer* Johnston Johansen, swali la nyongeza.

MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016 katika Jimbo letu la Bukoba Mjini tulipata athari ya tetemeko la ardhi, na wakati huo tulikuwa na ujenzi wa jengo la ghorofa katika shule yetu ya sekondari ya Rwamishenye.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutuma wataalamu kwenda kufanya tathmini ya ubora katika jengo hilo ili tuweze kuendelea na ujenzi ambao ulikwamba tangu kipindi hicho?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nimshukuru sana Mheshimiwa *Engineer* Johnston Johansen, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Mjini kwa kazi nzuri na kubwa anayofanya ya kuwasemea wananchi wa Bukoba Mjini. Mimi nikuhakikishie kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI tutaendelea kumpa ushirikiano ili kuhakikisha kuwa mazingira ya wananchi wa Bukoba Mjini yanaendelea kuboreshwa katika sekta ya elimu lakini pia katika sekta nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mwaka 2016 Manispaa ya Bukoba ilipata changamoto ya tetemeko la ardhi; na katika Shule ya Sekondari ya Rwamishenye ambayo ilikuwa inaondelea na ujenzi wa bweni la ghorofa ilisimama. Ninafahamu kwa muda huu wote hakuna hatua za ujenzi ambazo zimeendelea kwa sababu haijafanyika tathmini ya kujiridhisha na ubora wa jengo lile kama linaweza likaendelea na ujenzi ama vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba kutuma wataalamu wake (ma-*engineer)* kwenda katika shule hii ya Rwamishenye na kufanya tathmini za kitaalamu ili kujiridhisha; na ikiwa ghorofa lile linaweza likaendelea na ujenzi basi hatua za kibajeti ziendelee ili jengo liweze kukamilika na kuendelea kutumika na wanafunzi. Vinginevyo likiwa halikidhi vigezo basi tuweze kupata taarifa rasmi na kufanya maamuzi stahiki.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Abubakar Omari, swali la nyongeza.

MHE. ABUBAKAR A. OMARI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Shule ya Sekondari ya Simbo haina bweni na wanafunzi wake wanalala kwenye madarasa, ambapo inahatarisha watoto wa kike na ukizingatia shule yenyewe haina uzio.

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kujenga bweni angalau la wasichana katika hiyo shule?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Serikali imeweka utaratibu wa kujenga mabweni katika shule zetu za sekondari kwa kuzingatia vigezo maalum. Kigezo cha kwanza ni shule zile za kidato cha tano na sita ambazo zinapewa kipaumbele kuhakikisha kwamba zinakuwa na mabweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kigezo cha pili ni zile shule ambazo zina wanafunzi wenye mahitaji maalum. Kigezo cha tatu ni zile shule ambazo ziko katika mazingira hatarishi. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Abubakar Omari, kwamba tumechukua hoja hiyo na tutafanya tathmini kuona shule hiyo inaanguka kwenye kigezo kipi kati ya hivi vitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze sana Halmashauri kwa kuweza ku-*customize* na kuwezesha wanafunzi kukaa katika madarasa. Jambo la msingi ni kuhakikisha kwamba usalama wao unaendelea kuimarishwa wakati Serikali inafanya tathmini na kuona uwezekano wa kujenga mabweni katika shule hiyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Saasisha Sekondari iko pembezoni kidogo mwa Wilaya ya Hai na ina mazingira ambayo si rafiki sana. Serikali ilituahidi kujenga ukuta kwenye shule hii:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hii?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai kwa kufanikiwa ku-*defend* na kupata heshima kupata *PhD* yake hivi karibuni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Saashisha Elinikyo Mafuwe, hongera sana na hongera sana kwa wananchi wa Jimbo la Hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ziko shule ambazo zimejengwa, na shule hiyo imepata heshima ya jina la Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hilo. Tutafanya tathmini kuona uwezekano wa kuanza kutenga fedha kwa ajili ya kujenga wigo *(fence)* kwa kutumia fedha za mapato ya ndani pamoja na fedha ya Serikali Kuu kwa awamu ili tuweze kuboresha usalama wa wanafunzi katika Shule ya Sekondari ya Saashisha. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zuberi Mfaume, swali la nyongeza.

MHE. ZUBERI Y. MFAUME: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Katika Jimbo la Morogoro Kusini shule nyingi za msingi ni

chakavu sana lakini pia tuna maboma ya kutosha ya shule za msingi ambayo hadi sasa Serikali haijatuletea fedha kwa ajili ya umaliziaji:-

Je, ni lini sasa Serikali itatuletea fedha kwa ajili ya kumalizia maboma pia kukarabati shule za msingi za zamani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini, Zuberi Mfaume. Pia, ninamhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, kwanza Serikali tumefanya tathmini ya shule zote kongwe na chakavu ambazo zinahitaji kufanyiwa ukarabati na nyingine zinahitaji ujenzi mpya na tayari tumeanza hatua za kibajeti kote nchini. Yako maeneo ambayo tayari Serikali imeshapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule za msingi mpya katika maeneo ambayo shule zimechakaa kiasi ambacho ziko *beyond repair,* tutaendelea kutenga fedha hizo kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna andiko maalum la ukarabati wa shule kongwe ambalo Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tunashirikiana na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Wizara ya Fedha kufanya tathmini ya kupata fedha maalum kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa shule hizi. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kufanya hivyo. Vivyo hivyo tutaendelea kupeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma yaliyopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili yaweze kutoa huduma za elimu katika shule hizo. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Asha Juma Kombo, Mbunge wa Mfenesini, sasa aulize swali lake.

Na. 22

Pamba Kuchakatwa Nchini

MHE. ASHA JUMA KOMBO aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inachakata pamba na kuuza bidhaa za pamba badala ya kuuza pamba ghafi nje ya nchi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dennis Londo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Juma Kombo, Mbunge wa Mfenesini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ili kuhakikisha zao la pamba linasindikwa hapa nchini. Mikakati hiyo inahusisha masuala ya kikodi na yasiyo ya kikodi. Mikakati ya kikodi ni pamoja na kuondoa kodi ya ongezeko la thamani katika nguo zinazotengenezwa kwa kutumia pamba inayolimwa hapa nchini; kuondoa kodi ya ongezeko la thamani katika baadhi ya mashine zinazotumika katika viwanda vya kutengeneza nguo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeongeza ushuru wa kodi ya forodha *(import duty)* kutoka 25% - 35% kwa vitambaa vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi na Serikali inatoza ushuru wa forodha wa 25% kwa nyuzi za pamba ambazo zinaagizwa kutoka nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati isiyokuwa ya kikodi inajumuisha ujenzi wa miundombinu ya viwanda, kutoa ardhi bure kwa wawekezaji mahiri, uboreshaji wa upatikanaji wa umeme, na kuendelea kupambana na biashara zisizo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asha Juma Kombo, swali la nyongeza.

MHE. ASHA JUMA KOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa majibu mazuri aliyonipa lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza thamani ya malighafi zinazotokana na pamba ikiwemo kuanzisha usindikaji wa mafuta yatokanayo na mbegu za pamba?

Swali la pili, je, ukiacha masuala ya kikodi, ni vikwazo gani vingine vinavyokwamisha uchakataji wa malighafi zitokanazo na pamba hapa nchini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada ya Serikali sasa hivi ni kuhakikisha kwamba tunaenda kuwa na viwanda vingi nchini ambavyo vitakuwa vinatumia malighafi ambazo zinazalishwa hapa nchini, ikiwemo malighafi ambazo zinatokana na zao la pamba, ambalo kimsingi Kanda ya Ziwa ndiyo kitovu kikuu cha zao hili. Zaidi ya wakulima 500,000 wanajishughulisha moja kwa moja katika kilimo cha pamba katika Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafuta ambayo yanatokana na mbegu za pamba ni sehemu ya malighafi ambayo inapatikana baada ya pamba kuchakatwa. Pia, kuna baadhi ya viwanda ambavyo vinaendelea na kuchakata ama kupata mafuta kutokana na mbegu za pamba, hasa katika Kanda ya Ziwa. Jitihada zetu ni kuwawezesha kupitia *TISEZA* ambayo inatoa nafuu za kikodi, kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo ambayo inatoa msisitizo na mikopo kwa wajasiriamali na wawekezaji ambao wanajikita katika zao la

pamba na kuchakata bidhaa ambazo zinatokana na zao la pamba, ikiwemo mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia *Tanzania Cotton Board*, ambayo ni Bodi ya Pamba Tanzania, inaratibu tasnia ya pamba ambayo imejitahidi sasa kuunganisha wakulima wa pamba, viwanda vya pamba na wale ambao wana *interest* ya kuanzisha viwanda vya ukamuaaji wa mafuta ili malighafi ambayo inatokana na pamba itumike katika kuzalisha zao la mafuta na ili tupunguze utegemezi wa kuingiza mafuta nchini na tujitosheleze ndani kupitia malighafi ya pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Imamu Vuai, swali la nyongeza.

MHE. IMAMU MTUMWA VUAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa Serikali imeeleza kuwa imeongeza ushuru wa forodha kutoka 25% - 35%; je, hatua hiyo imechangia kwa kiasi gani kuongeza uzalishaji wa vitambaa vinavyozalishwa nchini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, hilo swali ni la kitakwimu kama unaweza ukalijibu au tutafanya utaratibu wa kulijibu kwa maandishi; karibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpe faraja Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua za kikodi ambazo zimechukuliwa na Serikali ikiwemo kuongeza kodi kwa bidhaa za pamba ama nyuzi ambazo zinatoka nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kimsingi zimeongeza uzalishaji wa vitambaa ndani ya nchi, lakini takwimu sahihi ninaomba lije kama swali rasmi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Mheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe, sasa aulize swali lake.

Na. 23

Gharama Kubwa za Kuunganisha Umeme Kayanga na Omurushaka

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA aliuliza:-

Je, kwa nini maeneo ya Mamlaka ya Mji wa Kayanga na Omurushaka ambayo kiuhalisia ni vijiji gharama za umeme ni shilingi 320,000 badala ya shilingi 27,000?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Salome Makamba, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Jimbo la Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 1020 la Mwaka 2020, linalosimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA),* ada ya kuunganisha umeme wa njia moja *(single phase)* hutofautiana kulingana na maeneo husika. Kwa wateja wa vijijini walio ndani ya mita 120 kutoka kwenye njia ya umeme, ada ni shilingi 27,000, wakati kwa wateja wa mjini walio ndani ya mita 30, ada ni shilingi 320,960.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Mamlaka ya Mji wa Kayanga na Omurushaka yanakidhi vigezo vya kundi la mjini vilivyowekwa kwenye Jedwali Na. 5 la Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya Mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa, mwezi Aprili, 2026 wakati wa uwasilishaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati ya mwaka wa fedha 2026/2027 iliibuka hoja kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ya kuiomba Serikali kuwezesha wananchi wanaoishi katika maeneo ya

miji yenye sura ya vijiji kuunganishiwa umeme kwa gharama ya shilingi 27,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa tayari Wizara imefanyia kazi maombi hayo ambapo jumla ya maeneo 2,292 yamebainishwa nchi nzima. Kwa upande wa Miji ya Kayanga na Omurushaka, maeneo yaliyobainishwa na kukidhi vigezo vya miji yenye sura ya vijiji ni pamoja na; Kagururu – Kabingo, Rwambale, Karaizo, Kayanga, Majengo Mapya, Katahoka, Kilimahewa, Galilaya, Tuwaka, Omgakorongo, Nyakanongo, Kashakamba, Golani, Kamahungu, Nyakahama, Karundu, Nyakahanga - Nyarutuntu, Nyakahanga - Akitoma na Kishao. Vigezo vilivyotumika katika kuyatambua maeneo hayo ni pamoja na kuangalia hali halisi za kiuchumi za wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuwahudumia wananchi wanaoishi maeneo ya mijini yenye sura ya vijijini kwa kulipa gharama ya shilingi 27,000 kuunganishiwa umeme kwa kufuata vigezo tajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Innocent Bashungwa, swali la nyongeza.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali. Pamoja na hayo nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Naibu Waziri, ninamuomba pia na muda ukimruhusu tunaweza tukaambatana. Maeneo ya Katinkimo, Chamezi, Katunguru, Rushwa au Chatoko, Nyakariri, Omukagera na Chankunguta, bado pia yana sura ya vijiji na yako katika maeneo ya Mamlaka ya Mji wa Kayanga na Omurushaka. Nimuombe sana,

pamoja na yale maeneo ambayo ameyataja, haya maeneo pia tuyaongeze na anaweza akafika katika maeneo haya kujiridhisha, hakika yana sura ya vijiji.

Swali la pili ni Mkoa wetu wa Kagera, zipo Wilaya ikiwemo Wilaya ya Karagwe, bado tunategemea umeme kutoka Uganda na umeme huu unakatika mara kwa mara, unaharibu mali za wananchi pia na kuzorotesha shughuli za kiuchumi kwa sababu umeme ni *centre* ya shughuli mbalimbali za uzalishaji. Je, ni lini Wilaya hizi ambazo hazijaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa ndani ya Mkoa wetu wa Kagera zitaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kwanza kabisa, ninampongeza Kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa kwa kufuatilia kuhusu suala la umeme, hasa wa bei nafuu kwa wananchi wake wa Jimbo la Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamtoa wasiwasi Mheshimiwa Bashungwa niko tayari kwenda kuangalia maeneo haya ambayo umeyaona yana sura ya vijiji lakini yako mijini. Wanasema "Kitanda usichokilalia hujui kunguni wake" na kwa sababu wewe ndiye Mbunge wa Jimbo hilo, wewe ndiye unajua shida za wananchi wa Karagwe. Kwa sababu hiyo, ninakuahidi kwamba tutakwenda kufanya tathmini na tutaangalia uwezekano wa kuweza kupeleka umeme kwa bei nafuu, kwa shilingi 27,000 kwenye maeneo haya ambayo hayajapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kuingiza Mkoa wa Kagera kwenye Gridi ya Taifa, Mheshimiwa Bashungwa pia umekuwa unafuatilia kwa karibu sana. Ninaamini unaona kazi kubwa inayofanyika kwa kasi ya kujenga *line* ya umeme ambayo itasaidia kupeleka umeme katika Mikoa yote na nchi jirani. Ninakuhakikishia, kasi ni kubwa na sasa tumeshavuka zaidi ya 90%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Nishati lengo lake anataka ifikapo angalau mwakani mwezi wa pili tuwe tumeuwasha Mkoa wa Kagera na tumeuingiza kwenye Gridi ya Taifa. Tuendelee kuomba Mungu, kasi ni kubwa, vijana wako kazini, na tunaamini Kagera itaingia kwenye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru nami niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ya miji ambayo ni vijiji, yapo pia katika Jimbo la Bunda Mjini na Wizara ilifika, ilituma wataalamu wake wakatembea kwenye Kata za pembezoni za Guta, Mcharo, Kunzugu, Sazira pamoja na maeneo mengine, Wariku, Manyamanyama na baadhi ya Maeneo ya Bunda Store. Vilevile, nikiwa kwenye mkutano wa hadhara, nilikupigia simu ukaongea na wananchi wangu ukawahakikishia, lakini hilo agizo bado halijatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini sasa agizo litatoka ili wananchi wale wasiokuwa na uwezo wanufaike na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuunganishiwa umeme kwa shilingi 27,000?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Ester Bulaya. Ni kweli, alisema hili jambo kwenye mkutano wa hadhara mbele ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu alituagiza kuhakikisha tunaongeza kasi ya tathmini ili tuweze kwenda kuwapelekea wananchi wake na ninawakumbuka vizuri wananchi wa Bunda *Store* na Manyamanyama ile siku tulikuwa pamoja nao pale kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Ester Bulaya, tathmini imeshafanyika, wananchi zaidi ya 170,000 watakwenda kunufaika na mradi huu. Mradi huu ni mkubwa, una gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 530 na maeneo zaidi ya 2,292 nchi nzima yatakwenda kunufaika na mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini imeshafanyika, sasa hivi Wizara ya Nishati na Wizara ya Fedha wanakaa pamoja kuona namna ya kupunguza gharama za kodi za mradi huu *(VAT)* ili uweze kuwafikia wananchi wengi zaidi, tunaamini *by the end of December,* mradi huu utaanza kutekelezwa na wananchi wataanza kuunganishiwa umeme kwa shilingi 27,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nina vikaratasi vingi sana vya maswali ya nyongeza. Ninaomba maswali yawe mafupi. Mheshimiwa Paschal Chinyele, swali la nyongeza.

MHE. PASCHAL I. CHINYELE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, wakazi wa Jimbo la Dodoma Mjini hasa waishio pembezoni wanaishukuru Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kwamba maeneo hayo yana sura ya vijiji na hivyo yanastahili umeme wa *REA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni lini sasa Serikali itaanza kutekeleza mpango wa kupeleka umeme wa *REA* katika Kata za Matumbulu, Mpunguzi, Mbabala, Chigongwe pamoja na Mbalawala?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia nimpongeze kaka yangu, Mheshimiwa Mbunge wa Dodoma Mjini, yeye ni mmoja kati ya watu waliokuwa wanaathirika sana, kwa sababu ikishaitwa Dodoma Mjini kwa mujibu wa mwongozo wa

Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tayari hao watu wanakuwa wametolewa kwenye mpango wa *REA* na hawawezi kunufaika na umeme wa shilingi 27,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ushauri wako kwa Wizara, tumeweza kufika hapa tulipofika leo na mpango unaanza kutekelezwa. Wananchi wa Kata hizo unazozisema, ni miongoni mwa yale maeneo 2,000 *plus* ambayo yatapelekewa umeme kwa shilingi 27,000. Tuwe na subira, ijapofika mwezi wa 12 mwaka huu, tutakuwa tayari tumeshapata fedha na tumeshapata rasilimali kwa ajili ya kuanza mradi kwa kuwapelekea wananchi zaidi ya 170,000 umeme wa shilingi 27,000 badala ya kulipa 320,000. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Profesa Ndalichako, swali la nyongeza.

MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri, katika Jimbo la Kasulu Mjini, Kata za Murufiti, Muhunga, Muganza, Msambara, Ruhita na Kigondo zina maeneo mengi ambayo yana sura ya vijiji lakini wananchi wanaunganishiwa umeme kwa shilingi 320,000.

Je, ni lini Serikali itaanza utaratibu huu wa kuunganishiwa umeme kwa shilingi 27,000 kwa sababu wengi wana hamu ya kupata umeme lakini uwezo wa kulipa hizi fedha inakuwa ni changamoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru pia kwa kunipa nafasi. Ninampongeza mama yangu Mheshimiwa Profesa Ndalichako kwa kazi kubwa anayoifanya.

Alitufuata akatukaba tumletee magari kwa ajili ya kuinua nguzo za zege na kule kwao wameshanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge; sasa hivi ninadhani Waheshimiwa Wabunge mliona, *TANESCO* pamoja na Benki ya *CRDB* walisaini mkataba, lengo lao lilikuwa ni kuhakikisha pia tunawafikia wananchi wa vijijini ambao wao waliunganishiwa umeme kwa kupitia *REA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari mradi ule umekabidhiwa *TANESCO* na hao nao walikuwa wanaanza kulipa ile pesa shilingi 320,000 ya *TANESCO*, kwa sasa hivi baada ya mkataba ule, kuna wananchi zaidi ya 500,000 ambao watanufaika kupitia mkopo, wataunganishiwa umeme bure halafu kadri wanavyoendelea kununua umeme taratibu, wananchi wale watakuwa wanalipa kwenye bili zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ndalichako ni mmoja kati ya wanufaika wa mradi huo, ninamtoa wasiwasi, Jimbo lake liko salama na wananchi wake watapata faida ya umeme mwingi ambao unazalishwa nchini kwa kuunganishiwa bure au kwa shilingi 27,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante. Usisahau Kata ya Magugu, Babati vijijini. Ahsante sana. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, mimi ni mmoja kati ya walezi wa Jimbo lako na ninakuhakikishia Kata ya Magugu wanajua kwamba mimi ni mlezi wao na tutawapelekea umeme kwa shilingi 27,000.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa John Stephano Luhende, Mbunge wa Bukene, sasa aulize swali lake.

Na. 24

Ujenzi wa Chuo cha *VETA* – Bukene

MHE. JOHN S. LUHENDE aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Chuo cha *VETA* katika Jimbo la Bukene ili kuwasaidia Vijana kujiajiri?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Wanu Hafidh, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Luhende, ninaomba nichukue dakika chache, moja, *actually,* kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, lakini pia na Watanzania kwa ujumla, kwa sala, maombi na jumbe za faraja wakati wa Msiba wa Mzee wetu Hafidh Ameir Hassan. Tunashukuru tumefarijika, Mungu awabariki na asiwapungukie kwa lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba nijibu swali Na. 24 la Mheshimiwa John Stephano Luhende, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi *(VETA)* 65 katika maeneo ambayo hayakuwa na vyuo hivyo. Wilaya ya Nzega, ambapo Jimbo la Bukene linapatikana, ni miongoni mwa wilaya zinazojengewa Chuo cha Ufundi Stadi *(VETA)*. Ujenzi wa Chuo hicho umefikia 85% na Serikali inaendelea na hatua za kukamilisha awamu ya kwanza ili kuanza kutoa mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali ikiendelea na hatua za kukamilisha ujenzi wa chuo hicho, wananchi wa Jimbo la Bukene wanashauriwa pia kutumia fursa za mafunzo zinazopatikana katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Nzega na Mwanhala,

ambavyo vinaendelea kutoa mafunzo na vina huduma za bweni kwa wanafunzi wanaotoka maeneo ya mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa John Stephano Luhende swali la nyongeza.

MHE. JOHN S. LUHENDE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu zipo Wilaya ambazo zina Jimbo moja la uchaguzi na kuna Wilaya zingine kama Nzega ina majimbo matatu ya uchaguzi na sababu inayosababisha yagawanywe majimbo matatu kwenye Wilaya moja ni wingi wa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Bukene ni Jimbo ambalo liko pembeni kabisa Nzega na lina idadi kubwa ya watu na halina hiyo huduma ya *VETA*. Swali langu ni kwamba, Serikali kwa nini msione umuhimu wa kutazama upya sera yenu na kujenga hivyo Vyuo vya *VETA* kwa kufuata Majimbo na si kufuata Wilaya?

Swali la pili, kwa kuwa wananchi wa Bukene tumeshajiandaa tayari na tumeshatenga eneo la ujenzi wa Chuo cha *VETA* eneo hilo lililokuwa kambi ya watu waliokuwa wanajenga bomba la mafuta wameshawakabidhi kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, na eneo hilo liko tayari. Serikali haioni umuhimu wa kutembelea eneo hilo na kuweza kuanza mikakati mara moja kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako ninaomba nimjibu Mheshimiwa Luhende, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Luhende kwa juhudi zake za kutaka kuona kwamba Bukene inapata chuo chake binafsi cha *VETA* ili kuona kwamba vijana wa Bukene wanapata fursa ya mafunzo ya ufundi stadi ili waweze kujiajiri ama kuajiriana, kiukweli huko ndiko ulimwengu unakoelekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba kwa sasa Serikali imejikita katika kukamilisha vyuo 64 na kile cha Mkoa wa Songwe 65, ambavyo vinaendelea kujengwa. Ujenzi huu *almost* unaelekea mwishoni, tumeshamaliza tunakamilisha tu kazi ndogo ndogo. Baada ya kukamilisha mpango wa ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi hivi 65 Serikali itaendelea kujenga vyuo katika maeneo ambayo hakuna vyuo kabisa kama kule Bukene.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili litawezekana tu pale ambapo uwezo wa fedha utakaporuhusu. Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameweka jitihada za kipekee katika hili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mara tu baada ya Serikali itakapokamilisha ujenzi wa vyuo 65 basi tutaanza ujenzi wa vyuo vingine katika maeneo ambayo hayana vyuo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutampa kipaumbele kwa kuwa aliweka jitihada za pekee katika kufuatilia jambo hili.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sheila Lukuba swali la nyongeza.

MHE. SHEILA E. LUKUBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ninampongeza Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Gairo ni wanufaika wa ujenzi wa Chuo cha *VETA* lakini ujenzi wake umekuwa wa kusuasua. Nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba ujenzi huu unakamilika na kuanza kutumika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na kusuasua kwa ujenzi wa vyuo hivi 65, lakini mwezi wa Septemba kuna fedha ambazo zilitoka na zimekwenda katika vyuo hivi na ujenzi umeanza kusogea kidogo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Sheila kwamba ujenzi ule unakwenda kukamilika na huduma ya vyuo vya ufundi stadi itapatikana katika eneo la Gairo asiwe na wasiwasi, tunakwenda kukamilisha na chuo hiki kitaanza rasmi hivi karibuni.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Tamima Haji Abbas, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 25

Mapitio ya Usajili wa Shule Binafsi Nchini

MHE. TAMIMA HAJI ABBAS aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya mapitio ya masharti ya usajili wa shule binafsi nchini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nijibu swali la Mheshimiwa Tamima Haji Abbas, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 na kuzingatia mabadiliko ya mahitaji ya sekta ya elimu, Serikali inafanya mapitio na kuboresha mwongozo wa uanzishaji na usajili wa shule wa mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za maboresho hayo zimewashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo wamiliki wa shule zisizo za Serikali ili kutoa maoni ya kusaidia kuhakikisha kuwa masharti ya uanzishaji na usajili wa shule yanaendana na hali halisi ya uendeshaji wa shule na mahitaji ya sasa ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia maboresho hayo, Serikali inalenga kurahisisha uwekezaji katika sekta ya elimu na kuweka mazingira wezeshi ya uanzishaji na uendeshaji wa shule binafsi bila kuathiri ubora wa elimu, usalama na ustawi wa wanafunzi pamoja na uzingatiaji wa sheria, taratibu na kanuni zilizowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tamima Haji Abbas swali la nyongeza.

MHE. TAMIMA HAJI ABBAS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nashukuru Serikali kwa majibu mazuri ambayo yanaleta matumaini. Naomba Serikali iharakishe kuendeleza hayo waliyoyasema ili wanafunzi wetu wapate unafuu kwa sababu kipindi cha mitihani wanafunzi wengi ambao wapo katika shule ambazo hazijasajiliwa wanapata changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali iharakishe huo mchakato ili shule zetu ziweze kupata usajili.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri naona ametoa ushauri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea ushauri wake na tutaufanyia kazi kwa haraka.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi, Mbunge Nyamagana sasa uliza swali lake.

Na. 26

Mikopo ya Wachuuzi wa Samaki Mwanza

MHE. JOHN F. NZILANYINGI aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kukopesha mtu mmoja mmoja na vikundi vya uchuuzi wa samaki katika mialo ya Jiji la Mwanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Damas Ng'wasi, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi ninaomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwawezesha watu binafsi na vikundi vya wafanyabiashara wa samaki katika maeneo yenye mialo nchini ikiwemo mialo yaJiji la Mwanza kwa kuwapa mikopo waombaji ili waweze kuendeleza shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara hao ni muhimu sana katika mnyororo wa thamani wa sekta ya uvuvi hususan katika ukusanyaji, usafirishaji na uuzaji wa samaki. Hivyo kuchangia kuongeza kipato, ajira na upatikanaji wa samaki kwa walaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB)* inatekeleza programu ya kuwawezesha vijana kiuchumi kupitia sekta ya mifugo na uvuvi kwa

kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu kwa mtu mmoja, vikundi na kampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa awamu ya kwanza jumla ya miradi 917 yenye thamani ya shilingi za kitanzania bilioni 5.86 imewezeshwa katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwemo pamoja na miradi nane yenye thamani ya shilingi milioni 74 kutoka Jiji la Mwanza. Aidha uchambuzi wa maombi 6,875 ya awamu ya pili unaendelea ikiwemo ni pamoja na maombi 79 kutoka Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi swali la nyongeza.

MHE. JOHN F. NZILANYINGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba tu niipongeze Serikali kwa kazi nzuri kupitia Wizara ya Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama utakumbuka takribani miezi sita pekee Wizara ya Uvuvi ilitoa mikopo kwa vijana ambapo ni majuzi tu ndani ya miezi sita vijana hao waliopo kule Luchelele wameweza kuvuna samaki wenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 127.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali basi ifanye mchakato na iharakishe ili walau sasa makundi hayo ya maombi 79 yaliyosalia yaweze kunufaika kwa wakati.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Mbunge ameridhika na majibu yako.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana tumepokea ushauri wake tutaufanyia kazi kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu miradi hii mingi ya vizimba iko kwenye Jimbo

lake la Nyamagana hasa yale maeneo ya Nyegezi, yeye amekuwa akitenga muda wake mwingi kutembelea vijana wetu kuwaasa pia, Halmashauri ya Jiji la Mwanza kupitia Mkurugenzi wake na wenyewe wamekuwa wakitembelea kwa vijana wetu mara kwa mara kuhakikisha wanawaasa na kuwasimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, wataalamu wetu wamekuwa wakiwatembelea na ndiyo hii imekuwa chachu ya vijana wetu kuweza kufanya vizuri. Tutaendelea kuufanyia kazi ushauri huu kuwawezesha vijana wetu kwa wingi ili kuhakikisha tunawakwamua kuwajengea ajira wao pamoja na familia zao.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Maji, Mheshimiwa Martha Festo Mariki Mbunge wa Viti Maalum, sasa ulize swali lake.

Na. 27

Utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050 Katika Sekta ya Maji Katavi

MHE. THOMAS K. MAGANGA K.n.y. MHE. MARTHA F. MARIKI aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutekeleza dira ya Taifa 2050 kwa kila mkazi wa Mkoa wa Katavi kupata maji safi nyumbani kwake?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer* Kundo majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050 ikiwa na lengo la kuhakikisha wananchi wote nchini wanapata huduma za majisafi na salama pamoja na huduma ya usafi wa mazingira ikiwemo wale wa Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia lengo hilo kwa Mkoa wa Katavi, Serikali inaendelea na utekelezaji wa jumla ya miradi 15 katika maeneo ya vijijini ambayo ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Vilevile Serikali inaendelea na mpango wa kufikisha huduma ya maji kwenye vijiji 1,575 nchini vikiwemo vijiji vinane ambavyo havina huduma ya maji kwenye Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maji mjini, Serikali inaendelea na utekelezaji wa jumla ya miradi mitano ikiwemo mradi wa miji 28 unaotekelezwa katika Mji wa Mpanda ambapo kwa jumla inagharimu shilingi bilioni 26. Kukamilika kwa miradi yote ya mjini kutawezesha kufikisha huduma ya majisafi na salama kwa 100% katika Mji wa Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kutoa maji Ziwa Tanganyika kwa lengo la kuhudumia Mikoa ya Kigoma, Rukwa pamoja na Katavi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Thomas Maganga Kampala swali la nyongeza.

MHE. THOMAS K. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninaomba kuipongeza Serikali kwa hatua inazochukua kwenye Mkoa wa Katavi, tunayo miradi mingi sana. Nina swali dogo moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mradi wa Bwawa la Nsenkwa kwenye Jimbo la Katavi, *speed* yake si nzuri sana. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha huo mradi unaisha kwa wakati ili wananchi wa Jimbo la Katavi wapate majisafi na salama?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kumpongeza sana Kaka yangu Mheshimiwa Maganga kwa namna ambavyo anaendelea kuwapigania wananchi wake na juhudi zake zimeonekana kwa namna ambavyo anaendelea kusimamia bwawa hili liweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe hofu tunayo maelekezo ya kuhakikisha kwamba tunaendelea kupeleka fedha ili wakandarasi waendelee kutekeleza miradi mbalimbali nchini, ikiwemo miradi 20 iliyoko katika Mkoa mzima wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hivyo, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Mkoa wa Katavi, katika vijiji 158, vijiji vyote 150 vimepitiwa na miradi na tumebaki na vijiji vinane tu na sambamba na hilo Bwawa la Nsenkwa. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutapeleka fedha ili liharakishwe na liweze kukamilika, wananchi wake wa Jimbo la Katavi waweze kupata huduma ya majisafi na salama.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Suma Fyandomo swali la nyongeza.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru sana Serikali kwa kutuletea mradi wa masoko *group* ambao unahudumu Kata tano, Kata ya Msasani, Masoko, Kisiba na Itagata pamoja na Bujera.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huo ulipokelewa vizuri sana na wananchi na uliwasaidia sana lakini kwa bahati mbaya bomba limepasuka kiasi kwamba sasa wananchi wana shida ya maji, ni miezi mitatu imepita na ukizingatia sasa wanawake ndiyo wanaosumbuka zaidi kutafuta maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapata simu nyingi sana, kwa siku, nikipata simu chache labda simu 20. Ninaomba sana kujua Serikali ni

lini itanunua bomba hilo ili kuunganisha sasa maji yaweze kuwafikia kata hizo tano za Wilaya ya Rungwe. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni suala la dharura, suala la bomba kupasuka, kwanza kabisa Serikali inaingia hasara katika uzalishaji wa maji ambayo yanapotea. Pili, wananchi wanakosa huduma ambapo inaweza ikasababisha changamoto ya magonjwa ya milipuko. Kwa hiyo, kwa muktadha huo kwa sababu huduma hii ilitakiwa ifikie wananchi katika maeneo ya Kata hizo tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji tunalipokea kwa mtazamo wa kidharura na tutakwenda kuhakikisha kwamba bomba linanunuliwa kwa haraka, kwa dharura hiyo ili kuhakikisha kwamba sasa liende likawe *fixed* pale ili wananchi waendelee kupata huduma majisafi na salama. Pia tukiokoa changamoto ya upotevu wa maji ambayo unaweza ukasababishwa na bomba hilo kupasuka, lakini pia bomba hilo hilo ambalo lilitakiwa kupeleka katika maeneo mengine na maeneo mengine yanaweza kuathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaichukua kwa uzito stahiki na tutaenda kulifanyia kazi na nimuombe Mheshimiwa Mbunge tukitoka hapa naomba tuonane ili tuweze kulifanyia kazi na bahati nzuri tuna kikao na baadhi ya watu na Mheshimiwa Waziri mchana naomba tukutane kwa pamoja Saa Saba Kamili ili tuweze kulifanyia kazi kwa dharura hiyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Agnes Hokororo swali la nyongeza.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Katika bajeti ya Wizara ya Maji bajeti ya 2025/2026 kulipangwa kuchimbwa mabwawa 10 kwa kutumia *force account* kwenye maeneo ambayo hayana mtandao wa maji, katika mabwawa hayo 10 kulikuwa na mabwawa mawili katika Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa moja Kata ya Lukuledi ambako kuna bwawa la asili lakini lina uchafu na mlisema hamuwezi kusafisha, Kata ya Lukuledi ipo Wilaya ya Masasi. Bwawa la pili Wilaya ya Nanyumbu, Kata ya Masuguru na bajeti hiyo imefika lakini kwenye bajeti hii mpya hakuna mpango wowote na wale wananchi tuliwaambia na wanaendelea kusubiri. Nini kauli ya Serikali?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na nimshukuru sana Dada yangu Mheshimiwa Agnes Hokororo kwa kuendelea kuwasemea wananchi wa Masasi pamoja na Nanyumbu na maeneo mengine yote ambayo yalitarajiwa kunufaika na mabwawa haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa na ninakiri kabisa kwamba Serikali tulikuwa na huo mpango na mpango huo bado upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoweza kukifanya Serikali ilikuwa inaendelea kutafuta fedha ili kuhakikisha kwamba tunakwenda kutekeleza uchimbaji wa mabwawa hayo kwa sababu yote yanahitaji fedha na Serikali katika mabwawa hayo 10 kuna mengine ambayo tuliweza kufanikiwa kupata fedha yakakamilika. Kwa hiyo, tunaamini kwamba utekelezaji wa awamu kwa awamu basi unatoa matumaini kwamba baada ya bwawa fulani kukamilika bwawa lingine linafuatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho tunakwenda kukifanya ni kwamba kuna mabwawa ambayo yalikuwa yamepangwa kutekelezwa kwa *force account* lakini tumeamua sasa kubadilisha utaratibu wa uchimbaji wa mabwawa kwamba kupitia mitambo ile *set* sita ambayo Mheshimiwa Rais alizinunua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunakwenda kuhakikisha kwamba kuna maeneo ambayo yatakuwa *dedicated* kulingana na changamoto ya upatikanaji wa maji katika maeneo husika, sasa

tunakwenda kupeleka mitambo ili sasa wakaanze kuchimba moja kwa moja na kuhakikisha kwamba watu wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mahitaji ni mengi nchi nzima lakini sisi kwa maeneo ya Masasi na Nanyumbu kwa sababu hawana mbadala na sisi tumeshayabainisha tayari. Kwa hiyo, nikutoe hofu kwamba tutaenda kuwapa kipaumbele ili kuhakikisha kwamba eneo lako pia linapata hiyo huduma safi.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swali lililofuata Mheshimiwa Devotha Daniel Mburarugaba, Mbunge wa Viti Maalum sasa ulize swali lake.

Na. 28

Kukamilisha Miradi ya Maji – Kyerwa

MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha miradi ya maji inakamilika Wilayani Kyerwa hususani Kata ya Nkwenda, Kaisho na Isingiro?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Daniel Mburarugaba, Mbunge Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa jumla ya miradi sita ikiwemo Runyinya - Chanya na Kaisho-Isingiro katika Wilaya ya Kyerwa, Mkoani Kagera. Mradi wa Runyinya - Chanya wenye thamani ya shilingi bilioni 5.7 umefikia wastani wa 92% za utekelezaji na umeanza kutoa huduma ya maji katika maeneo ya vijiji vya Nkwenda, Muhilile na baadhi ya maeneo ya Rwabwere. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2027 na utanufaisha

zaidi ya wananchi 51,000 waishio katika vijiji vinane vya Kata ya Nkwenda, Rabwere pamoja na Iteera.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine Serikali inakamilisha Awamu ya Kwanza ya utekelezaji wa mradi wa maji Kaisho - Isingiro kwa gharama ya shilingi bilioni 1.9 ambapo kazi zinazotekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji, ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 255,000 pamoja na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 17.4. Kwa sasa taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuanza Awamu ya Pili ya utekelezaji wa mradi huo wa Kaisho - Isingiro zinaendelea.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Devotha, swali la nyongeza.

MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na pia ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kabisa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana ndani ya Wilaya ya Kyerwa na inaonesha 75% ya miradi imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tunafahamu tunapofanya miradi tunakwenda ku-*impact the value of money* kwa maana kwamba huu mradi umefika 75% na bado wananchi wanapata adha ya maji, na akina Mama wa Mkoa huo wanapata adha ya maji ikiwemo Wilaya ya Kyerwa. Je, Serikali haioni haja ya kukamilisha miradi hii kwa wakati kwa sababu huu mradi umeandikwa kwenye ilani tatu? Maana yake ni nini? Hata Mbunge wa Wilaya ya Kyerwa amepambana sana kuelezea mradi huu.

Ni lini Serikali itapeleka fedha zilizobaki?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Daniel, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Devotha kwanza kabisa kwa kushirikiana vizuri kabisa na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo na Wabunge wengine katika Mkoa mzima wa Kagera lakini pia kwa kuendelea kusemea sana shughuli zote za maendeleo katika Jimbo la Kyerwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ni kweli kabisa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika maeneo ambayo imewekeza kwa kiwango kikubwa sana ni katika Jimbo la Kyerwa. Katika kipindi kilichopita ni zaidi ya miradi mitatu yenye gharama ya shilingi bilioni 4.08 imekamilika na inafanya kazi vizuri, sambamba na hilo, tuna miradi mitatu mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki moja tu iliyopita nilikuwepo Kagera na katika miradi ambayo niliifuatilia kwa ukaribu sana ni ya Jimbo la Kyerwa. Tunayo miradi ambayo ina gharama ya shilingi bilioni 12.9 ambayo inaendelea na tunafahamu kwamba upatikanaji wa huduma ya maji kwa Kyerwa kwa sasa ni 61% lakini miradi hii itakapokamilika tayari tutaweza kufikia upatikanaji wa maji kutoka 61% kwenda mpaka kwenye 80.2%.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaona kwamba uwekezaji huu una faida kubwa; tunatambua kwamba tunayo miradi ambayo kasi yake hairidhishi, tumeshatoa maelekezo namna ya kuhakikisha kwamba tunatoa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niliseme hili, tunayo changamoto moja ambayo sasa hivi inajitokeza kwamba pamoja na kwamba wakandarasi mara nyingine wanalalamika kwamba wamecheleweshewa malipo yao, siyo sababu ya kujenga miradi chini ya kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nirudie, pamoja na kwamba kuna namna ambavyo wakandarasi wanalalamika kucheleweshewa malipo yao, isiwe sababu ya wao kutekeleza miradi

chini ya kiwango. Haya yatatugharimu, tutakuwa na miradi ambayo *lifespan* yake badala ya kuwa miaka 30 kama ambavyo tuli-*design* inaishia miaka mitano, miaka mitatu, tunaiingiza Serikali kwenye hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitoe wito kwa wakandarasi, mkandarasi ambaye tutabaini mradi wake uko chini ya kiwango hata kama ameleta *certificate* ngapi, hatutomlipa. Tunahitaji kuona *value for money*, tunahitaji uwekezaji wenye tija, tunahitaji kuona kile ambacho Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekitarajia kukifanya kwa Watanzania hasa tunapoelekea kwenye Dira ya Taifa ya 2050 tuone matokeo ambayo *lifespan* na pesa yake inaendana na namna ambavyo mradi ulikuwa umekuwa *designed*. Kama ni miaka 30 tuone kweli kwamba huu mradi utaenda kukaa miaka 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa tumejipanga kufuatilia na tutawalipa wakandarasi ambao wanakidhi vigezo kulingana na utekelezaji wa mradi na ubora ambao tumekubaliana na sisi pesa tutawalipa. Serikali imeshaelekeza na pesa tayari Mheshimiwa Rais ameshaanza kutupatia na tutawalipa lakini kwa kuzingatia kile ambacho tumekubaliana katika mkataba. Nje ya hapo hatutatoa fedha kwa sababu miradi hiyo itakuja kuwa kichefuchefu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Adonis Bitegeko, swali la nyongeza.

MHE. ADONIS A. BITEGEKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Iroba uliopo katika Kata ya Bumbire, Jimbo la Muleba Kaskazini ni mradi ambao ni chakavu na umeshindwa kutoa huduma ya maji katika Vijiji vya Iroba na Kinagi. Katika mwaka huu wa fedha mradi huu umepangiwa kufanyiwa ukarabati kwa vile usanifu ushafanyika.

Je, ni lini Serikali itatoa kibali ili ukarabati huo ufanyike?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimesema nilikuwepo Kagera muda si mrefu na katika maeneo ambayo niliyapitia kwenye taarifa ni Kyerwa, Missenyi, Muleba Kusini pamoja na Muleba Kaskazini. Ninafahamu uhitaji wa Mheshimiwa Mbunge na amekuwa akipambania sana kuhusu hili suala.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe hofu kuna maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wa Maji ameshayatoa kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Maji. Hilo tunalifanyia kazi kwa sababu yeye ndiye mwenye idhini ya kutoa kibali kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa mradi, kwa hiyo tunafahamu umuhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchakavu wa mradi unatusababisha kwenda kwenye upotevu wa maji na sisi tunapambana na kuzuia ama kupunguza upotevu wa maji ambao ni hasara kubwa. Upotevu wa maji unaenda mpaka kwenye mnyororo mzima wa uzalishaji wa dawa lakini pia pamoja na umeme unaotumika. Vilevile, maji yanapoenda kupotea maana yake inakuwa ni hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo tumelibeba kwa uzito stahiki na tunaenda kulifanyia kazi na kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri, tutahakikisha kwamba hicho kibali kinatoka ili uweze kuanza kufanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa maswali mafupi, Mheshimiwa Joseph Musukuma, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Ninapenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, mradi tegemezi uliopo katika Kijiji cha Lwezera umejengwa kwa zaidi

ya 45% lakini umesimama kutokana na ukosefu wa fedha, kwa hiyo mkandarasi ameamua kuondoka lakini *material* yote yako pale.

Je, ni lini Mheshimiwa Waziri utapeleka pesa na uko tayari tuambatane wote baada ya Bunge hili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Kaka yangu ameendelea kufuatilia sana mradi huu. Pia wakati Mheshimiwa Waziri wa Maji anawasilisha bajeti Bungeni aliweka mikakati ya Wizara, mkakati wa kwanza ulikuwa ni kwenda kukamilisha miradi ambayo imefikia ukingoni, kwa mfano 80%, 90% na kadhalika ili tui-*phase out* tubaki na miradi ambayo inafuatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni miradi ambayo ni ya kimkakati, na eneo la tatu ni eneo ambalo kuna sehemu ambazo tayari tumeshanunua mabomba, mabomba yako *site,* ili kuyaokoa yasipotee ama kutokea dharura au *emergency* yoyote hayo ni maeneo ambayo tunaenda kuyapatia huduma kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge amesema limefikia 40% eneo la Lwezera, nikutoe hofu katika maeneo matatu ambayo Mheshimiwa Waziri aliyawasilisha kama mkakati wa Serikali na la kwake liko ndani ya hiyo mikakati. Kwa hiyo, nimtoe hofu tutaenda kulifanyia kazi. Vilevile, ninamwahidi nikitoka hapa Bungeni nitamtafuta mkandarasi, nitaongea naye na nitamwonesha mpango wetu lakini pia nitamwomba arejee *site* wakati tukiwa tunafanyia kazi madai yake ili kuhakikisha kwamba mradi huu usisimame na uendelee kutekelezwa kwa namna ambavyo tumeupanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Florent Kyombo, swali la nyongeza.

MHE. FLORENT L. KYOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Tunaipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutujengea mradi kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya Kata za Kashenye, Kanyigo na awamu ya pili, Kata ya Bwanjai.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huo ulikamilika na wananchi wakaanza kufaidi maji kwa takribani miezi michache lakini sasa hivi mradi huo haufanyi kazi kwa sababu baadhi ya mabomba yameungua moto.

Ni nini kauli ya Serikali kuelekeza mabomba hayo yaweze kuwekwa kwa haraka ili wananchi ndani ya Kata ya Kashenye na maeneo ya Kanyigo waweze kupata huduma ya maji? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Kaka yangu, Mbunge wa Missenyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwepo Kagera na hilo tatizo tayari ninalifahamu na nimeshalitolea maelekezo kwamba, mabomba yapatikane haraka sana ili mradi uendelee kufanya kazi kama ambavyo umekusudiwa. Ni kazi kubwa sana ambayo ameifanya Mheshimiwa Mbunge ya kutafuta huu mradi, kuusimamia na hatimaye umekamilika, lakini sasa changamoto hii iliyojitokeza tunakiri kwamba tunazo taarifa na ndiyo sababu kuu iliyonifanya nielekezwe na Mheshimiwa Waziri wa Maji kwenda Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeenda, nimejionea baadhi ya mambo na nikatoa maelekezo, hata hivyo, maelekezo hayo yako katika utaratibu wa kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Christina Mndeme, swali la nyongeza.

MHE. CHRISTINA S. MNDEME: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali imekuwa na mpango mzuri wa kupeleka huduma ya maji kwa wananchi nchini, tunaipongeza sana Serikali kwa kumtua mama ndoo kichwani.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha mradi wa maji wa Goweko, Kigwa, na Igalula ambao umesimama kwa muda mrefu na hivyo kusababisha changamoto ya ukosefu wa maji na hususan kwa wanawake? Mradi huu uko Wilaya ya Uyui Mkoani Tabora.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na niendelee kumpongeza Mheshimiwa Christine Mdeme, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Tabora kwa kuendelea kuwasemea wananchi wa Tabora kwa ujumla lakini leo *specifically* akiongelea Goweko pamoja na Kigwa, ambapo kule ni kwa kaka yangu, Mheshimiwa Kawamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa inayofanywa na Waheshimiwa Wabunge wa Tabora wakiongozwa na Mbunge wa akina mama ambaye ameamua kupambana kwelikweli kuhakikisha kwamba akina mama wa Tabora wanapata huduma ya maji safi na salama. Salamu njema za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, fedha tayari imeshaenda, imepelekwa wiki iliyopita na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo pia anajua kwamba mradi huu unaenda kuendelea. Awamu iliyopita wakati tunaongelea sana kuhusu mabomba, mabomba yalipelekwa na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo akapokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba *combination* yenu hii inaonesha kabisa kwamba kweli mmekubali kutembea na falsafa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani na sisi Wizara ya Maji chini ya

Mheshimiwa Jumaa Aweso, tutawashika mkono na mtawatua akina mama ndoo kichwani. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Madini, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 29

Sera ya *Technology Transfer Agreements*

MHE. ASMA ALI MWINYI K.n.y. MHE. ESTHER N. MATIKO aliuliza:-

Je, kuna sera ya kulazimisha *Technology Transfer Agreements* kwenye Miradi ya *Critical Minerals*?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini ambalo limeulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Asma Ali Mwinyi, Mbunge wa Welezo - Zanzibar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Madini ya mwaka 2009, hususan Ibara ya 5(12), inaweka msingi wa kuimarisha ujuzi na uwezo wa kitaalamu wa Watanzania kupitia mafunzo na ushirikiano na kampuni za madini. Aidha, Kifungu cha 135 cha Sheria ya Madini, Sura ya 123, kinawataka wamiliki wa leseni za madini kuweka utaratibu wa kuhawilisha maarifa na teknolojia, kujenga uwezo wa wataalamu wa ndani na kutoa taarifa za utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni za Madini za Ushirikishwaji wa Watanzania za mwaka 2018 hususan Kanuni za 27 hadi 29,

zinawataka wawekezaji kuandaa mipango ya uhawilishaji wa teknolojia na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wake kwa Tume ya Madini. Hivyo, uhawilishaji wa teknolojia ni takwa la kisheria katika miradi ya madini, ikiwemo miradi ya madini muhimu na madini mkakati. Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa mipango hiyo ili kuhakikisha uhawilishaji wa teknolojia unajenga uwezo wa kitaalamu na kiteknolojia kwa weneyeji na hivyo kuimarisha ujuzi wa uongezaji thamani madini nchini na manufaa ya rasilimali za madini kwa maendeleo endelevu ya Taifa. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asma Mwinyi, swali la nyongeza.

MHE. ASMA ALI MWINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ambayo tumeyapata kutoka kwa Serikali. Kwa niaba ya Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ana maswali mawili ambayo angependa nimuulizie.

Swali la kwanza, Serikali inajiridhisha vipi kwamba wawekezaji wanahamisha teknolojia sahihi ya madini kwa vitendo badala ya kuwasilisha ripoti za kiutawala pekee?

Swali la pili, Serikali ina mpango gani wa kuweka viashiria vinavyopimika (*KPIs)* vya *technology transfer* hususan kwenye uchenjuaji na uongezaji wa thamani wa madini mkakati?

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Matiko pamoja na aliyemuulizia swali kwa maswali haya mawili ya nyongeza na ya muhimu sana kwa Watanzania wote. Ninapenda kujibu maswali yote mawili kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Madini na Tume ya Madini ambazo ni taasisi za Serikali zimeunda kamati mahususi inayoitwa Kamati ya Usimamizi wa Ushirikishwaji wa Watanzania katika sekta ya madini. Kazi ya Kamati hii ni kuhakikisha kwamba kila mwekezaji wa

madini au mwenye kuendesha mitambo ya uchakataji wa madini nchini anaandaa mpango mahsusi unaoitwa Mpango wa Ushirikishwaji wa Watanzania *(Local Content Plan)*. Akishaandaa mkakati huo unaletwa Wizarani na Tume ya Madini kuuthibitisha, anarudishiwa na kutakiwa kila baada ya miezi mitatu atoe taarifa ya jinsi alivyoutekeleza kwa vitendo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kipengele cha pili cha swali la Mheshimiwa Matiko kuna viashiria za kupima matokeo na tunaangalia kwenye ile taarifa ya kila miezi mitatu, je ni Watanzania wangapi wamejengewa uwezo wa kutumia kama ni mitambo au kama ni ujuzi wa uchimbaji au uchenjuaji wa madini, uongezaji thamani, wamepata teknolojia hiyo? Je, ni ajira ngapi zimepatikana kwa Watanzania kupitia uwekezaji huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, kamati hiyo ina wajibu wa kwenda katika maeneo ya ndani katika migodi na mitambo mbalimbali kushuhudia jinsi Watanzania wanavyoshirikishwa katika kuipata hiyo teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, kwa sababu kuna dhana nyingine ya wachimbaji wadogo kupata wawekezaji tunaowaita *technical support providers,* anapokuja mtu anayempa teknolojia mchimbaji mdogo mtaji na hiyo teknolojia ya uchimbaji ambayo yeye hana tunamtaka mwenye mgodi naye akae naye bega kwa bega ili aweze kujifunza teknolojia hiyo ili baadaye akija kupata mgodi mwingine asihitaji tena *technical support* kwa sababu tayari amepata ujuzi huo. Kama ambavyo Sera ya Serikali ya Madini pamoja na Kanuni za Uhawilishaji wa Teknolojia zinamtaka kila Mtanzania anayefanya kazi na taasisi zenye teknolojia za kisasa, kukaa karibu na kujifunza teknolojia hiyo. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya swali la Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwakumbushe, kama siku ya swali lako haupo unamwachia Mbunge mwingine basi Kiti

kijulishwe. Kiti kiwe na taarifa kwamba haupo na swali lako linaulizwa kwa niaba yako na Mbunge mwingine.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Mary Daniel Surati, Mbunge wa Serengeti, sasa aulize swali lake.

Na. 30

Ujenzi wa Barabara ya Natta – Mugumu

MHE. MARY D. SURATI aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Natta – Mugumu kwa kiwango cha lami utaanza?

NAIBU SPIKA: Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Kadogosa, majibu.

WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Daniel Surati, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usanifu wa sehemu ya Barabara ya Natta – Mugumu kilometa 37 kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami umekamilika. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mary Daniel Surati, swali la nyongeza.

MHE. MARY D. SURATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Masanja Kadogosa kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara ya Ujenzi. Sambamba na hilo, ninatumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais; tumepokea takribani shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Barabara ya Sanzate, Nata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninaomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Jimbo la Serengeti lina takribani miaka 50 na ni moja kati ya majimbo ama wilaya ambayo ina mchango mkubwa kwa Taifa letu kupitia Sekta ya Utalii, na wilaya ile haina hata barabara moja ya kiwango cha lami inayotuunganisha na wilaya ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha Wilaya ya Serengeti inaenda kuunganishwa na majimbo mengine ya wilaya za pembeni? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninashukuru sana kwa swali zuri sana la nyongeza na Waheshimiwa Wabunge wamepiga makofi, ina maana suala hili linahusu majimbo mengi zaidi. Hata hivyo, kama dira yetu inavyosema, Serikali imejipanga kwanza kuunganisha mikoa yetu. Ninajua tuna mikoa kama miwili iliyobaki sasa hivi, lakini baada ya hapo tunaunganisha wilaya na makao makuu ya mikoa na tunashuka katika tarafa, *then* katika kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna yoyote hatuwezi kuyafanya yote haya kwa mkupuo, lakini kama Mheshimiwa Mbunge anavyojua, tunazungumzia kwa mfano Barabara ya Sanzate - Nata, Mkoa wa Mara kilometa 40. Ninafikiri ujenzi unaendelea na mkandarasi yuko *site*. Pia, kuna Nata - Ikoma, kilometa 30, usanifu umeshaisha, tunajiandaa kwa ajili ya kuanza ujenzi na kuna Mugumu - Nyamongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama nilivyosema Serikali imejipanga vizuri sana kuhakikisha Taifa letu linakuwa na *network* ambayo inapitika sehemu zote, kwa maana ya lami na changarawe vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Nape Nnauye, swali la nyongeza.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ya kukamilisha madaraja ya Barabara ya Dar es Salaam – Mingoyo ambayo yalikuwa yakitusumbua kwa muda mrefu hasa wakati wa mvua; na Mheshimiwa Waziri anajua kwamba barabara hiyo sasa ina mashimo makubwa sana. Sasa wakati tukisubiri utekelezaji wa kile tulichokipitisha hapa Bungeni cha kuijenga upya barabara hiyo, je, Serikali iko tayari kuyafukia walau hayo mashimo ili tupunguze masaa tunayotumia kusafiri kwa kutumia hiyo barabara ya Kusini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie tu, ninajua kwamba wakati wa bajeti, ilikuwa ni moja ya hoja yake kubwa sana, lakini sisi kama Wizara tumejipanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, na Waheshimiwa Wabunge ninajua barabara kule hazina hali nzuri sana, na siyo tu barabara hii ya kutoka Dar es Salaam kwenda Mingoyo, bali pia kuna barabara yetu ya kutoka Babati inayounganisha na Singida, barabara ya kutoka Mwanza kuja Musoma, na barabara yetu ya kutoka Dodoma kwenda Iringa mpaka Igawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kitu ambacho tumejipanga kama Wizara, kwanza ni kufanya *partial rehabilitation* kwa ajili ya kuziba mashimo ili ziendelee kupitika. Vilevile, kufanya *assessment* nimeshatoa maagizo kwa Mkurugenzi wa *TANROADS* kufanya *proper assessment* kwa sababu barabara ni ile *layer* ya chini *(base)*. Kwa hiyo, hapa juu mnaweza mkafanya *partial rehabilitation* lakini kama imeshaumia mpaka huku chini ndiyo maana huwa mnaona kwamba barabara mnaiziba leo baada ya

siku mbili tena shimo limerudi. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie namna tunavyotumia *resources.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie tu tumeshaanza na kilometa 50 kwa Mheshimiwa Nape; kuna kilometa kama 100 ambazo hali yake siyo nzuri sana, tutaanza na kilometa hizo 50 lakini baadaye tutaendelea na katika maeneo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge mnataka kuuliza maswali kama hayo. Tuishukuru sana Serikali. Ninapenda niishukuru sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha. Tumeanza kuletewa fedha, si ndiyo hivyo jamani? Mnaweza mkaona kuna kitu kinaendelea kule. Ukilinganisha na miezi kama mitano iliyopita na kile tunachokiona sasa hivi kitaendelea nchi nzima. Hilo ninataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge. Kama ulikuwa una swali kama hilo ninafikiri nitakuwa nimeshatoa jibu lake kabla hujauliza. Ninashukuru sana. *(Makofi/Vicheko)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hapa nina orodha ya karibia watu 10. Kwa hiyo, ninadhani limejibiwa si ndiyo? Haya Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

MHE. DEODATUS P MWANYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Mimi siulizi la *rehabilitation*, Barabara ya Itoni – Lusitu tumeambiwa maneno mengi sana hapa, mkandarasi yuko *site,* pesa imetolewa lakini hakuna kinachoendelea kinachoonesha kama kweli Serikali imetoa pesa. Nini kauli ya Serikali kuhusu suala hilo la Itoni – Lusitu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwanyika ninajua swali hili aliniuliza nje ya Bunge na sasa hivi ananiuliza hapa. Kwa maana ya msimamo wa Serikali ni kama ule niliozungumza mbele ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, ninafikiri tulipita kule na bahati nzuri uli-*raise* tena hii *issue*. Nilishakutana tayari na mkandarasi na tulikubaliana ndani ya siku 30 atakuwa amesharudisha zile *equipment* zote ambazo alikuwa ameshaziondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafikiri mmeona nimezungumza mahala hapa. Kuna *movement* ambayo siyo nzuri sana. Kwamba unakuta mkandarasi ameshalipwa *advanced payment* tume-*miss* kulipa hata *one certificate, contractor* hatakiwi kuondoa mitambo *site*. Kuondoa mitambo *impliedly* kimkataba ni kwamba unafanya *termination*. Sasa nimeshawaagiza *TANROADS managers* kuanzia na mkurugenzi kwamba tukikuta vifaa vimeondolewa *site* na anayetoa kibali ili vile vifaa vipite barabarani ni *TANROADS* na Wizara ya Ujenzi. Kuanzia yule *TANROADS Manager* anaondoka mpaka kule vile vifaa vinakokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ina maana kubwa sana *contractual* kwa sababu unapofanya *mobilisation,* maana yake unapolipa *advance payment* ni kwa ajili ya *mobilisation*. Sasa, kama umefanya *mobilisation equipment* 130 upande mmoja halafu unatoa tena unapeleka kwa sababu umepata *project* upande mwingine maana yake huo ni wizi na hili nitalifuatilia kwa nguvu zangu zote na nimeshatoa maelekezo na *I mean it*. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi ni Mbunge wa awamu ya nne Jimbo la Nyang'hwale. Nimekuwa nikifuatilia ahadi za Marais waliopita akiwemo Rais Dkt. Jakaya Kikwete, Hayati Dkt. Magufuli na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan; walituahidi kutujengea barabara kwa kiwango cha lami kuanzia Kahama – Nyang'hwale – Busisi. Ahadi hii ni lini itatekelezwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika utekelezaji huu kuna yale ambayo yako ndani ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi lakini vilevile kuna viongozi wakuu ambao wanapita wakati wa kampeni wanaahidi. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tunayo orodha na kweli kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, hatuwezi kuwa na fedha zote tukajenga mambo yote kwa mkupuo. Mheshimiwa Mbunge ninakuhakikishia

kwamba ahadi hiyo ni katika utekelezaji wa *priority* zetu zile, *priority* mojawapo ni ahadi za Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, tutafika huko uwe na subira tu, tutafika. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Agnes Marwa, swali la nyongeza.

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Mugumu – Nata ni barabara ambayo bado iko kwenye upembuzi yakinifu na haijawahi kuguswa hata mara moja tangu kuumbwa kwa Dunia hii. Mvua inaponyesha barabara hiyo ni hatari sana, magari mengi ya watalii huwa yanakwama na haipitiki kabisa. Ili kuongeza pato la Taifa hili na ikizingatiwa kuwa Serengeti ndiyo kitovu cha utalii Tanzania; je, ni lini Serikali itapeleka pesa na kumaliza huo upembuzi yakinifu ili barabara hiyo ijengwe?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi. Hatuwezi kuwa na pesa za kujenga nchi nzima kwa mkupuo lakini kama nilivyosema Serikali tumeainisha kuna *trunk roads* na *reginal roads* lakini kuna barabara nyingine ambazo zina umuhimu sana kiuchumi, zile tunatoa kipaumbele katika kuanza nazo. Kwa hiyo, kitu ambacho ninaweza kusema tu ni kwamba Serikali kadiri inavyoleta fedha tutafika katika maeneo hayo, Mheshimiwa Mbunge uwe na imani hiyo kwamba Serikali hii inajenga miundombinu ya nchi hii na tutafika huko. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tuendelee na swali linalofuata. Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya, Mbunge wa Mbozi, sasa aulize swali lake.

Na. 31

Malipo ya Mkandarasi Barabara ya Mlowo – Kamsamba

MHE. ONESMO M. MNKONDYA aliuliza:-

Je, lini Serikali itamlipa mkandarasi malipo ya awali ya ujenzi wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba yenye Kilometa 130?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Onesmo, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Mkataba wa ujenzi wa sehemu za Mlowo – Zelezeta (kilometa 5) na Mkonko – Kamsamba (kilometa 5) ulisaniwa mwezi Juni, 2025. Hata hivyo, kama nilivyosema, ninafikiri Mheshimiwa aliweza kuuliza hili swali, tulikuahidi kwamba mpaka mwisho wa mwezi Oktoba tutaleta pesa hiyo *(advance) 1.2 billion shillings* ili tuanze kujenga. Mheshimiwa Mbunge uwe na amani tu kwa sababu ndiyo tunaelekea mwishoni.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mnkondya, swali la nyongeza.

MHE. ONESMO M. MNKONDYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninashukuru kwa majibu haya ya Serikali na namna ambavyo inataka kumalizia hapo mwishoni. Pamoja na hayo, tarehe 15 hiyohiyo ambayo ulikuja na Mheshimiwa Makamu wa Rais kwenye ziara muhimu kabisa mbele ya Watanzania na maelfu ya Wanambozi na Wanasongwe uliahidi kwamba mwisho wa mwezi huu (Oktoba) unakwenda kumlipa mkandarasi malipo ya awali. Mwisho wa mwezi huu ndiyo leo tarehe 28, tumebakiwa na siku mbili kufika tarehe 30 mkandarasi hajalipwa. Wananchi wa Mbozi waamini kauli ipi,

uliyoitoa tarehe 15 mbele ya Makamu wa Rais au unayoitoa leo kwamba unaendelea na mchakato wa kutafuta fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kama Wananchi wa Mbozi na Bunge lako Tukufu litapokea majibu haya anayoyatoa Mheshimiwa Waziri, je, Mheshimiwa Waziri uliwadanganya Wananchi wa Mbozi kwamba unamlipa mkandarasi fedha za awali na hii ni tarehe 28 hujamlipa? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge Onesmo ninajua hili jambo uko *very passionate* nalo. Ulileta wazee wa Mbozi wote na waganga wa kienyeji wote lakini mwisho wa mwezi haujafika usihukumu mapema, tunaelekea. Kwa hiyo, uwe na amani kwa sababu ninafikiri *contract* yote ni kama shilingi bilioni nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Advance payment* yake ni kama *1.25 billion shillings* na nilikuahidi kwamba pesa ambazo zitakuja tutakazoletewa kwa maana ya mwezi huu tutajitahidi sana kubana tukuletee na siku ile ulizungumza kwa hisia sana mpaka na kulia kabisa. Sasa hiyo ni ngumu kwelikweli. Tunaelewa machungu uliyonayo lakini vilevile uwe na imani kwamba Serikali inaposema tutaleta basi ninafikiri ina maana kubwa sana hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yawe mafupi. Mheshimiwa Kafiti, swali la nyongeza.

MHE. KAFITI W. KAFITI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona na mimi niweze kuuliza kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Ilemela. Kwanza, na mimi ninampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa sababu leo ndiyo anasimama mara ya kwanza kwenye hiyo *podium.* Tunaamini maswali yetu leo yatapata majibu. Mimi...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa uliza swali la nyongeza.

MHE. KAFITI W. KAFITI: Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la nyongeza ni kuhusu Barabara ya *Airport* – Kayenze. Ni lini sasa Serikali itamlipa huyu mkandarasi *advance payment* ili aanze ujenzi huo? Zimekuwa ahadi za maneno tu, sasa Mheshimiwa Waziri leo utuambie lini mkandarasi huyu atalipwa ili ujenzi huo uweze kuanza? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kafiti kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, *airport* ni sehemu ambazo ni muhimu sana. Ninafikiri kuna wakati ambao Serikali ilishakuja hapa ikazungumza kuhusu kuunganisha *airport* lakini vilevile kuunganisha *station* zetu za *SGR*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kafiti ninafikiri nilizungumza na wewe lakini kwa sababu umezungumza tena hapa ninarudia tu yale niliyokwambia pale kwamba yanafanana na hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile barabara tutaijenga na uwe na imani kwamba hatua ambazo tunazichukuwa sasa hivi tutakufikia. Serikali hii inataka kuunganisha *airport,* ndiyo kufungamanisha kule, kama Dira yetu inavyosema na kuunganisha *SGR*. Ninajua kuna Waheshimiwa Wabunge hapa inawezekana msipate muda wa kuuliza, kuna baadhi tulishaanza tayari usanifu kwa ajili ya kuunganisha na *station* zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninajua inapozungumzwa barabara hivi inaonekana kama pengine hakuna kinachofanyika lakini katika Taifa letu sasa hivi tuna miradi *almost* kama 105 yenye thamani ya shilingi trilioni 9.5 inayoendelea nchi nzima na hilo tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ukiangalia miradi inayoendelea ambayo ni kilometa 3,933 *almost* ni 25% ya barabara zetu mtandao mzima tangu Baba wa Taifa alivyoanza kujenga mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, Serikali hii kwa kweli imejipambanua vizuri sana katika ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna yoyote ile Waheshimiwa Wabunge yapo mabadiliko ambayo tutayafanya. Kuna wakati tutafanya maamuzi kidogo ambayo yatakuwa ni magumu lakini tushirikiane kwa sababu tuna mahitaji makubwa kama Taifa. Maendeleo ni makubwa sana. Nilikuwa ninatoa *statistics* nilipoitwa na Kamati yetu ya Bajeti nikawaambia; mwaka 2016 bandari yetu ilipokea mizigo tani milioni 16, Juni, 2026 tumepokea mizigo milioni 39.899. Kwa hiyo, ni milioni 40, kutoka milioni 16 mpaka milioni 40. Kwa hili tumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa *transformation* kubwa ambayo ameifanya bandarini na matokeo ndiyo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maana yake ni nini? Kudumu kwa barabara ni mambo mawili; la kwanza ni *loading, over loading* inaharibu barabara lakini vilevile *frequency* ya kukanyagwa. Kitu kimoja tu ninataka nimalizie, sasa ukiangalia barabara yetu moja tu ya *TANZAM* ya kwenda Zambia, mwaka 2021 magari ambayo yaliingia yalikuwa 54,000 lakini mwaka jana 2025 yaliingia magari 158,000. Zaidi ya mara tatu, si ndiyo hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia magari ambayo sisi tulitoa nje mwaka 2021yalikuwa 121,000, mwaka jana yalitoka magari 287,000. Kwa hiyo, *obvious* ninajua kuna mambo yanaendelea kule. Watu wanaangalia katika udogo. Ni kwamba tuna kitu cha kuangalia *positive* kwamba tumeenda mbele sana kwa maana ya mabadiliko ambayo tumefanya katika bandari na kama barabara zetu zinaonekana kuelemewa ni kwa sababu kuna maendeleo.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni kazi ya kuona namna ambayo tutahimili, na ninasema kwamba tutafanya mabadiliko. Msije mkashangaa Waheshimiwa Wabunge tuna-*introduce road tolls* watu walipie barabara, watu walipie madaraja, si ndiyo hivyo jamani? Ndiyo vitu ambavyo Waheshimiwa Wabunge tutaweza kuhimili haya mabadiliko makubwa ambayo tunayaleta. Tutakapofika hapo, tuwe pamoja kwa sababu tusipopata pesa, haya yote ambayo tunazungumza hayatawezekana. Ninashukuru sana, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa majibu mazuri ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Tunaendelea Wizara ya Afya, Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 32

Ukamilishaji wa Wodi ya Wanawake Katika Hospitali ya Mkoa Songwe

MHE. JULIANA D. SHONZA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha ujenzi wa wodi ya wanawake katika Hospitali ya Mkoa wa Songwe unakamilika kwa asilimia mia moja?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Shonza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la wodi ya wanawake (jengo la mama na mtoto) katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe. Aidha, ujenzi unaendelea na umefikia 80%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeingia mkataba na mkandarasi mpya ambaye ameanza kazi ya ukamilishaji wa jengo hilo, na linatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2027. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, majibu ambayo yanaendana kabisa na uhalisia wa kile kinachoendelea kule *site*. Nitakuwa na swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sasa tuna uhakika kwamba wodi ya mama na mtoto inaenda kukamilika katika hospitali ya Mkoa wa Songwe, ninataka tu nifahamu, je, Serikali imejipangaje katika kuhakikisha kwamba mara baada ya hilo jengo kukamilika tunaletewa vifaa vyote muhimu ili wanawake wenzangu wa Mkoa wa Songwe waweze kupata huduma stahiki na kwa wakati?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge Juliana Shonza kwa kuwapigania wanawake na watoto wa Mkoa wa Songwe. Kwa kufanya hivyo anaungana na Mheshimiwa Rais Daktari Samia Suluhu Hassan, ambaye yeye ndiye kinara wa kupunguza vifo vya mama na mtoto Afrika. Nijibu swali lake dogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba majengo haya ya mama na mtoto yanayoendelea nchi nzima ikiwemo Songwe, yanapatiwa vifaatiba kwa ajili ya kuhudumia wanawake na Watoto. Serikali imetenga shilingi bilioni 23 kupitia mradi wa uwekezaji katika afya ya mama na mtoto nchini Tanzania *(TMCHIP)*. Kwa hiyo, ninaomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mara jengo litakapoisha, tutaliwekea vifaa ili tuweze kuwahudumia wanawake wa Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kiza Mayeye, swali la nyongeza.

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Ujenzi wa wodi ya wanawake kujifungulia unapaswa kwenda sambamba na uwekaji wa vifaa kwa wanawake. Sera ya Mwaka 2007 inasema mwanamke anapokwenda kujifungua, atatibiwa bure, lakini katika Jimbo la Kigoma Kaskazini wanawake wanapokwenda kujifungua kwenye hospitali zetu, wanaambiwa waende na mipira, waende na *gloves*, waende na vibana vitovu vya mtoto mpaka sindano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kauli ya Serikali, je, ni lini wanawake watakapokwenda kujifungua vifaa vyote vya kujifungulia watavikuta katika hospitali zetu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Kiza Mayeye, mdogo wangu kutoka Kigoma kwa kuwapigania wanawake wa Kigoma ili waweze kupata huduma hizi kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mara ya pili anauliza swali hili, na nilishamthibitishia kwamba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inatenga shilingi bilioni saba kwa kila mwaka kwa sababu ya vifaa vya kujifungulia akina mama. Hivyo niwaelekeze tena Waganga Wakuu wa hospitali zote nchini, kwamba wanawake hao wanapoenda kujifungua watumie vifaa vile ambavyo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshanunua nchi nzima ili kuwahudumia hao wanawake wanaokwenda kujifungua ikiwemo wanawake wa Kigoma Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninaomba nimkumbushe kwamba, Serikali imezindua bima ya afya awamu ya pili, ambayo sasa imekuja na mwongozo madhubuti wa kuwakatia bima wale watu wasiokuwa na uwezo na makundi maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kupitia hizi njia zote mbili, kwa maana ya vifaa vinavyonunuliwa na Serikali na Bima ya Afya kwa

Wote, ni muda mwafaka sasa kuwahamasisha Watanzania wote, wananchi wote wakate bima ya afya kwa sababu sasa ndiyo mkombozi wa kupata huduma kwa urahisi kwa maana *affordability, accessibility*, na *equity* ili waweze kupata huduma hizi kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume, Mbunge wa Morogoro Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 33

Kuboresha Uzalishaji wa Karafuu Morogoro Kusini

MHE. ZUBERI Y. MFAUME aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia wakulima wa karafuu kwa kuwapa elimu, mbegu bora na mikopo ya pembejeo ili kuongeza uzalishaji?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania *(TARI)* inaendelea kuzalisha na kusambaza miche bora ya zao la karafuu kwa wakulima. Jitihada hizo zinafanyika sambamba na utoaji wa elimu kuhusu kilimo bora cha karafuu ili kuongeza tija na uzalishaji wa zao hilo pamoja na kuhamasisha wakulima kutumia fursa ya mikopo kwa Taasisi za fedha ikiwemo Mfuko wa udhamini wa Pembejeo za Kilimo *(AGITF)* na Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa 2024/2025, *TARI* ilizalisha jumla ya miche bora 235,000 ya zao la karafuu ambayo ilisambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku, ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga ilipatiwa miche 55,000, Morogoro Mjini miche 25,000, Gairo miche 19,000, Kilosa miche 21,000, Ifakara miche 15,000, Mvomero miche 50,000 na Morogoro Vijijini miche 50,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika msimu wa 2026/2027, jumla ya miche 4,117 imeendelea kutunzwa katika kitalu cha *TARI* Mlingano kwa ajili ya kusambazwa katika maeneo ya uzalishaji ikiwemo Mkoa wa Morogoro.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zuberi Mfaume, swali la nyongeza.

MHE. ZUBERI Y. MFAUME: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, na ahsante Serikali kwa majibu yao mazuri. Nina maswali madogo mawili ya nyongeza. La kwanza, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro inaendeleza mpango wa kutoa miche 20 kwa kila mwanafunzi anayejiunga na kidato cha kwanza katika sekondari, ili watakapomaliza elimu ya sekondari waweze kujitegemea katika eneo hilo. Hata hivyo, wanashindwa kukamilisha mpango huu kutokana na rasilimali chache walizonazo:-

(a) Je, Wizara ina mpango gani kuunga mkono Ofisi ya Mkuu wa Mkoa katika kutoa mbegu bora za miche ya karafuu kwa wanafunzi?

(b) Je, Wizara pia ina mpango gani sasa katika kuhakikisha ukusanyaji na uuzaji wa karafuu unarasimishwa ili kuondokana na walanguzi wanaovamia soko la karafuu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Zuberi Yahya Mfaume kwa maswali mawili ya msingi ya nyongeza ambayo yana faida kubwa kwa Mkoa wa Morogoro pamoja na jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimthibitishie tu kwamba tunatambua jitihada kubwa zinazofanywa na Ofisi ya Mkoa wa Morogoro. Sisi kama Wizara ya Kilimo katika mwaka wa fedha 2026/2027 tumetenga fedha kwa ajili ya mazao ya viungo, ikiwemo karafuu kwa ajili ya kuzalisha miche pamoja na kununua miche mingine ambayo imekuwa ikizalishwa na wadau wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, fedha hizo zipo na tunatumia fedha hizo kwa ajili ya mpango wa ruzuku kwa ajili ya kuwafikisha wananchi. Katika sehemu ya fedha hizo ambazo tumezitenga kupitia *COPRA*, Mkoa wa Morogoro ni sehemu ya watu ambao tutapeleka hiyo miche ambayo sasa ninafikiri katika ule mpango wa mkoa, na hizo fedha tutakazopeleka na hiyo miche tutakayowapatia, maana yake itaongeza ile nguvu ambayo Mkoa wa Morogoro imeanzisha. Kwa hiyo, tayari jambo hilo ninalifahamu na lipo katika huo mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kuhusu urasilimishaji wa mazao hayo hasa katika ukusanyaji na utunzaji, ni kwamba Wizara kupitia *COPRA* tayari tumeshatengeneza mwongozo ambao utasimamia ukusanyaji na uuzaji wa zao hili, ikiwemo biashara ambayo inafanyika kutokana na mazao ya viungo, ikiwemo karafuu. Kwa hiyo, tayari lipo, na mwongozo huu tumepanga utaanza kwa ajili ya kutumika kwa ajili ya Mkoa wa Morogoro pamoja na mkoa wa Tanga. Jambo hili linaanza katika mwaka huu wa fedha. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge maswali yawe mafupi, muda wetu umekwenda. Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Serikali iliahidi kuwapatia miche bora ya ruzuku wakulima wa parachichi nchini. Je, ni lini sasa wakulima wa Jimbo la Kilolo watafikiwa kupata mbegu bora na ya ruzuku?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Kilolo. Mpango huo ni endelevu na tunaendelea nao sisi Wizara ya Kilimo kutoa miche ya parachichi kupitia bodi zetu. Mwaka huu tunategemea kufanya hivyo. Niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge, katika maeneo ambayo wanalima parachichi, tutalitekeleza hilo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Nuwas Emanuel, Swali la nyongeza.

MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza niishukuru Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwasaidia wakulima wa zao la dengu kwa kuwawezesha kuuza mazao yao katika maeneo yao kwa kuboresha uuzaji. Hili limesaidia wakulima hawa kupata bei nzuri ya dengu kutoka shilingi 700 kwa kilo kwa mwaka 2025, na mwaka 2026 kuwa shilingi 1,400 kwa kilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, kwa kuwa wakulima hao wamekuwa wakizalisha zao hili bila kupata mbegu bora, je, Serikali ina mkakati geni kuwasaidia wakulima wa dengu kupata mbegu bora ili kuongeza uzalishaji?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Nuwas Emanuel, Mbunge wa Mbulu Vijijini kwa swali lake la msingi. Mkakati wa Serikali ni kwamba, Wizara ilishaelekeza watu wetu wa taasisi ya *TARI* kufanya tafiti na

kupata mbegu ambayo inazalisha zaidi dengu. Wapo kwenye hatua za mwisho za utafiti. Wakishakamilisha ule utafiti sasa, mbegu hizo tutazipeleka *ASA* kwa ajili ya uzalishaji na tuzilete kwa wakulima wetu. Kwa hiyo jambo hilo tayari lipo katika utekelezaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masache Kasaka, swali la nyongeza.

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Wakulima wangu wa tumbaku katika Wilaya ya Chunya, takribani vyama vya ushirika vitano vinadai malipo yao kutokana na kuuza tumbaku yao kwa mwaka wa kilimo uliopita. Je, Serikali ina mpango upi wa kuhakikisha inayabana yale makampuni ili wakulima hao walipwe pesa zao kwa kuwa msimu wa kilimo ndiyo tunaenda kuanza sasa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Chunya kwa swali lake zuri la msingi. Nimthibitishie tu kwamba nilikuwa ninazungumza muda siyo mrefu na Mkurugenzi wa Bodi ya Tumbaku, na katika moja ya maelekezo aliyoniambia ni kwamba walishakubaliana na yale makampuni yote kwamba kabla ya msimu kuanza, watahakikisha kwamba wamewalipa wakulima ili sasa tunapokwenda kuanzisha msimu mwingine kusiwe na madai yale yanayohusika na madeni. Kwa hiyo, tutakwenda kulifuatilia ili tuone sasa hizo *AMCOS* zake tano wanalipwa kwa wakati, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Hawa subira Mwaifunga, Mbunge wa Tabora Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 34

Elimu Kuhusu Nishati Safi ya Kukausha Tumbaku

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA aliuliza:-

Ni lini Serikali itatoa elimu kwa wakulima wa tumbaku wa Tabora kuhusu matumizi ya nishati safi ya kukaushia Tumbaku?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku imeendelea kutoa elimu mbalimbali, ikiwemo mbinu ya kilimo bora cha tumbaku, udhibiti wa wadudu na magonjwa, uvunaji na ukaushaji kwa kutumia nishati safi, ambapo elimu hiyo imelenga kuboresha majiko ya mabani ya kukaushia tumbaku kwa kutumia majiko sanifu ambayo yanatumia kuni kidogo na nyembamba (matawi ya miti) badala ya magogo ambayo hupatikana kwa kukata mti. Aidha, hadi kufikia Septemba, 2026, wakulima 2,000 wamepatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya nishati safi ya kukaushia tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tafiti za kupata nishati safi na endelevu zinaendelea kufanyika ili kupata mbadala wa nishati ya kuni za kukaushia tumbaku, ikiwa ni pamoja na matumizi ya makaa ya mawe kwa kushirikiana na *STAMICO* ambayo imetengeneza tofali za makaa ya mawe zinazoitwa *Rafiki Briquetts.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendeleza jitihada za uhifadhi wa mazingira, Bodi imeendelea kuhamasisha kilimo cha tumbaku inayokaushwa kwa hewa na tumbaku inayokaushwa kwa njia ya jua *(sun cured variety)*. Tumbaku hizi ni rafiki kwa mazingira na zimeanza kupata mwitikio katika Mkoa wa Ruvuma, Tabora (Nzega), Geita (Chato) Iringa na Singida (Manyoni na Ikungi).

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, swali la nyongeza.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Zaidi ya 60% ya tumbaku nchini inalimwa Tabora, hivyo tunaona ni kwa namna gani ambavyo mazingira yamekuwa yakiathirika kutokana na ukaushaji wa tumbaku katika Mkoa wa Tabora. Elimu ya kutumia nishati safi katika Mkoa wa Tabora wakulima wetu bado elimu hiyo hawajaipata kwa ukamilifu wake, kwa sababu hata hayo mabani ambayo yamezungumzwa hapo, Tabora hayapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni kuwa sasa umefika wakati wa kushirikiana na wadau mbalimbali wa tumbaku ili kuhakikisha kuwa tunaondokana na nishati chafu ambayo inatumika kwa sasa ili tuingie kwenye nishati safi kwa ajili ya kukausha tumbaku zetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, bado ipo changamoto kubwa sana ya namna ambavyo haya makaa rafiki yanaweza kutumiwa na wakulima, katika kuhakikisha kwamba tunakwenda kuondokana na kutumia magogo na sasa kwenda kwenye nishati safi. Wakulima wamekuwa wakilalamika kwamba ni makaa ambayo hayawezi kabisa kufanya shughuli ya kukausha tumbaku. Je, Serikali ina mpango gani wa kuja na nishati mbadala kuhakikisha kwamba tunaunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais za kutumia nishati safi katika zao hili la tumbaku?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Tabora Mjini, dada yangu Mheshimiwa Hawa Mwaifunga kwa maswali yake mazuri na ya msingi. Nimwondoe shaka tu kwamba kilimo cha tumbaku unapoanza msimu, sharti la kwanza ambalo tunaendana na masharti ya dunia ni kwamba, mkulima hawezi kulima tumbaku bila kusajiliwa na Bodi ya Tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakulima kabla hujaingia kwenye msimu wa tumbaku, ni lazima asajiliwe na bodi, na bodi inampa namba maalum ambayo atakapokuja kuuza tumbaku, maana yake watakuwa wana uwezo wa kukum-*trace* wakati ule anasajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunakuwa tunawasajili, tunawapa elimu kuhusu kilimo cha tumbaku, ikiwemo majiko ambayo unapaswa utumie kwa ajili ya kukaushia tumbaku. Vilevile sharti lingine ambalo tumekuwa tukiwapa wakulima, ni pamoja na kupanda miti ili kutunza mazingira. Jambo ambalo sasa wakulima watapanda, lakini sasa kwenye utunzaji hiyo ni kesi nyingine ambayo wakulima wengi wamekuwa hawalifuatilii jambo hilo. Kwa hiyo, hilo tumekuwa tukilifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Mbunge ameuliza hapa, kwamba je, Serikali tuko tayari kushirikiana na wadau? Ni kweli Serikali tuko tayari muda wote na tumekuwa tukishirikiana na wadau mbalimbali katika kumsaidia mkulima wa tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kama sasa hivi Bodi ya Tumbaku tunashirikiana na Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela ambacho na wao wamekuja na jiko bora kabisa kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wa tumbaku, linalotumia mkaa kidogo na kuboresha ile tumbaku yake. Hicho ndiyo kitu ambacho tumekuwa tukikifanya ili kuhakikisha kwamba tunaondokana na huu utaratibu wa kukata miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusu makaa, ni kweli tunafanya utafiti, na sasa hivi tupo kwenye yale mashamba yetu darasa tunayatumia kwa ajili ya kuona ile tumbaku kama bado inaweza kulinda ubora wake *(quality)* kutokana na majiko haya. Tukishamaliza, maana yake sasa tukiona ubora umekuwa *maintained*, maana yake tutayapeleka sasa kwa wakulima kwa ajili ya matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho tumetenga fedha mwaka huu karibu shilingi milioni 450 kwa ajili ya ujenzi wa majiko banifu ya sola ambayo nayo yatakuwa kwa ajili ya msaada kwa ajili ya kuwapelekea wakulima, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, Mbunge wa Itigi sasa aulize swali lake.

Na. 35

Udhibiti wa Wanyama Waharibifu (Tembo) Jimbo la Itigi

MHE. YOHANA S. MSITA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti Wanyama waharibifu hususan tembo wanaosababisha uharibifu wa mazao na mali Jimbo la Itigi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Chande, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kusimamia Utatuzi wa Migogoro baina ya Binadamu na Wanyamapori kwa kuchukua hatua mbalimbali na za haraka katika kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu hususan tembo wanaovamia na kusababisha uharibifu wa mazao na mali za wananchi kwenye maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Jimbo la Itigi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa jitihada hizo ni pamoja na kuendelea kutumia kituo cha kudumu cha askari kilichopo katika Kijiji cha Doroto na kambi za muda mfupi tatu, kwenye vijiji vya Chisingisa, Sanjaranda, na Kitaraka kwa ajili ya kuitikia kwa haraka kwenye matukio na kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu; kuendelea kuimarisha doria za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu; kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu mbinu rafiki za kudhibiti wanyamapori hao; kuendelea kugawa kwa wananchi nyenzo na vifaa rafiki vya kudhibiti na kufukuza tembo kwenye vijiji mbalimbali; kuendelea kutumia teknolojia ya ndege nyuki *(drones);* na kuendelea kushirikiana na wadau ambapo Serikali kwa kushirikiana na shirika lisilo la Kiserikali la *Southern Tanzania Elephant Program (STEP)* imetengeneza vihenge 24 vya kuhifadhi mazao vilivyoboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hatua hizo, Serikali imevuna tembo wawili waliokuwa wakihatarisha usalama wa maisha na mali za wananchi katika vijiji vya Doroto na Sanjaranda, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, swali la nyongeza.

MHE. YOHANA S. MSITA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kupitia Naibu Waziri, lakini Jimbo la Itigi ambalo linapakana na mapori ya hifadhi matatu (Kizigo, Muhesi na Rungwa) na vijiji takribani 10 vinaathirika sana na wanyama waharibifu hawa tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vya Doroto, Kitaraka, Kihanju, Sanjaranda, Aghondi, Njirii, Kamenyanga, Idodyandole, Damwelu na Gurungu kuna makundi makubwa sana ya tembo kwenye vijiji hivi na kwenye majibu ya Serikali kwamba wamevuna tembo wawili. Sasa je, Serikali haioni iko haja sasa ya kuongeza uvunaji kwa sababu tembo wameongezeka kwa kiwango kikubwa na wanaoathirika ni zaidi ya vijiji 10?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa Askari wetu wa wanyamapori ni wachache na takribani kata tano zote zinaathirika na hivi vijiji 10 ambavyo nimevitaja, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Askari wa Wanyamapori ili kuweza kudhibiti hii hali ya uharibifu wa hawa wanyama waharibifu kama tembo kwenye Jimbo la Itigi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Msita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu ninaomba uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Msita amekuwa na yeye ni sehemu ya hifadhi na namna anavyoshirikiana na wananchi wake, anavyoshirikiana na Serikali katika kufukuza na kuwaweka mbali tembo katika makazi ya watu, nimpongeze sana ndugu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza, ni kweli kwamba Serikali ilivuna tembo wawili na kwa sasa kadhia hiyo ambayo ipo kule Itigi Serikali inatambua jambo hilo, lakini lazima tunapotaka kuvuna wale tufuate sheria, kanuni na taratibu. Kwa hivyo, bado tupo katika misingi hiyo. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwa na subira, wataalamu wetu wanafanya utafiti kwa wale tembo ambao wamekuwa ni hatarishi zaidi na hawadhibitiki, basi Serikali inaweza kuchukua hatua ya kuvuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili hili, kwanza tumshukuru na tumpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa idadi ya Askari ambao ametoa kibali, ndani ya mwaka huu tu, ametoka kibali cha Askari 652 na tayari hivi tunavyozungumza wameshaajiriwa vijana hao 652 (Askari na Maafisa mbalimbali). Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ajira hii kubwa kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe maelekezo kwa Kamishna wa *TAWA,* vijana hao wanapoanza mgao, basi waangalie kwa jicho maalum hili Jimbo la Itigi kupeleka vijana wa kutosha kabisa pamoja na Majimbo mengine ambayo yanapata changamoto kama hizi, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa muda umekwenda sana. Mheshimiwa Sara Msafiri atamalizia Mheshimiwa Yahya Mhata.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba uniruhusu kwanza nitoe salamu za pole kwa wananchi wangu wa Jimbo la Mvomero kwa kuondokewa na Mwenyekiti wa Kijiji, Kata ya Mkata ambaye amefariki jana kwa ajali ya tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameongea mikakati mingi ya Serikali katika kudhibiti wanyama wakali tembo, na Jimbo la Mvomero lina kata tano: Kata ya Msongozi, Melela, Doma, na Mangae ambayo hali ya wanyama waharibifu imekuwa kubwa ambapo wananchi wamepoteza mali, wamejeruhiwa, na wanaendelea kufariki:-

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini sasa Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuja kwenye maeneo haya ya kata tano ndani ya Jimbo la Mvomero ili kuongea na wananchi hawa kuwapa matumaini makubwa na kuwaeleza mipango ya kugawa vifaa hivyo alivyosema vya kudhibiti wanyama wakali wanapoendelea na shughuli zao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nami nichukue fursa hii kumpa pole sana Mheshimiwa Mbunge, na familia ya watu hao ambao limetokea jambo hilo. Nitoe maelekezo kwa Kamishna wetu wa *TAWA* aende eneo hilo kabla ya mimi kuambatana na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tukimaliza Bunge tu tutaenda huko kwanza kutoa faraja kwa wale ambao wamepata huo msiba, lakini pili, kuhakikisha

kwamba nako tumegawa vifaa rafiki ambavyo wanaweza kujikinga kwa kiasi fulani au kukabiliana na wanyama hao wakali na waharibifu, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yahya Mhata, swali la nyongeza.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nami ninaomba nichukue nafasi hii kwanza kuipongeza sana Serikali kwanza kwa kutupatia watumishi wapya wa hifadhi ambao wamekuja ndani ya Jimbo langu, ninashukuru sana. Pia, tumepokea ndege nyuki ambayo imesaidia sana kukabiliana na wanyama waharibifu hasa tembo. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Rais wetu kwa ahadi ambayo ameitoa na ameitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ombi letu kwa Wizara. Kwa kuwa tunayo madhara makubwa ambayo yalisababishwa na hawa wanyama waharibifu, watu wamepoteza maisha na baadhi ya maeneo mali zao zimeharibiwa, lakini hadi sasa hivi hawajalipwa fidia, je, nini kauli ya Wizara kuhakikisha kwamba wananchi wangu wote waliopata madhara haya wa Jimbo la Nanyumbu sasa wanalipwa fidia kwa wakati?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na nimpongeze sana Mheshimiwa Yahya kwa ufuatiliaji wa karibu sana, na yeye amekuwa kama sehemu ya uhifadhi sasa. Kweli wako watu ambao hawajafikiwa na kifuta jasho na kifuta machozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake hatuwezi kukiita fidia, ni kifuta jasho na kifuta machozi. Kweli wako ambao hawajafikiwa na ziko changamoto mbalimbali ambazo zilitokea pengine mtu katika kujaza kwenye mfumo wetu ule wa *PAIS* namba ya simu aliyoiweka usajili wake ni wa jina la mtu mwingine. Sasa hii kidogo inaleta usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Yahya, tukitoka hapa twende kukaa, mimi na yeye anipe orodha ya wale ambao hawajapata kifuta jasho hicho na nimhakikishie Mheshimiwa Yahya ndani ya miezi hii miwili hao watalipwa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwetu na majibu kutoka upande wa Serikali na muda wetu umekimbia kweli kweli.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo. Kwanza ni wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Spika kutoka Jijini Dar es Salaam. Tunaye Ndugu Rajab Ndomondo, Mkurugenzi wa *Rajai Foundation;* Ndugu Saleh Omar Saleh, Mjumbe wa Kamati ya Amani ya Viongozi wa Dini; na Ndugu Shafii Bora aliyekuwa Mkurugenzi wa Kwanza wa Klabu ya Simba na Mfadhili wa Klabu ya Majimaji, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine 20 wa Mheshimiwa Spika, tunao Wanafunzi na Walimu wa *First Years Academy* kutoka Kata ya Upanga, Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mkurugenzi Ndugu Zoheb Bora, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, mgeni huyo ni Dkt. Fred Msemwa, Katibu Mkuu Uwekezaji, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wengine 12 wa Mheshimiwa Profesa Mkumbo ambao ni Menejimenti ya Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji na Menejimenti ya Tume ya Taifa ya Mipango, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wengine wawili wa Mheshimiwa Profesa Mkumbo ambao ni Viongozi kutoka Ofisi ya Mbunge, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Paul Christian Makonda, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni Ndugu Gerson Msigwa, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, karibu sana, karibu sana Mheshimiwa Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Pia, tunaye Ndugu Jihan Dimack, Mshindi wa *Miss Grand International,* ahsante. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Saumu Juma Ally, *Matron* wa *Miss Grand International,* ahsante. *(Makofi)*

Wageni wengine saba wa Mheshimiwa Makonda ni Viongozi wa *Miss Grand* Tanzania na Watendaji wa Wizara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine 11 wa Mheshimiwa Makonda ambao ni Mashabiki wa *Miss Grand International* waliomsaidia kwenye kampeni ya ushindi wakiongozwa na Ndugu Vincent Njau au Kiredio. Ndugu Vincent Njau ni maarufu kama Kiredio. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine nane wa Mheshimiwa Makonda ambao ni viongozi na washindi mbalimbali wa mashindano ya ulimbwende kuanzia mwaka 2023 hadi 2026, karibuni sana Bungeni wageni wetu. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga ambao ni Walimu wa Shule ya Sekondari Kariakoo kutoka Mkoani Tabora. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo ambaye pia ni Naibu Waziri, hawa ni marafiki zake kutoka *Johari Rottana Hotel* ya Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni 45 wa Mheshimiwa Mary Daniel Surati ambao ni Washindi wa Programu ya Samia Uthubutu *Awards,* Wanafunzi na Walimu wa Sekondari Makundusi na Namanga kutoka Jimbo la Serengeti Mkoani Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 45 wa Mheshimiwa Kafiti William Kafiti ambao ni Madiwani 26 wakiongozwa na Meya wa Manispaa ya Ilemela, Mheshimiwa Sarah Ngwani pamoja na wataalamu na Wakuu Idara na Vitengo 22 wakiongozwa na Ndugu Ummy Wayayu, Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wetu wote karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya Mafunzo. Tunao Wajumbe wa Bodi wa Wawakilishi 53 kutoka Taasisi ya *Africa Initiatives Development Foundation Tanzania* kutoka Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Pwani, na Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 40 na walimu sita wa Shule ya Awali na Msingi *Theresian Sister's* kutoka Wilaya ya Ubungo, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana na ahsanteni sana.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Mwongozo wa Kiti, Mheshimiwa Ester Bulaya.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mwongozo wako kwa kanuni nambari 79; kwa ruhusa yako naomba niisome. "Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa na kama haliruhusiwi kwa majibu kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yanaweza kutolewa papo hapo au baadaye kwa kadiri anavyoona inafaa."

Mheshimiwa Naibu Spika, punde tu umetoka kumtambulisha Mgeni wa Waziri wa Michezo, Mheshimiwa Paul Christian Makonda ambaye Mgeni wake ni *Miss Grand International* Jihan ambaye

amepata ushindi huo hivi karibuni tarehe 10 nchini Thailand, yuko hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumempongeza kwa makofi, lakini ushindi wake umetangaza Taifa letu, umetangaza utalii, umeleta heshima kwa nchi yetu na ushindi huu uliunganisha Taifa kiasi kwamba watu walisahau Simba na Yanga, walikuwa wanazungumza Jihan na mashindano yanayoendelea Thailand.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Kiti chako kitaona inafaa na inawezekana kwa mujibu wa kanuni ambayo nimeitaja, walau tupate dakika chache kama Wabunge, tumpongeze na iingie kwenye *Hansard* kwa jambo kubwa la kihistoria ambalo ameifanyia nchi yetu, Mwanamke wa kwanza kutoka Afrika, Mwanamke wa kwanza kutoka Tanzania kubeba taji la Dunia kupitia tasnia ya urembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Ester Bulaya kwa kanuni yetu ya 79 akiomba Mwongozo wa Kiti kwa jambo ambalo limetokea hivi punde hapa ndani ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa jambo hili kama ambavyo amesema Mheshimiwa Ester Bulaya linagusa maslahi ya Taifa na limetangaza Tanzania Kimataifa, ninatoa mwongozo kwamba nitawapa nafasi Wabunge watatu akiwepo Mheshimiwa Ester Bulaya waweze kuchangia hoja hii ambayo ina maslahi makubwa kwa Taifa letu.

Ataanza mwenyewe Mheshimiwa Ester Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Halamga, atamalizia Mheshimiwa Zainab Abdallah. Mheshimiwa Ester Bulaya karibu. *(Makofi)*

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Mbele yetu ndani ya Bunge hili yuko binti wa Kitanzania pale juu jina lake anaitwa Jihan Dimack, kwa heshima kubwa ana sifa zote za kupongezwa kwa kuliletea heshima Taifa letu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester, dakika tatu tatu.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, dalili za kuliletea heshima Taifa letu zilianza kwenye vazi lake la Taifa ambalo lilibeba na kuuza mbuga za wanyama wetu, vazi ambalo lilibeba na kuiuza Zanzibar, vazi ambalo lilionyesha Utanzania wetu, vazi ambalo lilionyesha utamaduni wa kimasai na alipita kwa madaha, aliiuza nchi yake, aliiuza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mlimbwende huyu wa Dunia, *Miss Grand* kutoka Tanzania aliizungumzia vizuri nchi yetu na hasa suala la amani na utulivu wa nchi yetu, anapaswa sana kupongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ukampongeza Jihan leo bila kumtaja Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, bila kutaja uwekezaji mzuri kwenye Wizara hii inayoongozwa na kaka yangu mhamasishaji niliyemwachia kijiti Mheshimiwa Paul Christian Makonda kwani walifanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ushindi wa Jihan utafungua njia. Tukumbuke Mashindano ya *Miss World* yanafanyika kwenye Taifa letu. Nina hakika ushindi wake utaongeza morali kwa walimbwende hasa mlimbwende wetu atakayewakilisha Taifa letu katika Mashindano ya *Miss World* ambayo yanafanyika nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze sana sana *Gen Z* wa nchi hii *(Influencer)* katika mitandao ya jamii, mchezo huu ulikuwa wa *social media*. Vijana wa Kitanzania walisimama kufanya kampeni na mashindano haya unatumia gharama kupiga kura, walichangishana.

Niwapongeze Wizara, waliongoza kampeni hiyo, Mheshimiwa Rais pia aliongoza kampeni hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nimtaje Niffer, nimtaje Vincent Njau, nimtaje Catherine Ngowo, maarufu kama Carry Mastory, Niffer nimemtaja hapa ni Jenifer Jovin, Kiredio nimemtaja hapa. Hao wote waliongoza kampeni na wakashawishi Mataifa mengine yakiwepo ya Afrika ambao walikuwa wana wagombea kwenye mashindano hayo kama *Nigeria*, wote kuungana na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza vijana wa Kitanzania wakiamua wanaungana kubeba Taifa lao. Mmeonyesha mfano mzuri na mimi kama dada yenu niliyeanzia Ubunge wa vijana, ninawaambia tuungane, tutumie mitandao ya kijamii kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu; tutumie mitandao ya kijamii kwa ajili ya kutangaza biashara zenu ninyi vijana. Sasa hivi *social media* kuna pesa. Tusitumie mitandao ya kijamii kufarakanisha Taifa letu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, tusitumie mitandao ya kijamii kwa kutumika vibaya kutaka kuleta machafuko kwenye nchi yetu. Tutumie mitandao ya jamii kwa kutengeneza pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, ninakushukuru. Ninarudia kumshukuru na kumpongeza Rais wetu kwa kuwekeza katika Wizara hii. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara yake, kwa kazi kubwa wanayoifanya. Nami ninamwahidi, tutawaunga mkono, tunaona matokeo na Taifa hili linataka watu wanaoleta matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Atafuatia Mheshimiwa Asia Halamga, Mheshimiwa Zainab Abdallah ajiandae, lakini mwisho tutamalizia na Mheshimiwa Waziri wetu wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Paul Makonda.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami ya kuungana katika pongezi ya kumpongeza kijana wa Kitanzania aliyeweza kupasua mawimbi ya Afrika, pia akaenda kwenye fainali kule duniani. Mashindano ya *Miss Grand International* ambayo kijana wa Kitanzania ameweza kuchukua taji la ushindi, ndugu yetu Jihan Dimack, tunachukua nafasi hii kulipongeza Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote, kwa kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwashika vijana wa Kitanzania wale wote ambao wanapata fursa ya kuweza kuvuka ng'ambo na kwenda kushindana katika Mataifa mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashindano haya yalikuwa takribani nchi 70. Tunaweza kuona ndani ya nchi 70 bendera ya Tanzania, ndugu yetu Jihan ameweza kuchukua taji hili. Nini maana yake? Maana yake ni kwamba, ni mwendelezo wa ile diplomasia ambayo Mheshimiwa Rais ameweza kuitengeneza katika nchi yetu dhidi ya Mataifa mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, inatufungua sasa kwamba, mabinti wa Kitanzania wana uwezo wa kufanya maajabu makubwa duniani. Hapa tunatoa wito kwa mabinti wote, kwamba mabinti wa Kitanzania tunaweza. Tunaweza kufanya mambo makubwa, kila mmoja ajiamini. Jihan ametuonyesha kwamba wasichana wanaweza kuwa viongozi, wanaweza kuwa wapeperushaji wa bendera ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukue nafasi hii, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Rais na Wizara kwa kazi kubwa, kazi kubwa ambayo imefanyika kwa vijana wa Kitanzania kuhakikisha wamepiga kura kuhakikisha wamehamasisha ushindi huu, umepatikana. Kama alivyosema Mheshimiwa Ester Bulaya, dada yetu Niffer, akina Kiredio, akina Juma Lokole, vijana wa Kitanzania ma-*influencer* wamefanya kazi kubwa ya kuhakikisha ushindi unakuja katika Taifa letu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonyesha vijana wa Kitanzania tuna uwezo wa kulijenga Taifa na siyo kulibomoa Taifa. Tusonge mbele *(aluta continua)*, vijana wa Tanzania tunaweza kwa mafanikio makubwa zaidi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zainab Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Paul Makonda.

MHE. ZAINAB ABDALLAH ISSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kuwakilisha sauti za vijana wa Tanzania, na kwa upekee vijana ambao tunawawakilisha ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna ya kipekee kabisa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya kupitia Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninasema Mheshimiwa Rais amefanya uwekezaji mkubwa sana kwenye Wizara hii. Moja ya mambo makubwa ambayo ameyafanya kupitia sekta hii ya urembo na ulimbwende, Mheshimiwa Rais kwa miaka mitatu mfululizo nchi yetu imeweza kuandaa *Miss and Mister Deaf International*, jukwaa ambalo limeweza kuwaunganisha wanamitindo kutoka sehemu mbalimbali duniani, hivyo, kuifanya Tanzania kuweza kutambulika Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kupitia Mheshimiwa Rais, pia Mheshimiwa Waziri wetu Mheshimiwa Paul Makonda, nchi yetu mwakani inaenda kuwa mwenyeji wa mashindano ya *Miss World*. Haya ni mafanikio makubwa sana ndani ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu, kwa mwaka huu *Miss World* imeweza kuunganisha washiriki 111 kutoka Mataifa mbalimbali duniani. Tunaamini ujio wa Mataifa haya Tanzania utaenda kuitangaza nchi, pia utaenda kukuza sanaa na mitindo kwa vijana wetu wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee kabisa tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwezesha na kuunga mkono mchakato mzima wa kumpata *Miss Grand International*, ambaye sio mwingine, ni ndugu yetu Jihan Dimack ambaye anatokea ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameunga mkono jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upekee, tunampongeza Ndugu Jihan Dimack. Ndugu Jihan Dimack mwaka 2016 alikuwa *Miss Universe*, lakini mwaka 2026 aligombea *Miss Grand Tanzania* na hatimaye akashinda nchini, na akaiwakilisha nchi na akawa *Miss Grand International*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jihan Dimack anatuachia somo kubwa vijana kwamba, kwa kipindi cha miaka 10 ya mchakato mzima mpaka amekuja kuwa *Miss Grand International*, Jihan Dimack ni mtu ambaye ameamini kwamba mafanikio ni hatua. Hii ni salamu kwa vijana wenzetu, tusikate tamaa. Mafanikio ni hatua, hakuna mafanikio yanayokuja kwa siku moja. Lazima tujiandae na tumtangulize Mungu na tuwe wepesi wa kuwa na subira tukiamini kwamba ipo siku zamu yetu itafika. Kwa hiyo, tunampongeza sana Jihan Dimack na tunamtakia kila la heri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninaomba ninukuu maneno ya John F. Kennedy, Rais wa zamani wa Marekani, aliwahi kusema, "*Don't ask what America has done for you, ask how much you have done for the Americans.*" Usiulize Marekani imekufanyia nini? Hebu

wewe jiulize, umeifanyia nini Marekani? Vijana wenzangu tusiulize Tanzania imetufanyia nini? Nasi tuna wajibu wa kujiuliza tumeifanyia nini Tanzania? Hatuna nchi nyingine, kwa hiyo, tuipende nchi yetu, tuipiganie na tuitangaze kwa nguvu zetu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Paul Makonda, Waziri wetu wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, nami kwa unyenyekevu mkubwa ninaungana na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza sana binti yetu wa Kitanzania Jihan kwa ushindi na heshima kubwa aliyoileta kwa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiniuliza mimi kama Waziri wa Habari ushindi huu nani apewe sifa, nitasema ushindi huu sifa ziende kwa *Gen Z* wote wa Tanzania walioamua kuliweka Taifa lao mbele, wakaweka Utanzania wao mbele, uzalendo ukatangulia, tofauti za vyama zikakaa pembeni. *Resources*, uelewa, taaluma walizonazo na *skills* zao zikatumika kusema sasa ni wakati wa Tanzania. *Gen Z* ninawapongeza sana na ushindi huu ni wenu. Hongereni sana, sana, sana, sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini *Gen Z* wamefanikiwa kuuleta ushindi huu? Wamefanikiwa kwa sababu wanaye kiongozi anayeruhusu mawazo ya vijana, anayeruhusu uhuru wa vijana wa kujieleza; anayeruhusu vijana watumie vipaji walivyonavyo kutengeneza maisha yao. Naye sio mwingine bali ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Rais anayejenga diplomasia ya kulifanya Taifa liheshimike na kuaminika, ndiye Rais anayeweza kutengeneza fursa ya vijana wake kuvuka nje ya mipaka ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mashindano haya wakati yanaendelea, tuliweza kuona vijana wakijitokeza na kuhamasisha.

Ilianza katika mtu mmoja tu kama ambavyo jambo jema huwa linaanza na mtu mmoja. Dada yetu, au mdogo wetu Niffer alipoona ya kwamba mashindano yanaendelea, Watanzania hawana habari, akaamua yeye mwenyewe kujipa jukumu la kuhabarisha Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakwambia, Niffer alienda mbali zaidi, aliona pia Wizara yangu imelala, akaamua kutengeneza *title* ya Wizara ya Habari kupitia BASATA, iki-*promote* kampeni ya kumpigania Jihan. Hiyo kazi aliifanya Niffer peke yake. Hii stori nimesema niiseme leo kwenye Bunge lako Tukufu ili Watanzania waweke rekodi sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pale nikaona wataalamu wa *bureaucracy* kama kawaida yao wamejipanga kwenda kumwadhibu Niffer. Nilimpigia simu Katibu Mkuu nikawaambia, Niffer haadhibiwi. Kwanza atiwe moyo, cha pili apongezwe, cha tatu ateuliwe kuwa balozi wa haya mapambano. Ninyi wote kaeni pembeni, acheni vijana wachukue nafasi yao kulipigania Taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote tunayoyaona ni matokeo, ni kazi kubwa ambayo ilifanywa na wakaungana na akina Kiredio, akina Carry Mastory, na leo tunafurahia matokeo mazuri ambayo vijana wametuonyesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii tumepata funzo kubwa. Vijana hawa tukiwapa nafasi, wana uwezo wa kuiheshimisha nchi kwa namna yoyote ile. Vijana hawa tukizidi kuwapa nafasi, wana uwezo wa kuliunganisha hili Taifa kwa namna yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tumeshuhudia *derby* ya Simba na Yanga iliyokuwa inacheza siku ya tarehe 10, tumekuja kugundua baadaye matokeo. Mimi mwenyewe nilikuja kuona matokeo baadaye usiku saa nane, ya kwamba kuna mtu kapigwa goli. Kimsingi hatukuweza kujua, wote tulikuwa tunajadili ushindi wa Jihan.

Kwa hiyo, ninaomba kabisa kwa unyenyekevu mkubwa niwapongeze vijana hawa na kuwatia moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, mashindano haya yametupa heshima kama Taifa, Afrika iliungana. Nilipata nafasi ya kuongea na rafiki zetu kutoka *Kenya*, *Nigeria*, *South Africa*, wote wakasema sasa ni zamu ya Afrika. Unaona jambo lilivyokuwa, limeanza na mtu mmoja mwenye ndoto, likawainua vijana wa Taifa, likaweka misingi na sera na taratibu zilizowekwa na Mheshimiwa Dkt. Samia na hatimaye Afrika yote ikaungana kupigania ushindi wa Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, tunapokwenda kumpongeza Jihan, tujue amefungua mlango kwa Taifa letu kupeperusha bendera duniani. Mwakani tunapoenda ku-*host* mashindano ya *Miss World*, mashindano ambayo yanakwenda kufanyika Tanzania, na ninaomba kuwaomba Waheshimiwa Wabunge waelewe, mazungumzo yanayoendelea chini ya maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia, Mungu akituwezesha mashindano haya yatafanyika miaka mitatu mfululizo ndani ya Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba vijana wote ambao hawajapata nafasi ya kuoa wasiwe na haraka. Vijana ambao wako kwenye Taifa hili hawajaoa wasiwe na haraka. Wasubiri kuanzia mwaka 2027, 2028, 2029, mashindano ya *Miss* wa dunia yanafanyika hapa Tanzania. Wapate nafasi ya kuona namna gani ya kuweza kuona hiyo fursa. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale dada zangu ambao hawajapata bahati ya kuolewa pia ni fursa. Wanapokuja wageni tunachanganya pia.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu dakika zangu zimeisha,...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Malizia Mheshimiwa, muda umeisha.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninamalizia kwa kusema hivi, leo hii kuna watu wakimwona Jihan wanahoji. Huyu sio wa kwetu; ninaomba kuwaambia, huyu ni Mtanzania halisi. Ni mtoto wa Kitanzania, tena kwa bahati nzuri zaidi ni mtoto wa Kanda ya Ziwa. Kwa hiyo, wasiwe na shaka na uraia wake, wasiwe na shaka na uhalali wake. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, huyu ni zao letu, ni mtoto wetu tuendelee kunufaika na kufurahia mafanikio yake na tumtie nguvu kwa kuendelea kum-*support* ili mwaka huu aliopewa kuiwakilisha dunia kupitia *Miss Grand*, aiwakilishe pia bendera ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa heshima uliyotupatia. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninaungana na Mheshimiwa Waziri wetu wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kuanzia Mheshimiwa Ester Bulaya aliyeomba Mwongozo, kumpongeza binti yetu Jihan kwa heshima aliyoiletea Taifa letu.

Tunampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi anavyofungua Taifa na kukuza diplomasia ya Kimataifa. Leo tunashuhudia nchi inatangazwa Kimataifa. Itafungua fursa ya kiuchumi ikiwepo na utalii. Mheshimiwa Waziri ikiwezekana ukae na

Waziri mwenzako wa Maliasili na Utalii mumpe heshima hata akawe balozi wa utalii katika kukuza uchumi wa Taifa letu.

Kwa hiyo, mimi ninawapongeza sana kwa kazi kubwa iliofanyika. Vijana wa Kitanzania tuendelee kushikamana kwa ajili ya maslahi mapana ya nchi yetu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa Kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028;

na

Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaanza na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo. Mtoa hoja, karibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Kanuni ya 116(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025, ninaomba kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru Mungu kwa uhai, afya njema, ulinzi, rehema na baraka zake alizotukarimu na kutupa nafasi ya kukutana tena tunapoanza Mkutano wa Tano wa Bunge la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea kuwasilisha mapendekezo haya, ninapenda kutumia fursa hii kutoa shukrani na pongezi kama ifuatavyo:-

(i) Ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake na dhamira yake ya kujenga Taifa letu, Taifa jumuishi lenye ustawi, haki, linalojitegemea;

(ii) Ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuteuliwa kwake kushika nafasi hiyo. Ninampongeza kwa uongozi wake makini ambao ameuonyesha tangu aliposhika nafasi hiyo;

(iii) Ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake na juhudi anazoendelea kuzifanya katika kuendeleza ajenda ya maendeleo Zanzibar;

(iv) Ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake makini, dhamira yake ya dhati na bidii yake kubwa katika kuratibu shughuli za Serikali na kusukuma mbele utekelezaji wa vipaumbele vya maendeleo ya Taifa letu;

(v) Ninawashukuru na kuwapongeza wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuendelea kuijenga nchi yetu. Aidha, ninawashukuru kwa kuendelea kudumisha amani na

utulivu ambao ndiyo msingi mkuu wa utekelezaji wa Dira 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuungana na Bunge lako Tukufu kutoa pongezi maalumu kwa nchi yetu kwa kufanikisha maandalizi ya Mkutano wa 153 wa *IPU*. Ninapenda kuwashukuru na kuwapongeza hususan wafuatao kwa kufanikisha mkutano huo:-

(i) Ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake uliowezesha Tanzania kupata fursa ya kuandaa mkutano huu;

(ii) Ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri na mafanikio ya kuandaa na kuendesha mkutano huu kwa mafanikio makubwa;

(iii) Ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani 2023 – 2026, kwa uongozi wake katika kuiongoza taasisi hiyo muhimu inayounganisha Mabunge kutoka Mataifa mbalimbali duniani. Uongozi wake ni fahari kwa Tanzania na Afrika na ni ushahidi wa uwezo wa Tanzania kuchangia katika uongozi wa taasisi za Kimataifa;

(iv) Kwa namna ya pekee ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid, kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Afya ya Umoja wa Mabunge, *IPU*. Uchaguzi huu ni utambuzi wa uwezo wake na ni fursa muhimu kwa Tanzania kuendelea kuchangia katika mijadala na maamuzi ya Kimataifa inayohusu afya na ustawi wa wananchi.

(v) Ninapenda kuwapongeza na kuwashukuru viongozi na Wananchi wa Mkoa wa Arusha kwa kuwakilisha vyema katika kuwakirimu wageni wote wa Mkutano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya kwa pamoja ni fahari kwa Taifa letu, hongereni sana Watanzania kwa mafanikio haya makubwa, Mungu ibariki Tanzania, Mungu libariki Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwasilishe mfumo wa utekelezaji wa Dira. Kama ambavyo tumeeleza kila mara, Dira ya 2050 si waraka mwingine tu wa Serikali bali ni dhamira yetu ya kitaifa ya kubadilisha uchumi wa Tanzania, kuimarisha uwezo wa wananchi, kuboresha maisha yao na kuhakikisha kwamba tunajenga ustawi kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utekelezaji wake si jukumu la Serikali pekee, unahitaji ushiriki wa Bunge, sekta binafsi, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, mashirika ya umma, taasisi za elimu ya juu na asasi za kiraia, washirika wa maendeleo, Watanzania waishio nje na kila mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha kwanza katika kipindi cha robo mwaka ya kwanza ya utekelezaji wa Dira 2050 imekuwa ni kuweka msingi wa mfumo utakaotumika kutekeleza Dira ya 2050. Serikali imeendelea kuweka misingi imara katika utekelezaji wa Dira hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa usimamizi wa utekelezaji wa Dira 2050 unajumuisha mpango elekezi kama ambavyo tumewasilisha mara kadhaa. Mpango wa Maendeleo wa Nne pamoja na mipango ya maendeleo na bajeti ya kila mwaka ikiwemo Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2026/2027. Lengo la mfumo huu ni kuhakikisha kwamba matarajio ya muda mrefu ya nchi yanatafsiriwa katika programu mahsusi, miradi, mahitaji ya fedha, majukumu ya taasisi na malengo yanayoweza kupimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia inaendelea kuimarisha uratibu kati ya taasisi zinazohusika na mipango, bajeti, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini. Lengo letu ni kupunguza mgawanyo wa utekelezaji, kuondoa urudufu usio wa lazima na kuhakikisha kwamba taasisi za Serikali zinafanya kazi kwa kuzingatia matokeo ya pamoja ya kitaifa. Hatua hii ni muhimu kwa sababu Dira ya 2050 kama nilivyosema si jukumu la Wizara moja, ni jukumu la Serikali nzima na Taifa zima kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba utekelezaji wenye ufanisi unahitaji pia mabadiliko ya utamaduni wa utendaji katika taasisi. Tunapaswa kuachana na hali ambayo mafanikio yanapimwa zaidi kwa shughuli zilizofanyika, mikutano iliyofanyika au taarifa zilizoandaliwa. Mwelekeo wetu ni kuona kuwa tunapima mafanikio kwa kuzingatia bidhaa na huduma zilizotolewa, matokeo yaliyopatikana, matumizi bora ya rasilimali na maboresho yaliyofanyika katika maisha ya wananchi. Hii ndiyo nidhamu ya utekelezaji inayotakiwa na Dira 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, Serikali imeelekeza kila taasisi kujua kikamilifu inachotakiwa kutekeleza, muda wa kutekeleza, taasisi ambazo zinazohitajika na hatua zitakazochukuliwa pale ambapo tumeshindwa kufikia makubaliano ya utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu letu kwa sasa ni moja tu, kuhama kutoka kwenye Dira kwenda kwenye utekelezaji na kuhama kutoka kwenye utekelezaji kwenda kwenye matokeo yanayopimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwasilishe ufuatiliaji, tathmini na uwajibikaji kwa kutumia teknolojia. Eneo lingine muhimu katika utekelezaji wetu wa Dira linahusu ufuatiliaji, tathmini na matumizi ya taarifa sahihi katika kufanya maamuzi. Serikali inaendelea kuimarisha mifumo inayohitajika kufuatilia utekelezaji wa programu za maendeleo, kubaini ucheleweshwaji na kuchukua hatua za kurekebisha mapungufu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu muhimu ya juhudi hizi ni kuanzisha mfumo wa elektroniki wa kitaifa wa usimamizi wa mipango na miradi ya maendeleo *(e-Delivery)* pamoja na mifumo husika ya utoaji wa taarifa na ufuatiliaji katika taasisi. Mifumo hii inalenga kuimarisha upatikanaji wa taarifa kuhusu miradi ya maendeleo na kuongeza uwezo wa kufuatilia hatua za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali katika kuanzisha Mfumo wa *e-Delivery* ni kuhakikisha kwamba viongozi na wasimamizi wanaweza kubaini si tu kama mradi umeidhinishwa au umefadhiliwa bali pia kama unaendelea kutekelezwa kulingana na ratiba, kama matumizi ya fedha yanazalisha matokeo yaliyokusudiwa na kama changamoto zinazojitokeza zinaweza kushughulikiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa sahihi ni msingi wa utekelezaji wenye ufanisi, pale ambapo taarifa hazijakamilika Serikali tutakiri mapungufu hayo na kuweka ratiba ya kuyatatua. Pale ambapo utendaji upo chini ya matarajio, taasisi husika lazima zieleze sababu na kubainisha hatua za kurekebisha hali hiyo. Hatuwezi kusimamia kwa ufanisi ajenda ya mabadiliko ya miaka 25 ijayo bila ya kuwa na ushahidi unaoaminika, taarifa zinazowasilishwa kwa utaratibu unaofanana na utayari wa kuchukua hatua kutokana na kile kilichooneshwa na ushahidi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwasilishe mwenendo wa Uchumi wa Taifa. Kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu ya mwezi Septemba, katika robo ya kwanza na ya pili (Januari – Machi, 2026 na Aprili – Juni, 2026). Pato halisi la Taifa lilikuwa kwa 6.0% na 6.5% mtawalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kilitoa mchango mkubwa zaidi katika ukuaji huo kwa 19.2%, kikifuatiwa na huduma za fedha na bima kwa 16.7%, utawala na ulinzi 9.2%, ujenzi asilimia tisa na uzalishaji viwandani 6.6%. Huduma za fedha na bima ziliongoza kwa kasi ya ukuaji kwa 22.5%, zikifuatiwa na utawala na ulinzi 12.8%, umeme 11.8%, sanaa na burudani 11%, habari na mawasiliano 10.3%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mwenendo huu uchumi unatarajiwa kukua kwa 6.3% mwaka 2026 na 6.6% mwaka 2027 kulingana na mwelekeo wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei uliendelea kuwa katika kiwango cha chini na himilivu katika mwaka wa fedha 2025/2026. Mfumuko wa bei ulifikia wastani wa 3.6% ikilinganishwa na 3.1% kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Mwenendo huu uliakisi utekelezaji wa sera makini za fedha na bajeti pamoja na kupungua kwa kasi ya ongezeko la bei za bidhaa zisizo za chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuanzia Aprili hadi Juni, 2026 mfumuko wa bei ulivuka asilimia nne kwa mara ya kwanza tangu Mei, 2023 na kufikia 4.3% mwezi Septemba, 2026. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kupanda kwa bei za nishati katika soko la dunia kufuatia kuongezeka kwa migogoro Mashariki ya Kati, hali iliyoathiri bei za mafuta nchini na kuongeza gharama za usafirishaji bidhaa na huduma nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shinikizo hilo, mfumuko wa bei unaendelea kuwa ndani ya lengo la kitaifa la asilimia tatu hadi tano. Kigezo cha *EAC* kisiwe chini ya asilimia nane na wigo wa *SADC* wa asilimia tatu hadi asilimia saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa uchumi uliendelea kuungwa mkono na kuongezeka kwa mikopo katika sekta binafsi katika mwaka ulioishia Juni, 2026. Mikopo hiyo ilikua kwa wastani wa 21.1% ikilinganishwa na 15.4% katika kipindi kama hicho mwaka 2025 na kuongezeka zaidi hadi 33% mwezi Agosti, 2026 kutoka 28.1% mwezi Juni, 2026. Ukuaji huo uliakisi sera za kifedha na bajeti zinazochochea shughuli za kiuchumi pamoja na kuimarika kwa uzalishaji na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda kutoa taarifa kuwa katika kipindi cha robo ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa Mwaka 2026/2027, Serikali ilikamilisha ujenzi wa

Mji wa Serikali Mtumba ambao unatarajiwa kuzinduliwa rasmi tarehe 30 Oktoba, mwaka 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa uwekezaji wa sekta binafsi. Dira ya 2050 inaitambua na kuiweka sekta binafsi kama injini ya mageuzi ya kiuchumi. Dira ya 2050 inalenga kujenga sekta binafsi yenye ushindani, ustahimilivu jumuishi na inawajibika ikichagizwa na sekta binafsi ndogo na ya kati inayoendeshwa kisasa na katika mfumo ulio rasmi kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Muda Mrefu *(LTPP)* umeimarisha mwelekeo huu kwa kutambua mitaji ya uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kutoka sekta binafsi kama chanzo kikuu cha kugharamia maendeleo ya muda mrefu ikitarajiwa kuwa sekta binafsi itachangia 70% ya uwekezaji unaohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa mwelekeo huu upo katika ukweli kwamba sekta binafsi inaajiri sehemu kubwa ya nguvu kazi na kumiliki sehemu kubwa ya shughuli za kiuchumi na uzalishaji. Kwa mfano, taarifa ya utafiti ajira ya kipato ya mwaka 2024/2025 inaonesha kuwa kati ya ajira milioni 4.6 zilizobainishwa, ajira milioni 3.2 (70.5%) zilikuwa katika sekta binafsi na ajira milioni 1.3 zilikuwa katika sekta ya umma ikiwa ni 29.5% pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji wa sekta binafsi umeendelea kuongezeka, mwaka wa fedha 2025/2026 miradi 934 ya uwekezaji yenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 12.5 ilisajiliwa ikitarajiwa kuzalisha ajira 307,743. Katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2026/2027 miradi 243 yenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 3.4 ilisajiliwa, ambapo 57.2% ni ya viwanda. Vilevile, miradi ya ubia katika utekelezaji imeongezeka hadi kufikia 10 ikiwemo kituo cha biashara cha Kariakoo, Mabasi Yaendayo Kasi na Reli ya *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi Serikali imebaini na itasukuma utekelezaji wa miradi ya maendeleo 131 ya ubia inayostahili kutekelezwa kwa ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa sekta ya uwekezaji nchini siyo takwimu katika makaratasi tu, ni ajira na maisha kwa Watanzania halisi. Ninazungumzia kwa mfano, vijana 10,000 watakaoajiriwa katika kongani ya viwanda inayojengwa na Kampuni ya *HWTZ* Bagamoyo ifikapo mwaka wa fedha 2030/2031. Ninazungumzia vijana 2,000 walioajiriwa katika Kiwanda cha *ITRACOM* Nala hapa Dodoma. Ninazungumzia vijana 3,000 ambao wameajiriwa na Kiwanda cha Nguo cha Kampuni ya *Sinovest* Bagamoyo na vijana 10,000 watakaoajiriwa na Kiwanda hicho ifikapo mwaka wa fedha 2030/2031.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumzia vijana 6,000 watakaoajiriwa katika mradi wa kongani za viwanda wa Kampuni ya *HWTZ* Songea. Ninazungumzia vijana 12,940 walioajiriwa katika Kiwanda cha Sukari Kilombero. Ninazungumzia vijana 4,800 walioajiriwa katika Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa Morogoro. Ninazungumzia vijana 5,061 walioajiriwa katika Kiwanda cha *Mkulazi Holding* Morogoro. Ninazungumzia vijana 11,262 watakaoajiriwa katika Mradi wa Kampuni ya *Eagle Agrotech* Mkulazi pale Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumzia vijana 498 watakaoajiriwa katika mradi wa kuchakata mazao ya kilimo ya Kampuni ya *KOM Food Products Company Limited* pale Mjini Kahama. Kwa hiyo, hatuzungumzii takwimu kwenye makaratasi, ni maisha na ajira za Watanzania ambazo zinaendelea katika sehemu mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mieze mitatu ya utekelezaji wa Dira 2050 imetupatia matumaini makubwa kwamba malengo makubwa tuliyojiwekea yanatekelezeka na yanafikika. Mambo matano katika kipindi hiki ni bayana: kwanza, tuna msingi imara wa ukuaji uchumi. Uchumi unakua kwa kasi nzuri na unatarajiwa kukua kwa 6.7% mwaka 2027 na tunatarajia kwamba ukuaji huo uweze kukidhi shabaha ambayo tumejiwekea kwenye Mpango wa Tano wa Maendeleo. Mfumuko wa bei umeendelea kuwa chini ya asilimia tano kama tulivyojipangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, sekta ya fedha ya umma imeendelea kufanya vizuri ambapo katika mwaka mmoja tumefikia shabaha ya kutenga dola bilioni 8.1. Tumejiwekea kwenye Mpango wa Maendeleo kwamba, angalau Serikali iweze kutenga shilingi bilioni 8.1 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali ilitenga jumla ya shilingi trilioni 20.82 sawa na Dola za Kimarekani bilioni 8.2. Kwa hiyo, tayari tumefikia lengo ambalo tumejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, bajeti ya maendeleo imeendelea kuongezeka ambapo sasa ni 7.7% ya pato la Taifa, ikionesha kuongezeka kwa uwekezaji wa sekta ya umma katika shughuli za maendeleo. Kwa mfano, katika miaka mitatu iliyopita mwaka wa fedha 2024/2025 bajeti ya maendeleo ilikuwa 32.9%; mwaka wa fedha 2025/2026 ikawa 33.5%; mwaka wa fedha 2026/2027 ni 36.4%. Kwa hiyo, bajeti ya maendeleo inaenda kuongezeka kama ambavyo tumejiwekea kwenye malengo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, umaskini wa mahitaji ya msingi umeendelea kupungua kutoka 34.4% mwaka 2007 hadi kufikia 35.1% mwaka 2025. Tano, tunayo Dira inayoeleweka na ambayo imepokelewa vizuri na umma wa Watanzania wa kada zote. Aidha, tunazo nyenzo thabiti za utekelezaji na taasisi imara za usimamizi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwasilishe vipaumbele vya robo mwaka ya pili (2026/2027) ambayo ni Oktoba – Disemba 2026. Kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika robo ya kwanza, Serikali itaweka mkazo katika vibaumbele sita vifuatavyo: -

(i) Tutaendelea kuimarisha ulinganifu wa mipango na malengo ya Dira 2050;

(ii) Tutaboresha ukamilifu na uaminifu wa takwimu za msingi, viashiria vya utendaji na mifumo ya utoaji taarifa za robo mwaka;

(iii) Tutaimarisha ufuatiliaji wa miradi ya kipaumbele ya maendeleo kwa kuzingatia hatua za utekelezaji matumizi ya bajeti na utatuzi wa changamoto kwa wakati;

(iv) Tutaongeza juhudi za kuhamasisha, kufuatilia na kufanya tathmini ya hali ya uwekezaji wa sekta binafsi na kuboresha mazingira ya biashara nchini kwa kutambua kwamba shughuli za uzalishaji za sekta binafsi ni muhimu katika mabadiliko ya uchumi wetu;

(v) Tutaongeza uratibu kati ya Wizara, Idara, wakala, mikoa na mamlaka ya Serikali za mitaa ili kuhakikisha kwamba vipaumbele vya maendeleo ya Taifa vinazaa matokeo katika ngazi za maeneo husika; na

(vi) Tutaimarisha uwajibikaji kwa kutaka taasisi zinazotekeleza programu kueleza sababu za tofauti kubwa kati ya malengo na matokeo halisi na kuonesha hatua zitakazochukuliwa kurekebisha mapungufu yaliyobainika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele hivi vitaungwa mkono na mapitio ya mara kwa mara ya utendaji na mifumo ya utoaji taarifa itakayohakikisha kwamba mafunzo yanayopatikana katika utekelezaji yanaingizwa katika maamuzi katika kipindi chote cha mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwasilishe vipaumbele tunavyopendekeza katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2027/2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka wa fedha 2027/2028 yameandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele, malengo, shabaha, na afua za kimkakati zilizoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano wa 2026/2027 – 2030/2031 *(FIDP-IV)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya yanalenga kuendeleza utekelezaji wa vipaumbele vya kimkakati vitakavyochochea mageuzi ya kiuchumi na kijamii, kuongeza tija na ushindani wa uchumi pamoja na kuboresha ustawi wa wananchi. Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa Dira 2050 yenye lengo la kuifanya Tanzania kuwa Taifa jumuishi lenye ustawi, haki, linalojitengemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka wa fedha 2027/2028 yamejikita katika maeneo sita ya kipaumbele kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani. Hapa tutaweka mkazo katika maeneo sita, niyataje matatu: -

(i) Kuongeza tija katika uzalishaji;

(ii) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ikiwemo kurahisisha mifumo ya udhibiti na kurasimisha shughuli zisizo rasmi; na

(iii) Kuimarisha uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ndani na mauzo ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ni kujenga uwezo wa watu na maendeleo ya jamii. Hapa tuna maeneo muhimu nane, niyataje matano:

(i) Kuboresha upatikanaji wa ubora wa elimu, mafunzo ya ujuzi na elimu inayozingatia mahitaji ya soko la ajira hususan katika sayansi, teknolojia, uhandisi na ithibati;

(ii) Kuendelea na maandalizi ya utekelezaji wa elimu ya sekondari kwa wote kuanzia mwaka 2028;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wanafahamu kuanzia mwaka 2028 watoto wetu wote wanaomaliza elimu ya msingi watalazimika kwenda *form one*. Kwa hiyo, katika eneo hili kipaumbele kikubwa sana cha Serikali ni kuhakikisha kwamba tunakamilisha maandalizi kwa ajili ya hatua hiyo.

(i) Kuimarisha upatikanaji wa ajira kwa vijana na maendeleo ya biashara ndogo na za kati ili kutumia fursa ya ongezeko la watu wenye umri wa kufanya kazi;

(ii) Kuendelea na utekelezaji wa programu ya Bima ya Afya kwa Wote; na

(iii) Kuanza kutekeleza afua mahususi zinazolenga kuondoa umaskini uliokithiri miongoni mwa wananchi kwa kuzingatia kiwango cha umaskini katika maeneo ya kijiografia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi. Hapa tuna maeneo makubwa manne. Nitaje moja; ni kuendeleza miji iliyopangwa matumizi endelevu ya ardhi na Bahari, uhifadhi na urejeshaji wa misitu na mabonde rasilimali za bahari. Pia, kutumia fursa za uchumi wa *blue* na biashara ya *carbon* kama vyanzo vya ukuaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la nne ni vichocheo vya maendeleo na hapa nitaje maeneo mawili ya kipaumbele. Kwanza ni kuendelea kuwekeza katika uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati ya uhakika, nafuu na endelevu ili kusaidia uzalishaji wa ndani, biashara na huduma za jamii. Pili, ni kuendeleza uwekezaji katika miundombinu ya barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na mifugo ya usafirishaji fungamanishi ili kupunguza gharama za biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tano ni kuimarisha utekelezaji wa sekta za mageuzi. Dira 2050 imezitambua sekta za kimageuzi tisa ambazo zina uwezo mkubwa wa kuchochea ukuaji wa uchumi,

kuzalisha ajira, kuongeza mapato ya Serikali na kuongeza mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi. Sekta hizo ni pamoja na kilimo, uzalishaji viwandani, madini, mafuta na gesi, ujenzi, ardhi na makazi, utalii, michezo, sanaa na ubunifu, fedha, biashara na ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele katika eneo hili vitakuwa saba. Ninaomba nivitaje vitano. Kwanza ni kuongeza tija katika uzalishaji, usindikaji na kuimarisha mnyororo wa thamani. Pili, kukamilisha miradi ya umwagiliaji. Tunayo miradi zaidi ya 146 ambayo inaendelea na msukumo mkubwa katika mwaka huu tunataka kuona kwamba miradi hii inakamilika na Tume ya Taifa ya Mipango haitaweza kuruhusu mradi mpya hadi tukamilishe kwanza hii ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuendelea na utekelezaji wa *Grid* ya Taifa ya Maji (*National Water Grid)* kwa kutumia kikamilifu rasilimali za maji za Taifa zikiwemo maziwa makubwa na mito mikubwa kama vile Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Mto Rufiji. Aidha, msisitizo hapa ni kwamba pamoja na upatikanaji wa maji safi ya kunywa msukumo wa kipekee utawekwa katika kuhakikisha kwamba rasilimali hizi za maji katika mradi huu zinatumika kuchochea uzalishaji katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi. Hatutarajii Mradi huu wa *National Water Grid* utumike kwa matumizi tu ya kawaida ya maji ya kunywa. Tunataka kutumia mradi huu kuimarisha uzalishaji katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, ni kuimarisha upatikanaji wa mitaji kwa sekta za uzalishaji ikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi. Hapa Waheshimiwa Wabunge kikubwa sana tunataka kuanzisha mkakati mahususi na maalumu wa ufadhili au ugharamiaji wa sekta za uzalishaji kama kilimo, mifugo na uvuvi ili kuweza kuwa na uhakika na mitaji katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la sita ni kuimarisha misingi mikuu ya uendelevu wa Taifa na hapa kipaumbele kikubwa ni kuendelea kuimarisha utawala bora, demokrasia, usalama na utulivu pamoja na kuongeza uwezo na ufanisi wa taasisi za Serikali. Kuimarisha uwezo wa

Serikali za mitaa ili kuwezesha mipango ya utekelezaji wa maendeleo kwa kuzingatia mahitaji halisi ya wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya ya vipaumbele yatachagizwa na utekelezaji wa programu za kielelezo ambazo zipo katika mpango wetu wa maendeleo. Katika kukuza maendeleo ya sekta binafsi nchini Serikali itatekeleza mkakati wa pili wa kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini yaani *Mkumbi II*. Hatua zitakazochukuliwa katika kutekeleza *Mkumbi II* ni pamoja na kutunga Muswada wa Sheria ya Maendeleo ya Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze kidogo kuhusu kuimarisha mnyororo wa thamani. Mpango wa Nne wa Maendeleo yaani *FYDPIV* umebainisha na kufungamanisha minyororo ya thamani katika programu za kielelezo ili kuhakikisha kwamba zinakuwa na manufaa ya kibiashara, uzalishaji na kukuza ushindani. Katika mwaka wa fedha 2027/2028, maeneo sita ya mnyororo wa thamani yatapewa kipaumbele cha kipekee. Maeneo haya ni;

(i) Kilimo cha maua na mazao ya bustani;

(ii) Ufugaji wa viumbe hai;

(iii) Utafiti, uchimbaji na kuongeza thamani ya madini;

(iv) Uzalishaji wa mafuta ya kula;

(v) Uzalishaji wa nguo na mavazi kwa kuimarisha mnyororo wa thamani wa pamba; na

(vi) Kuimarisha uzalishaji wa mazao ya kilimo ikiwemo korosho, sukari, ngano, chai na kahawa na uongezaji wa thamani wa mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeeleza pia ugharamiaji wa mpango wa maendeleo ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2027/2028 ambayo kwa kiasi kikubwa itakuwa kama ilivyo kwa mwaka huu wa

fedha na *formular* yetu ni ile ile; 30% sekta ya umma na 70% sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina tumeonyesha kwenye kitabu, lakini nieleze kidogo kuhusu usimamizi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa ambao tunaupendekeza kwa mwaka wa fedha 2027/2028. Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka wa fedha 2027/2028 utategemea mfumo wa uratibu wa kitaifa ambao nimeueleza kwamba upangaji, uidhinishaji, ugharamiaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini na utoaji wa taarifa kama ambavyo tumeainisha katika miongozo yetu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miongozo hiyo Mpango wa Maendeleo wa Taifa utatumia mbinu ya maabara yaani *Lab Delivery Approach*. Ili kuimarisha uratibu na ufanisi mfumo wa kitaasisi wa utekelezaji wa mpango umeainisha majukumu mahususi ya taasisi za umma na wadau mbalimbali katika hatua za upangaji wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya mgawanyo kuanzia juu, kuanzia kwa Mheshimiwa Rais na viongozi wetu wa juu, kwa Waziri Mkuu ambaye ndiyo Mratibu Mkuu wa Shughuli za Serikali, *then* tunakuja kwenye ngazi za wizara kwa kuanzia na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, tunaenda Wizara ya Fedha, Tume ya Taifa ya Mipango, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Msajili wa Hazina, *then* Wizara, Idara, Wakala na Serikali za Mikoa. Kwa hiyo, tutatumia mfumo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze wajibu wa Bunge na wadau wengine wa kitaifa. Utekelezaji wenye mafanikio wa Dira 2050 unahitaji umiliki wa kitaifa na usimamizi madhubuti. Bunge lina nafasi muhimu katika kuchambua sera, kuidhinisha bajeti, kufuatilia matumizi ya rasilimali za umma na kuhakikisha kwamba utekelezaji unaendelea kuendana na matarajio ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inathamini ushirika wa Waheshimiwa Wabunge katika kubaini mapungufu ya utekelezaji,

kuchambua mgao wa rasilimali na kupendekeza hatua zinazoweza kuboresha matokeo na ndiyo maana tumeleta mapendekezo haya ili tupate maoni ya Waheshimiwa Wabunge tuweze kukamilisha mchakato husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeeleza pia ushiriki wa sekta binafsi ambayo kazi yake kubwa ni kuongeza uwekezaji wenye tija, taasisi za elimu ya juu, kazi yao kubwa ni kuchangia ushahidi wa kisayansi na maendeleo ya ujuzi. Tumeeleza majukumu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambao kazi yao ni kutafsiri vipaumbele vya kitaifa katika fursa za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeeleza pia nafasi ya washirika wetu wa maendeleo na mwisho tumeeleza kwa kina nafasi ya mashirika ya kiraia yaani *CSOs* pamoja na *NGOs,* mashirika ya dini na mashirika ya kijamii katika utekelezaji wa Dira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; ninapohitimisha maelezo yangu ninapenda kusisitiza tena kwamba taarifa ya utekelezaji wa mpango kwa robo ya kwanza ni wa kwanza katika utekelezaji wa Dira 2050 na ni mwanzo wa safari ndefu ya maendeleo ya Taifa letu. Hatutarajii kuona mafanikio makubwa ya utekelezaji wa dira katika miezi hii mitatu, lakini tunatambua kwamba ni muhimu katika kuweka msingi imara wa utekelezaji wake. Jukumu letu kubwa katika hatua ya sasa ni kujenga mfumo wa maendeleo unaounganisha matarajio ya muda mrefu na vipaumbele vya kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma yetu ya kitaifa ni kujenga Tanzania ambayo ustawi wake unawanufaisha wananchi wengi zaidi, ajira zenye tija zinaongezeka, biashara zina ushindani zaidi, huduma za umma zinaimarika na vizazi vijavyo vinarithi nchi yenye fursa nyingi zaidi kuliko zile ambazo sisi tunazo. Azma hii inawezekana tukichanganya mipango bora na utekelezaji wenye nidhamu, uwajibikaji kwa umma na ushirikiano imara kati ya Serikali na sekta zote za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira 2050 lazima iwe zaidi ya dira tunayojivunia, lazima iwe mabadiliko tunayotekeleza, ahadi tunayopima na urithi tunaoacha kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo, ninaomba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na litoe maoni na ushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha 2027/2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa shukrani. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Pius Steven Chaya, Naibu Waziri, kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kuongoza Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Ninawashukuru viongozi wenzangu wengine, Makatibu Wakuu, Dkt. Tausi Mbaga Kida, Katibu Mkuu anayeshughulikia mipango ambaye pia ni Katibu Mtendaji wa Tume. Dkt. Fred Msemwa, Katibu Mkuu anayeshughulikia uwekezaji, Naibu Makatibu Watendaji, Dkt. Mosali Milanzi, Dkt. Abdamina Kilama, Ndugu Sostenes Kewe na *management* na watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Tume ya Taifa ya Mipango kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuongoza taasisi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hotuba yangu hii na kitabu cha mapendekezo tulichowasilisha viingie katika kumbukumbu za Bunge. Kwa heshima na taadhima ninaomba kuwasilisha.

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - MIPANGO NA UWEKEZAJI, MHE. PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA UNAOKUSUDIWA KUTEKELEZWA NA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2027/28 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

I. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia Kanuni ya 116 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge (Toleo la Mwaka 2025) ninaomba kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2027/2028.

2. ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote, ninamshukuru Mungu kwa uhai, afya njema, ulinzi, rehema na baraka zake alizotukarimu na kutupa nafasi ya kukutana tena tunapoanza Mkutano wa Tano wa Bunge la 13.

3. ***Mheshimiwa Spika***, kabla sijawasilisha mapendekezo ya Mpango, ninapenda kutumia fursa hii kutoa shukrani na pongezi zangu za dhati kwa viongozi wa nchi yetu kama ifuatavyo:

3.1 ***Kwanza***, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake na dhamira yake ya kujenga Taifa jumuishi, lenye ustawi, haki na linalojitegemea.

3.2 ***Pili***, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuteuliwa kwake kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninampongeza kwa uongozi wake makini ambao ameuonesha tangu alipoteuliwa kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais na mipango ya maendeleo ya Taifa letu kwa ujumla.

3.3 ***Tatu,*** ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake na juhudi anazoendelea kuzifanya katika kuendeleza ajenda ya maendeleo ya Zanzibar.

3.4 ***Nne***, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mbunge), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake makini, dhamira yake ya dhati na bidii bayana katika kuratibu shughuli za Serikali na kusukuma mbele utekelezaji wa vipaumbele vya maendeleo ya taifa letu.

II. PONGEZI MAALUM KWA MAFANIKIO YA TANZANIA KUANDAA MKUTANO WA 153 WA UMOJA WA MABUNGE DUNIANI (IPU)

4. ***Mheshimiwa Spika***, Kwa namna ya pekee, napenda kutoa pongezi maalum kwa nchi yetu kwa kufanikisha maandalizi ya Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU).

4.1 ***Kwanza***, ninampongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa uongozi wake uliowezesha Tanzania kupata fursa ya kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Mafanikio haya ni kielelezo cha heshima na imani ambayo Tanzania imejijengea katika medani za kimataifa, pamoja na uwezo wetu wa kuandaa na kuendesha mikutano mikubwa ya kimataifa.

4.2 ***Pili,*** napenda kukupongeza wewe **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mbunge), Spika wa Bunge la Tanzania**, kwa uongozi wako mahiri na mafanikio ya kuandaa na kuendesha kwa mafanikio mkutano huo muhimu. Mafanikio haya yameongeza hadhi ya Bunge letu na kuimarisha nafasi ya Tanzania katika diplomasia ya kibunge duniani.

4.3 ***Tatu,*** napenda kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU)**

2023 - 2026, kwa uongozi wake katika kuiongoza taasisi hiyo muhimu inayounganisha mabunge kutoka mataifa mbalimbali duniani. Uongozi wake ni fahari kwa Tanzania na Afrika, na ni ushahidi wa uwezo wa Watanzania kuchangia katika uongozi wa taasisi za kimataifa.

4.4 ***Nne***, kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid** kwa kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Afya ya Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Uchaguzi huu ni utambuzi wa uwezo wake na ni fursa muhimu kwa Tanzania kuendelea kuchangia katika mijadala na maamuzi ya kimataifa yanayohusu afya na ustawi wa wananchi.

5. Mheshimiwa Spika, mafanikio haya kwa pamoja ni fahari kwa taifa letu. Yanadhihirisha kuwa Tanzania ina uwezo, ina viongozi wenye sifa na ina nafasi muhimu katika kuimarisha ushirikiano wa kimataifa kupitia diplomasia ya kibunge.

Hongereni sana kwa mafanikio haya makubwa. Mungu ibariki Tanzania; Mungu libariki Bunge letu.

III. WASILISHO

6. Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo na pongezi hizo, ninayo heshima ya kuwasilisha mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2027/28 katika maeneo makuu matatu kama ifuatavyo: ***Kwanza***, ni taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26. ***Pili***, ni taarifa ya robo ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27, ambayo pia ni taarifa ya robo ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31) na Dira 2050 katika kipindi hicho. ***Tatu***, ni mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28.

7. *Mheshimiwa Spika*, Taarifa hizi zinaweka msingi wa maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28, ambao ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27–2030/31 (FYDP IV) ambao ni mpango wa kwanza wa muda wa kati wa utekelezaji wa Dira 2050.

8. *Mheshimiwa Spika*, taarifa ya robo ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 ina umuhimu wa pekee kwa sababu kuu tatu.

8.1 ***Kwanza***, inaashiria mwanzo wa hatua mpya katika safari ya maendeleo ya muda mrefu ya nchi yetu. Baada ya kukamilika kwa kipindi cha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Tanzania ilianza kutekeleza Dira 2050 tarehe 1 Julai 2026.

8.2 ***Pili***, hii ni fursa ya kwanza kwa Serikali kutoa taarifa Bungeni kuhusu hatua zilizopigwa katika kutafsiri malengo ya Dira 2050 na kuyageuza kuwa hatua za utekelezaji, majukumu ya taasisi, programu za maendeleo na matokeo yanayoweza kupimika.

8.3 ***Tatu***, taarifa hii inaweka msingi wa uwajibikaji katika kipindi chote cha miaka 25 ijayo. Inatoa fursa kwa Bunge letu tukufu kutathmini kama nchi yetu inaweka mifumo, rasilimali na nidhamu ya utekelezaji inayohitajika ili kufikia matarajio ya Dira 2050.

IV. MFUMO WA UTEKELEZAJI: KUTOKA KWENYE DIRA KWENDA KWENYE VITENDO

9. *Mheshimiwa Spika*, kama ambavyo tumeeleza kila mara, Dira 2050 si waraka mwingine wa Serikali tu, bali ni dhamira yetu ya kitaifa ya kuubadilisha uchumi wa Tanzania, kuimarisha uwezo wa wananchi, kuboresha maisha yao na kuhakikisha kwamba tunajenga ustawi kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Kwa hiyo, utekelezaji wake si jukumu la Serikali pekee. Unahitaji ushiriki wa Bunge, sekta binafsi, mamlaka za serikali za mitaa, mashirika ya umma, taasisi za elimu ya juu na

utafiti, asasi za kiraia, washirika wa maendeleo, Watanzania waishio nje ya nchi na kila mwananchi.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** kipaumbele cha kwanza katika kipindi cha robo mwaka ya kwanza ya utekelezaji wa Dira 2050 kilikuwa kuweka msingi wa mfumo utakaotumika kutekeleza Dira 2050. Serikali inaendelea kuweka misingi imara katika utekelezaji wa mipango ya muda mrefu, wa kati ya mwaka unaounganisha matarajio ya Dira 2050 na programu halisi za maendeleo.

11. ***Mheshimiwa Spika***, mfumo wa usimamizi wa utekelezaji wa Dira 2050 unajumuisha Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu (LTPP) wa mwaka 2026/27 hadi 2050/51, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wa mwaka 2026/27 hadi 2030/31, pamoja na mipango ya maendeleo na bajeti za mwaka zinazohusika. Lengo la mfumo huu ni kuhakikisha kwamba matarajio ya muda mrefu ya nchi yanatafsiriwa katika programu mahususi, miradi, mahitaji ya fedha, majukumu ya taasisi na malengo yanayoweza kupimika.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** Dira ya taifa inaweza kutekelezwa kwa ufanisi pale tu kunapokuwa na uhusiano wa wazi kati ya kile ambacho nchi inataka kufikia mwaka 2050 na kile ambacho kila taasisi ya umma inapaswa kutekeleza katika mwaka husika wa fedha. Katika kipindi cha taarifa hii, Serikali ilitathmini maendeleo ya kuoanisha mipango ya taasisi, bajeti, vipaumbele vya maendeleo na mifumo ya utekelezaji na malengo ya Dira 2050. Tathmini ya awali inaonesha kuwa, kwa kiasi kikubwa, mipango ya maendeleo ya kitaifa imeshabihiana vyema na mipango mikakati ya sekta, taasisi za umma na mamlaka za serikali za mitaa. Nitoe wito kwa Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na taasisi za umma ambazo bado hazijaoanisha mipango mikakati yao na mipango ya maendeleo ya kitaifa kufanya hivyo kabla ya Juni 2027. Mipango hii iwasilishwe Tume ya Taifa ya Mipango kwa uchambuzi na uidhinishaji.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia inaendelea kuimarisha uratibu kati ya taasisi zinazohusika na mipango, bajeti, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini. Lengo letu ni kupunguza mgawanyiko wa utekelezaji, kuondoa urudufu usio wa lazima na kuhakikisha kwamba taasisi za Serikali zinafanya kazi kwa kuzingatia matokeo ya pamoja ya kitaifa. Hatua hii ni muhimu kwa sababu Dira 2050 si jukumu la wizara moja. Ni jukumu la Serikali nzima na taifa zima kwa ujumla.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatambua kwamba utekelezaji wenye ufanisi unahitaji pia mabadiliko ya utamaduni wa utendaji katika taasisi. Tunapaswa kuachana na hali ambayo mafanikio yanapimwa zaidi kwa shughuli zilizofanyika, mikutano iliyofanyika au taarifa zilizoandaliwa. Mwelekeo wetu ni kuona kuwa tunapima mafanikio kwa kuzingatia bidhaa na huduma zilizotolewa, matokeo yaliyopatikana, matumizi bora ya rasilimali na maboresho yaliyofanyika katika maisha ya wananchi. Hii ndiyo nidhamu ya utekelezaji inayotakiwa na Dira 2050. Hivyo basi, Serikali imeelekeza kila taasisi kujua kikamilifu inachotakiwa kutekeleza, muda wa kutekeleza, rasilimali ilizonazo na hatua zitakazochukuliwa pale inaposhindwa kufikia makubaliano ya utendaji.

15. ***Mheshimiwa Spika***, jukumu letu sasa ni moja: ***kuhama kutoka kwenye Dira kwenda kwenye utekelezaji, na kutoka kwenye utekelezaji kwenda kwenye matokeo yanayopimika.***

V. UFUATILIAJI, TATHMINI NA UWAJIBIKAJI KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA

16. ***Mheshimiwa Spika,*** eneo lingine muhimu katika utekelezaji wa Dira 2050 linahusu ufuatiliaji, tathmini na matumizi ya taarifa sahihi katika kufanya maamuzi. Serikali inaendelea kuimarisha mifumo inayohitajika kufuatilia utekelezaji wa programu za maendeleo, kubaini ucheleweshaji na kuchukua hatua za kurekebisha mapungufu kwa wakati.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** sehemu muhimu ya juhudi hizi ni kuanzisha Mfumo wa kielektroniki wa Kitaifa wa Usimamizi wa Mipango na Miradi ya Maendeleo, yaani *e-Delivery*, pamoja na mifumo husika ya utoaji wa taarifa na ufuatiliaji katika taasisi. Mifumo hii inalenga kuimarisha upatikanaji wa taarifa kuhusu miradi ya maendeleo na kuongeza uwezo wa kufuatilia hatua za utekelezaji.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** lengo la Serikali katika kuanzisha mfumo wa *edelivery* ni kuhakikisha kwamba viongozi na wasimamizi wanaweza kubaini si tu kama mradi umeidhinishwa au umefadhiliwa, bali pia kama unaendelea kutekelezwa kulingana na ratiba, kama matumizi ya fedha yanazalisha matokeo yaliyokusudiwa na kama changamoto zinazojitokeza zinashughulikiwa.

19. ***Mheshimiwa Spika***, taarifa sahihi ni msingi wa utekelezaji wenye ufanisi. Pale ambapo taarifa hazijakamilika, Serikali tutakiri mapungufu hayo na kuweka ratiba ya kuyatatua. Pale ambapo utendaji uko chini ya matarajio, taasisi husika lazima zieleze sababu na kubainisha hatua za kurekebisha hali hiyo. Hatuwezi kusimamia kwa ufanisi ajenda ya mabadiliko ya miaka 25 bila kuwa na ushahidi unaoaminika, taarifa zinazowasilishwa kwa utaratibu unaofanana na utayari wa kuchukua hatua kutokana na kile kinachooneshwa na ushahidi huo.

VI. MWENENDO WA UKUAJI WA UCHUMI WA TAIFA

20. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu ya mwezi Septemba 2026, katika robo ya kwanza na ya pili ya mwaka 2026, Pato Halisi la Taifa lilikua kwa asilimia 6.0 na asilimia 6.5, mtawalia. Kilimo kilitoa mchango mkubwa zaidi katika ukuaji huo wa asilimia 19.2, kikifuatiwa na huduma za fedha na bima kwa asilimia 16.7, utawala na ulinzi (asilimia 9.2), ujenzi (asilimia 9.0), na uzalishaji viwandani (asilimia 6.6). Huduma za fedha na bima ziliongoza kwa kasi ya ukuaji wa asilimia 22.5, zikifuatiwa na utawala na ulinzi (asilimia 12.8), umeme (asilimia 11.8), sanaa na burudani (asilimia 11.0), na habari na mawasiliano (asilimia 10.3). Kwa kuzingatia mwenendo huo, uchumi unatarajiwa

kukua kwa asilimia 6.3 mwaka 2026 na asilimia 6.6 mwaka 2027, kulingana na mwelekeo wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27–2030/31.

21. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi, mfumuko wa bei uliendelea kuwa katika kiwango cha chini na himilivu. Katika mwaka 2025/26, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 3.6, ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2024/25. Mwenendo huo uliakisi utekelezaji wa sera makini za fedha na bajeti, pamoja na kupungua kwa kasi ya ongezeko la bei za bidhaa zisizo za chakula. Hata hivyo, kuanzia Aprili hadi Juni 2026, mfumuko wa bei ulivuka asilimia 4.0 kwa mara ya kwanza tangu Mei 2023 na kufikia asilimia 4.3 mwezi Septemba 2026. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kupanda kwa bei za nishati katika soko la dunia kufuatia kuongezeka kwa migogoro Mashariki ya Kati, hali iliyoathiri bei za mafuta nchini na kuongeza gharama za usafirishaji, bidhaa na huduma nyingine. Pamoja na shinikizo hilo, mfumuko wa bei uliendelea kuwa ndani ya lengo la kitaifa la asilimia 3.0 hadi 5.0, kigezo cha EAC kisichozidi asilimia 8.0 na wigo wa SADC wa asilimia 3.0 hadi 7.0.

22. ***Mheshimiwa Spika***, ukuaji wa uchumi uliendelea kuungwa mkono na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi. Katika mwaka ulioishia Juni 2026, mikopo hiyo ilikua kwa wastani wa asilimia 21.1, ikilinganishwa na asilimia 15.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2025, na kuongezeka zaidi hadi asilimia 33.0 mwezi Agosti 2026 kutoka asilimia 28.1 mwezi Juni 2026. Ukuaji huo uliakisi sera za fedha na bajeti zinazochochea shughuli za kiuchumi, pamoja na kuimarika kwa uzalishaji na biashara. Mikopo kwa shughuli za uchimbaji wa madini na mawe iliongoza kwa ukuaji wa asilimia 45.2, huku mikopo kwa biashara, uchukuzi na mawasiliano, pamoja na kilimo ikikua kwa zaidi ya asilimia 30 katika kila shughuli. Mikopo kwa watu binafsi, ambayo sehemu kubwa hutumika kugharamia shughuli za uzalishaji za biashara ndogo na za kati, ilichangia asilimia 35.5 ya mikopo yote kwa sekta binafsi, ikifuatiwa na biashara asilimia 14.5 na kilimo asilimia 13.7. Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa ukuaji wa mikopo unaelekezwa zaidi katika shughuli za uzalishaji ili kuongeza uwekezaji, ajira, mauzo ya nje na ushindani wa uchumi.

VII. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2026/27 KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA

23. ***Mheshimiwa Spika*****,** Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 ni wa kwanza katika utekelezaji wa FYDP IV na Dira 2050. Mpango huu una maeneo sita (6) ya kipaumbele kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele ya FYDP IV. Aidha, Mpango huu una jumla ya viashiria 305 vya ufuatiliaji na upimaji, kama ifuatavyo:

i) Msingi mkuu: Utawala bora, demokrasia, amani na usalama: viashiria 21

ii) Uchumi imara, jumuishi na shindani: viashiria 33

iii) Uwezo wa watu na maendeleo ya jamii: viashiria 117

iv) Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabia nchi: viashiria 19

v) Vichocheo vya maendeleo: viashiria 36

vi) Sekta za kimageuzi: viashiria 79

24. ***Mheshimiwa Spika***, aidha, Mpango huu unatekeleza programu saba (7) za kielelezo zinazounganisha miradi katika minyororo ya thamani. Programu hizo ni: Mji wa Ikolojia ya Bahari Bagamoyo na Usafirishaji Fungamanishi; Kitovu Changamani cha Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga; Kiwanda cha Kuchakata Gesi Asilia kuwa Kimiminika Lindi; Kitovu cha Teknolojia na Uchakataji wa Madini Adimu Dodoma (katika eneo la Nala); Programu ya Kitaifa ya Umwagiliaji na Mageuzi ya Viwanda vya Uchakataji wa Mazao ya Kilimo; Kitovu cha Kisasa cha Viwanda na Uchumi wa Buluu katika Ukanda wa Maziwa Makuu; na Programu Shirikishi ya Uendelezaji wa Miji Nchini.

25. ***Mheshimiwa Spika***, katika robo ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/27 (Julai – Septemba 2026), utekelezaji wa baadhi ya miradi katika programu za kielelezo ni pamoja kuendelea na ujenzi wa SGR kipande cha

Morogoro – Makutupora umefikia asilimia 98.79 na kipande cha Isaka – Mwanza asilimia 69.31; ujenzi wa viwanja vya ndege vya Sumbawanga, Tabora na Geita umekamilika; na ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Kigoma umefikia asilimia 75.5, Shinyanga (asilimia 96.5), Musoma (asilimia 70), Iringa - Awamu ya II (asilimia 47); barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge sehemu ya Tanga – Pangani (km 50) umefikia asilimia 77, Tungamaa – Mkange (km 95.2) asilimia 79 na daraja la Pangani asilimia 64. Aidha, ujenzi wa bandari ya uvuvi – Kilwa umekamilika. Vilevile, huduma ya Mkongo wa Taifa inaendelea kusambazwa katika wilaya mbalimbali nchini, na ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam unaendelea kuimarika kupitia ushiriki wa sekta binafsi. Aidha, leseni 273 za uchimbaji wa madini zimetolewa kwa vikundi 2,550 vya wanawake na vijana; mkataba wa kuuza gesi asilia kwa kiwanda kidogo cha kuchakata gesi cha Mkuranga umesainiwa; na mali 48,713 katika makazi yasiyopangwa zimerasimishwa.

26. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha robo ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27, Serikali ilikamilisha ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba ambao unatarajiwa kuzinduliwa rasmi tarehe 30 Oktoba 2026.

VIII. MWENENDO WA UWEKEZAJI WA SEKTA BINAFSI

27. ***Mheshimiwa Spika***, Dira 2050 inaitambua na kuiweka sekta binafsi kama injini ya mageuzi ya kiuchumi. Dira 2050 inalenga kujenga sekta binafsi yenye ushindani, ustahimilivu, jumuishi na inayowajibika, ikichagizwa na sekta binafsi ndogo na za kati (MSMEs) inayoendeshwa kisasa na katika mfumo ulio rasmi wa uchumi. Mpango wa Maendeleo wa Muda Mrefu (LTPP 2026/27 – 2050/51) umeimarisha mwelekeo huu kwa kutambua mitaji ya uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kutoka sekta binafsi kama chanzo kikuu cha kugharamia maendeleo ya muda mrefu, ikitarajiwa kuwa sekta binafsi itachangia asilimia 70 ya uwekezaji unaohitajika.

28. ***Mheshimiwa Spika***, msingi wa mweleko huu upo katika ukweli kwamba sekta binafsi inaajiri sehemu kubwa ya nguvu kazi na kumiliki sehemu kubwa ya shughuli za uzalishaji. Kwa mfano, taarifa ya utafiti ya ajira na kipato ya mwaka 2024/25 (Employment and Earnings Survey of 2024/25) ilibaini kuwa kati ya ajira 4,565,960

zilizobainishwa, ajira 3,220,452 (70.5%) zilikuwa katika sekta binafsi na ajira 1,345,508 (29.5%) zilikuwa katika sekta ya umma.

29. ***Mheshimiwa Spika***, uwekezaji wa sekta binafsi umeendelea kuongezeka. Mwaka 2025/26, miradi 934 ya wawekezaji yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 12.5 ilisajiliwa, ikitarajiwa kuzalisha ajira 307,743. Katika robo ya kwanza ya 2026/27, miradi 243 yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 3.44 ilisajiliwa, ambapo asilimia 57.2 ni ya viwanda. Vilevile, miradi ya ubia iliyo katika utekelezaji imeongezeka hadi 10, ikiwemo Kituo cha Biashara cha Kariakoo, mabasi yaendayo haraka na reli ya TAZARA.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi, serikali imebaini na itasukuma utekelezaji wa miradi ya maendeleo 131 ya ubia inayostahili kutekelezwa kwa ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma. Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na tutaitolea taarifa zaidi katika taarifa ya nusu mwaka. Aidha, Serikali inaandaa sera mpya ya uwekezaji wa sekta binafsi pamoja na muswada wa sheria wa maendeleo ya sekta binafsi.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 na robo ya kwanza ya mwaka 2026/27 yanapatikana katika **Sura ya Tatu ya Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28.**

IX. VIPAUMBELE VYA ROBO MWAKA YA PILI YA MWAKA 2026/27

32. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika robo mwaka ya kwanza, Serikali itaweka mkazo katika vipaumbele sita (6) katika kipindi cha Oktoba–Desemba 2026.

32.1 ***Kwanza***, tutaendelea kuimarisha ulinganifu wa mipango na bajeti za taasisi na malengo ya Dira 2050.

32.2 ***Pili***, tutaboresha ukamilifu na uaminifu wa takwimu za msingi, viashiria vya utendaji na mifumo ya utoaji taarifa za robo mwaka.

32.3 ***Tatu***, tutaimarisha ufuatiliaji wa miradi ya kipaumbele ya maendeleo, kwa kuzingatia hatua za utekelezaji, matumizi ya bajeti na utatuzi wa changamoto kwa wakati.

32.4 ***Nne***, tutaongeza juhudi za kuhamasisha, kufuatilia na kufanya tathmini ya hali ya uwekezaji wa sekta binafsi na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, kwa kutambua kwamba shughuli za uzalishaji za sekta binafsi ni muhimu katika mabadiliko ya uchumi wetu.

32.5 ***Tano***, tutaongeza uratibu kati ya wizara, idara, wakala, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa ili kuhakikisha kwamba vipaumbele vya maendeleo ya kitaifa vinazaa matokeo katika ngazi za maeneo.

32.6 ***Sita***, tutaimarisha uwajibikaji kwa kutaka taasisi zinazotekeleza programu kueleza sababu za tofauti kubwa kati ya malengo na matokeo halisi, na kuonesha hatua zinazochukuliwa kurekebisha mapungufu yaliyobainika.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele hivi vitaungwa mkono na mapitio ya mara kwa mara ya utendaji na mifumo ya utoaji taarifa itakayohakikisha kwamba mafunzo yanayopatikana katika utekelezaji yanaingizwa katika maamuzi katika kipindi chote cha mwaka wa fedha.

X. VIPAUMBELE VYA MPANGO KWA MWAKA 2027/28

34. ***Mheshimiwa Spika,*** Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 yameandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele, malengo, shabaha na afua za kimkakati zilizoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27–2030/31 (FYDP IV). Mapendekezo haya yanalenga kuendeleza utekelezaji wa vipaumbele vya kimkakati vitakavyochochea mageuzi ya kiuchumi na kijamii, kuongeza tija na ushindani wa uchumi, pamoja na kuboresha ustawi wa wananchi. Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa Dira 2050, yenye lengo la kuifanya Tanzania kuwa Taifa Jumuishi Lenye Ustawi, Haki

na Linalojitegemea. Kwa msingi huo, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 yamejikita katika maeneo sita (6) ya kipaumbele, kama ifuatavyo:

34.1 Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani

Katika eneo hili, Mpango utaweka kipaumbele katika kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani kwa kuimarisha utulivu wa uchumi jumla, uhimilivu wa kifedha na ustahimilivu wa sekta ya nje. Msisitizo utawekwa katika:

i) Kuongeza tija katika uzalishaji;

ii) Kupanua minyororo ya thamani na kuongeza uwezo wa Tanzania kushiriki katika masoko ya kikanda na kimataifa;

iii) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ikiwemo kurahisisha mifumo ya udhibiti, na kurasimisha shughuli zisizo rasmi;

iv) Kukuza ushiriki wa sekta binafsi kuwekeza katika sekta zenye tija kubwa, matumizi ya teknolojia na mitambo ya kisasa;

v) Kuimarisha uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ndani na mauzo ya nje;

vi) Kuongeza uwezo wa kukusanya mapato ya ndani; na vii) Kuimarisha masoko ya mitaji na kutumia vyanzo bunifu vya fedha.

34.2 Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii

Mpango unatambua rasilimali watu kuwa msingi wa mageuzi na maendeleo ya Taifa. Kwa hiyo, juhudi zitaelekezwa katika:

i) Kuboresha upatikanaji na ubora wa elimu, mafunzo ya ujuzi na elimu inayozingatia mahitaji ya soko la ajira, hususan katika sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati;

ii) Kujenga nguvu kazi yenye ujuzi, tija na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya uchumi;

iii) Kuendelea na maandalizi ya utekelezaji wa elimu ya sekondari kwa wote kuanzia mwaka 2028;

iv) Kuimarisha upatikanaji wa ajira kwa vijana na maendeleo ya biashara ndogo na za kati ili kutumia fursa ya ongezeko la watu wenye umri wa kufanya kazi;

v) Kuendelea na utekelezaji wa programu ya bima ya afya kwa wote;

vi) Kuimarisha uwekezaji wa viwanda vya uzalishaji dawa na vifaa tiba;

vii) Kuimarisha malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto;

viii) Kuanza kutekeleza afua mahsusi zinazolenga kuondoa umaskithiri uliokithiri miongoni mwa wananchi kwa kuzingatia kiwango cha umaskini katika maeneo ya kijiografia.

34.3 Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi

Mpango utaweka uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi kama sehemu muhimu ya maendeleo endelevu. Vipaumbele vimejielekeza katika:

i) Kuendeleza miji iliyopangwa, matumizi endelevu ya ardhi na bahari, uhifadhi na urejeshaji wa misitu, mabonde ya maji na rasilimali za bahari;

ii) Kuimarisha mifumo ya kukabiliana na majanga na tahadhari za mapema. Lengo ni kupunguza athari za majanga na mabadiliko ya tabia nchi kama vile El-nino;

iii) Kuendeleza uchumi wa kijani kupitia uzalishaji wenye kiwango kidogo cha hewa ukaa, matumizi bora ya rasilimali na teknolojia rafiki kwa mazingira; na

iv) Kutumia fursa za uchumi wa buluu na biashara ya kaboni kama vyanzo vya ukuaji na mapato.

34.4 Vichocheo vya Maendeleo

Vichocheo vya maendeleo vitawezesha utekelezaji wa nguzo za Mpango na kuongeza kasi ya mageuzi ya uchumi. Vipaumbele vitajikita katika:

i) Kuendelea kuwekeza katika uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati ya uhakika, nafuu na endelevu ili kusaidia uzalishaji viwandani, biashara na huduma za jamii;

ii) Kuendeleza uwekezaji katika miundombinu ya barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na mifumo ya usafirishaji fungamanishi ili kupunguza gharama za biashara, kuunganisha maeneo ya uzalishaji na masoko na kuiwezesha Tanzania kuwa kitovu cha usafirishaji na biashara;

iii) Kuimarisha uwekezaji katika sayansi, teknolojia, utafiti na ubunifu; na

iv) Kuongeza miundombinu ya TEHAMA, huduma za Serikali kidijitali, mifumo ya takwimu na matumizi ya teknolojia mpya.

34.5 Kuimarisha Utekelezaji wa Sekta za Mageuzi

Mheshimiwa Spika, Dira 2050 imezitambua sekta za kimageuzi tisa (9) ambazo zina uwezo mkubwa wa kuchochea ukuaji wa uchumi, kuzalisha ajira, kuongeza mapato ya serikali na kuongeza mauzo ya nje. Sekta hizo ni pamoja na kilimo, uzalishaji viwandani, madini, mafuta na gesi, ujenzi, ardhi na makazi, utalii, michezo, sanaa na ubunifu, fedha, biashara na ujasiriamali. Vipaumbele vitakuwa:

i) Kuongeza tija katika uzalishaji, usindikaji na kuimarisha minyororo ya thamani;

ii) Kukamilisha miradi ya umwagiliaji;

iii) Kuendelea na utekelezaji wa gridi ya taifa ya maji (*National Water Grid*) kwa kutumia kikamilifu rasilimali za maji za taifa, zikiwemo maziwa makubwa na mito mikubwa kama vile Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Mto Rufiji. Aidha, pamoja na upatikanaji wa maji safi ya kunywa, msukumo wa kipekee utawekwa katika kuhakikisha kuwa rasilimali za maji katika mradi huu zinatumika kuchochea uzalishaji katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi;

iv) Kuunganisha wazalishaji katika minyororo ya thamani na kuongeza mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani;

v) Kuendelea na maandalizi ya mashindano ya AFCON 2027

vi) Kuongeza thamani ya mauzo ya huduma za utalii, michezo, sanaa na ubunifu kwa kuitangaza Tanzania kimataifa; na

vii) Kuimarisha upatikanaji wa mitaji kwa sekta ya uzalishaji ikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuanzisha mkakati maalum wa ufadhili/ugharamiaji wa sekta hizi.

34.6 Kuimarisha Misingi ya Uendelevu wa Taifa

Eneo hili limelenga kuimarisha uwazi, uwajibikaji, maadili na tunu za kidemokrasia, pamoja na amani na utulivu, na kuimarisha utumishi wa umma unaoendana na mahitaji ya wananchi. Afua zitakazotekelezwa katika eneo hili ni:

i) Kuendelea kuimarisha utawala bora, demokrasia, usalama na utulivu pamoja na kuongeza uwezo na ufanisi wa taasisi za Serikali;

ii) Kuimarisha uwezo wa Serikali za Mitaa ili kuwezesha mipango na utekelezaji wa maendeleo kwa kuzingatia mahitaji halisi ya wananchi na maeneo husika;

iii) Kuimarisha uwajibikaji na ushiriki wa wananchi katika utoaji wa huduma za umma;

iv) Kuboresha sheria ili kuendana na Dira 2050;

v) Kuimarisha matumizi ya teknolojia za kidijitali na takwimu sahihi katika kupanga, kutekeleza na kufuatilia maendeleo;

vi) Kuweka msukumo katika mabadiliko ya mtazamo, fikra na utamaduni wa utendaji ili kujenga nidhamu, ubunifu, uwajibikaji na uzalendo katika utumishi wa umma na jamii; na

vii) Kusisitiza maadili ya uadilifu, uwajibikaji, ujumuishi, uendelevu na ubunifu kama msingi wa kuhakikisha mageuzi yanatekelezwa kwa ufanisi na manufaa yake yanafikia wananchi wote.

35. *Mheshimiwa Spika*, maeneo ya vipaumbele vya Mpango wa 2027/28 yatatekelezwa kupitia programu za kielelezo saba (7), miradi shikizi 38 na maeneo ya minyororo ya thamani 34 kama yalivyoainishwa katika FYDP IV. Utekelezaji wa programu hizi pamoja na maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa unatarajiwa kuwezesha ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 6.3 mwaka 2026 na asilimia 6.6 mwaka 2027, kutoka asilimia 5.9 mwaka 2025; uzalishaji wa wastani wa ajira mpya 1,700,000 mwaka 2027, kutoka ajira 981,000 mwaka 2025; uwezo wa kuzalisha umeme kufikia MW 4,804, Juni 2028 kutoka MW 4,606.14, Septemba 2026; na wanufaika wa bima ya afya kufikia asilimia 32.38 mwaka 2027/28 kutoka makadirio ya asilimia 25 mwaka 2026/27. Kwa upande wa miundombinu na biashara ya nje, mizigo inayosafirishwa kwa reli ya kati inatarajiwa kufikia tani 1,000,000 mwaka 2027/28 kutoka tani 810,000 mwaka 2026/27, huku mchango wa bidhaa za viwandani

katika mauzo yote ya nje ukitarajiwa kufikia asilimia 16.9 mwaka 2027/28 kutoka asilimia 15.5 mwaka 2025.

36. *Mheshimiwa Spika*, maelezo ya kina kuhusu vipaumbele vya Mpango yanapatikana katika ***Sura ya Nne ya Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28.***

XI. USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI KATIKA MPANGO WA TAIFA WA MAENDELEO WA MWAKA 2027/28

37. *Mheshimiwa Spika*, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV) umebainisha na kufungamanisha minyororo ya thamani katika programu za kielelezo ili kuhakikisha zinakuwa na manufaa kwa biashara, uzalishaji, kukuza ushindani, kupanua wigo wa mapato, mauzo nje na kuongeza ajira. Kwa msingi huo, katika Mwaka 2027/28 Serikali itaendelea kuweka mazingira yatakayo wezesha sekta binafsi kuwa mshirika mkuu wa uwekezaji na utekelezaji wa Mpango. Fursa muhimu zitakazopewa kipaumbele ni pamoja na: kilimo cha maua na mazao ya bustani; ufugaji wa viumbe maji; uchimbaji na uongezaji thamani wa madini; uzalishaji wa mafuta ya kula; na viwanda vya nguo na mavazi. Katika maeneo haya, uwekezaji utahusisha hatua zote za minyororo ya thamani, kuanzia uzalishaji na uchakataji hadi uhifadhi, usafirishaji na masoko.

38. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha kuwa sekta binafsi, inashiriki kikamilifu katika uwekezaji wa maeneo yaliyobainishwa, Serikali itatoa kipaumbele katika kupunguza vihatarishi na kuboresha mazingira ya uwekezaji, kuboresha upatikanaji wa taarifa kuhusu fursa zilizopo, kuharakisha maamuzi yanayohitajika na kuimarisha uratibu kati ya taasisi za Serikali na wawekezaji. Aidha, sekta binafsi itaendelea kushiriki katika majadiliano, mashauriano na vikao kazi katika maandalizi ya mipango ya kisekta, utekelezaji, utatuzi wa changamoto na tathmini ya miradi ya maendeleo.

39. *Mheshimiwa Spika*, katika kukuza maendeleo ya sekta binafsi nchini, Serikali itatekeleza Mkakati wa Pili wa Kuimarisha Mazingira

ya Biashara na Uwekezaji Nchini (MKUMBI II). Hatua zitakazochukuliwa katika kutekeleza MKUMBI II ni pamoja na kutunga muswada wa sheria wa maendeleo ya Sekta Binafsi.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu ushiriki wa sekta binafsi katika Mpango yanapatikana katika **Sura ya Tano ya Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28.**

41. ***Mheshimiwa Spika***, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV) umebainisha na kufungamanisha minyororo ya thamani katika programu za kielelezo ili kuhakikisha zinakuwa na manufaa kwa biashara, uzalishaji, kukuza ushindani, kupanua wigo wa mapato, mauzo nje na kuongeza ajira. Kwa msingi huo, katika Mwaka 2027/28 Serikali itaendelea kuweka mazingira yatakayo wezesha sekta binafsi kuwa mshirika mkuu wa uwekezaji na utekelezaji wa Mpango.

42. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2027/28 maeneo matano ya minyororo ya thamani yatapewa kipaumbele. Maeneo hayo ni:

1. ***Kilimo cha maua na mazao ya bustani*** (matunda, mbogamboga, maua na viungo), ambapo uwekezaji utakuwa katika utafiti, pembejeo, uzalishaji, uhifadhi na uchakataji hadi usafirishaji kwenda masoko ya nje;

2. ***Ufugaji wa viumbe maji***, unaojumuisha uzalishaji wa mbegu na chakula cha viumbe hai, vifaa vya ufugaji, miundombinu ya baridi, matumizi ya kidijitali na uendelezaji wa masoko;

3. ***Utafiti, Uchimbaji na kuongeza thamani ya madini*** kwa kutumia teknolojia na ubunifu katika uchimbaji, uchakataji na upanuzi wa masoko ya nje;

4. ***Uzalishaji wa mafuta ya kula*** kupitia mbegu bora, kilimo cha kibiashara na ujenzi wa viwanda vya uchakataji, na

5. ***Uzalishaji wa nguo na mavazi***

6. Kuimarisha uzalishaji wa mazao ya kilimo, ikiwemo korosho, sukari na ngano pamoja na uongezaji wa thamani wa mazao haya.

XIII. UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2027/28

43. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2027/28 utatumia mfumo wa uwekezaji na ugharamiaji wa sekta ya umma na sekta binafsi kwa kuzingatia uwiano wa 30:70 ulioanishwa katika FYDP IV kwa Serikali na Sekta Binafsi. Hivyo, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 unakadiriwa kugharimu trilioni 89.3 Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 20.7 zinatarajiwa kutoka katika bajeti ya Serikali, shilingi trilioni 6.3 kutoka katika uwekezaji wa mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara, na shilingi trilioni 62.3 kutoka sekta binafsi.

44. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kuhakikisha upatikanaji wa fedha hizo, vyanzo vya ugharamiaji vinajumuisha mapato ya ndani ya kodi na yasiyo ya kodi, faida za mashirika ya umma, mikopo na misaada, uwekezaji wa moja kwa moja wa ndani na nje, pamoja na ubia wa sekta ya umma na binafsi. Serikali pia itahamasisha vyanzo mbadala na bunifu vya ugharamiaji, vikiwemo hati fungani za kijani na za miundombinu, na kutumia taasisi za fedha za maendeleo, mifuko ya hifadhi ya jamii, kampuni za bima, benki na masoko ya mitaji.

45. ***Mheshimiwa Spika*****,** maelezo ya kina kuhusu ugharamiaji wa Mpango yanapatikana katika **Sura ya Sita ya Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28.**

XIV. USIMAMIZI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2027/28

46. ***Mheshimiwa Spika***, Utekelezaji wa Mpango 2027/28 utategemea mfumo wa uratibu wa kitaifa unaofungamanisha upangaji, uidhinishaji, ugharamiaji, utekelezaji, ufuatiliaji, tathmini

na utoaji taarifa kama ilivyoanishwa katika Mwongozo wa Kitaifa wa Uandaaji wa Mipango, Mwongozo wa Kitaifa wa Uidhinishaji wa Miradi, Mwongozo wa Kitaifa wa Upimaji wa Matokeo na Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo pamoja na Mfumo wa Usimamizi wa Miradi (e-Delivery).

47. *Mheshimiwa Spika*, Pamoja na miongozo iliyobainishwa, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 utatumia Mbinu ya Maabara (Lab Delivery Approach). Mbinu hii inalenga kufanya mageuzi katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kuleta matokeo makubwa na yanayopimika. FYDP IV imejengwa juu ya programu saba za kielelezo zinazotekelezwa kupitia miradi shikizi 51 (anchor projects) inayohitaji rasilimali nyingi na uratibu wa karibu wa wadau wengi. Kwa kutumia mbinu ya maabara, kila eneo la kipaumbele litachambuliwa kwa kina, kubainisha mahitaji halisi ya rasilimali, muda, wahusika, na viashiria vinavyopimika vyenye kuleta matokeo tarajiwa na kuongeza uwajibikaji ili kufikia malengo makubwa yaliyowekwa katika Dira 2050 na Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP IV).

48. *Mheshimiwa Spika*, Ili kuimarisha uratibu na ufanisi, mfumo wa kitaasisi wa utekelezaji wa mpango umeainisha majukumu mahsusi ya taasisi za umma na wadau mbalimbali katika hatua za upangaji na utekelezaji. Mgawanyo huu unalenga kuondoa mwingiliano wa majukumu na kuimarisha uwajibikaji. Majukumu hayo ni kama ifuatavyo:

a. ***Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji***: Kusimamia maandalizi na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 na kuwasilisha mapendekezo hayo Bungeni.

Tume ya Taifa ya Mipango itaratibu maandalizi, uidhinishaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa lengo la kuhakikisha ufungamanishaji wa Dira 2050, Mpango wa IV, Mpango wa mwaka na mipango ya kisekta na kitaasisi.

b. ***Wizara ya Fedha*** itaratibu utafutaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele vya mpango pamoja na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

c. ***Ofisi ya Waziri Mkuu*** – TAMISEMI itaratibu utekelezaji katika ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha vipaumbele vya kitaifa vinatafsiriwa katika mipango na bajeti za ngazi hizo.

d. ***Ofisi ya Msajili wa Hazina*** itakuwa na jukumu la kusimamia utendaji na usimamizi wa mashirika ya umma, hususan katika kuongeza ufanisi wa mashirika ya umma katika utekelezaji wa vipaumbele vya kitaifa.

e. ***Wizara, Idara, Wakala, na Sekretarieti za Mikoa:*** zitawajibika kutekeleza programu na miradi kwa mujibu wa majukumu yao, bajeti zilizoidhinishwa, viashiria vya utendaji na matokeo yaliyokusudiwa.

XV. WAJIBU WA BUNGE NA WADAU WENGINE WA TAIFA

49. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wenye mafanikio wa Dira 2050 unahitaji umiliki wa kitaifa na usimamizi madhubuti. Bunge lina nafasi muhimu katika kuchambua sera, kuidhinisha bajeti, kufuatilia matumizi ya rasilimali za umma na kuhakikisha kwamba utekelezaji unaendelea kuendana na matarajio ya wananchi wa Tanzania.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inathamini ushiriki wa Waheshimiwa Wabunge katika kubaini mapungufu ya utekelezaji, kuchambua mgao wa rasilimali na kupendekeza hatua zinazoweza kuboresha matokeo.

51. ***Mheshimiwa Spika***, wadau wengine muhimu katika utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo lazima nao waendelee kuchukua nafasi zao. Hawa ni pamoja na:

a. ***Sekta binafsi*** inapaswa kuendelea kuongeza uwekezaji wenye tija, kuendeleza biashara zinazoweza kushindana na kuzalisha ajira.

b. ***Taasisi za elimu ya juu na utafiti*** zinapaswa kuchangia ushahidi, ubunifu na maendeleo ya ujuzi.

c. ***Mamlaka za Serikali za Mitaa*** zinapaswa kutafsiri vipaumbele vya kitaifa katika fursa za kiuchumi za maeneo yao na huduma bora kwa wananchi.

d. **Washirika wa maendeleo** wanapaswa kuelekeza ushirikiano wao katika vipaumbele vya kitaifa, wakati Watanzania waishio nje ya nchi na wadau wengine wanaweza kuchangia kupitia uwekezaji, maarifa, teknolojia na ubia wa kimkakati.

e. **Mashirika ya kiraia** (**CSOs**) ikiwemo mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), mashirika ya kidini, na mashirika ya kijamii wataendelea kushirikiana na jamii kwa lengo la kufuatilia shughuli za Serikali zinazolenga kuchochea maendeleo ya watu na ustawi wa jamii.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** muhimu zaidi, ***Wananchi*** lazima waendelee kuwa kiini cha utekelezaji. Dira 2050 itahukumiwa kwa kuzingatia kama inaboresha fursa zao, kipato, maisha na ustawi wao.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu usimamizi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa yanapatikana katika **Sura ya Saba ya Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28.**

XVI. HITIMISHO

54. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapohitimisha maelezo yangu, ninapenda kusisitiza tena kwamba taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27, ambao ni wa kwanza katika utekelezaji wa Dira 2050, ni mwanzo wa safari ndefu ya maendeleo ya taifa letu. Hatutarajii kuona mafanikio makubwa ya utekelezaji wa Dira 2050 katika miezi hii mitatu ya kwanza, lakini tunatambua umuhimu wake katika kuweka msingi imara wa utekelezaji. Jukumu letu kubwa katika hatua ya sasa ni kujenga mfumo wa maendeleo unaounganisha matarajio ya muda mrefu na vipaumbele vya mwaka, unaoelekeza rasilimali za umma katika malengo yanayopimika, unaohamasisha uwekezaji binafsi na unaowawajibisha watendaji kwa matokeo.

55. ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio ya Dira 2050 hayataamuliwa na ubora wa waraka pekee. Yataamuliwa na maamuzi tunayofanya, rasilimali tunazokusanya, taasisi tunazoimarisha na matokeo tunayoyapata kadiri muda unavyokwenda. Kwa hiyo, dhamira yetu lazima iwe kutofautisha wazi kati ya mipango iliyotangazwa, shughuli zilizofanyika, matokeo ya moja kwa moja yaliyopatikana na mabadiliko halisi yaliyojitokeza katika maisha ya wananchi. Lazima tuwe wakweli kuhusu changamoto, tuchukue hatua madhubuti kuzitatua na tuwe na msimamo thabiti katika kupima maendeleo.

56. ***Mheshimiwa Spika***, azma yetu ya kitaifa ni kujenga Tanzania ambayo ustawi wake unawanufaisha wananchi wengi zaidi, ajira zenye tija zinaongezeka, biashara zina ushindani zaidi, huduma za umma zinaimarika na vizazi vijavyo vinarithi nchi yenye fursa nyingi zaidi kuliko zile tulizonazo leo. Azma hii inawezekana tukichanganya mipango bora na utekelezaji wenye nidhamu, uwajibikaji kwa umma na ushirikiano imara kati ya Serikali na sekta zote za jamii.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** **Dira 2050 lazima iwe zaidi ya dira tunayojivunia. Lazima iwe mabadiliko tunayotekeleza, ahadi tunayopima na urithi tunaouacha kwa vizazi vijavyo.**

58. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa maelezo hayo, ninaomba Bunge lako tukufu lipokee, lijadili na litoe maoni na ushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2027/28.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba Hotuba yangu hii na Kitabu cha Mapendekezo tulichowasilisha viingie katika kumbukumbu za Bunge.

60. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kuwasilisha.

Prof. Kitila Alexander Mkumbo **(Mb.)**,
WAZIRI WA NCHI,
OFISI YA RAIS MIPANGO NA UWEKEZAJI

Oktoba, 2026

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2027/28 – KAMA ULIVYOWASILISHWA MEZANI

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Dira 2050) imeweka mwelekeo wa muda mrefu wa kuifanya Tanzania kuwa Taifa Jumuishi Lenye Ustawi, Haki na Linalojitegemea. Katika kipindi cha miaka 25 ijayo, Dira 2050 inalenga kujenga uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu, ulio mseto, himilivu, jumuishi na shindani; kuboresha maisha na ustawi wa wananchi; kuhakikisha matumizi endelevu na yenye tija ya rasilimali za taifa; pamoja na kujenga jamii yenye ujuzi, ubunifu na uwezo wa kutumia teknolojia za kisasa katika kuongeza ushindani wa Taifa.

Ili kufikia malengo hayo, utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 wenye dhima ya "Mageuzi kwa ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji Ajira" unalenga kuweka mazingira na kutekeleza hatua zitakazowezesha Tanzania kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi, tija na ushindani, kuongeza uwekezaji, fursa za ajira na kipato kwa wananchi pamoja na kukuza uzalishaji.

Kwa kipindi cha mwaka 2027/28, Mpango wa Maendeleo wa Taifa ambao ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27-2030/31 utaweka mkazo katika kuongeza tija na thamani ya uzalishaji, kuimarisha ushindani wa bidhaa na huduma, kuchochea uwekezaji wa ndani na nje, kuongeza ushiriki wa sekta binafsi na kuboresha huduma za kijamii na ustawi wa wananchi. Aidha, maandalizi ya Mpango huu

yamezingatia mafunzo muhimu yaliyotokana na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2026/27. Aidha, yamezingatia hali, mwenendo, na mazingira ya ndani, kikanda na kimataifa yanayoweza kuathiri ukuaji wa uchumi, biashara, uwekezaji, ajira, ustawi wa wananchi na uwezo wa kutekeleza vipaumbele vya maendeleo.

Hivyo, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 utaweka mkazo katika kuongeza tija na thamani ya uzalishaji, kuimarisha ushindani wa bidhaa na huduma, kuchochea uwekezaji wa ndani na nje na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi. Vilevile, Mpango unalenga kuendeleza miundombinu wezeshi, kukuza biashara na masoko, kuongeza fursa za ajira na kipato pamoja na kuboresha huduma za kijamii na ustawi wa wananchi.

1.2 Malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28

Mapendekezo haya yanatoa msingi wa maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28. Lengo kuu la Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 ni kuendelea kutekeleza afua za kimkakati ili kuleta mageuzi kwa ajili ya ukuaji jumuishi wa uchumi na uzalishaji wa ajira.

Malengo mahsusi ya Mpango ni: kuimarisha ukuaji wa uchumi, mazingira ya biashara na uwekezaji; kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi; na kuongeza fursa za ajira na kipato. Kadhalika, kuchochea maendeleo ya watu na ustawi wa jamii; kuboresha miundombinu na kuendeleza vichocheo vya mageuzi; kuimarisha ustahimilivu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi; pamoja na kuimarisha utawala, uratibu na utekelezaji wa Mpango.

1.3 Mfumo wa Kusimamia Utekelezaji wa Matokeo

Utekelezaji wa Mpango 2027/28 utategemea mfumo wa uratibu wa kitaifa unaofungamanisha upangaji, uidhinishaji, ugharamiaji, utekelezaji, ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa kama ilivyoanishwa katika Mwongozo wa Kitaifa wa Uandaaji wa Mipango, Mwongozo wa Kitaifa wa Uidhinishaji wa Miradi, Mwongozo wa Kitaifa wa Upimaji wa Matokeo na Utekelezaji wa

Mipango ya Maendeleo pamoja na Mfumo wa Usimamizi wa Miradi (e-Delivery).

Pamoja na miongozo iliyobainishwa, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 utatumia Mbinu ya Maabara (Lab Delivery Approach). Mbinu hii inalenga kufanya mageuzi katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kuleta matokeo makubwa na yanayopimika. FYDP IV imejengwa juu ya programu saba za kielelezo zinazotekelezwa kupitia miradi shikizi (anchor projects) inayohitaji rasilimali nyingi na uratibu wa karibu wa wadau wengi. Kwa kutumia mbinu ya maabara, kila eneo la kipaumbele litachambuliwa kwa kina, kubainisha mahitaji halisi ya rasilimali, muda, wahusika, na viashiria vinavyopimika vyenye kuleta matokeo tarajiwa na kuongeza uwajibikaji ili kufikia malengo makubwa yaliyowekwa katika Dira 2050 na Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP IV).

Ili kuimarisha uratibu na ufanisi, mfumo wa kitaasisi wa utekelezaji wa mpango umeainisha majukumu mahsusi ya taasisi za umma na wadau mbalimbali katika hatua za upangaji na utekelezaji. Mgawanyo huu unalenga kuondoa mwingiliano wa majukumu na kuimarisha uwajibikaji. Majukumu hayo ni kama ifuatavyo:

(i) Tume ya Taifa ya Mipango itaratibu maandalizi, uidhinishaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa lengo la kuhakikisha ufungamanishaji wa Dira 2050, Mpango wa IV, Mpango wa mwaka na mipango ya kisekta na kitaasisi.

(ii) Wizara ya Fedha itaratibu utafutaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele vya mpango pamoja na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

(iii) Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI itaratibu utekelezaji katika ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha vipaumbele vya kitaifa vinatafsiriwa katika mipango na bajeti za ngazi hizo.

(iv) Ofisi ya Msajili wa Hazina itakuwa na jukumu la kusimamia utendaji na usimamizi wa mashirika ya umma, hususan

katika kuongeza ufanisi wa mashirika ya umma katika utekelezaji wa vipaumbele vya kitaifa.

(v) Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa: zitawajibika kutekeleza programu na miradi kwa mujibu wa majukumu yao, bajeti zilizoidhinishwa, viashiria vya utendaji na matokeo yaliyokusudiwa.

(vi) Sekta binafsi na washirika wa maendeleo watawajibika kutafasiri uwekezaji na ugharamiaji wa mipango yao kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa.

(vii) Mashirika ya kiraia (CSOs)—ikiwemo mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), mashirika ya kidini, na mashirika ya kijamii wataendelea kushirikiana na jamii kwa lengo la kufuatilia shughuli za Serikali zinazolenga kuchochea maendeleo ya watu na ustawi wa jamii.

1.4 Mawanda ya Mpango

Mawanda ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 yatazingatia maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV), kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa vipaumbele vya Taifa na kufikia matokeo tarajiwa ya kiuchumi na kijamii. Mpango utajikita katika vipaumbele vya uzalishaji, huduma za jamii na miundombinu katika ngazi ya Taifa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Utekelezaji utaelekezwa kwenye Programu za Kielelezo saba (7) za FYDP IV, kwa kuhakikisha miradi shikizi iliyobainishwa inaandaliwa na kutekelezwa kwa wakati kwa kuzingatia utayari wa miradi. Kwa msingi huo, Mpango huu utazingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika sekta za uzalishaji, kijamii na miundombinu katika ngazi zote za kitaifa, mikoa na halmashauri.

1.5 Mbinu za Uandaaji wa Mpango wa Mwaka 2027/28

Maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2027/28 yatatumia mbinu shirikishi, zinazotegemea ushahidi (evidence-based) na zinayozingatia matokeo. Mbinu hizo zitawezesha kubainisha vipaumbele vya Mpango 2027/28

vitafikiwa kikamilifu kama vilivyoainishwa katika Mpngo wa IV na Dira 2050. Kwa msingi huo, maandalizi ya Mpango yatahuisha majadiliano ya wadau mbalimbali kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta binafsi, Mashirika ya Umma na Washirika wa Maendeleo. Aidha, maandalizi ya mpango huu yatazingatia uchambuzi wa takwimu na ushahidi wa kiuchumi, kijamii na kimazingira pamoja na mapitio ya mipango ya maendeleo ya kitaifa, ajenda za kikanda na kimataifa ikiwemo Dira ya Jumuia ya Afrika Mashariki, Dira ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Ajenda 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na Ajenda 2063 ya Umoja wa Mataifa.

1.6 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2027/28 Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2027/28 utahitaji mfumo wa uwekezaji na ugharamiaji wa sekta ya umma na sekta binafsi kwa kuzingatia uwiano wa 30:70 ulioanishwa katika Mpango wa IV. Serikali itazingatia uwezo halisi wa rasilimali zilizopo, uhimilivu wa deni la Serikali, thamani ya fedha na umuhimu wa kuelekeza rasilimali katika maeneo yenye matokeo makubwa ya kiuchumi na kijamii. Kwa kuzingatia azma ya kuongeza nafasi ya sekta binafsi katika utekelezaji wa Dira 2050, Serikali itaendelea kuimarisha mifumo itakayowezesha sekta binafsi kushiriki katika uwekezaji na kugharamia utekelezaji wa miradi na programu za kimkakati.

Vyanzo vya mapato vitakavyotumika katika utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2027/28 ni kama ifuatavyo: mapato ya ndani ya kodi na yasiyo ya kodi, uwekezaji unaotokana na faida za mashirika ya umma; mikopo nafuu ya biashara na misaada; mitaji ya sekta binafsi kupitia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi pamoja na uwekezaji wa moja kwa moja wa ndani na kutoka nje Vilevile, vyanzo bunifu vya ufadhili ikiwemo hati fungani za kijani na za miundombinu vitatumika katika Mpango huu. Aidha, Benki ya Uwekezaji, Benki ya Kilimo, mifuko ya hifadhi ya jamii, kampuni za bima, benki za biashara, taasisi za fedha za maendeleo na masoko ya mitaji zitakuwa sehemu muhimu ya mfumo wa kukusanya

rasilimali fedha kwa ajili ya kuwekeza katika sekta na miradi yenye umuhimu wa kimkakati.

1.7 Mpangilio wa Kitabu

Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 kimegawanyika katika sura nane (8). Sura ya kwanza ni utangulizi unaojumuisha usuli, malengo na mfumo wa utekelezaji na matokeo. Sura ya pili inawasilisha mapitio ya viashiria muhimu vya kiuchumi na kijamii na mwelekeo kwa mwaka 2027/28. Sura ya tatu inaelezea kwa muhtasari utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango ya Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Vile Vile, sura hii inaelezea uchambuzi na mapitio ya utekelezaji wa vipaumbele na programu zilizotekelezwa katika mwaka 2026/27. Sura ya nne inaainisha maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2027/28. Sura ya tano inaelekeza ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango 2027/28. Sura ya sita inabainisha mahitaji ya fedha, vyanzo vya fedha, mgawanyo wa rasilimali na mikakati ya kuongeza ufanisi na uendelevu wa ugharamiaji wa Mpango. Sura ya saba inafafanua mfumo wa kufuatilia utekelezaji, viashiria vya matokeo, majukumu ya taasisi, mifumo ya taarifa na taratibu za tathmini. Sura ya nane inajadili vihatarishi vya kiuchumi, kifedha, kimazingira, kiteknolojia na kiutendaji vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa Mpango, pamoja na hatua za kukabiliana navyo.

SURA YA PILI

HALI YA UCHUMI

2.1 Utangulizi

Sura hii inatoa tathmini ya mwenendo wa viashiria vya kiuchumi na kijamii katika ngazi ya dunia, kikanda, na kitaifa kwa mwaka 2025 na 2026, pamoja na matarajio kwa mwaka 2027. Uchambuzi wa viashiria vya hali ya uchumi ni muhimu katika kupanga maendeleo ya Taifa kwa kuwa unawezesha kutathmini ufanisi wa sera, mipango na mikakati ya maendeleo; kulinganisha mwenendo wa uchumi wa ndani na mazingira ya kikanda na

kimataifa; kubaini maeneo yanayohitaji hatua za kisera; na kuweka msingi wa maamuzi ya kimkakati. Viashiria vilivyochambuliwa katika sura hii ni pamoja na Pato la Taifa, mfumuko wa bei, mwenendo wa sekta ya nje, sekta ya fedha, deni la Taifa, demografia na maendeleo ya watu.

2.2 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda

2.2.1 Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia umeendelea kukua licha ya changamoto mbalimbali, ikiwemo migogoro ya kikanda na kutotabirika kwa sera za biashara. Kwa mujibu wa taarifa ya World Economic Outlook (WEO) Update ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Oktoba 2026, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia ilikuwa asilimia 3.5 mwaka 2025. Hata hivyo, kasi ya ukuaji inatarajiwa kupungua hadi asilimia 3.1 mwaka 2026 kunatokana na athari za migogoro inayoendelea Mashariki ya Kati, ambayo imeongeza shinikizo katika bei za nishati, kuathiri minyororo ya ugavi na kudhoofisha mazingira ya biashara na uwekezaji duniani. Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajiwa kuongezeka na kufikia asilimia 3.4 mwaka 2027 kutokana na kuongezeka kwa mahitaji yanayochochewa na maendeleo na matumizi ya teknolojia, hususan ongezeko la uwekezaji unaohusishwa na maendeleo na matumizi ya teknolojia ya akili unde (Artificial Intelligence - AI).


Kwa upande wa Tanzania, kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia kunaweza kupunguza mtiririko wa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje, kudhoofisha mahitaji na bei za baadhi ya bidhaa zinazouzwa katika soko la dunia, kuongeza gharama za nishati na usafirishaji, pamoja na kupunguza upatikanaji wa misaada na mikopo yenye masharti nafuu. Ili kupunguza athari hizo na kutumia fursa zinazotokana na mabadiliko ya teknolojia duniani, Serikali itaendelea kuimarisha vyanzo vya ndani vya ukuaji wa uchumi, kupanua na kutofautisha masoko ya bidhaa na huduma, kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini, kuimarisha usalama wa nishati na minyororo ya ugavi, pamoja na kukuza uwekezaji wa ndani na matumizi ya teknolojia mpya kupitia ushiriki mpana wa sekta binafsi.

2.2.2 Uchumi wa Kikanda

Ukuaji wa uchumi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ulifikia asilimia 4.5 mwaka 2025. Hata hivyo, kasi ya ukuaji inatarajiwa kuimarika na kufikia asilimia 4.5 kwa mwaka 2026 na 2027. Pamoja na mwelekeo huo wa jumla, matarajio ya ukuaji yanatofautiana kati ya nchi na nchi kutokana na tofauti katika nafasi ya utekelezaji wa sera, kasi na ufanisi wa utekelezaji wa mageuzi ya kimuundo, pamoja na kiwango cha kuathiriwa na mishtuko kutoka nje. Nchi zinazoagiza mafuta na zile ambazo uchumi wake hautegemei kwa kiasi kikubwa rasilimali asilia zinatarajiwa kuathirika zaidi kutokana na ongezeko la bei za nishati na chakula, kupungua kwa misaada rasmi ya maendeleo (Official Development Assistance - ODA), pamoja na ushiriki mdogo katika fursa za ukuaji wa teknolojia duniani zinazochochewa na maendeleo na matumizi ya akili unde (Artificial Intelligence - AI). Hali hii inaonesha umuhimu wa nchi hizo kuimarisha uthabiti wa uchumi, kuongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali za ndani, kuharakisha mageuzi ya kimuundo na kupanua matumizi ya teknolojia ili kupunguza athari za mishtuko ya nje na kuendeleza ukuaji jumuishi.


Ukuaji wa uchumi wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ulikua kwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2025 na unatarajiwa kukua kwa kiwango hicho kwa mwaka 2026 na 2027. Kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 11.1 mwaka 2025 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.2 mwaka 2026 na asilimia 6.0 mwaka 2027. Aidha, kuimarika kwa uchumi kwa mwaka 2027 kunatarajiwa kuchangiwa na ukuaji imara nchini Uganda, Rwanda na Tanzania.

Kielelezo Na. 2.1: Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) Mwaka 2025 na Maoteo kwa mwaka 2026 na 2026



Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF)
*Takwimu za maoteo

Kielelezo Na. 2.2: Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Mwaka 2025 na Maoteo kwa Mwaka 2026 na 2027



Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa
*Takwimu za maoteo

***Katika kutoa taswira ya hali ya uchumi wa kikanda, mapitio na maoteo ya takwimu za Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) hutumika ili kufanya ulinganifu sahihi baina ya nchi za kanda husika. Hivyo, katika eneo hili takwimu maoteo ya uchumi ya Tanzania yamezingatia maoteo ya IMF.

Aidha, utofauti wa takwimu za IMF na za ndani ya nchi unasababishwa na utofauti wa moduli zinazotumika katika kuandaa takwimu husika; viashiria vinavyotumika; na misingi (assumptions) iliyotumika katika maandalizi ya takwimu husika.

2.2.3 Mfumuko wa Bei wa Dunia

Kwa mujibu wa taarifa ya IMF ya Oktoba 2026, mfumuko wa bei wa dunia unategemea kuongezeka kutoka wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2025 hadi asilimia 4.7 mwaka 2026, kabla ya kupungua hadi asilimia 4.1 mwaka 2027. Ongezeko linalotarajiwa mwaka 2026 linatokana na kupanda kwa bei za nishati na chakula kufuatia athari za mgogoro wa Mashariki ya Kati. Aidha, mwenendo wa mfumuko wa bei unatofautiana kutokana na tofauti katika athari za mabadiliko ya kiwango cha ubadilishaji wa fedha kwenye bei za ndani, kuendelea kwa shinikizo la bei katika sekta ya huduma, hali ya masoko ya ajira na mazingira mahususi ya kila nchi.

2.2.4 Mfumuko wa Bei wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara

Kwa mujibu wa taarifa ya IMF ya Oktoba 2026, nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 12.6 mwaka 2025. Hali hiyo ya mfumuko wa bei ilitokana na sababu mbalimbali ikiwemo athari za kushuka kwa thamani ya fedha pamoja na uzalishaji usioridhisha katika shughuli za kilimo. Nchi zilizokuwa na mfumuko wa bei wa juu ni pamoja na Sudan Kusini (asilimia 97.6), Zimbabwe (asilimia 81.4), Burundi (asilimia 34), Malawi (asilimia 28.4), Nigeria (asilimia 23.0) na Angola (asilimia 20.2). Mfumuko wa bei katika ukanda huo unakadiriwa kupungua zaidi hadi asilimia 8.6 mwaka 2026 na 2027.

Aidha, wastani wa mfumuko wa bei katika nchi za SADC ulipungua hadi asilimia 10.5 mwaka 2025 kutoka asilimia 22.4

mwaka 2024. Mfumuko wa bei katika ukanda huo unakadiriwa kupungua zaidi hadi asilimia 6.1 mwaka 2026 na kuongezeka hadi asilimia 6.2 mwaka 2027 (**Jedwali Na. 2.1**)

Jedwali Na. 2.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

Nchi/ Miaka	2024	2025	2026 (Maoteo)	2027 (Maoteo)
Angola	28.2	20.2	10.6	10.2
Botswana	2.8	2.8	7.2	7.4
Comoros	5	3.2	4.0	3.2
DRC*	17.7	7.4	4.3	7.4
Eswatini	4	3.1	2.9	3.2
Lesotho	5.2	4.4	4.6	3.9
Madagascar	7.6	8	8.4	8
Malawi	32.2	28.4	21.9	25
Mauritius	3.6	3.7	4.7	5.5
Namibia	4.2	3.5	4.1	4.2
Mozambique	3.2	4.4	5.6	6.8
Seychelles	0.3	0.3	0.9	2.3
Afrika ya Kusini	4.4	3.2	4.4	3.9
Tanzania	3.1	3.3	4.0	4.2
Zambia	15	13.9	8.0	7.5
Zimbabwe	736.1	81.4	4.0	5

***Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo
Chanzo: Shirika la Fedha Duniani - IMF.

2.2.5 Mfumuko wa Bei katika Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki Mfumuko wa bei katika nchi za EAC uliendelea kutofautiana mwaka 2025. Sudani Kusini ilirekodi kiwango cha juu zaidi cha wastani wa mfumuko wa bei cha asilimia 97.6, ikilinganishwa na asilimia 99.8 mwaka 2024. Nchi hiyo ilifuatiwa na Burundi ambapo mfumuko wa bei uliongezeka kutoka asilimia 20.2 mwaka 2024 hadi

asilimia 34 mwaka 2025. Katika nchi nyingine wanachama, mfumuko wa bei ulikuwa DRC (asilimia 7.4), Rwanda (asilimia 7.0), Kenya (asilimia 4.1), na Uganda (asilimia 3.6). Tanzania imeendelea kudumisha utulivu wa bei, ambapo mwaka 2025 mfumuko wa bei umefikia wastani wa asilimia 3.3. Utulivu huu ulichangiwa na utekelezaji wa sera thabiti za fedha, utulivu wa soko la chakula na kupungua kwa bei za bidhaa katika masoko ya kimataifa. Hali hii inaonesha tofauti ya hali ya kiuchumi ndani ya ukanda wa EAC. Hata hivyo, baadhi ya nchi zinakabiliwa na shinikizo kubwa la bei na nyingine zimeendelea kudumisha uthabiti wa bei.

Jedwali Na. 2.2: Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Mwaka 2022 - 2025 na Maoteo kwa mwaka 2026

Nchi/ Miaka	2024	2025	2026 (Maoteo)	2027 (Maoteo)
Burundi	20.2	34	10.5	12.2
DRC*	17.7	7.4	4.3	7.4
Kenya	4.5	4.1	6.0	5.0
Rwanda	4.8	7	12.3	7.9
Sudani Kusini	99.8	97.6	27.6	28.3
Tanzania	3.1	3.3	4.0	4.2
Uganda	3.3	3.6	4.2	5.3
Wastani	19.9	20.2	7.2	10.043

*Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo **Chanzo:** Shirika la Fedha Duniani – IMF

Katika kipindi cha kufikia Juni 2026, mfumuko wa bei katika nchi wanachama wa EAC kwa ujumla uliendelea kuwa ndani ya kiwango cha mtangamano kilichowekwa isipokuwa Rwanda. Aidha, nchi zote wanachama zilishuhudia ongezeko la mfumuko wa bei hali iliyochangiwa kwa kiasi kikubwa na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia kufuatia mgogoro wa Mashariki ya Kati.


Kielelezo 2.3: Mfumuko wa Bei katika Nchi Teule za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kipindi cha kufikia Juni 2026

2.3 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa

2.3.1 Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Taifa

Uchumi umeendelea kuonesha ukuaji mzuri, ambapo Pato la Taifa halisi lilikua kwa asilimia 5.9 mwaka 2025, ikilinganishwa na asilimia 5.6 mwaka 2024 (**Kielelezo Na. 2.3**). Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi; kuboreshwa kwa miundombinu ya usafirishaji; kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo na madini; kuongezeka kwa shughuli za ujenzi; pamoja na kuendelea kwa utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya Serikali na uwekezaji wa sekta binafsi, hususan katika sekta za nishati, usafirishaji na huduma za jamii.


Kielelezo 2.3: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Taifa, Mwaka 2021 - 2025



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2025, shughuli za kiuchumi zilizoongoza kwa ukuaji ni fedha na bima asilimia 15.7, uzalishaji umeme (asilimia 11.8) pamoja na uchimbaji madini na mawe (asilimia 9.4). Shughuli za kilimo ziliongoza kwa kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa kwa kuchangia asilimia 24.3, ikifuatiwa na ujenzi (asilimia 11.9), madini (asilimia 10.3), biashara na matengenezo (asilimia 8.6), na usafirishaji na uhifadhi mizigo (asilimia 8.3) (Kielelezo Na. 2.4).


Kielelezo 2.4: Mchango wa Baadhi ya Shughuli za Kiuchumi Katika Pato la Taifa, Mwaka 2021-2025



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Katika robo ya kwanza ya mwaka 2026, Pato la Taifa halisi lilikua kwa asilimia 6.0, ikilinganishwa na asilimia 4.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2025 (Kielelezo Na. 2.5). Muundo wa uchumi uliendelea kuwa kwa kiasi kikubwa bila mabadiliko, ambapo shughuli za kilimo na ujenzi kwa pamoja zilichangia takriban theluthi moja ya Pato la Taifa. Ukuaji wa uchumi katika kipindi hicho ulichangiwa zaidi na shughuli za kilimo na huduma za fedha na bima, ambazo zilichangia ukuaji kwa asilimia 16.8 na asilimia 16.7 mtawalia. Huduma za fedha na bima ziliongoza kwa kuwa na kiwango cha juu zaidi cha ukuaji cha asilimia 20.5 kutokana na kuendelea kuongezeka kwa matumizi ya bidhaa na huduma za kifedha, zikifuatiwa na huduma za afya na ustawi wa jamii zilizokua kwa asilimia 13.1 na elimu kwa asilimia 11.3. Tathmini ya mwenendo wa Pato la Taifa katika robo ya kwanza na mwenendo wa viashiria vingine vya uchumi katika nusu ya kwanza ya mwaka 2026 inaonesha kuwa uchumi unaendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha. Hivyo, uchumi unatarajiwa kukua kwa makadirio ya asilimia 6.3 mwaka 2026 na asilimia 6.6 mwaka 2027 kulingana na mwelekeo uliowekwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27-2030/31).

Kielelezo Na. 2.5: Mwenendo wa Uchumi wa Taifa kwa Robo ya Kwanza ya Mwaka 2026




Chanzo: Wizara ya Fedha

2.3.2 Mfumuko wa Bei Nchini

Mfumuko wa bei nchini uliendelea kubaki katika kiwango cha chini na himilivu katika mwaka 2025/26, ambapo ulifikia wastani wa asilimia 3.6 ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2024/25 (Kielelezo Na. 2.6). Mwenendo huo ulichangiwa na utekelezaji wa sera thabiti za kibajeti na fedha, pamoja na kupungua kwa kasi ya ongezeko la bei za bidhaa zisizo za chakula. Hata hivyo, katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2026, mfumuko wa bei ulivuka asilimia 4.0 kwa mara ya kwanza tangu Mei 2023, kutokana zaidi na kuongezeka kwa bei za nishati katika soko la dunia kufuatia kuongezeka kwa migogoro Mashariki ya Kati. Mabadiliko ya bei za nishati duniani yaliathiri bei za mafuta katika soko la ndani na kuongeza bei za bidhaa na huduma nyingine, hususan kupitia ongezeko la gharama za usafirishaji. Aidha, mwezi Agosti, 2026 mfumuko wa bei ulifikia asilimia 4.3.

Pamoja na ongezeko hilo, mfumuko wa bei uliendelea kuwa ndani ya lengo la kitaifa la muda wa kati la asilimia 3.0 hadi 5.0, wigo wa mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki usiozidi asilimia 8.0, na kigezo cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika cha asilimia 3.0 hadi 7.0.

Kielelezo Na. 2.6: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Nchini, Mwaka 2023 hadi 2026.



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)

2.3.3 Sekta ya Nje

Sekta ya nje iliendelea kuwa himilivu mwaka 2025/26 licha ya changamoto katika mazingira ya uchumi wa dunia. Kuendelea kwa mgogoro wa Mashariki ya Kati kuliongeza shinikizo katika bei za nishati na gharama za usafirishaji wa mizigo. Pamoja na changamoto hizo, mauzo ya bidhaa na huduma nje yaliendelea kukua kwa kasi, yakichangiwa na bei nzuri ya dhahabu katika soko la dunia, kuendelea kuimarika kwa sekta ya utalii na kuongezeka kwa biashara ya kikanda. Hata hivyo, uagizaji wa bidhaa na huduma uliongezeka kwa kasi kuliko mauzo ya nje kutokana na mahitaji makubwa ya malighafi za viwandani, bidhaa za petroli na bidhaa za mitaji, pamoja na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji. Kutokana na mwenendo huo, nakisi ya urari wa malipo

ya kawaida iliongezeka kwa asilimia 8.8, kutoka dola za Marekani milioni 2,178.9 mwaka 2024/25 hadi dola za Marekani milioni 2,370.4 mwaka 2025/26.

Mwaka 2026/27, nakisi ya urari wa malipo ya kawaida inatarajiwa kupungua hadi asilimia 2.4 ya Pato la Taifa kutoka asilimia 2.5 mwaka 2025/26, na kufikia wastani wa asilimia 2.3 katika kipindi cha muda wa kati. Matarajio hayo yanatokana na uagizaji wa bidhaa na huduma kutarajiwa kukua kwa kasi ndogo ikilinganishwa na mauzo ya bidhaa na huduma nje. Mauzo ya nje yanatarajiwa kuendelea kuimarika kutokana na bei nzuri ya dhahabu, kuongezeka kwa mapato ya utalii na kupanuka kwa biashara ya kikanda. Mwenendo huo unatarajiwa kupunguza shinikizo katika urari wa malipo ya kawaida na kuimarisha ustahimilivu wa sekta ya nje katika kipindi cha muda wa kati.

(a) Mwenendo wa Mauzo ya Bidhaa Nje na Mapato ya Huduma

Mwaka 2025/26, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 15.5 na kufikia dola za Marekani milioni 19,625.0, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 16,987.0 mwaka 2024/25. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuimarika kwa mauzo ya dhahabu, mapato ya huduma za utalii, bidhaa za viwandani na bidhaa asilia, hususan tumbaku, korosho na kahawa.

Katika kipindi hicho, mauzo ya dhahabu nje ya nchi yalifikia dola za Marekani milioni 5,578.9, sawa na ongezeko la asilimia 37.8 ikilinganishwa na mwaka 2024/25. Dhahabu iliendelea kuwa chanzo kikuu cha mapato ya mauzo ya bidhaa na huduma nje kwa kuchangia asilimia 28 ya mapato yote ya mauzo ya nje. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na bei nzuri ya dhahabu katika soko la dunia na kuimarika kwa mauzo ya bidhaa za viwandani na bidhaa asilia hususan tumbaku, korosho na kahawa.

Mapato yatokanayo na huduma zinazotolewa nje yaliongezeka kwa asilimia 12.0 na kufikia dola za Marekani milioni 7,971.5 mwaka 2025/26, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 7,115.4 mwaka 2024/25. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kuimarika kwa mapato ya huduma za utalii, ambayo yaliongezeka

kwa asilimia 5. Mwenendo huo uliendana na ongezeko la asilimia 4.5 la idadi ya watalii walioingia nchini na kufikia watalii 2,291,479 mwaka 2025/26.

Mwaka 2026/27, uwiano wa mauzo ya bidhaa na huduma nje kwa Pato la Taifa unatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 21.1 kutoka asilimia 20.3 mwaka 2025/26. Ongezeko hilo linatarajiwa kuchangiwa na kuendelea kuimarika kwa sekta ya utalii na mauzo ya dhahabu, pamoja na kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji viwandani kufuatia kukamilika kwa Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) na kuongezeka kwa upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa shughuli za uzalishaji. Aidha, uwiano wa mauzo ya bidhaa na huduma nje kwa Pato la Taifa unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 20.4 katika kipindi cha muda wa kati.

(b) Mwenendo wa Uagizaji wa Bidhaa na Huduma

Thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka kwa asilimia 15.1 mwaka 2025/26 na kufikia dola za Marekani milioni 20,285.7, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 17,629.8 mwaka 2024/25. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa uagizaji wa vifaa vya usafirishaji kwa ajili ya shughuli za viwandani, mitambo na vifaa vya kimakanika, malighafi za viwandani na bidhaa za petroli. Katika kipindi hicho, thamani ya bidhaa pekee zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka kwa asilimia 16.5 na kufikia dola za Marekani milioni 16,858.1, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 14,465.9 mwaka 2024/25.

Malipo ya huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 8.3 na kufikia dola za Marekani milioni 3,427.5 mwaka 2025/26, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,163.9 mwaka 2024/25. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kupanda kwa malipo ya usafirishaji wa mizigo, sambamba na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje.

Mwaka 2026/27, uwiano wa uagizaji wa bidhaa na huduma kwa Pato la Taifa unatarajiwa kubaki katika asilimia 21.0, sawa na kiwango cha mwaka 2025/26. Katika kipindi cha muda wa kati, uwiano huo unatarajiwa kupungua hadi wastani wa asilimia 19.9 kutokana na uagizaji wa bidhaa na huduma kutarajiwa kukua kwa

kasi ndogo baada ya kukamilika kwa baadhi ya miradi mikubwa ya kimkakati.

2.3.4 Akiba ya Fedha za Kigeni

Hadi Agosti 2026, akiba rasmi ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,888.2. Kiasi hicho kilitosheleza kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi 4.2, kiwango ambacho kilikuwa juu ya lengo la nchi la kuwa na akiba inayotosheleza uagizaji kwa angalau miezi minne. Utoshelevu wa akiba hiyo ulichangiwa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi pamoja na kuendelea kutekelezwa kwa programu ya Benki Kuu ya ununuzi wa dhahabu katika soko la ndani.

2.3.5 Sekta ya Fedha

Katika mwaka 2026/27, Benki Kuu inatarajia kutekeleza sera ya fedha inayolenga kupunguza ukwasi ili kudhibiti athari za awamu ya pili za kupanda kwa bei za bidhaa duniani, sambamba na kuendeleza mageuzi ya kuelekea uchumi unaopunguza matumizi ya fedha taslimu (cash-lite economy) na kuongeza ujumuishaji wa kifedha. Sanjari na hili, mnamo mwezi Julai 2026, Kamati ya Sera ya Fedha iliamua kuongeza Kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) kutoka asilimia 5.75 ya mwezi Juni 2026 hadi asilimia 6.25 kwa robo mwaka inayoishia Septemba 2026 kabla ya kuamua kutokubadili riba hiyo katika kikao kilichofanyika mwezi Oktoba 2026. Uamuzi huu unalenga kudhibiti athari zinazoweza kutokana na ongezeko la bei za mafuta, mbolea na gharama za usafirishaji kutokana na mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati. Kwa muktadha huo, utekelezaji wa sera ya fedha umeendelea kuhakikisha riba ya mikopo ya siku saba baina ya mabenki (7-day IBCM rate) inabaki ndani ya wigo wa asilimia 4.75 hadi asilimia 7.75, sawa na asilimia 1.5 juu au chini ya Riba ya Benki Kuu.

Hadi kufikia mwezi Septemba 2026, utekelezaji wa sera ya fedha ulikuwa wa kuridhisha, huku ukihakikisha uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi katika sekta ya kibenki. Hali hii iliakisiwa na mwenendo wa riba ya mikopo ya siku saba baina ya mabenki ambayo ilikuwa tulivu ikiwa, na ndani ya wigo unaokubalika. Aidha,


Benki Kuu imeendelea kusimamia ukwasi katika mfumo wa kibenki kwa kutumia mikopo ya muda mfupi "reverse repo" na mauzo ya dhamana za serikali za muda mfupi.

(a) Viwango vya Riba

Katika mwaka 2025/26, riba za mikopo na amana zilibaki bila mabadiliko makubwa ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Wastani wa riba za mikopo ulipungua hadi asilimia 15.19 kutoka asilimia 15.42 mwaka 2024/25. Mwenendo huo uliakisi utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kuongeza ukwasi katika mzunguko wa fedha. Aidha, wastani wa riba za amana uliongezeka hadi asilimia 8.49 kutoka asilimia 8.22 mwaka 2024/25. Kutokana na mwenendo huo, tofauti kati ya wastani wa riba za mikopo na amana ilipungua hadi nukta za asilimia 6.70 mwaka 2025/26 kutoka nukta za asilimia 7.20 mwaka 2024/25, hali inayoashiria kupungua kwa kiasi kwa gharama za mikopo ikilinganishwa na mapato yatokanayo na amana (**Kielelezo 2.7**).

(b) Viwango vya Riba

Kielelezo Na. 2.7: Wastani wa Viwango vya Riba za Mikopo na Amana



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania


(c) Mikopo kwa Sekta Binafsi

Katika mwaka ulioishia Juni 2026, mikopo iliyotolewa na benki za biashara kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 21.1, ikilinganishwa na asilimia 15.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Hadi kufikia mwezi Agosti 2026, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 33, ikilinganishwa na asilimia 28.1 ya mwezi Juni, 2026. Ongezeko hilo liliakisi utekelezaji wa sera za fedha na bajeti zinazochochea shughuli za kiuchumi, pamoja na kuendelea kuimarika kwa shughuli za uzalishaji na biashara nchini.


Katika mwaka 2025/26, mikopo iliyoelekezwa katika shughuli za uchimbaji wa madini na mawe iliongoza kwa kukua kwa asilimia 45.2, hali iliyochangiwa zaidi na utekelezaji wa jitihada za Serikali za kuboresha upatikanaji wa fedha kwa wachimbaji wadogo na wa kati. Mikopo kwa shughuli za biashara, uchukuzi na mawasiliano, pamoja na kilimo, pia ilikua kwa zaidi ya asilimia 30 kwa kila shughuli. Aidha, mikopo kwa watu binafsi, ambayo kwa sehemu kubwa hutumika kugharamia shughuli za uzalishaji za biashara ndogo na za kati, iliendelea kuchukua sehemu kubwa zaidi ya mikopo kwa sekta binafsi kwa kuchangia asilimia 35.5, ikifuatiwa na biashara kwa asilimia 14.5 na kilimo kwa asilimia 13.7. **Kielelezo Na. 2.9** kimeainisha mchanganuo wa mikopo kwa sekta binafsi.

Kielelezo Na. 2.9a: Mchanganuo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi

Chanzo: Benki kuu ya Tanzania



Kielelezo Na. 2.9b: Mchanganuo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi



Chanzo: Benki kuu ya Tanzania

(d) Ukwasi na Faida za Biashara katika Benki

Hali ya ukwasi katika sekta ya benki iliendelea kuwa ya kuridhisha na juu ya kiwango cha chini kinachohitajika kisheria. Uwiano wa ukwasi (Liquidity Coverage Ratio - LCR) ulikuwa asilimia 232.86 Juni 2026, ikilinganishwa na asilimia 255.24 Juni 2025, na hivyo kuendelea kuwa juu ya kiwango cha chini cha kisheria cha asilimia 100. Aidha, uwiano wa mtaji wa msingi kwa rasilimali zilizopimwa kwa vihatarishi pamoja na shughuli zilizo nje ya mizania ulikuwa asilimia 18.57 Juni 2026, ikilinganishwa na asilimia 18.69 Juni 2025, na kuendelea kuwa juu ya kiwango cha chini cha kisheria cha asilimia 10. Hali hii inaonesha kuwa benki zilikuwa na ukwasi na mtaji wa kutosha kugharamia shughuli zake za kila siku, ikiwemo kutoa mikopo.

Mapato ya benki yatokanayo na rasilimali (Return on Assets - ROA) yalikuwa asilimia 4.88 Juni 2026, ikilinganishwa na asilimia 5.36 Juni 2025. Vilevile, mapato yatokanayo na mtaji (Return on Equity - ROE) yalikuwa asilimia 23.29 Juni 2026, ikilinganishwa na asilimia

24.96 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Pamoja na kupungua kwa kiasi kwa viashiria hivyo vya faida, sekta ya benki iliendelea kuwa himilivu na yenye uwezo wa kutengeneza faida.

2.3.6 Deni la Serikali

Hadi kufikia Juni 2026, deni la Serikali Kuu lilifikia shilingi bilioni 117,384.01 kutoka shilingi bilioni 109,441.30 mwezi Juni 2025, sawa na ongezeko la asilimia 7.2. Kati ya kiasi hicho, deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 78,058.16, sawa na asilimia 66.5 ya deni lote, na deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 39,325.85. Ongezeko la deni lilitokana na mikopo mipya kuzidi marejesho ya mikopo iliyoiva, pamoja na kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani.

Uhimilivu wa Deni

Tathmini ya uhimilivu wa deni ya Novemba 2025 ilionesha kuwa deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda wa kati na mrefu. Katika mwaka 2025/26, thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ilikuwa asilimia 24.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ilikuwa asilimia 123.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180; malipo ya deni la nje kwa mapato yatokanayo na mauzo ya nje yalikuwa asilimia 12.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 15; na malipo ya deni la nje kwa mapato ya ndani yalikuwa asilimia 15.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 18. Aidha, thamani ya sasa ya jumla ya deni la ndani na nje kwa Pato la Taifa ilikuwa asilimia 39.6 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55.

Uwezo wa Nchi Kukopa na Kulipa Madeni katika Masoko ya Kimataifa

Mwezi Februari 2026, Moody's Ratings iliendelea kuipa Tanzania daraja la B1 lenye mtazamo thabiti (Stable Outlook), kutokana na ukuaji imara wa uchumi, uthabiti wa mfumuko wa bei, maboresho katika usimamizi wa sera za uchumi na deni la Serikali linaloendelea kuwa himilivu. Aidha, mwezi Agosti 2026, Fitch Ratings iliithibitisha Tanzania katika daraja la B+ na kuboresha mtazamo wa nchi kutoka thabiti (Stable) kwenda chanya

(Positive), kutokana na kuimarika kwa uhimilivu wa deni la umma na sekta ya nje, pamoja na kuboreka kwa mtazamo na uaminifu wa sera za uchumi. Matokeo hayo yanaweza kuimarisha imani ya wawekezaji na wakopeshaji kuhusu uthabiti wa uchumi na uwezo wa Serikali kuhudumia deni, na hivyo kuboresha upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

2.3.7 Demografia na Maendeleo ya Watu

2.3.7.1 Demografia

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) idadi ya watu inakadiriwa kufikia milioni 67.9 mwaka 2026 na milioni 69.7 mwaka 2027 kwa Tanzania Bara. Kasi ya ongezeko la idadi ya watu inatoa fursa chanya zikiwemo uwepo wa nguvu kazi ya kutosha pamoja na misingi ya kuchochea mageuzi ya kidigitali katika shughuli mbalimbali za uzalishaji kutokana na uwepo wa kundi kubwa la vijana wenye umri wa miaka 15-35 ambao ni asilimia 33.7 ya watu wote Tanzania Bara kwa mwaka 2027. Aidha, ongezeko hili linaashiria uhitaji wa kuwekeza zaidi katika huduma za kijamii pamoja na mageuzi katika mifumo mbalimbali ya elimu na utendaji pamoja na kutekeleza mikakati mahsusi ya kuwawezesha vijana kuzalisha kwa tija. Utekelezaji wa mikakati hii utawezesha rasilimali watu ya nchi kuwa shindani kimataifa hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi.

2.3.7.2 Hali ya Umaskini Nchini

Serikali imeendelea kutekeleza hatua mbalimbali zinazolenga kuimarisha ustawi wa jamii, kupunguza umaskini na kuongeza fursa za kiuchumi kwa wananchi. Hatua hizo zinajumuisha kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za msingi, hususan maji, elimu na afya; kuendeleza miundombinu ya nishati, usafiri na barabara; pamoja na kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji na kupata fursa za kiuchumi ili kufikia shabaha za FYDP IV za kupunguza kiwango cha umaskini hadi chini ya asilimia 15 ifikapo mwaka 2030/31.

Taarifa ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi Tanzania wa mwaka 2025 inabainisha kuwa asilimia 24.9 ya watu

nchini wanaishi katika umaskini wa mahitaji ya msingi. Kiwango hicho ni asilimia 25.1 kwa Tanzania Bara na asilimia 19.9 kwa Tanzania Zanzibar. Kwa Tanzania Bara, kiwango cha umaskini kimepungua kutoka asilimia 34.4 mwaka 2007 hadi asilimia 28.2 (mwaka 2012), asilimia 26.4 (mwaka 2017/18) na asilimia 25.1 (mwaka 2025). Aidha, kiwango cha umaskini ni kikubwa zaidi vijijini ambapo asilimia 30.7 ya watu wa Tanzania Bara wanaishi katika umaskini wa mahitaji ya msingi, ikilinganishwa na asilimia 14.8 mijini. Kwa upande wa kina cha umaskini, pengo la umaskini (poverty gap) nchini ni asilimia 6.2 na ukali wa umaskini (poverty severity) ni asilimia 2.2. Vile vile, utafiti unaonesha kuwa utofauti wa kipato na matumizi bado ni mkubwa, ambapo kipimo cha gini ni 0.42 nchini, ambapo Tanzania Bara (0.41) na Tanzania Zanzibar (0.44). Matokeo haya yanaonesha umuhimu wa kuchochea ukuaji wa uchumi jumuishi, kuongeza ajira zenye tija na kipato, pamoja na kuongeza tija katika kilimo na shughuli nyingine za uchumi vijijini. Afua hizi ni muhimu ili kuwezesha Tanzania kufikia lengo lililowekwa katika DIRA 2050 la kuondoa umaskini uliokithiri na kupunguza umaskini wa mahitaji ya msingi kuwa chini ya asilimia 5.

2.3.7.3 Ajira

Matokeo ya Utafiti wa Watu wenye Uwezo wa Kufanya Kazi – ILFS wa mwaka 2025 yanabainisha kuwa, kiwango cha Ushiriki wa Nguvu kazi (Labour Force Participation Rate) kimefikia asilimia 75.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 73.2 mwaka 2024. Idadi kubwa ya nguvu kazi ikiwa imeajiriwa kwa masharti ya muda (dependent contractors) kwa asilimia 51.5 na asilimia 13.2 zikiwa ni ajira zenye ujira wa kulipwa mishahara. Sekta ya Kilimo imeendelea kuwa uti wa mgongo kwa kuajiri takriban asilimia 54.4 ya nguvu kazi mwaka 2025 ikifuatiwa na sekta ya huduma (asilimia 35.5), na kiwango cha nguvu kazi kilichoajiriwa katika sekta ya viwanda ni asilimia 10.1 mwaka 2025.

Kwa upande wa kiwango cha ukosefu wa ajira kimepungua na kufikia asilimia 5.9 mwaka 2025, ukilinganisha na asilimia 6.2 mwaka 2024. Aidha, kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana

(miaka 15 – 35) kimepungua hadi asilimia 7.5 mwaka 2025 kutoka asilimia 8.1.

2.3.7.4 Maendeleo ya Watu

Serikali imeendelea na jitihada za kuboresha maendeleo ya watu kwa lengo la kuimarisha maisha ya watu ili kufikia matamanio yaliyoainishwa katika Dira 2050. Juhudi hizo ni pamoja na: kuendelea kutoa elimu bila ada; kuendelea kuboresha upatikanaji wa maji mijini na vijijini; kuendelea kuboresha ushiriki wa sekta binafsi katika kutoa huduma za afya hususan maeneo ya vijijini; kuendelea na ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali; na kuendelea na ujenzi wa barabara za kufungua fursa za kiuchumi katika maeneo ya mijini na vijijini. Kutokana na utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo, kumekua na matokeo chanya katika viashiria vya maendeleo ya watu 1 ikiwemo:

(i) Kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 68.0 mwaka 2024 hadi miaka 68.3 mwaka 2025. Aidha, wastani wa umri wa kuishi kwa kuzingatia jinsia, umefikia miaka 70.7 kwa wanawake na miaka 65.9 kwa wanaume mwaka 2025; Hii ni kwa mujibu wa makadirio yaliyotakana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022;

(ii) Kupungua kwa vifo vya watoto wa umri chini ya miaka mitano na kufikia vifo 43 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2022 kutoka vifo 81 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2019/20;

(iii) Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2019/20 hadi vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022;

(iv) Kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya sekondari kutoka asilimia 47.4 mwaka 2021 hadi asilimia 53.1 mwaka 2025;

(v) Kuongezeka kwa idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba kama chanzo kikuu kutoka asilimia 72.3 mwaka 2020/21 hadi asilimia 83 mwaka 2024/25;

(vi) Kuunganishwa na huduma ya umeme kwa vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara mwaka 2026/27 na kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa kuunganisha vitongoji vyote nchini;

(vii) Fahirisi ya maendeleo ya watu imefikia 0.556 mwaka 2024 kutoka 0.529 mwaka 2019, fahirisi hii inaashiria kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za jamii za muhimu kama vile afya, elimu na maji pamoja na kuimarika kwa kiwango cha maisha. Hii ni kwa mujibu wa taarifa za UNDP.

2.4 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2027/28

Uchumi wa Tanzania unatarajiwa kuendelea kukua kwa wastani wa asilimia 6.3 mwaka 2026 na asilimia 6.6 kwa mwaka 2027. Ukuaji huu utachangiwa na uwekezaji katika sekta za mageuzi na maeneo yanayochochea mageuzi ya kiuchumi ili kufikia malengo ya Dira 2050. Hili kufikia matarajio ya ukuaji wa uchumi Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2027/28 yanajielekeza katika maeneo sita (6) mahsusi:

(i) Kujenga Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani;

(ii) Mageuzi katika sekta za Kimkakati

(iii) Kujenga uwezo wa Rasimali Watu na Maendeleo ya Jamii;

(iv) Kuhifadhi mazingira na kujenga ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi;

(v) Kutumia kikamilifu vichocheo vya maendeleo; na

(vi) Kuimarisha Misingi ya Uendelevu wa Taifa.

2.4.1 Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi Jumla

Malengo na shabaha za msingi za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 6.3 na 6.6 kwa mwaka 2026 na 2027 mtawalia, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.9 kwa mwaka 2025;

(ii) Kudhibiti mfumuko wa bei kubaki katika wigo wa asilimia 3.0 – 5.0 katika kipindi cha muda wa kati, ili kulinda uwezo wa wananchi kumudu mahitaji muhimu;

(iii) Kuongeza mapato ya ndani kufikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa mwaka 2027/28, kutoka asilimia 17.0 mwaka 2026/27;

(iv) Kuongeza mapato ya kodi kufikia asilimia 13.9 ya Pato la Taifa mwaka 2027/28, kutoka asilimia 13.8 mwaka 2026/27;

(v) Kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa mwaka 2027;

(vi) Kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na

(vii) Kuongeza uzalishaji wa wastani wa ajira 1,700,000 kwa mwaka 2027.

Maoteo ya ajira zinazotarajiwa kuzalishwa mwaka 2027/28 yanaonesha kuwa kati ya lengo la ajira mpya milioni 1.7, sekta ya kilimo, misitu, na uvuvi inatarajiwa kuongoza kwa kuzalisha ajira 935,000 sawa na asilimia 55 ya ajira zote; ikifuatiwa na biashara jumla, rejareja pamoja na matengenezo ya magari na pikipiki (261,800); Utengenezaji (91,800); Huduma za malazi na chakula (78,200); Usafirishaji na uhifadhi (74,800). Kwa ujumla, maoteo haya yanaakisi mabadiliko ya kimuundo yanayolenga kukuza ajira kupitia sekta za kimageuzi na huduma zenye athari pana katika uchumi.

Jedwali Na. 2.3: Mchanganuo wa Maoteo ya Fursa za Ajira Zitakazozalishwa katika Mwaka 2027/28

Shughuli za Kiuchumi	Idadi	Asilimia
Kilimo, misitu na uvuvi	935,000	55.00
Uchimbaji wa madini na michanga	20,400	1.20
Utengenezaji	91,800	5.40
Umeme, gesi, mvuke na viyoyozi	3,400	0.20
Usambazaji wa maji, majitaka, na usimamizi wa taka	1,700	0.10
Ujenzi	51,000	3.00
Biashara jumla, rejareja pamoja na matengenezo ya magari na pikipiki	261,800	15.40
Usafirishaji na uhifadhi	74,800	4.40
Huduma za malazi na chakula	78,200	4.60
Habari na mawasiliano	4,250	0.25
Shughuli za kifedha na bima	8,840	0.52
Shughuli za mali isiyohamishika	1,700	0.10
Shughuli za kitaalamu, kisayansi na uhandisi	3,230	0.19
Shughuli za utoaji wa huduma mbalimbali	52,700	3.10
Utawala wa umma na ulinzi na shughuli za hifadhi ya jamii	8,500	0.50
Elimu	30,600	1.80
Afya ya binadamu na shughuli za kijamii	12,070	0.71
Sanaa burudani na starehe	5,100	0.30
Shughuli nyingine za utoaji wa huduma	12,410	0.73
Shughuli za kaya kama muajiri	42,500	2.50
Jumla	**1,700,000**	**100.00**

2.4.2 Misingi ya Mpango kwa Mwaka 2027/28

Ufanisi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2027/28 utajengwa katika misingi ifuatayo:

(i) Kuendelea kuwepo kwa demokrasia, amani, usalama na utulivu wa ndani na katika nchi jirani, inayowezesha shughuli za kiuchumi, kijamii na uwekezaji kustawi;

(ii) Kudumisha misingi ya utawala bora na utawala wa sheria, ikiwa ni pamoja na uwajibikaji, uadilifu, uwazi na ufanisi katika matumizi bora na endelevu ya rasilimali za umma;

(iii) Kuendeleza miundombinu wezeshi hususan nishati, bandari, barabara na reli kwa ili kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara, viwanda na usafirishaji katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na Kusini;

(iv) Kuimarika kwa ubunifu na matumizi ya teknolojia za kidijitali katika huduma za kijamii na uzalishaji;

(v) Utekelezaji wa mageuzi ya kitaasisi na kiutawala ili kuongeza ufanisi, uwazi, uwajibikaji na tija katika utekelezaji wa majukumu;

(vi) Kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji na biashara kupitia ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na fursa zinazotokana na ushirikiano wa kikanda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika;

(vii) Kuendelea kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, majanga ya asili na yasiyo ya asili, ikiwemo ukame, mafuriko, milipuko ya magonjwa, migogoro ya kikanda na misukosuko ya kiuchumi duniani;

(viii) Kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa;

(ix) Kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini; na

(x) Kuwepo kwa mifumo thabiti ya uratibu, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha kuwa programu, miradi na afua zilizopangwa zinatekelezwa kwa wakati na kuleta matokeo yanayotarajiwa.

SURA YA TATU

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO

3.1 Utangulizi

Sura hii inaainisha mapitio ya utekelezaji wa Mpango ambayo yanalenga kupima hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa afua, programu na miradi iliyopangwa, kwa lengo la kubaini mafanikio na maeneo yanayohitaji hatua za ziada, pamoja na kuweka msingi wa vipaumbele vya Mpango wa mwaka 2027/28. Mapitio ya utekelezaji wa Mpango yamegawanyika katika sehemu kuu mbili (02) ambazo ni sehemu A na sehemu B. Sehemu A inahusu mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2025/26 ambao ni Mpango wa Tano na wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III). Vilevile, Mpango wa Mwaka 2025/26 ni Mpango wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Aidha, Sehemu B inahusu mapitio ya robo ya kwanza (Julai – Septemba 2026) ya Mpango wa Mwaka 2026/27 ambao ni Mpango wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV) na ni Mpango wa Kwanza wa mwaka katika utekelezaji wa Dira 2050.

SEHEMU A: UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA 2025/26

Sehemu hii inaeleza mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26. Mapitio hayo yamejikita katika miradi ya kielelezo na miradi ya kimkakati. Vilevile, sehemu hii inaonesha matokeo ya utekelezaji wa afua na miradi pamoja na viashiria vya mpango kwa kulinganisha hatua iliyofikiwa mwaka 2025/26 na hatua ya utekelezaji kwa mwaka 2024/25.

Miradi ya Kielelezo

Hadi Juni 2026, Serikali ilifanikiwa kukamilisha ufungaji wa mitambo yote tisa (9) ya Bwawa la Julius Nyerere (MW 2,115) na kuunganisha umeme wake katika Gridi ya Taifa; kukamilisha madaraja ya JPM (Kigongo – Busisi) na Tanzanite pamoja na barabara za juu za Uhasibu na Chang'ombe; kukamilisha ujenzi reli

ya SGR kwa vipande vya SGR vya Dar es Salaam – Morogoro (km 300) na Morogoro – Makutupora (km 422); na kukamilika kwa Kiwanda cha Sukari Mkulazi. Miradi ya umeme wa maji ya Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222), kiwanda cha LNG, Mchuchuma na Liganga imeendelea na hatua mbalimbali za maandalizi ya utekelezaji, ambapo hadi kufikia Juni 2026 majadiliano na mwekezaji kuhusu miradi ya Mchuchuma na Liganga yalikuwa yamekamilika, huku mradi wa Magadi Soda Engaruka ukiendelea na mchakato wa kutafuta mwekezaji wa kushirikiana naye katika ujenzi na uendeshaji wa kiwanda unaendelea.

Vilevile, mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la EACOP (km 1,443) utekelezaji wake ulifikia asilimia 86; ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko ulifikia asilimia 97; utafutaji wa mafuta na gesi katika vitalu vya Eyasi – Wembere na Mnazi Bay ulifikia asilimia 40;, miradi iliyosajiliwa katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi iliongezeka kutoka 29 mwaka 2024/25 hadi 35 mwaka 2025/26; na thamani ya uwekezaji katika miradi hiyo ilikuwa Dola za Marekani milioni 430.586 hadi Juni 2026, ikilinganishwa na milioni 430.62 mwaka 2024/25, huku ajira 15,076 zikizalishwa mwaka 2025/26.

3.2 Mageuzi katika Sekta za Kimkakati

3.2.1 Sekta ya Kilimo

Utekelezaji wa Mpango uliwezesha: ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji; upanuzi wa miundombinu ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), ambapo uwezo wa kuhifadhi uliongezeka hadi tani 776,000 mwaka 2025/26, kutoka tani 251,000 mwaka 2024/25; kuimarisha upatikanaji wa pembejeo, huduma za ugani na masoko ya mazao; na kuimarisha vyama vya ushirika, ambapo viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika viliongezeka kutoka 329 mwaka 2024 hadi 336 mwaka 2025, na wanachama wa vyama vya ushirika walipungua hadi kufikia milioni 2.1 mwaka 2025, kutoka milioni 2.8 mwaka 2024. Kupungua kwa wanachama wa ushirika kulitokana na jitihada zilizochukuliwa na Serikali za kutumia mfumo wa kidijitali wa usimamizi wa vyama vya ushirika (MUVU) unaoratibiwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II); Programu ya

Mifumo Himilivu ya Chakula Tanzania (TFSRP); Mradi wa Upatikanaji wa Pembejeo (TAISP); Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT); na Programu ya Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi (AFDP).

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: eneo la kilimo cha umwagiliaji liliongezeka kutoka hekta 727,280.6 mwaka 2024 hadi hekta 983,466.1 mwaka 2025; mchango wa sekta katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 24.3 mwaka 2025, kutoka asilimia 24.9 mwaka 2024; sekta ilikua kwa asilimia 5.5 mwaka 2025, kutoka asilimia 5.1 mwaka 2024; utoshelevu wa chakula ulifikia asilimia 130 mwaka 2025/26, kutoka asilimia 128 mwaka 2024; uzalishaji wa mazao ya chakula ulifikia tani 23,783,128 mwaka 2024/25, mazao ya bustani tani 9,781,236.74 na mazao asili ya biashara tani 1,596,311.18, kutoka tani 17,148,290, 7,304,723 na 973,436, mtawalia, mwaka 2023/24; thamani ya mauzo ya nje ya mazao ya kilimo ilifikia Dola za Marekani bilioni 3.73 mwaka 2025, kutoka bilioni 3.54 mwaka 2024; na upotevu wa mazao baada ya kuvuna ulipungua hadi asilimia 30 mwaka 2025/26, kutoka asilimia 35 mwaka 2024.

3.2.2 Sekta ya Mifugo

Utekelezaji wa Mpango uliwezesha upatikanaji na matumizi ya chanjo za mifugo; ujenzi na ukarabati wa majosho na kuongeza mwitikio wa uogeshaji wa mifugo; upatikanaji wa mbari bora za mifugo ikiwemo madume na mitamba; na kuongeza uzalishaji na uongezaji thamani wa mazao ya mifugo. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Mradi wa Mageuzi ya Tasnia ya Maziwa kwa Kuzingatia Mabadiliko ya Tabianchi (C-SDTP); Mageuzi ya Mifumo ya Chakula Usangu; na Jenga Kesho Iliyo Bora – Vijana na Kilimo Biashara.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: matukio ya vifo vya mifugo yalipungua kwa asilimia 11.5, kutoka 34,029 mwaka 2024/25 hadi 30,109 mwaka 2026; kiwango cha magonjwa ya mifugo kilipungua kutoka asilimia 2.5 Desemba 2024 hadi asilimia 1.8 Desemba 2025; kiwango cha uogeshaji wa mifugo kiliongezeka kutoka asilimia 82 hadi 85, na utoaji wa chanjo uliongezeka na kufikia 70 kutoka asilimia 42 katika kipindi hicho; uzalishaji wa maziwa uliongezeka kutoka lita bilioni 4.1 Desemba

2024 hadi lita bilioni 4.2 Juni 2026; na mauzo ya nyama nje ya nchi yalifikia tani 12,763.77 Juni 2026, ikilinganishwa na tani 13,112.44 mwaka 2024/25.

3.2.3 Sekta ya Uvuvi

Utekelezaji wa Mpango uliwezesha ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko ambao utekelezaji umefikia asilimia 97; upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya uvuvi ikiwemo boti na vizimba; na kuongeza uzalishaji wa vifaranga vya samaki, ambao uliongezeka hadi kufikia 202,657,335 Juni 2026 kutoka vifaranga 140,018,196 mwaka 2024/25. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko; mradi wa TASFAM; Bandari ya Uvuvi Bagamoyo; uhuishwaji wa TAFICO; na Mradi wa Uchumi wa Buluu.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: sekta ilikua kwa asilimia 6.3 mwaka 2025 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.0 mwaka 2024, na mchango wake katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.0 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 2.3 mwaka 2024; uzalishaji wa mazao ya uvuvi uliongezeka na kufikia tani 659,242.69 Juni 2026 kutoka tani 575,000 mwaka 2024/25; hadi Juni 2026 mauzo ya mazao ya uvuvi nje yalifikia tani 37,988.30 zenye thamani ya shilingi bilioni 493.16 ikilinganishwa na tani 52,565.56 kwa mwaka mzima wa 2024/25; na viwanda vikubwa vya kuchakata samaki viliongezeka hadi 64 mwaka 2025 kutoka 25 mwaka 2024, na vidogo 38 kutoka 32.


3.2.4 Sekta ya Viwanda

Utekelezaji wa Mpango uliwezesha kuongeza uzalishaji wa viwandani ikiwemo Kiwanda cha Sukari Mkulazi ambacho kiliongeza uzalishaji hadi tani 26,470 za sukari msimu wa 2025/26, kutoka tani 19,124 msimu wa 2024/25; kulipwa kwa asilimia 98.7 ya fidia kwa mradi wa Magadi Soda Engaruka; na kuongezeka kwa miradi iliyosajiliwa katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi hadi 35 mwaka 2025/26 kutoka 29 mwaka 2024/25, yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 430.6. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Engaruka Soda Ash/Lake Natron; Integrated Industrial Development Programme; Tanzania Mini Tiger Plan; Export

Processing Zone Development; Liganga Vanadium Titanium; na Mchuchuma.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: sekta ilikua kwa asilimia 5.2 mwaka 2025, kutoka asilimia 4.9 mwaka 2024; mchango wa sekta katika Pato la Taifa ulipungua hadi asilimia 5.9 mwaka 2025, kutoka asilimia 6.8 mwaka 2024; watu walioajiriwa viwandani waliongezeka hadi 397,953 mwaka 2025 kutoka 391,275 mwaka 2024; na mauzo ya bidhaa za viwandani yalifikia Dola za Marekani milioni 1,264.6 katika soko la EAC na milioni 3,545 katika soko la SADC mwaka 2025, kutoka milioni 1,160.5 na milioni 2,968.3, mtawalia, mwaka 2024. Kielelezo Na: 3.1

Kielelezo Na.3.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Sekta ya Viwanda na Mchango wake katika Pato la Taifa, 2019 – 2025



Chanzo: Wizara ya Fedha


3.2.5 Sekta ya Ujenzi

Mpango uliwezesha kukamilika kwa madaraja makubwa ya JPM (Kigongo – Busisi) na Tanzanite pamoja na barabara za juu za

Uhasibu na Chang'ombe; kuendelea na ujenzi wa Daraja la Jangwani ambao umefikia asilimia 42; kukamilika kwa madaraja 81 ya dharura yaliyoathiriwa na mvua za El-Nino na Kimbunga Hidaya; na kukamilika kwa ujenzi wa km 243.13 za barabara za lami na km 94.36 za changarawe mwaka 2025/26. Aidha, utekelezaji wa miradi takriban 103 ya barabara uliendelea katika hatua mbalimbali, ikiwemo: barabara ya Tanga – Pangani (km 50) iliyofikia asilimia 77; Tungamaa – Mkange (km 95.2) asilimia 63; daraja la Pangani asilimia 68.85; upanuzi wa Uyole – Ifisi (km 29) asilimia 46; kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mkiu – Mavanga – Madaba (km 112); na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Kigamboni – Chanika – Kibaha – Mbweni (km 77.5). Vilevile, ukarabati na matengenezo yaliendelea katika barabara za Arusha – Moshi – Holili ipo katika hatua ya manunuzi, Mtwara – Mingoyo – Masasi, Lot I asilimia 27.13 na Lot II asilimia 5.3 Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi, Sehemu ya Vikonge – Luhafwe (km 25) asilimia 60.24 na Sehemu ya Luhafwe – Mishamo/Bulamata Jct Section (km 37.35) asimilia 22.6 , Geita – Bulyanhulu – Kahama, asilimia 87, BRT awamu ya (I – V), BRT I Awamu ya kwanza asilimia 83.13, BRT II imekamilika, BRT III awamu ya kwanza imekamilika, awamu ya pili imefikia asilimia 19.12, BRT IV Lot I asilimia 64.24, Lot II asilimia 51.16, Lot III asilimia 35.0 DMDP II, na Uendelezaji wa Bonde la Msimbazi.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: mtandao wa barabara kuu na za mikoa zinazopitika wakati wote uliongezeka hadi km 37,734.41 Juni 2025 kutoka km 37,435 mwaka 2024; sekta ilikua kwa asilimia 4.0 mwaka 2025, kutoka asilimia 3.0 mwaka 2024; mchango wa sekta katika Pato la Taifa ulipungua hadi asilimia 11.9 mwaka 2025, kutoka asilimia 12.5 mwaka 2024; mchango wa kampuni za ndani katika soko la ujenzi uliongezeka hadi asilimia 60 ya thamani ya miradi mwaka 2025/26 kutoka asilimia 40 mwaka 2023; na ajira katika miradi ya ujenzi zilifikia 18,988 hadi Desemba 2025, ikilinganishwa na ajira 21,527 kwa mwaka 2024. Kielelezo Na: 3.2

Kielelezo Na. 3.2: Mwenendo wa Ukuaji wa Sekta ya Ujenzi na Mchango wake katika Pato la Taifa, 2019 – 2025



Chanzo: Wizara ya Fedha

3.2.6 Sekta ya Madini na Uchimbaji


Mpango uliwezesha kuimarishwa kwa masoko na vituo vya ununuzi wa madini; kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kusafisha na kuchenjua madini nchini; kuwezesha wachimbaji wadogo na wa kati; na kutekeleza tafiti za kina za jiolojia, ambapo asilimia 16 ya eneo la nchi imefanyiwa tafiti hizo mwaka 2025/26 huku Serikali ikipanga kuongeza kiwango hicho hadi kufikia asilimia 34 kupitia utafiti wa kina katika maeneo ya mikoa 10 ambayo hayajafanyiwa utafiti wa kina ya Kigoma, Kagera, Rukwa, Katavi, Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Ruvuma na Tabora. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP); Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC); na TEITI.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: ukuaji wa sekta uliongezeka hadi asilimia 9.4 mwaka 2025, kutoka asilimia 8.1 mwaka 2024; mchango wa sekta katika Pato la Taifa uliongezeka hadi asilimia 10.3 mwaka 2025 kutoka asilimia 7.8 mwaka 2024; na thamani ya mauzo ya madini nje ilifikia Dola za Marekani milioni 5,401.9 mwaka 2025, kutoka milioni 3,116.4 mwaka 2021. Aidha, asilimia ya madini kati ya bidhaa sisizo asilia zilizouzwa

nje iliongezeka kufikia asilimia 63.8 mwaka 2025 kutoka asilimia 54.1 mwaka 2021

Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na makusanyo ya maduhuli kufikia shilingi trilioni 1.39 mwaka 2025/26 ikilinganishwa na shilingi bilioni 624.61 mwaka 2021/22; kuwezesha ununuzi wa dhahabu tani 27.79 kufikia Juni 2025; kati ya mwaka 2021 na mwaka 2025 watoa huduma na wakandarasi wa ndani walichangia manunuzi yenye thamani ya dola bilioni 5.07, sawa na asilimia 87 kupitia local content; kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa nane (08) kwa ajili ya shughuli za uongezaji thamani madini katika kituo cha TGC jijini Arusha; kusainiwa kwa mkataba wa kuendeleza mradi wa uchimbaji madini ya niobium wa Panda Hill, wenye thamani ya dola za Marekani milioni 442; uwepo wa viwanda vya ungezaji thamani madini mbalimbali ikiwemo dhahabu kama Mwanza Precious Metal, Geita Gold Refinery na ununuzi wa mitambo 15 ya uchorongaji kwa ajili ya kutoa huduma kwa wachimbaji wadogo wa madini. **Kielelezo Na 3.3**

Kielelezo Na. 3.3: Mwenendo wa Ukuaji wa Sekta ya Madini na Mchango wake katika Pato la Taifa, 2019 – 2025




Chanzo: Wizara ya Fedha

3.2.7 Sekta ya Utalii

Mpango umewezesha kutangaza utalii ndani na nje ya nchi; kuibua na kuendeleza mazao mapya ya utalii ya kimkakati; kuboresha miundombinu ya utalii na uhifadhi; na kuimarisha vyuo vya utalii na ukarimu. Tanzania ilishika nafasi ya 11 duniani mwaka 2025 kwa ongezeko la wageni wa kimataifa. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: miradi ya TANAPA; Kuendeleza Utalii Kusini mwa Tanzania; Mradi wa TAWA; Kujenga Uwezo wa NCT; Capacity Building in Game Reserves; na Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio (MICE) pamoja na programu ya Royal Tour.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: idadi ya watalii iliongezeka hadi 5,935,561 sawa na ongezeko la asilimia 10.7 Desemba 2025, kutoka watalii 5,360,247 mwaka 2024; watalii wa kimataifa waliongezeka kwa asilimia 7.1, kutoka 2,141,895 hadi 2,294,495; watalii wa ndani waliongezeka kwa asilimia 13.1, kutoka 3,218,352 hadi 3,641,066; na mapato yatokanayo na watalii wa kimataifa yaliongezeka kwa asilimia 12.8, kutoka Dola za Marekani bilioni 3.9 mwaka 2024 hadi bilioni 4.4 mwaka 2025. Kielelezo Na. 3.4.

Kielelezo Na. 3.4: Idadi ya Watalii wa Kimataifa, 2019 – 2025



Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

3.2.8 Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

Mpango ulilenga kuwezesha ujenzi wa miundombinu saba (7) mipya ya michezo, na hivyo kufikisha jumla ya miundombinu 37 mwaka 2025/26, kutoka 30 mwaka 2024/25; kuimarisha mifumo ya usajili na ulinzi wa kazi za sanaa; na kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili kikanda na kimataifa. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: ujenzi wa Maeneo Changamani ya Michezo Arusha na Dodoma; National Sports Complex; Mfuko wa Maendeleo ya Michezo; Akademia ya Michezo Malya; upanuzi wa usikivu wa TBC; na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: filamu (TFB) na muziki (BASATA) zilizoidhinishwa zilifikia 14,581 mwaka 2025/26, kutoka 4,342 mwaka 2024/25; wasanii waliosajiliwa katika tasnia ya ubunifu walifikia 15,667, kutoka 7,310; wataalamu wa tasnia ya ubunifu waliopata mafunzo walifikia 4,656, ikilinganishwa na wataa 11,500; wanariadha walioshiriki mashindano nje ya nchi walifikia 132, kutoka 62; michezo na mashindano ya kimataifa yaliyoandaliwa au kushirikiwa na Tanzania yalifikia 337, kutoka 110; na wataalamu wa Kiswahili wanaofanya kazi nje ya nchi walifikia 678, kutoka 384mwaka 2024/25.

3.2.9 Biashara na Uwekezaji

Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, ambapo sheria na kanuni 28 ziliboreshwa mwaka 2025/26 dhidi ya lengo la 12; kuimarisha Kituo cha Huduma za Mahali Pamoja kwa wawekezaji, ambacho kimefikia taasisi 15 kati ya 18 zilizolengwa; kuendeleza Maeneo Maalum ya Kiuchumi, yakiwemo Benjamin William Mkapa SEZ, Bagamoyo SEZ na Mtwara SEZ ambapo miradi iliyosajiliwa imeongezeka kutoka 29 hadi 35; kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za viwandani katika masoko ya EAC na SADC; kusajiliwa kwa miradi ya kimkakati ukiwemo mradi wa kuhifadhi gesi ya LPG wa Chongoleani, Tanga (Dola za Marekani milioni 125); na kusajiliwa kwa miradi ya ubia (PPP) yenye thamani ya shilingi trilioni 6.9 hadi Februari 2026, ambapo miradi ya PPP iliyofikia hatua ya utekelezaji iliongezeka kutoka mitano (5) mwaka 2024/25 hadi saba (7) mwaka 2025/26. Miradi saba (7) ya PPP iliyo katika utekelezaji ni pamoja na Kariakoo One Stop Commercial Complex (shilingi bilioni 37), DART Awamu I na II, Bandari ya Dar es Salaam – DPW, Bandari ya Dar es Salaam –

ADANI na TAZARA, huku majadiliano ya mkataba yakiendelea kwa miradi 3, miradi 4 ikiwa katika ununuzi wa wabia, 22 katika upembuzi yakinifu na 33 katika upembuzi wa awali.

Hadi Juni 2026, jumla ya miradi 114 iliibuliwa ambapo miradi tisa (9) imefikia hatua ya utekelezaji kwa utaratibu wa PPP katika sekta mbalimbali yenye thamani ya shilingi trilioni 8.5. Miradi hiyo ni Ujenzi wa Kituo cha Biashara (Business Complex) cha DDC Kariakoo; Uboreshaji wa Miundombinu na Uendeshaji wa Bandari (TPA na DP World); Uboreshaji wa Miundombinu na Uendeshaji wa Bandari (TPA na ADANI); Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza (DART na TRANSDAR); Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili (DART na MOFAT); Mradi wa Njia Mlishi za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili (DART na Metro Link City Company Ldt); Mradi wa Njia Mlishi za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili (DART na Y.K City Link Ltd); Mradi wa Vituo vya Ukaguzi wa Vyombo vya Moto (Shirika la Uzalishaji Mali la Polisi na Kampuni ya MVI –TANZANIA Ltd); na Mradi wa Ukarabati na Uendeshaji wa Reli ya TAZARA. Aidha, miradi mingine 105 ipo katika hatua za maandalizi, ununuzi na majadiliano ya mkataba kwenye Mamlaka mbalimbali za Serikali. (miradi 3 ipo hatua ya majadiliano ya mkataba, miradi 3 ikiwa katika ununuzi wa wabia, 21 katika upembuzi yakinifu na 36 upembuzi awali na dhana ya maandiko (concept note ni miradi 42).

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa na TISEZA ilifikia 934 mwaka 2025/26, kutoka 940 mwaka 2024/25; thamani ya miradi ya uwekezaji iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 11,267.29 mwaka 2024/25 hadi milioni 12,500 mwaka 2025/26; ajira zinazotarajiwa kutoka miradi hiyo ziliongezeka kutoka 151,284 hadi 307,743; jumla limbikizi ya tozo, ada na ushuru uliofutwa au kupunguzwa iliongezeka kutoka 452 hadi 697; na ardhi iliyotengwa kwa uwekezaji iliongezeka kutoka ekari 391,030.94 hadi ekari 420,516.29.

3.2.9.1 Mwenendo wa Uwekezaji na Utekelezaji wa Miradi kwa Ushirikiano na Sekta Binafsi

Katika mwaka 2025/26, jumla ya miradi 934 ya uwekezaji yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 12.5 ilisajiliwa, ikitarajiwa

kuzalisha ajira 307,743. Aidha, katika kipindi cha Julai hadi tarehe 15 Oktoba 2026, miradi 243 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 3.44 ilisajiliwa, ikitarajiwa kuzalisha ajira 55,836. Sekta ya viwanda iliendelea kuongoza kwa idadi na thamani ya miradi iliyosajiliwa. Vilevile, katika robo ya kwanza ya mwaka 2026/27, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), kwa kushirikiana na sekta binafsi, liliendelea na hatua za utekelezaji wa miradi minne (4) ya mafuta na gesi asilia yenye gharama zinazokadiriwa kufikia dola za Marekani bilioni 20.03 na shilingi bilioni 20.41. Miradi hiyo inahusisha uchakataji wa gesi asilia, ujenzi wa mtambo wa kusafisha mafuta, ukarabati wa miundombinu ya kuhifadhi mafuta na uendelezaji wa Kitalu cha Ruvuma.

Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa kwa Kisekta katika Kipindi cha Julai 2025 hadi Juni 2026

Sekta	**Idadi ya Miradi**	**Fursa za Ajira**	**Mtaji (Dola za Marekani, Milioni)**
Kilimo	96	57,299	3,341.63
Biashara	100	33,318	1,116.71
Teknolojia ya Kompyuta	2	82	5.15
Miundombinu ya Kiuchumi	25	21,761	811.63
Nishati	11	680	137.60
Huduma za Fedha	1	7	1.92
Rasilimali Watu	5	407	11.62
Viwanda	457	65,374	4,288.23
Madini na Petroli	18	106,266	335.32
Huduma	21	1,066	175.72
Mawasiliano ya Simu	3	177	125.26
Utalii	90	6,741	1,389.47
Uchukuzi	105	14,565	759.74
Jumla	**934**	**307,743**	**12,500.00**

Chanzo: TISEZA

Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa kwa Kisekta katika Kipindi cha Julai hadi tarehe 15 Oktoba 2026

Sekta	**Idadi ya Miradi**	**Fursa za Ajira**	**Mtaji (Dola za Marekani, Milioni)**
Kilimo	13	16,405	56.58

Biashara	39	3,473	927.14
Miundombinu ya Kiuchumi	14	3,680	672.24
Nishati	4	449	184.82
Viwanda	139	28,697	1,455.05
Madini na Petroli	2	78	12.25
Huduma	2	295	2.00
Utalii	21	1,662	74.23
Uchukuzi	9	1,097	55.05
Jumla	**243**	**55,836**	**3,439.36**


Miradi Inayotekelezwa Na TPDC Kwa Kushirikiana Na Sekta Binafsi Kwa Robo Ya Kwanza Ya Mwaka Wa Fedha 2026/27 (Julai – Septemba, 2026)

NA	JINA LA MRADI	ENEO LA MRADI	JINA LA SEKTA BINAFSI	HATUA ILIYOFIKIWA	GHARAMA ZA MRADI
1.	Miradi Midogo ya Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (Mini - LNG).	Mkoa wa Pwani (Mkuranga)	Rosetta Energy Solutions.	• Mkataba wa Mauziano ya Gesi Asilia (Gas Sales Agreement – GSA) ulisainiwa tarehe 05 Agosti, 2026. • Kwa sasa mkandarasi anaendelea na kazi ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) katika eneo la mradi.	Dola marekani milioni 11.5.
2.	Mradi wa Ujenzi wa Mtambo wa Kusafisha Mafuta (Refinery) chini ya mpango wa Tanga Reginal Energy Hub	Tanga	Vitol Bahrain Energy Company	• Mkataba wa Makubaliano (MoU) ulisainiwa kati ya UNOC, TPDC na Vitol B. E. Company tarehe 06 Agosti, 2026. • Kazi inayoendelea sasa ni maandalizi ya Upembuzi Yakinifu	Dola za Marekani Bilioni 20.
3.	Mradi wa Ukarabati Tenki Na. 8	Dar es Salaam (Kigamboni)	BSL Infrastructure Ltd	• Mkandarasi na TPDC walisaini mkataba ya ujenzi tarehe 10 Agosti, 2026. • Mkandarasi anaendelea na kazi ya mobilization ya vifaa vya ujenzi huku akiendelea na kazi nyingine za awali za ukarabati.	Gharama za mradi ni TZS 20.41 bilioni
4.	Mradi wa uendelezaji wa kitalu cha Ruvuma (eneo la Ntorya. – Uchimbaji kisima cha Ntorya 3.	Mtwara (Mtwara vijijini)	ARA Petroleum	Award letter imetolewa tarehe 18 Septemba, 2026 kwa ajili ya kazi za uchimbaji wa kisima cha Ntorya 3 kwa Mkandarasi CPTDC.	Gharama za mradi USD 20 million.

Chanzo: TPDC

Uchambuzi wa mwenendo wa uwekezaji unaonesha kuendelea kuimarika kwa nafasi ya sekta binafsi katika kuchochea shughuli za uzalishaji na maendeleo ya uchumi, hususan katika sekta za viwanda, biashara, miundombinu na nishati. Sekta ya viwanda imeendelea kuwa kinara katika kuvutia uwekezaji,

ambapo mchango wake katika idadi ya miradi yote iliyosajiliwa uliongezeka kutoka asilimia 48.9 katika mwaka 2025/26 hadi asilimia 57.2 katika kipindi cha Julai hadi tarehe 15 Oktoba 2026. Aidha, mchango wa sekta hiyo katika thamani ya mtaji wa miradi iliyosajiliwa uliongezeka kutoka asilimia 34.3 hadi asilimia 42.3 katika vipindi hivyo, hali inayoashiria kuendelea kuelekezwa kwa uwekezaji katika shughuli za uzalishaji viwandani. Kwa upande wa ajira, sekta ya viwanda ilichangia asilimia 51.4 ya fursa zote za ajira zilizotarajiwa kutokana na miradi iliyosajiliwa katika kipindi cha Julai hadi tarehe 15 Oktoba 2026. Vilevile, ushirikiano kati ya TPDC na sekta binafsi katika miradi ya mafuta na gesi asilia unaonesha fursa za kuongeza uwezo wa ndani wa kuchakata na kuhifadhi bidhaa za nishati, kuimarisha usalama wa upatikanaji wa nishati, kuongeza thamani ya rasilimali za ndani na kupanua fursa za ajira na uwekezaji.



Aidha, katika kipindi cha mwaka 2025/26, Serikali iliendelea kuimarisha ushirikiano na Sekta Binafsi katika sekta mbalimbali. Katika sekta ya afya, Sekta Binafsi ilikuwa na vituo 5,460, sawa na asilimia 40 ya vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini, na ilifungua vituo vipya 241. Aidha, Serikali ilishirikiana na Hospitali za

Mashirika ya Kidini katika kugharamia mishahara ya watumishi na vifaa tiba, huku hospitali za Bugando na KCMC zikichangia utoaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi. Vilevile, Taasisi ya Mifupa (MOI) na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road ziliendelea na hatua za upembuzi yakinifu kwa ajili ya kupata wabia wa kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini.

Katika sekta ya madini, Kampuni ya Panda Hill Tanzania Limited ilisaini mkataba wa kuendeleza mradi wa uchimbaji madini ya Niobium wa Panda Hill, wenye thamani ya dola za Marekani milioni 442, na mitambo 15 ya uchorongaji ilinunuliwa kwa ajili ya kuboresha huduma kwa wachimbaji wadogo. Aidha, uzalishaji uliendelea katika migodi ya Geita Gold Mine, Shanta Gold Mine, North Mara na Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira – Songwe. Kwa upande wa shughuli za uongezaji thamani madini ziliendelea katika viwanda mbalimbali, ikiwemo Mwanza Precious Metals, Geita Gold Refinery na Eyes of Africa. Vilevile, uendelezaji wa migodi ya dhahabu ya Nyanzaga – Sengerema, urani ya Mkuju River – Namtumbo na Nikeli ya Kabanga uliendelea. Hatua hizi zilichangia kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi, kupanua uwekezaji, kuongeza thamani ya rasilimali za madini nchini na kuweka mazingira ya kukuza ajira na shughuli za kiuchumi.

Miradi ya Ushirikiano na Uwekezaji na Sekta Binafsi katika Sekta ya Madini

Na.	Jina la Mradi	Kampuni ya Ubia	Eneo	Jina la Sekta Binafsi	Umiliki wa Hisa (%)	Thamani ya Uwekezaji
1.	Mradi wa Uchimbaji madini ya dhahabu katika mgodi wa Madini ya dhahabu, Northmara (Northmara Gold Mine)	Twiga Minerals Corporation	Nyamongo, Tarime	Barrick Gold Corporation (Barrick)	Barrick 84% Serikali 16%	USD 827,125,000
2.	Mradi wa Uchimbaji madini ya dhahabu katika mgodi wa Madini ya dhahabu, Bulyanhulu	Twiga Minerals Corporation	Kahama, Shinyanga	Barrick Gold Corporation (Barrick)	Barrick 84% Serikali 16%	USD 856,740,000
3.	Mradi wa Uchimbaji madini ya dhahabu katika mgodiwa madini ya dhahabu, Buzwagi kupitia kampuni ya Pangea Minerals	Twiga Minerals Corporation	Kahama, Shinyanga	Barrick Gold Corporation (Barrick)	Barrick 84% Serikali 16%	USD (103,564,000)
4.	Mradi wa Uchimbaji madini ya almasi katika mgodi wa Almasi wa Mwadui.	Williamson Diamond Limited (WDL)	Mwadui, Shinyanga	Pink Diamond (Subsidiary of Taifa Mining Group)	Pink 63% Serikali 37% Ambapo kwa upande wa Serikali 21% ni hisa za daraja A na 16% ni hisa za daraja B	USD (312,339,757)

					zisizohafifishwa.	
5.	Mradi wa Kabanga Nickel	Tembo Nickel Corporation Ltd	Ngara, Kagera	Lifezone Metals Ltd (Lifezone)	Lifezone 84% Serikali 16%	USD (6,423,074)
6.	Mradi wa Uchimbaji madini mchanga katika mgodi wa madini mchanga Fungoni	Nyati Mineral Sands Ltd	Kigamboni, Dar es Salaam	Shenghe Resources Ltd (Shenghe)	Shenghe 84% Serikali 16%	TZS (14,822,321,000)
7.	Mradi wa Uchimbaji madini mchanga katika Mgodi wa madini mchanga Fungoni	Nyati Mineral Sands Ltd	Pangani, Tanga	Shenghe Resources Ltd (Shenghe)	Shenghe 84% Serikali 16%	
8.	Mradi wa Uchimbaji madini Kinywe katika mgodi wa madini kinywe Mahenge madini mchanga Tajiri	Faru Graphite Ltd	Mahenge, Morogoro	BlackRock Mining Ltd (Black Rock)	Black Rock 84% Serikali 16%	USD (5,011,450)
9.	Mradi wa Uchimbaji madini ya dhahabu	Sotta Mining Co. Ltd	Sengerema, Mwanza	Perseus Mining Ltd (Perseus)	Perseus 84% Serikali 16%	USD (3,134,228)

	katika mgodi wa Madini ya dhahabu Nyanzaga					
10.	Mradi wa uchimbaji wa madini muhimu Ngualla (Ngualla Rare Earth Project)	Mamba Minerals Corporation Ltd	Songwe, Songwe	Shenghe Resources Ltd (Shenghe)	Shenghe 84% Serikali 16%	TZS 22,005,540,000
11.	Mradi wa Uchimbaji madini Kinywe Epanko (Epanko Graphite Project)	Duma TanzGraphite Ltd	Mahenge, Morogoro	EcoGraf Ltd	EcoGraf Ltd 84% Serikali 16%	TZS (1,581,842)
12.	Uchimbaji madini Kinywe Chilalo (Chilalo Graphite Project)	Graphite Ltd	Lindi	Energy Minerals	Energy Minerals 84% Serikali 16%	3,757,496
13.	Mradi wa Uchimbaji madini ya niobium Panda Hill (Panda Hill Niobium Project)	Chui Niobium Mining	Mbeya Rural District, Mbeya.	Tremond Investment & Cradle Resources Ltd	Tremond Investment & Cradle Resources Ltd 84% Serikali 16%	New Company
14.	Mradi wa Uchimbaji madini ya Helium kusini mwa Rukwa (Southern Rukwa Helium Project)	Songwe Helium Ltd	Mombaand Sumbawanga, Rukwa.	HeliumOne Global	HeliumOne Global 83% Serikali 17%	New Company

15.	Mradi wa Uchimbaji madini kinywe Lindi Jumbo (Lindi Jumbo Graphite Mine)	Ndovu Graphite Ltd	Ruangwa, Lindi.	Walkabout Resources Ltd (Under Germcorp Administration)	Walkabout ResourcesLtd 84% Serikali 16%	New Company
16.	Mradi wa uchimbaji wa madini Kinywe Graphica	Graphica Graphite Corporation Ltd	Ruangwa, Lindi.	Graphica Resources Limited	Graphica Resources Limited 83% Serikali 17%	New Company
17.	Mradi wa uchimbaji wa madini kinywe Eminent	Swala Graphite Corporation	Ruangwa, Lindi.	Eminent Minerals Limited	Eminent Minerals Limited 83% Serikali 17%	New Company
18.	Mradi wa uchimbaji wa madini kinywe Yudi Graphica	Yudi Mining Ltd	Morogoro, Morogoro.	Yudi Mining	Yudi Mining 83% Serikali 17%	New Company

Chanzo: OTR

3.3 Kujenga Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii

3.3.1 Elimu

Mpango uliwezesha kuongezeka kwa: ujenzi wa vyumba vya madarasa hadi 254,393 mwaka 2025/26 kutoka 191,708 mwaka 2024/25, shule za msingi hadi 17,986 kutoka 16,406, shule za sekondari hadi 4,894 kutoka 3,863 maktaba hadi 2,665 kutoka 1,537, maabara hadi 8,710 kutoka 8,072, mabweni hadi 3,245 kutoka 2,245, mabwalo hadi 1,004 kutoka 871, nyumba za walimu hadi 60,429 kutoka 58,637, na matundu ya vyoo hadi 286,243 kutoka 206,670 katika shule za msingi na hadi 131,152 kutoka 92,724 katika shule za sekondari; kuajiri walimu 68,279, wakiwemo walimu 7,000 wa sayansi na hisabati; kutoa ruzuku ya Elimu Bila Ada ya shilingi bilioni 510.97, kutoka shilingi bilioni 484.3 mwaka 2024/25; na kuongeza bajeti ya mikopo ya elimu ya juu hadi shilingi bilioni 916.7,

kutoka shilingi bilioni 878.0 mwaka 2024/25. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Mikopo ya Elimu ya Juu; HEET; ESPJ II; EP4R; Support to VET and Teacher Education; SEQUIP; na Mfuko wa Elimu Tanzania (TEA).

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: uwiano wa wanafunzi kwa darasa katika elimu ya msingi uliboreka kutoka 1:75 mwaka 2020 hadi 1:62 mwaka 2025, na uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu mwenye sifa uliboreka kutoka1:51 mwaka 2024 hadi 1:50; uandikishaji jumla katika sekondari ya chini uliongezeka kutoka asilimia 51.7 mwaka 2024 hadi 53.1 mwaka 2025, na katika sekondari ya juu kutoka asilimia 9.1 hadi 9.8; uandikishaji jumla katika vyuo vya elimu ya ufundi ulifikia asilimia 10.4, kutoka asilimia 5.8 mwaka 2023/24; wahitimu wa elimu ya ufundi waliongezeka kutoka 89,967 hadi 129,766; wanafunzi waliopata mikopo ya elimu ya juu waliongezeka kutoka 229,652 mwaka 2024 hadi 248,331 mwaka 2024/25; wahitimu wa vyuo vikuu waliongezeka kutoka 56,520 hadi 62,570; ufaulu wa kidato cha nne ulikuwa asilimia 92.37 mwaka 2024, na ufaulu wa darasa la saba na kidato cha sita ulifikia asilimia 81.8 na 99.62 mwaka 2025, mtawalia, kutoka asilimia 80.9 na 99.9 mwaka 2024.

Nguvu Kazi, Vijana na Ajira

Mpango ulilenga kuwezesha utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi, ambapo vijana 5,746 walipata mafunzo ya uanagenzi, 2,500 mafunzo ya utarajali, mafunzo ya kuongeza ujuzi kwa wafanyakazi 1,365, na vijana 7,826 mafunzo ya kushindania fursa za ajira. Vile vile, kutoa mikopo ya shilingi bilioni 52.2 kwa vikundi 5,199 vya vijana; kuwezesha vikundi 299 vya vijana (vijana 2,226) kupata zabuni za umma zenye thamani ya shilingi bilioni 13.2 kupitia mfumo wa NeST; na kuanzisha mfuko wa ruzuku kwa vyama vya watu wenye ulemavu. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Programu ya Ukuzaji Ujuzi; Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; na Uimarishaji wa Mifumo ya Kitaifa kwa Maendeleo ya Vijana.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: ajira 981,000 zilizalishwa mwaka 2025/26, kutoka 876,916 mwaka 2024/25; wigo wa kinga ya jamii ulifikia asilimia 28 mwaka 2025/26,

kutoka asilimia 27.4 mwaka 2024/25; na watu waliopata mafunzo ya ujuzi walifikia 168,667 mwaka 2025/26, kutoka 157,867 mwaka 2024/25.

3.3.2 Ustawi na Maendeleo ya Jamii

Mpango uliwezesha utekelezaji wa programu za uwezeshaji wanawake kiuchumi na kurasimisha wafanyabiashara wadogo, ambapo wafanyabiashara 6,735 walipata mikopo; kusajili vituo vya kulelea watoto wadogo mchana; na kuwapatia wazee 229 wanaohudumiwa katika makazi 13 ya Serikali bima ya afya. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: PAMOJA; TASAF; Mfuko wa Machinga; na Jinsia na Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: vituo vya kulelea watoto mchana vilivyosajiliwa viliongezeka hadi 4,916 mwaka 2025/26 kutoka 4,178 mwaka 2024/25; na wafanyabiashara wadogo waliotambuliwa na kusajiliwa waliongezeka hadi 138,438 kutoka 84,318, ambapo asilimia 60 ni wanawake.

3.3.3 Afya

Mpango uliwezesha kuongeza vituo vya kutolea huduma za afya kufikia 10,540 mwaka 2025/26 (zahanati 8,706, vituo vya afya 1,359 na hospitali 475), kutoka 10,044 mwaka 2024/25; kuongeza watumishi wa sekta ya afya kufikia 177,711, kutoka 126,925 mwaka 2024; na kuongeza viwanda vya dawa nchini kutoka 11 hadi 12. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Dawa na Bidhaa za Afya; Uimarishaji wa Huduma za Chanjo; Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa; Programu ya Afya ya Mama na Mtoto; Hospitali ya Taifa Muhimbili; Hospitali Maalum ya Mama na Mtoto Dodoma; na Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: chanjo ya Penta iliwafikia watoto 2,361,592 sawa na asilimia 95 mwaka 2025, kutoka asilimia 96.5 mwaka 2024; wastani wa umri wa kuishi uliongezeka kutoka miaka 66.8 mwaka 2022 hadi miaka 68.3 mwaka 2025; vifo vya watoto chini ya miaka mitano vilipungua kutoka 67 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2015/16 hadi 43 mwaka

2022; na vifo vitokanavyo na uzazi vilipungua kutoka 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2015/16 hadi 104 mwaka 2022.

Kwa upande wa bima ya afya, jumla ya kaya 198,709 kati ya kaya 276,004 zimehakikiwa na kupatiwa kadi, sawa na asilimia 72 ya lengo. Vilevile, idadi ya wanufaika 542,829 wamepatiwa kadi kati ya wanufaika 1,206,319 waliolengwa sawa na asilimia 45. Aidha, jumla ya wazee 196 wamepatiwa kadi za bima ya afya kati ya wazee 205 waliopo kwenye makazi ya Serikali sawa na asilimia 83 ya lengo. Vilevile, watoto 205 kati ya 255 waliopo kwenye makao ya Serikali wamepatiwa kadi za bima ya afya sawa na asilimia 80 ya lengo. Vilevile, kaya 6,591 sawa na asilimia 35 zimehakikiwa na kupatiwa kadi kati ya kaya 18,844 zilizolengwa sawa na wanufaika 6,545 kati ya 51,871 waliolengwa sawa na asilimia13 ya lengo. Kwa upande wa wazee na watoto wanaokaa kwenye Makazi na makao maalumu, jumla ya wazee 196 wamepewa kadi kati ya wazee 235 waliolengwa. Hadi Juni 2026, wanachama wa Bima ya afya nchini ikijumuisha wanachama wa bima ya afya kwa wote na bima zingine imefikia asilimia 11.3 ya Watanzania wote ikilinganishwa na lengo la asilimia 25 ya Watanzania wote mwezi Juni 2027.

3.3.4 Maji na Usafi wa Mazingira

Katika kipindi cha mwaka 2025/26, Wizara ya Maji iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma endelevu ya majisafi na usafi wa mazingira kwa wananchi wote, mijini na vijijini. Ili kufikia lengo hilo, Wizara ilitekeleza kazi zifuatazo:

(a) Usimamizi na uendelezaji wa Rasilimali za Maji

Serikali iliendelea kusimamia rasilimali za maji nchini kupitia Bodi tisa (9) za Maji za Mabonde zilizoanzishwa ili kuhakikisha usimamizi na uendelezaji endelevu wa rasilimali hizo. Katika kipindi husika, mtandao wa vituo 1,186 vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji umeanzishwa, na zaidi ya miti milioni 6 rafiki kwa maji imepandwa ili kuimarisha uhifadhi wa vyanzo vya maji. Aidha, vyanzo 106 vya maji vimetangazwa katika Gazeti la Serikali kwa ajili ya ulinzi na uhifadhi, vibali 247 vya utupaji wa maji taka vimetolewa ili kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji, na vibali 14,536 vya matumizi ya maji vimetolewa ili kudhibiti matumizi ya maji. Vilevile,

ili kuimarisha ushirikishwaji wa jamii katika kutunza na kuhifadhi vyanzo vya maji, Kamati 34 za Vidaka Maji na Jumuiya 272 za Watumia Maji zimeanzishwa.

(b) Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini

Huduma ya maji vijijini inatekelezwa na kusimamiwa na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA). Ili kuimarisha upatikanaji wa huduma hii, katika mwaka 2025/26 Serikali ilipanga kutekeleza jumla ya miradi 1,318 kwenye maeneo ya vijijini. Utekelezaji huo ulihusisha kukamilisha miradi iliyokuwa inaendelea, kujenga miradi mipya, pamoja na kupanua na kukarabati miundombinu ya maji.

Kwa upande wa usambazaji wa maji vijijini, RUWASA iliendelea kutekeleza miradi ya maji na usafi wa mazingira, ambapo jumla ya miradi 54 yenye vituo 946 vya kuchotea maji imekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi wapatao 493,932 wanaoishi katika vijiji 151. Aidha, utekelezaji wa miradi 992 yenye vituo 29,865 unaendelea, ikiwa katika hatua mbalimbali; miradi hiyo itakapokamilika itahudumia wananchi wapatao 38,611,800 wanaoishi katika vijiji 7,030.

(c) Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo iliendelea kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira mijini kupitia ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya maji. Katika mwaka 2025/26, jumla ya miradi 226 ilipangwa kutekelezwa ambapo jumla ya miradi 12 imekamilika na inahudumia wananchi wapatao 880,633. Jumla ya miradi 190 inaendelea na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na miradi 16 imefikia zaidi ya asilimia 95 na imeanza kutoa huduma kwa wananchi. Aidha, miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Ukarabati na Upanuzi wa Maji Mijini; Ziwa Victoria – Kahama – Shinyanga; WSDP; Uboreshaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini; LVWATSAN Awamu ya II; na Tanga Water Supply and Sanitation.

Vilevile, utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: upatikanaji wa maji ya bomba vijijini uliongezeka kutoka asilimia 83.1 mwaka 2024/25 hadi asilimia 85.2 mwaka 2025/26;

katika makao makuu ya mikoa uliongezeka kutoka asilimia 90.6 hadi 92.5; na kaya za vijijini zenye miundombinu bora ya usafi wa mazingira ziliongezeka kutoka asilimia 72.0 hadi 78.5 katika kipindi hicho.

3.3.4.1 Mazingira

Mpango ulilenga kupandwa kwa miti milioni 276 ambapo kwa mwaka 2025/26 miti milioni 241 ilipandwa, kati ya hiyo, miti milioni 184.1 imestawi sawa na asilimia 76; vibali 212 vya usimamizi wa taka hatarishi vilitolewa kwa wadau; kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki ambapo jumla ya tani 60 zilikamatwa na kuteketezwa; kukusanywa kwa tani 150,000 za taka za chupa za plastiki, ambapo tani 75,000 zilirejelezwa. Katika uhifadhi wa mazingira, miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Kuimarisha Usimamizi wa Mashamba ya Miti ya Serikali; Programu ya Kujenga Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi Kigoma katika halmashauri za Kasulu, Kibondo na Kakonko; Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mifumo Ikolojia, Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai Tanzania katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Katavi na Rukwa; Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Katika Jamii zinazozunguka Misitu ya Miombo Tanzania Bara na Zanzibar; Mradi wa "Scaling Up Locally Led Climate Action - SLR"; na FOLUR.

3.3.5 Ardhi na Maendeleo ya Makazi

Mpango uliwezesha kuimarisha miundombinu ya TEHAMA katika ofisi za ardhi za mikoa na halmashauri zote nchini, kusambaza Mfumo wa e-Ardhi, kutoa elimu na kuwajengea uwezo watumiaji katika upimaji na umilikishaji wa ardhi. Aidha miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Uboreshaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani (LDI) wenye thamani ya shilingi bilioni 56.32. Mradi wa Uboreshaji wa Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP); na Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK), huku Shirika la Nyumba la Taifa likijenga nyumba za gharama nafuu.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: Viwanja na mashamba yaliyopimwa yalifikia 3,079,886 mwaka 2025/26, kutoka 2,857,349 mwaka 2024/25; hati zilizotolewa zilifikia 2,675,848 mwaka 2025/26, kutoka 2,573,849 mwaka 2024/25; na vijiji

vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi vilifikia 4,953 asilimia 40.47, kutoka vijiji 4,672 asilimia 37.76 mwaka 2024/25.


3.4 Vichocheo vya Maendeleo

3.4.1 Nishati

Mpango uliwezesha kukamilika kwa ufungaji wa mitambo yote tisa (9) ya Bwawa la Julius Nyerere (MW 2,115); kuunganishwa kwa Mkoa wa Katavi na Gridi ya Taifa na kufikisha mikoa 24 kati ya 26, hatua iliyookoa takriban shilingi bilioni 68.4 za gharama za kuzalisha umeme kwa mafuta; kuunganishwa na umeme kwa vijiji vyote 12,318 na vitongoji 39,003 kati ya 64,359; kuendelea na ujenzi wa EACOP uliofikia asilimia 86 Juni 2026; na kuendelea na utafutaji wa mafuta na gesi kwa mradi wa Eyasi-Wembere na mradi wa Lindi-Mtwara. Miradi ya Ruhudji, Rumakali, Kakono (MW 87) na LNG imebaki katika hatua za maandalizi, utekelezaji wa mradi wa Malagarasi (MW 49.5) umefikia asilimia 29.25 na ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa nishati ya jua cha Kishapu, Shinyanga (MW 50, Awamu ya Kwanza) umekamilika. Aidha, Awamu ya Pili ya mradi wa Shinyanga/Kishapu Solar (MW 100) imeanza kutekelezwa.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme uliongezeka kutoka MW 4,437.53 Juni 2025 hadi MW 4,606.14 Juni 2026; urefu wa Gridi ya Taifa ya umeme uliongezeka kutoka km 7,809.67 hadi km 8,500.38, na mtandao wa usambazaji umeme kutoka km 200,266.25 hadi km 233,133; wateja waliounganishwa na umeme waliongezeka kwa asilimia 12.97 kutoka 5,336,415 mwaka 2024/25 hadi 6,131,695 mwaka 2025/26; kaya zilizounganishiwa huduma ya umeme ziliongezeka kutoka asilimia 39.9 mwaka 2019/20, na kufikia asilimia 52.1 mwaka 2024/25. Aidha, wananchi waliofikiwa na huduma ya umeme waliongezeka kutoka asilimia 78.4 mwaka 2019/20 hadi asilimia 85.5 mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 7.12; matumizi ya umeme kwa mtu yaliongezeka kutoka kWh 170 mwaka 2024/25 hadi kWh 243 mwaka 2025/26; na vituo vya kujazia gesi asilia kwenye vyombo vya moto viliongezeka kutoka vituo 9 mwaka 2025 hadi 19 mwaka 2026. Kielelezo Na. 3.5

Kielelezo Na. 3.5: Mwenendo wa Uwezo wa Mitambo ya Kuzalisha Umeme (MW), 2019/20 – Juni 2026 na Shabaha za FYDP IV



3.4.2 Mifumo ya Usafirishaji na Uchukuzi Fungamanishi

Mpango ulilenga kuimarisha mifumo ya usafirishaji na uchukuzi kwa kupanua na kuboresha miundombinu ya reli, bandari, usafiri wa anga na miundombinu shikizi. Katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali iliendelea kutoa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya reli ya SGR katika vipande vya kutoka Dar es Salaam –Morogoro na Morogoro – Makutupora ambavyo ujenzi wake ulikamilika. Aidha, ujenzi katika kipande cha kutoka Makutupora - Tabora, Tabora – Isaka, Isaka – Mwanza na Tabora – Kigoma na Uvinza – Musongati uliendelea na kwa ujumla urefu ulikamilishwa ujenzi wake ulifikia kilomita 722 hadi kufikia mwezi Juni, 2026.

Katika ujenzi na ukarabati wa meli, Serikali ilikamilisha Ujenzi wa Meli ya Abiria na Mizigo ya MV. Mwanza pamoja na kukamilisha MV. Liemba katika Ziwa Tanganyika. Ukarabati wa MT. Ukerewe katika Ziwa Victoria ulifikia asilimia 95. Katika eneo la bandari, Serikali iliendelea na ujenzi na ukarabati wa bandari kavu saba (7). Kati ya hizo, bandari kavu za Kwala, Ex-NASACO na Mwambani zilianza kutoa huduma za kibandari na bandari nyingine ziliendelea na ukarabati na ujenzi. Aidha, mifumo ya usimamizi wa taarifa za viwanja vya ndege ilifungwa katika viwanja 10 kati ya 14; jumla ya mitambo 103 kati ya 71 ya ulinzi (X-ray machines) kwenye viwanja vya ndege ilinunuliwa na jumla ya viwanja vya ndege 26 kati ya 27


vilizungushiwa uzio wa usalama na rada tano (5) kati ya saba (7) za hali ya hewa zilikuwa zimefungwa. Hatua hizi za kuboresha miundombinu zinatarajiwa kuongeza ufanisi wa huduma za uchukuzi na kurahisisha mnyororo wa usafirishaji wa mizigo nchini.

Utekelezaji wa viashiria unaonesha kuwa sekta ya uchukuzi ilikua kwa asilimia 8.0 mwaka 2025, kutoka asilimia 4.2 mwaka 2024, na mchango wake katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 7.5 hadi 8.3. Mapato ya fedha za kigeni kutokana na huduma za uchukuzi yaliongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 2.35 mwaka 2024 hadi bilioni 2.79 mwaka 2025.

Utendaji wa Sekta ya Uchukuzi uliimarishwa ambapo huduma za usafiri wa anga kupitia ATCL zilitolewa katika vituo 33 kwa mwaka 2025/26 ikilinganishwa na 27 kwa mwaka 2024/25 kwa kutumia ndege 16 zilizonunuliwa na Serikali. Hivyo, abiria 1,427,439 walisafirishwa kwa mwaka 2025/26, ikilinganishwa na abiria 1,178,025 katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia, sawa na ongezeko la asilimia 21.2. Kwa upande wa shehena iliyohudumiwa nchini iliongezeka kutoka tani milioni 32.753 zilizohudumiwa mwaka 2024/25 hadi kufikia tani milioni 39.899 mwaka 2025/26 sawa na ongezeko la asilimia 21.8. Wastani wa makasha yaliyohudumiwa kwa mwezi ulifikia TEUs 102,000, kutoka TEUs 61,000 sawa na ongezeko la asilimia 40, wakati muda wa kuhudumia meli za makasha gatini ulipungua hadi wastani wa siku 3 na muda wa meli kusubiri nangani ulipungua hadi siku 7 katika kipindi hicho.

Usafirishaji wa abiria na mizigo kwa reli ya SGR ilisafirisha abiria 3,552,650, ikilinganishwa na abiria 2,862,088 mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 24.12. Aidha, Shirika la Reli Tanzania (TRC) ilisafirisha jumla ya tani 501,155 ikilinganishwa na shehena ya tani 246,824 iliyosafirishwa mwaka 2024/25. Mamlaka ya reli ya Tanzania na Zambia – TAZARA kupitia reli ya TAZARA ilisafirisha jumla ya tani 214,848 ikilinganishwa na tani 207,928 zilizosafirishwa mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 3.3.

Kielelezo Na. 3.6: Shehena Iliyosafirishwa kwa Reli, 2024/25 na 2025/26 (Tani)



Chanzo: Wizara ya Uchukuzi

3.4.3 Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

Mpango uliwezesha kuimarika kwa Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Sayansi na Teknolojia (MTUSATE) ambao umekusanya zaidi ya shilingi bilioni 129, zikiwemo zaidi ya shilingi bilioni 85 kutoka Serikalini; kuzinduliwa kwa programu ya Grand Challenges Tanzania Juni 2026; na kuimarisha ulinzi wa ubunifu wa ndani kupitia haki miliki.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: hataza zilizotolewa na BRELA ziliongezeka hadi 61 mwaka 2025/26 kutoka 30 mwaka 2024/25; alama za biashara na huduma zilizosajiliwa ziliongezeka hadi 3,455 kutoka 3,148; na nafasi ya Tanzania katika Fahirisi ya Ubunifu Duniani ilikuwa ya 121 kati ya nchi 139 mwaka 2025, kutoka nafasi ya 120 kati ya nchi 133 mwaka 2024.

3.4.4 Utafiti na Takwimu

Mpango uliwezesha utekelezaji wa Vipaumbele vya Taifa vya Utafiti vya 2021/22–2025/26 na Mpango Kabambe wa Pili wa Takwimu (TSMP II), pamoja na kuimarisha matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 katika upangaji, ufuatiliaji na tathmini ya maendeleo.

Utekelezaji wa viashiria katika eneo hili unaonesha kuwa alama ya Tanzania katika Kiashiria cha Utendaji wa Kitakwimu cha Benki ya Dunia (Statistical Performance Indicators – SPI) ilikuwa 68.2 mwaka 2024. Kiashiria hiki hutathmini uwezo na utendaji wa mfumo wa kitaifa wa takwimu katika uzalishaji, upatikanaji na matumizi ya takwimu kwa ajili ya maamuzi na upangaji wa maendeleo.

3.4.5 Mapinduzi ya Kidijitali, TEHAMA na Mawasiliano

Mpango uliwezesha kukamilisha ujenzi wa minara 758 ya mawasiliano katika kata 688 inayohudumia takriban watu milioni 8.5, na kupandisha hadhi minara 304 kutoka 2G kwenda 3G/4G; kukamilika kwa minara 495 kati ya 636 ya awamu inayofuata; kupanua Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano hadi km 15,167 kati ya km 16,280 zilizopangwa; Kuunganisha Wilaya 10 Nchini na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kufanya jumla ya wilaya 122 kati ya 139 na nchi jirani saba (7) kati ya nane (8) kuunganishwa; kutoa huduma ya Wi-Fi kwa umma katika maeneo 50; na kusajili anwani 12,857,892 katika Mfumo wa Anwani za Makazi (NaPA). Aidha, ukarabati wa vituo 32 vya kutolea huduma za Serikali katika eneo na dirisha moja uliendelea, pamoja na utekelezaji wa miradi ya ICT Parks na Tanzania ya Kidijitali.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: uwiano wa watumiaji wa intaneti uliongezeka hadi asilimia 85 mwaka 2025 kutoka asilimia 74 mwaka 2024; ueneaji wa intaneti uliongezeka hadi asilimia 89.7 Juni 2026 kutoka asilimia 79.3 mwaka 2025; wananchi waliofikiwa na mitandao ya simu waliongezeka hadi asilimia 98.65 kutoka asilimia 98.4; upatikanaji wa mtandao wa 4G uliongezeka hadi asilimia 94.39 Juni 2026 kutoka asilimia 90 mwaka 2024, na wa 5G hadi asilimia 34.18 kutoka asilimia 26; majengo yenye anwani za makazi yaliongezeka hadi 18,558,268 mwaka 2025/26 kutoka 18,186,000 mwaka 2024/25; na makosa ya kimtandao yaliyoripotiwa Polisi yaliongezeka hadi 1,323 kutoka 748 kati ya Julai – Aprili ya mwaka 2024/25 na 2025/26; na upenyo wa simu janja uliongezeka hadi asilimia 44.74 Juni 2026 kutoka asilimia 37 mwaka 2025.

Kielelezo Na. 3.7: Mwenendo wa Upatikanaji wa Mitandao ya 3G, 4G na 5G (Asilimia ya Watu), 2020/21 – 2025/26



Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

3.5 Misingi ya Uendelevu wa Taifa

3.5.1 Utawala Bora, Demokrasia, Usalama na Utulivu

Mpango uliwezesha kukamilika kwa Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki (IJC) tisa (9) vipya; kukamilika kwa majengo 72 ya Mahakama za Mwanzo; kutafsiriwa kwa sheria kuu 433 kwa lugha ya Kiswahili; kuanzishwa kwa madawati ya msaada wa kisheria katika Mamlaka 184 za Serikali za Mitaa; kufikia Ofisi za Mashtaka za Wilaya 118; na kuendelea na ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba uliofikia asilimia 94, ambapo wizara 15 kati ya 25 zimehamia. Kituo cha Menejimenti ya Maafa Nzuguni kimefikia asilimia 70. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Vitambulisho vya Taifa (NIDA); Upatikanaji wa Haki kwa Maendeleo Endelevu; PSRP III; e-Justice; na Strengthening Anti-Human Trafficking.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki vinavyotoa huduma viliongezeka hadi 18 Juni 2026 kutoka 9 mwaka 2024/25; wananchi wanaoishi katika

mikoa yenye Mahakama Kuu inayofanya kazi waliongezeka hadi asilimia 97 mwaka 2025/26 kutoka asilimi 69 mwaka 2024/25, baada ya huduma kupanuka kutoka mikoa 14 hadi 25; majengo ya Mahakama za Mwanzo yaliongezeka hadi majengo 746 kutoka 674; wastani wa muda wa kutoa hukumu katika Mahakama Kuu ulipungua hadi siku 202 kutoka siku 730; watumishi waliopata mafunzo ya maadili ya utendaji katika utumishi wa umma waliongezeka hadi watumishi 30,966 mwaka 2025/26 kutoka watumishi 6,000 mwaka 2024/25; taasisi zinazotumia e - Mrejesho ziliongezeka hadi taasisi 207 mwaka 2024/25 kutoka 40 mwaka 2024/25; Tanzania ilishika nafasi ya 14 kati ya nchi 35 katika Fahirisi ya World Justice Project ya 2025, kutoka nafasi ya 15 kati ya 37; na makosa makubwa ya jinai yaliyoripotiwa yalipungua hadi 39,027 kutoka 40,022 kati ya Julai – Aprili ya mwaka 2024/25 na 2025/26, huku ajali za barabarani zikipungua kwa asilimia 6.7 na vifo vitokanavyo na ajali kwa asilimia 16.4; na kiwango cha uhalifu nchini kilipungua hadi asilimia 3.2 mwaka 2024/25, kutoka asilimia 5.2 katika mwaka wa kizio.

3.5.2 Serikali za Mitaa

Mpango uliwezesha kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, matumizi ya mifumo ya kidijitali katika usimamizi wa mapato na utendaji, pamoja na kuimarisha uwezo wa rasilimali watu katika Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri. Utekelezaji wa viashiria unaonesha kuwa bajeti ya mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2025/26 ilikuwa shilingi trilioni 1.68. Hadi Desemba 2025, makusanyo halisi yalifikia shilingi bilioni 774.0, sawa na asilimia 94.4 ya makadirio ya shilingi bilioni 820.1 kwa kipindi cha Julai–Desemba 2025. Kwa mwaka mzima wa 2024/25, mapato ya ndani ya Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 1,437.3.

3.5.3 Utawala wa Kidijitali

Mpango uliwezesha kuunganisha mifumo 252 ya taasisi 200 kupitia GovESB, ikiwemo mifumo mipya 28; kuzindua Orodha ya Huduma za Serikali (Government Services Directory) tarehe 24 Juni 2026 ikiwa na huduma 9,777 za taasisi 554; kuzindua Mfumo wa Ngao wa usalama wa mtandao unaotumiwa na taasisi zaidi ya

700; kuunganisha taasisi 147 na mfumo wa NIDA; na kuanza kutumika kwa mfumo wa e-Utendaji katika taasisi zote 571 za umma.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: watu waliosajiliwa na NIDA waliongezeka kutoka 879,213 mwaka 2024/25 hadi kufikia watu 1,772,985 mwaka 2025/26, na kufikisha jumla ya watu 27,374,283 hadi kufikia Juni 2026; taasisi zinazotumia mfumo wa e-Office zilifikia 425 kati ya 571 na zinazotumia saini za kidijitali 528 kati ya 780 Juni 2026.

3.5.4 Uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi

Mpango uliwezesha uboreshaji wa taswira ya Tanzania katika medani ya kimataifa kwa kuimarisha diplomasia ya siasa na uchumi kupitia ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa; kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika jumuiya na mashirika ya kikanda na kimataifa kwa maslahi ya Taifa; na kuchangia juhudi za kukuza amani, ulinzi na usalama kwa maendeleo jumuishi.

Utekelezaji wa Mpango umechangia: kuongezeka kwa uwakilishi wa Tanzania nje kupitia balozi 45 na konseli kuu tano; kuimarika kwa ushiriki wa Tanzania katika mikutano mbalimbali na kufanikisha Tanzania kushiriki mikutano 110 ya kikanda na kimataifa; Kufanyika kwa ziara 90 za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nje ya nchi na ziara 33 za viongozi wa nchi, Serikali na Mashirika mbalimbali nchini Tanzania. Aidha, ziara na mikutano hiyo imewezesha kusainiwa kwa mikataba na hati za makubaliano 81, kuanzishwa kwa safari za ndege za moja kwa moja katika baadhi ya vituo vya kimkakati, kuongezeka kwa mchango wa Diaspora katika maendeleo ya Taifa, pamoja na Tanzania kupata nafasi za kimkakati katika jumuiya za kikanda na kimataifa.

Vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha matumizi na uenezaji wa Kiswahili katika ngazi ya kikanda na kimataifa. Juhudi hizo zimechangia kuongezeka kwa idadi ya nchi na watu wanaojifunza na kutumia Kiswahili, pamoja na kuimarisha nafasi ya lugha hiyo katika majukwaa ya kimataifa.

SEHEMU B: MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2026/27 KWA ROBO YA KWANZA

Serikali imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 kwa kuzingatia FYDP IV ili kufikia malengo ya Dira 2050. Katika kipindi cha mwaka 2026/27, Serikali ililenga kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani, kujenga uwezo wa watu na maendeleo ya jamii, uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, kutumia kikamilifu vichocheo vya maendeleo, mageuzi katika sekta za kimkakati, na kuimarisha misingi ya uendelevu wa taifa.

Katika kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani: Serikali imeendelea kudhibiti mfumuko wa bei, kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kuhakikisha kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje, kuimarisha ukuaji wa uchumi, kusimamia matumizi ya Serikali pamoja na sera za fedha na bajeti.

Kujenga uwezo wa watu na maendeleo ya jamii: Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo, 2014 toleo la 2023 kwa kuandaa na kutekeleza mitaala mipya, ili kujenga rasilimaliwatu yenye ujuzi unaohitajika kufikia malengo ya Dira 2050. Aidha, Serikali imeendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na ruzuku ya elimu bila ada kwa shule za msingi na sekondari, pamoja na kutekeleza miradi ya HEET, ESPJ II, EP4R, Support to VET, SEQUIP, GPE-TSP na Mfuko wa Elimu Tanzania. Vilevile, Serikali inaendelea kutoa ufadhili kupitia Samia Scholarship kwa wanafunzi kusoma Sayansi ya Data na Akili Unde nje ya nchi. Serikali imeendelea kuongeza fursa za ajira kupitia miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa na utekelezaji wa miradi mbalimbali. Aidha, Serikali inaendelea kuwajengea uwezo makandarasi wazawa na kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Urasimishaji wa Wafanyabiashara Ndogondogo ili kuwawezesha kiuchumi.

Serikali imeendelea kuwawezesha vijana kiuchumi kupitia upatikanaji wa mitaji, ujuzi na fursa za uzalishaji, ambapo mikopo 1,473 imetolewa kwa vikundi vya vijana vyenye wanufaika 40,263, huku vijana 30,137 wakipatiwa elimu ya fedha, ujasiriamali, usimamizi wa biashara na fursa za kiuchumi. Aidha, vituo viwili vya

ubunifu vimetathminiwa kwa ajili ya ukarabati na kuimarisha ufanisi, na vikundi saba (07) vya vijana vyenye wanachama 80 vimeunganishwa na kuunda Vijana AMCOS, vikapatiwa mkopo wa pembejeo na zana za kilimo wenye thamani ya shilingi milioni 361.63 pamoja na kutengewa ekari 300 kwa ajili ya uzalishaji wa mahindi.

Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi: Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa mazingira kupitia utekelezaji wa shughuli mbalimbali, ikiwemo utoaji wa vibali kwa miradi mikubwa inayohitaji Tathmini za Athari kwa Mazingira na Kaguzi za Mazingira, ambapo vyeti 189 vya mazingira vilitolewa. Aidha, vibali 66 vya usimamizi wa taka hatarishi vilitolewa kwa wadau, hatua iliyowezesha usimamizi salama na urejelezaji wa taka hizo. Serikali pia imeendelea kuratibu hatua za kukabiliana na athari za mvua za El Niño katika maeneo ya mijini na vijijini, kuhamasisha matumizi ya nishati safi katika taasisi za umma, pamoja na kuratibu biashara ya kaboni, ambapo mapato yatokanayo na mauzo ya nje ya viwango vya kaboni yameongezeka kufikia Dola milioni 2. Aidha, mapato ya utalii yalifikia shilingi bilioni yalifikia bilioni 1.07.

Kutumia kikamilifu vichocheo vya maendeleo: Serikali imeendelea na ujenzi wa Reli ya Kati ya SGR ambapo hadi Agosti 2026 utekelezaji wa vipande vya Dar es Salaam – Morogoro (km 300) umekamilika na Morogoro – Makutupora (km 422) asilimia 98.79, Makutupora – Tabora (km 368) asilimia 15.54, Tabora – Isaka (km 165) asilimia 9.12; Isaka – Mwanza (km 341) asilimia 69.31, Tabora – Kigoma (km 506) asilimia 11.35 na Uvinza – Musongati (km 282) asilimia 0.62. Aidha, ujenzi wa viwanja vya ndege katika mikoa mbalimbali unaendelea na imefikia hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo, viwanja vya ndege vya Sumbawanga, Tabora na Geita ujenzi wake umekamilika. Ujenzi wa kiwanja cha Ndege cha Kigoma umefikia asilimia 75.5, Shinyanga (asilimia 97.5), Musoma (asilimia 70), Iringa (Awamu ya II) (asilimia 47), Tanga (asilimia 11.18), Moshi (asilimia 69), na Lake Manyara (asilimia 12.2). Aidha usimikaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege katika kiwanja cha ndege cha Arusha umekamilika. Vilevile, huduma ya Mkongo wa Taifa inaendelea kusambazwa katika wilaya

mbalimbali nchini, na ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam unaendelea kuimarika kupitia ushiriki wa sekta binafsi.

Katika utekelezaji wa Mradi wa Reli ya TAZARA kwa upande wa Tanzania: upembuzi yakinifu na usanifu wa reli umefikia asilimia 95; maandalizi ya michoro na usanifu wa jengo la kuongozea treni, kituo cha mafunzo, Stesheni ya Kurasini na ukarabati wa Stesheni ya Dar es Salaam vimekamilika; ujenzi wa karakana ya Kongolo umefikia asilimia 85; ununuzi wa tani 5,250 za reli umekamilika; na mikataba ya ununuzi wa mabehewa 760 na utengenezaji wa vichwa vitatu vya treni vilisainiwa, ambapo uzalishaji wa mabehewa 300 na vichwa hivyo ulianza nchini China. Aidha, mradi umeajiri Watanzania takribani 296.

Serikali imepiga hatua katika kuongeza mtandao wa usambazaji wa gesi asilia na uwezo wa kuzalisha umeme hivyo kuweka msingi imara wa upatikanaji wa nishati ya uhakika kwa shughuli za uzalishaji na matumizi ya nyumbani. Aidha, uzalishaji wa gesi asilia ulikuwa futi za ujazo milioni 16,778, uwezo wa mitambo ya uzalishaji wa umeme ulifika MW 4,606.14, urefu wa Gridi ya Taifa ya umeme uliongezeka hadi km 8,845.38, kuunganishwa na umeme kwa vijiji vyote 12,318 na vitongoji 41,038 kati ya 64,359 sawa na asilimia 64, kuongezeka kwa vituo vya kujazia gesi asilia kwenye vyombo vya moto kufikia 22, na ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania (EACOP) umefikia asilimia 92.7. Vilevile, huduma ya Mkongo wa Taifa inaendelea kusambazwa katika wilaya mbalimbali nchini, na ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam unaendelea kuimarika kupitia ushiriki wa sekta binafsi.

Mageuzi katika sekta za kimkakati: Serikali imeendelea kuimarisha usalama wa chakula, kupunguza upotevu wa mazao na kuongeza mauzo ya nje ya mazao ya kilimo. Vilevile, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya biashara, hatua iliyowezesha kuongezeka kwa uwekezaji wa moja kwa moja na kupungua kwa muda wa kuanzisha biashara. Hadi Septemba 2026, uwekezaji wa miradi ya Ubia wa sekta ya umma na sekta binafsi umeongezeka na kufikia miradi kumi (10). Miradi hiyo inajumuisha: ujenzi wa kituo cha biashara Kariakoo; ujenzi wa kituo cha usaifirishaji; uendeshaji na ukarabati wa bandari ya Dar es Salaam; ukarabati, uendeshaji, na usimamizi wa reli ya Tanzania - Zambia (TAZARA); ujenzi wa vituo

vya ukaguzi wa magari; na uendeshaji wa mabasi yaendayo haraka Awamu ya Kwanza na ya Pili Dar es Salaam.

Katika maeneo mengine, Serikali inaendelea na umilikishaji wa viwanja na mashamba, ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama, na uendelezaji wa michezo, sanaa na ubunifu. Serikali imeendelea kuongeza upatikanaji wa taarifa za msingi za rasilimali madini kupitia utafiti wa kina wa jiofizikia, jiokemia na jiolojia. Hadi Septemba 2026, Sekta ya Madini imefanikiwa kubaini maeneo yatakayofanyiwa utafiti kupitia Mfuko wa Utafiti wa Madini; kuzindua programu ya kuendeleza wanawake vijana na makundi maalumu (Mining for Brighter Tomorrow - MBT) ambao utekelezaji wake umeanza kwa kutoa leseni 273 kwa vikundi 2,550 vya wachimbaji katika Mikoa ya Mara, Kagera, Shinyanga, Morogoro, Dodoma na Njombe; kuzindua programu ya kuendeleza wachimbaji wadogo; kuendelea kusimamia makusanyo ya maduhuli ya takribani shilingi bilioni 411.7; na kuendelea kushirikiana na wawekezaji kusimamia ujenzi wa miradi mikubwa ya madini ikiwemo ya Sengerema, Mantra na Mradi wa Niobium wa Panda Hili.

Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi na matumizi bora ya ardhi kupitia upimaji, urasimishaji, upangaji na usajili wa milki. Asilimia ya ardhi iliyopimwa imefikia asilimia 28, huku viwanja na mashamba mashamba na viwanja vilivyopimwa ikifikia 59,795. Aidha, mali 48,713 katika makazi yasiyopangwa zimerasimishwa na leseni 3,239 za makazi zimetolewa kwa wamiliki wa mali. Vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha mipango ya matumizi bora ya ardhi vijijini, huku ramani 88 za msingi zikiwa zimehuishwa, na Hatimiliki za Milki (CROs) 41,843 zimesajiliwa katika kipindi hicho. Vilevile, jumla ya hekta 265,804.51 zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji na ekari 875,360 zimetengwa na kulindwa kwa matumizi ya umma.

Serikali imewezesha kusainiwa kwa Mikataba na Hati za Makubaliano 16 katika sekta za kilimo, madini, ajira, usafirishaji na utalii. Aidha, ushirikishwaji wa Diaspora umeimarishwa kupitia Diaspora Mapping na uzinduzi wa Zanzibar Diaspora Registration Portal, huku juhudi za kukuza Kiswahili zikiendelea katika nchi mbalimbali. Vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha taswira ya Tanzania nje ya nchi kupitia ujenzi na ukarabati wa majengo ya

uwakilishi, ikiwemo Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu Arusha (asilimia 59), Ubalozi Tanzania Uingereza (asilimia 38) na Ubalozi Tanzania Marekani (asilimia 35).

Sekta za michezo na ubunifu imeendelea kuimarika ambapo Tanzania imepiga hatua katika viwango vya kimataifa vya michezo, hususan kwa wanawake, huku nafasi katika viwango vya CAF ikifikia nafasi ya 18 kwa wanawake. Aidha, wachezaji 1,075 wameendelea kushiriki michezo ya kitaalamu, wakiwemo wanaume 825 na wanawake 250, huku wasanii watatu (03) wa muziki na wadau sita (06) wa filamu wakipokea tuzo za kimataifa. Vilevile, miradi 48 ya filamu imepatiwa mikopo, hatua inayochochea uwekezaji, ajira na ukuaji wa sekta za ubunifu na maudhui ya kidijitali.

Kuimarisha misingi ya uendelevu wa taifa: Serikali imeendelea kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika utumishi wa umma kupitia utoaji wa mafunzo ya maadili ya utendaji kwa watumishi 1,474 na kuwezesha taasisi za umma 22 kutumia Mfumo wa e-Mrejesho, hatua inayolenga kuongeza uwajibikaji, uwazi na mapambano dhidi ya rushwa katika utumishi wa umma.

SURA YA NNE

VIPAUMBELE VYA MPANGO KWA MWAKA 2027/28

4.1 Utangulizi

Vipaumbele vya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 vimeandaliwa kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele, malengo, shabaha na afua za kimkakati zilizoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 (FYDP IV). Vipaumbele hivi vinachangia katika utekelezaji wa malengo, shabaha na matarajio ili kufikia lengo kuu la Dira 2050 inayolenga kuifanya Tanzania kuwa taifa jumuishi lenye ustawi, haki na linalojitegemea.

4.2 Maeneo ya Kipaumbele ya Mpango

Mapendekezo ya Mpango kwa mwaka 2027/28 yamejikita katika maeneo sita (6) ya kimkakati yaliyoainishwa katika FYDP IV ambayo ni: (i) Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani; (ii) Kujenga Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii; (iii) Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi; (iv) vichocheo vya maendeleo; (v) Mageuzi katika Sekta za Kimkakati; na (vi) Kuimarisha Misingi ya Uendelevu wa Taifa

4.2.1 Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani

Kipaumbele hiki kinalenga kuweka mazingira thabiti ya usimamizi wa uchumi, kuongeza imani ya wawekezaji na kuwezesha utabirifu wa mwenendo wa uchumi. Maeneo yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na:

4.2.1.1 Utulivu na Utabirifu wa Uchumi Jumla

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kufikia ukuaji wa uchumi wa asilimia 6.6 mwaka 2027. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuhakikisha uthabiti wa sera za bajeti;

(ii) Kuimarisha ushirikiano wa kimataifa;

(iii) Kuongeza uwezo wa ufuatiliaji na kujenga uwezo wa kukabiliana na athari za mitikisiko ya nje;

(iv) Kutekeleza mageuzi ya kimfumo yatakayolenga kuboresha na kupanua minyororo ya ugavi wa ndani;

(v) Kudhibiti mfumuko wa bei za chakula; na

(vi) Kuongeza matumizi ya mifumo ya kidijitali katika malipo.

4.2.1.2 Kuimarisha Uwezo wa Kifedha wa Serikali

Katika mwaka 2027/28, Mapendekezo ya Mpango yanalenga kudumisha nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3 ya Pato la Taifa. Ili kufikia malengo hayo, vipaumbele vitakua katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha usimamizi wa vihatarishi vya kifedha;

(ii) Kuongeza uhimilivu wa kiuchumi;

(iii) Kufungua vyanzo vipya vya mapato yasiyo ya kodi; na

(iv) Kuboresha matumizi ya rasilimali za umma.

4.2.1.3 Uhimilivu na Usetushaji wa Sekta ya Nje

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kudumisha nakisi ya urari wa malipo ya kawaida usiozidi asilimia 2.5 ya Pato la Taifa. Ili kufikia shabaha hizo utekelezaji katika afua zifuatazo:

(i) Kupunguza utegemezi wa bidhaa ghafi;

(ii) Kujenga uchumi mseto wa uzalishaji na mauzo ya nje yaliyoongezwa thamani;

(iii) Kuongeza uzalishaji viwandani na uchakataji wa bidhaa za kilimo;

(iv) Kuwekeza katika mifumo ya uwezeshaji wa biashara na miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi; na Kuimarisha mtangamano katika biashara ya kikanda

4.2.2 Mageuzi katika Sekta za Kimkakati

4.2.2.1 Sekta ya Kilimo

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kufikia ukuaji wa sekta ya kilimo wa asilimia 6.46 mwaka 2027/28 na mapato ya mauzo ya nje ya sekta ya kilimo kufikia dola za Marekani bilioni 4.12. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuongeza thamani ya bidhaa za kilimo;

(ii) Kuzalisha bidhaa bora na ajira zenye staha;

(iii) Kujenga kongani za viwanda na kuendeleza ujuzi;

(iv) Kuongeza wigo wa upatikanaji wa mitaji kwa wakulima na wawekezaji wadogo na kati;

(v) Kuimarisha mifumo ya udhibiti;

(vi) Kuasili matumizi ya teknolojia za kidijitali ili kuimarisha ufuatiliaji wa vyanzo wa mazao na huduma za ugani;

(vii) Kuimarisha miundombinu wezeshi kwa ajili ya kuongeza mauzo ya nje ya mboga mboga;

(viii) kukuza ufugaji wa samaki katika maziwa na maeneo ya nchi kavu; na

(ix) Kuhimiza matumizi ya mbinu bora za kilimo.

4.2.2.2 Sekta ya Viwanda

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza mchango wa sekta ya uzalishaji viwandani kufikia asilimia 7.58 ya Pato la Taifa mwaka 2027/28 na mchango wake katika mapato ya mauzo ya

nje kufikia asilimia 12. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuendeleza kongani za viwanda na maeneo maalumu ya uchumi;

(ii) Kuendeleza viwanda vya kimkakati;

(iii) Kukuza ubunifu kupitia maeneo mahsusi ya ukuzaji wa teknolojia;

(iv) Kujenga ikolojia ya mfumo imara wa viwanda unaojiendesha kwa ufanisi;

(v) Kuziunganisha biashara ndogo, za kati na kubwa, katika minyororo ya biashara ya ugavi ya kimataifa;

(vi) Kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula;

(vii) Kukuza viwanda vya nguo na mavazi;

(viii) Kuongeza thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi; na

(ix) Kuzingatia viwango vya kimataifa vya ubora wa bidhaa na mazingira.

4.2.2.3 Sekta ya Ujenzi

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza mchango wa sekta ya ujenzi kufikia asilimia 13.88 ya Pato la Taifa mwaka 2027/28. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuwezesha wakandarasi na makampuni ya ndani ya ujenzi kushindana na kuongeza ushiriki katika miradi mikubwa ya ujenzi;

(ii) Kuwezesha matumizi ya mifumo ya kuasili na uhawilishaji wa teknolojia za kisasa za ujenzi, sambamba na hatua za kuendeleza ujuzi wa wahandisi wa ndani; na

(iii) Kuongeza tija, ubora na kuinua ufanisi katika sekta ya ujenzi.

4.2.2.4 Sekta ya Madini na Uchimbaji

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza mchango wa sekta ya madini kufikia asilimia 11.06 ya Pato la Taifa mwaka 2027/28 na mchango wake katika mapato ya mauzo ya nje kufikia asilimia 49.6. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:-

(i) Kuvutia uwekezaji mkubwa katika uchenjuaji, usafishaji, uchakataji na utumiaji wa madini kwa ajili ya kutengeneza bidhaa za viwandani zenye thamani kubwa;

(ii) Kukamilisha utafiti wa kijiolojia;

(iii) Kuimarisha usimamizi wa uendeshaji wa sekta ya madini;

(iv) Kuimarisha nafasi ya Tanzania katika soko la kimataifa la madini; na

(v) Kurasimisha na kusaidia wachimbaji wadogo kwa kuwawezesha wanawake na vijana.

4.2.2.5 Sekta ya Mafuta na Gesi

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza mtandao wa usambazaji wa gesi asilia kufika kilometa 289.57. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kukuza matumizi ya gesi asilia, ukichagizwa na mikakati ya kujenga uchumi wa viwanda vya ndani; na

(ii) Kuanzisha kituo cha umahiri cha kuendeleza ujuzi unaohitajika katika sekta.

4.2.2.6 Sekta ya Utalii

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza mchango wa sekta ya utalii katika mapato ya mauzo ya nje kufikia asilimia 30.2. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuendeleza utalii wa kimataifa wa fukwe, utamaduni, matukio na mikutano; na

(ii) Kuongeza msukumo katika uwekaji wa mifumo ya kidijitali kupitia majukwaa ya utalii mamboleo.

4.2.2.7 Sekta ya Fedha

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza ujumuishaji, upanuzi, na uimara wa huduma za fedha. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha usimamizi wa vihatarishi, na kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha kwa biashara ndogo na za kati, sekta ya kilimo na wakazi wa vijijini;

(ii) Kuimarisha taasisi za fedha za maendeleo na kukuza ikolojia ya upatikanaji wa mitaji ya ubia;

(iii) Kuimarisha masoko ya mitaji; na

(iv) Kupanua wigo wa huduma za bima, sanjari na kuendesha programu za elimu ya fedha kitaifa.

4.2.2.8 Sekta ya Michezo, Sanaa na Ubunifu

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza ukuaji halisi wa sekta ya michezo, sanaa na ubunifu kufikia asilimia kufikia asilimia 10. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kukuza biashara, weledi na upatikanaji wa mapato kutokana na kazi za ubunifu;

(ii) Kujenga minyororo jumuishi ya thamani kupitia uwekezaji katika miundombinu, maendeleo ya vipaji, mifumo ya fedha na biashara ya kazi za ubunifu;

(iii) Kujenga vyuo vya kikanda vya vijana vya kukuza vipaji na kituo cha kitaifa cha michezo ya ubora wa juu na ubunifu;

(iv) Kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya viwanja kwa ajili ya AFCON; na

(v) Kuboresha mfumo wa usajili wa waandaaji wa maudhui ya kidijitali, ulinzi wa hakimiliki, na ukuzaji wa ushirikiano na majukwaa ya kimataifa ya kidijitali.

4.2.2.9 Maendeleo ya Makazi na Biashara ya Ardhi na Majengo

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza ardhi iliyopimwa kufikia asilimia 42.92. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha usimamizi wa ardhi, kupanua upatikanaji wa fedha za ujenzi wa nyumba, na kuharakisha maendeleo ya miji iliyopangwa;

(ii) Kulinda haki miliki za ardhi, kuboresha mifumo ya umiliki, kuongeza matumizi ya mifumo ya kidijitali katika umilikishaji wa ardhi na miamala, pamoja na kuongeza upatikanaji wa ardhi iliyopimwa iliyohudumiwa na iliyopangwa vizuri;

(iii) Kuimarisha taasisi za fedha za nyumba, kupunguza gharama za mikopo ya nyumba kuongeza matumizi ya masoko ya mitaji kupitia dhamana za uwekezaji katika majengo; na

(iv) Kuboresha maendeleo ya miji ya kisasa yatakayoimarisha upatikanaji wa usafiri wa umma, maeneo ya biashara na vituo vya ugavi.

4.2.2.10 Mageuzi ya Biashara na Shughuli za Kibiashara

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza thamani ya mauzo ya nje kwa Pato la Taifa kufikia asilimia 21.1 na kuongeza mchango wa Tanzania kwenye biashara baina ya nchi wanachama kikanda kufikia asilimia 17.8. Ili kufikia malengo hayo, vipaumbele vitakuwa katika afua zifuatazo:

(i) Kuondoa utegemezi wa mauzo ya bidhaa ghafi na kuelekea katika mfumo shindani unaotumia teknolojia ya kidijitali na kushiriki kikamilifu katika minyororo ya thamani ya kikanda na kimataifa;

(ii) Kutumia kikamilifu fursa za usindikaji wa mazao ya kilimo, matumizi ya madini yanayohitajika katika uzalishaji wa bidhaa muhimu za viwandani, pamoja na uwekezaji adilifu katika utafiti na maendeleo;

(iii) Kujenga majukwaa ya kisasa ya biashara mtandao na mifumo ya malipo ya kidijitali katika biashara za kikanda na kimataifa;

(iv) Kuimarisha biashara ya ndani na miundombinu ya masoko na maghala; na

(v) Kuwezesha ushiriki wa wafanyabiashara ndogo na za kati, wanawake na Vijana katika minyororo ya thamani ya kikanda na kimataifa.

4.2.2.11 Kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza mchango wa uwekezaji wa sekta binafsi kwenye rasilimali za kudumu kufikia asilimia 77. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kufanya mapitio ya kina ya mfumo wa taasisi, udhibiti na urekebu, kupunguza gharama za kutimiza masharti, kurahisisha taratibu za kisheria, kutoa motisha kwa wafanyabiashara, na kujenga mazingira ya biashara yanayokidhi viwango vya kimataifa;

(ii) Uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu na teknolojia za kidijitali, katika biashara ndogo na za kati, kuziwezesha kujiunga na minyororo ya thamani ya Kimataifa; na

(iii) Kuwekeza katika viwanda vinavyotumia nguvukazi kwa wingi, hususan katika mikoa yenye kiwango cha chini cha maendeleo ya kiuchumi pamoja na kuimarisha ushiriki wa Watanzania katika uwekezaji wa kigeni kupitia mifumo ya kisheria na kiutendaji.

4.2.2.12 Mikakati ya Ushirikiano kati ya Nchi, Kikanda na Kimataifa katika Dunia Inayobadilika

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza hisa za uwekezaji wa nje kufikia dola za Marekani milioni 386.18. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi;

(ii) Kutumia kikamilifu shughuli za kidiplomasia katika kutangaza biashara na uwekezaji;

(iii) Kubaini na kutumia fursa za ushirikiano na washirika wa kimkakati kwa kuzingatia mabadiliko ya uchumi wa dunia, maslahi ya Taifa na fursa za uwekezaji, biashara, teknolojia na maendeleo ya viwanda na

(iv) Kusasisha miundombinu ya biashara, usafirishaji na uchukuzi kwa kuwekeza katika bandari za kisasa, matumizi ya akili unde, mifumo ya kidijitali ya biashara na usimamizi wa kanzidata, pamoja na nyenzo za kisasa za kidiplomasia.

4.2.2.13 Urasimishaji wa Uchumi na Usimamizi Wake

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kupunguza mchango wa sekta isiyo rasmi katika Pato la Taifa kufikia asilimia 44.6. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kupunguza vikwazo vya kiutawala na kifedha vinavyokwamisha biashara, kwa kuunganisha biashara mbalimbali katika mkondo wa uchumi rasmi;

(ii) Kuanzisha mifumo ya kidijitali ya usajili kupitia taasisi moja, kutoa motisha zinazolenga biashara mahsusi, pamoja na utekelezaji wa programu za kuinua ujuzi; na

(iii) Kutoa fursa kwa biashara zisizo rasmi kuingia katika minyororo rasmi ya ugavi, kupata mikopo na ulinzi wa kisheria.

4.2.3 Kujenga Uwezo wa Rasilimali Watu na Maendeleo ya Jamii Eneo hili linalenga kuimarisha uwekezaji katika elimu, afya, huduma za maji safi na salama ili kujenga nguvukazi yenye afya, maarifa na ujuzi unaokidhi mahitaji ya soko la ajira. Maeneo muhimu yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na:

4.2.3.1 Jamii Iliyoelimika, Yenye Ujuzi na Inayojifunza

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha IV kwenda V kufikia asilimia 26.24. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za malezi na makuzi ya watoto na elimu bora ya awali kwa wote ili kuimarisha maandalizi yao ya kielimu na maisha;

(ii) Kuwekeza kimkakati katika maendeleo ya walimu, hususan katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati;

(iii) Kuendelea na maandalizi ya kundi rika mbili (Double cohort) na

(iv) Kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia kwa kutumia zana za kidijitali na miundombinu ya kisasa.

4.2.3.2 Nguvukazi Yenye Uwezo na Ari

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza nguvukazi yenye uwezo wa juu kufikia asilimia 6.6, na yenye uwezo wa kati asilimia 21. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuwianisha mifumo ya elimu na mafunzo ili kuendana na mahitaji ya sasa ya uchumi wa viwanda; na

(ii) Kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za elimu na sekta ya uzalishaji kwa kuweka msisitizo wa mafunzo kwa vitendo kwa ubia kati ya sekta za umma na binafsi.

4.2.3.3 Demografia na Idadi ya Watu

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kupunguza kiwango cha utegemezi wa umri kufikia asilimia 84.2. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuwianisha kwa makusudi, mifumo ya elimu na mafunzo ya ufundi na stadi za kazi na mahitaji halisi ya ujuzi kwa uchumi wa kisasa;

(ii) Kujenga utamaduni wa ujasiriamali kwa vijana na kuwaunganisha na fursa za uchumi wa kidijitali na ajira mtandao;

(iii) Kuimarisha usawa wa kijinsia kwa kuwawezesha wanawake na vijana;

(iv) Kukuza ushiriki wenye tija wa watanzania waishio ughaibuni; na

(v) Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya ya uzazi na mifumo imara ya kinga ya jamii kwa wazee.

4.2.3.4 Soko na Taratibu za Ajira

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza kiwango cha ushiriki wa nguvukazi kufikia asilimia 73.76. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kupunguza utegemezi wa ajira katika shughuli zisizo rasmi na zenye tija ndogo na kujielekeza kwenye ajira zenye staha na tija kubwa kwa kuweka mazingira wezeshi ya kukuza biashara changa, ndogo na za kati zinazotumia teknolojia za kisasa;

(ii) Kuweka mazingira ya kuvutia uwekezaji mkubwa unaotoa ajira nyingi kwa wakati mmoja;

(iii) Kuwianisha moja kwa moja uendelezaji wa ujuzi na mahitaji halisi ya sekta zenye kasi kubwa ya ukuaji; na

(iv) Kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji wa ubia kati ya sekta za umma na binafsi.

4.2.3.5 Jamii Yenye Hifadhi na Muundo Jumuishi

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza kiwango cha waliojiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii kufikia asilimia 13.31. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuunganisha sekta isiyo rasmi katika mifumo ya kinga ya jamii;

(ii) Kubadili mifumo ya kinga ya jamii kwa kushirikisha sekta binafsi na kuongeza kipato na shughuli za kujikimu;

(iii) Kuimarisha usalama wa watumishi katika maeneo ya kazi; na

(iv) Kujumuisha huduma muhimu, ikiwemo afya ya akili katika mifumo ya elimu na maisha.

4.2.3.6 Huduma Bora za Afya kwa Wote

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kupunguza kiwango cha vifo vya watoto wachanga kufikia 30.6 kwa kila vizazi hai 1000, na kuongeza kiwango cha wazazi wanaohudumiwa na wataalamu wa afya kufikia asilimia 86.12. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo: -

(i) Kuimarisha kinga dhidi ya magonjwa kama malaria;

(ii) Kuwekeza katika mifumo ya afya ya kinga, ubunifu wa kidijitali na uzalishaji wa bidhaa za afya nchini;

(iii) Kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya;

(iv) Kuwekeza katika wataalamu wa afya;

(v) Kuimarisha uwekezaji wa viwanda vya uzalishaji dawa na vifaa tiba nchini;

(vi) Kuendelea na ujenzi wa hospitali bingwa na bobezi kwa ajili ya tiba utalii; na

(vii) Kuongeza huduma za bima ya afya kwa wote.

Usalama wa Chakula na Lishe Ulioimarishwa

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kupunguza kiwango cha utapia mlo mkali wa dharura wa watoto wenye umri wa miezi 0 – 59 kufikia asilimia 2.46 na kupunguza kiwango cha udumavu kwa watoto wenye umri wa miezi 0 – 59 kufikia asilimia 23.9. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuongeza upatikanaji wa vyakula vyenye virutubisho muhimu;

(ii) Kuhakikisha usalama wa chakula;

(iii) Kuwekeza katika kilimo kinachostahimili athari za mabadiliko ya tabianchi;

(iv) Kupunguza upotevu baada ya mavuno; na

(v) Kuimarisha minyororo ya thamani.

4.2.3.7 Upatikanaji na Uunganishaji wa Maji na Usafi wa Mazingira

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza upatikanaji wa maji katika maeneo ya mjini na vijijini kufikia asilimia 93.4 na 85.76 mtawalia. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kubadili mwelekeo kutoka kuongeza huduma za usambazaji pekee na kuwekeza katika usimamizi jumuishi, wenye ufanisi na unaostahimili athari za mabadiliko ya tabianchi;

(ii) Kuendeleza matumizi ya nishati jadidifu hususan katika mifumo ya maji inayotumia umeme wa jua;

(iii) Kuimarisha usimamizi, uhifadhi, na uendelezaji wa rasilimali za maji; na

(iv) Kuhakikisha huduma bora za usafi wa mazingira kwa wote.

4.2.3.8 Jamii yenye Mshikamano, Inayowajibika na Kushirikiana

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kupunguza kiwango cha ukatili wa kijinsia kufikia asilimia 31.34. na kupunguza alama ya wastani ya farihisi ya uhalifu kufikia 51.04. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kukuza usawa wa kijinsia kupitia mageuzi ya kisheria na programu za kimkakati za uongozi kwa wanawake katika sekta zote;

(ii) Kuweka mkazo katika maadili kupitia mfumo wa elimu;

(iii) Kuimarisha malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto;

(iv) Kuimarisha familia katika malezi na makuzi; na

(v) Kuhamasisha majadiliano ya kijamii kupitia sanaa na utamaduni.

4.2.3.9 Maendeleo Jumuishi Vijijini

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza farihisi ya maendeleo vijijini kufikia 0.38. Ili kufikia malengo hayo, vipaumbele vitakua katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha usalama wa umiliki wa ardhi,

(ii) Kuwekeza katika miundombinu ya kilimo inayostahamili mabadiliko ya tabianchi;

(iii) Kuboresha barabara vijijini; na

(iv) Kuongeza upatikanaji wa huduma na elimu za kifedha kwa wanawake na vijana.

4.2.3.10 Mageuzi ya Vyama vya Ushirika

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika kufikia 13,231,000. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuboresha miundo na mifumo ya utawala wa vyama vya ushirika ili kuongeza uwajibikaji , uwazi na ushindani; na

(ii) Kuongeza upatikanaji wa mitaji kwa gharama nafuu.

4.2.3.11 Kupanua Tabaka la Kipato Cha Kati

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza idadi ya watu walioko katika tabaka la kipato cha kati kufikia

asilimia 14.4. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuinua kipato cha jamii kwa kutumia njia mseto na jumuishi;

(ii) Kuwawezesha wananchi kumiliki ardhi na mali zisizohamishika; na

(iii) Kuendeleza sekta za uchumi wa kijani na buluu.

4.2.4 Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi Eneo hili linalenga kujenga uchumi endelevu, unaostahimili mabadiliko ya tabianchi na unaotumia maliasili kwa ufanisi, huku ukilinda mazingira, kuongeza fursa za kiuchumi na kuboresha ustawi wa wananchi. Maeneo mahsusi ya kipaumbele ni:

4.2.4.1 Uhifadhi wa Mazingira

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza nafasi ya Tanzania katika nchi za Afrika kwenye farihisi katika kukabiliana na athari za mazingira kufikia 16.8 na farihisi ya utendaji katika uhifadhi wa mazingira kufikia 17.4. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa mazingira;

(ii) Kukabiliana na athari za El-Nino;

(iii) Kuzingatia vigezo vya mazingira, utawala bora katika uwekezaji na ugharamiaji wa miradi; na

(iv) Kuiwezesha jamii kulinda rasilimali katika maeneo yao na kuchochea ukuaji wa uchumi unaotokana na uhifadhi wa mazingira.

Ukuaji Endelevu wa Miji Iliyopangika na Kusimamiwa Vizuri

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kupunguza kiwango cha ardhi yenye makazi yasiyo rasmi kufikia asilimia 45.4

na kuongeza mikoa yenye mipango kabambe na mipango miji kufikia asilimia 88.6. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuchukua hatua zinazozingatia mbinu za kisasa za usimamizi wa ujenzi wa miji;

(ii) Kuimarisha afya na ustawi wa wananchi kwa kutumia mifumo ya kisasa, mathalan mifumo ya usafiri wa umma ya kisasa; na

(iii) Kutumia mfumo wa ubia kati ya serikali na sekta binafsi katika kupunguza nakisi ya nyumba za makazi.

4.2.4.2 Mageuzi kwa Usimamizi Endelevu wa Ardhi

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza kiwango cha ardhi iliyosajiliwa na kupatiwa hatimiliki kufikia asilimia 40. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kujumuisha masuala ya tabianchi katika mipango ya maendeleo;

(ii) Kuhamasisha mbinu bunifu za fedha, kama hatifungani za kijani, ili kugharamia afua za maendeleo;

(iii) Kufanya maboresho ya kina ya sheria yatakayowezesha upatikanaji wa ardhi kwa usawa;

(iv) Kuanzisha mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa ardhi;

(v) Kuanzisha benki ya kitaifa ya ardhi; na

(vi) Kuandaa mipango maalumu ya matumizi ya ardhi kwa maendeleo ya viwanda.

4.2.4.3 Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kupunguza kiwango cha uharibifu wa ardhi kufikia asilimia 15.2. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kufungamanisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika mipango ya kitaifa;

(ii) Kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu na teknolojia zinazozingatia athari za mabadiliko ya tabianchi katika kilimo, uchukuzi na viwanda;

(iii) Kuweka mifumo imara ya taifa ya kukabiliana na athari za mazingira; na

(iv) Kuongeza bima dhidi ya vihatarishi vya kimazingira.

4.2.4.4 Uwezo wa Taasisi na Mifumo ya Utoaji wa Tahadhari

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza idadi ya watu wanaopata taarifa tahadhali ya mapema kwa wakati sahihi kufikia asilimia 13.2.

4.2.4.5 Kuimarisha ushiriki katika Biashara ya Kaboni

(i) Kujenga mfumo wa kidijitali wa kiwango cha kimataifa wa ufuatiliaji, upimaji, utoaji taarifa na uthibitishaji;

(ii) Kuanzisha mfumo wazi wa uhifadhi wa kumbukumbu za kitaifa unaothibitisha uadilifu na kuvutia mitaji ya kimataifa ya programu na biashara za kaboni;

(iii) Kutengeneza kanzidata ya miradi inayokidhi masharti ya biashara ya kaboni katika sekta za misitu, uchumi wa buluu na mbinu endelevu za uendeshaji wa kilimo; na

(iv) Kuweka mifumo ya uwazi inayowezesha ushiriki wa jamii, vyama vya ushirika vya maeneo husika, pamoja na mgawanyo wa manufaa kutasaidia kuhakikisha kuwa biashara hii inakuwa jumuishi.

4.2.4.6 Kuchagiza Manufaa ya Uchumi wa Buluu

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza mchango wa uvuvi na ufugaji wa viumbe wa majini katika Pato la

Taifa kufikia asilimia 2.42. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuboresha miundombinu ya bahari, maziwa na mito ili iwe katika kiwango cha kimataifa;

(ii) Kuimarisha usafirishaji wa majini kwa kutumia teknolojia za kisasa za bandari; na

(iii) Kuongeza udhibiti wa maeneo ili kulinda ikolojia.

4.2.5 Kutumia Kikamilifu Vichocheo vya Maendeleo

4.2.5.1 Nishati

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza uwezo wa mitambo wa uzalishaji wa umeme kufikia MW 4,804 na kuongeza kiwango cha matumizi ya umeme kwa kila mtu kufikia kWh 342. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuboresha miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme;

(ii) Kufanya mabadiliko ya kimkakati kuelekea matumizi mseto ya vyanzo vya uzalishaji, hususan nishati jadidifu.

4.2.5.2 Mifumo ya usafirishaji na Uchukuzi Fungamanishi

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza mchango wa sekta ya uchukuzi katika Pato la Taifa kufikia asilimia 8.8 na kuongeza ukuaji halisi wa sekta ya uchukuzi kufikia asilimia 5.96. Ili kufikia malengo hayo, vipaumbele vitakua katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikiwemo bandari, reli, barabara na viwanja vya ndege; na

(ii) Kushirikisha sekta binafsi katika uendelezaji na uendeshaji wa huduma za uchukuzi.

4.2.5.3 Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza kiwango cha matumizi ghafi ya utafiti na maendeleo katika Pato la Taifa kufikia asilimia 0.67. Ili kufikia malengo hayo, vipaumbele vitakua katika afua zifuatazo:

(i) Kuanzisha mifumo maalum ya ugharamiaji wa shughuli za ubunifu; na

(ii) Kuimarisha ulinzi wa miliki za ubunifu.

(iii) Kuimarisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

4.2.5.4 Utafiti na Maendeleo

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza matumizi ya kitaifa katika utafiti na maendeleo kama asilimia ya Pato la Taifa kufikia asilimia 0.67. Ili kufikia malengo hayo, vipaumbele vitakua katika afua zifuatazo:

(i) Kuanzisha mfumo wa kitaifa unaounganisha moja kwa moja uvumbuzi wa kisayansi na matumizi ya kibiashara; na

(ii) Kuanzisha ushirikiano madhubuti kati ya sekta za umma na binafsi.

4.2.5.5 Matumizi ya Takwimu

(i) Kuimarisha ushirikiano wa kimkakati kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; na

(ii) Kujenga uwezo wa rasilimali watu katika maeneo mahususi.

4.2.5.6 Mapinduzi ya Kidijitali

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza idadi ya watu wanaotumia intaneti ya kasi kufikia asilimia 52 na

kuongeza mchango wa TEHAMA katika Pato la Taifa kufikia asilimia 12.58. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuongeza upatikanaji wa huduma za intaneti ya kasi nchi nzima; na

(ii) Kukuza sekta ya ndani ya ubunifu.

4.2.5.7 Miundombinu na Huduma za TEHAMA

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza upenyo wa intaneti kufikia asilimia 86.78. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuongeza upatikanaji wa miundombinu na vifaa vya kidijitali vilivyo salama, vyenye kasi, na gharama nafuu;

(ii) Kuimarisha mawasiliano katika kila pembe ya nchi;

(iii) Kujenga nguvukazi yenye ujuzi na uelewa wa kidijitali kupitia taasisi maalum za mafunzo, mitaala ya kisasa, na programu endelevu za kuwajengea uwezo wataalamu; na

(iv) Kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

4.2.5.8 Huduma za Mawasiliano na Posta

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza idadi ya watu wanaoweza kupata huduma za posta ndani ya kilometa tano (5) kufikia asilimia 83 na kuongeza idadi ya watu wanaofikiwa na intaneti ya kasi ya mkononi (5G) kufikia asilimia 43.6. Ili kufikia malengo hayo, vipaumbele vitakua katika afua zifuatazo:

(i) Kuunda mtiririko jumuishi na wenye ufanisi wa bidhaa, habari, na huduma; na

(ii) Kuunganisha mifumo ya posta usafirishaji wa vifurushi na biashara mtandaoni.

4.2.5.9 Mazingira Wezeshi ya Biashara na Uwekezaji

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza farihisi ya ubora na udhibiti kufikia 0.33. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kupitia mpango wa kuboresha mazingira na biashara;

(ii) Kuendeleza maeneo maalumu ya kiuchumi;

(iii) Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi kupitia utaratibu wa ubia; na

(iv) Kufanya urasimishaji wa shughuli za uchumi.

4.2.6 Kuimarisha Misingi ya Uendelevu wa Taifa

Kipaumbele hiki kinalenga: Kuimarisha uwazi, uwajibikaji, maadili, na tunu za kidemokrasia, pamoja na amani na utulivu; kuimarisha utumishi wa umma unaoendana na mahitaji ya wananchi, unaowajibika na unaozingatia maadili; na kuimarisha uadilifu na kuaminika kwa taasisi zinazosimamia mahusiano ya wananchi. Maeneo yatakayopewa kipaumbele katika eneo hili ni:

4.2.6.1 Utawala Bora, Demokrasia, Usalama na Utulivu

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza farihisi ya utulivu wa kisiasa, kutokuwepo kwa ghasia na ugaidi kufikia 0.01 na kuongeza farihisi ya ufanisi wa Serikali kufikia -0.4. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuweka mfumo imara wa kudhibiti uhalifu wa mtandaoni;

(ii) Kuimarisha mifumo ya utawala bora;

(iii) Kuboresha sheria ili kuendana na utekelezaji wa Dira 2050; na

(iv) Kuimarisha uwajibikaji.

4.2.6.2 Serikali za Mitaa Thabiti na Zenye Ufanisi

Katika kipindi cha mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza idadi ya huduma zilizowekwa kidigitali katika ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kufikia asilimia 47. na kupunguza alama ya wastani ya farihisi ya uhalifu kufikia 51.04. Ili kufikia malengo hayo, vipaumbele vitakua katika afua zifuatazo:

(i) Kuziwezesha Serikali za Mitaa na jamii kuwa wadau wakuu na injini za maendeleo;

(ii) Kujenga mifumo madhubuti ya wananchi kutoa mrejesho wa maoni; na

(iii) Kujenga uwezo wa serikali za mitaa.

4.2.6.3 Matumizi Sahihi ya Takwimu

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza idadi ya watu wenye vitambulisho vya kidigitali vilivyounganishwa na huduma za baruapepe za umma kufikia asilimia 60. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha utawala wa kidijitali unaotumia mifumo inayowasiliana na takwimu sahihi; na

(ii) Kuunganisha majukwaa ya TEHAMA yaliyogawanyika hadi ngazi ya chini.

4.2.6.4 Mabadiliko ya Mitazamo na Fikra

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza alama ya Tanzania katika farihisi ya maendeleo ya jamii kufikia 60.64.

4.3 Programu za Kielelezo

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 utaendelea kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa Programu za

Kielelezo ikijumisha miradi shikizi na maeneo ya minyororo ya thamani kama zilivyoainishwa katika FYDP IV. Programu hizo ni:

(i) Mji wa Ikolojia ya Bahari Bagamoyo na Usafirishaji Fungamanishi;

(ii) Kitovu Changamani cha Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga;

(iii) Programu ya Kitaifa ya Umwagiliaji na Mageuzi ya Viwanda vya Uchakataji wa Mazao;

(iv) Kitovu cha Teknolojia na Uchakataji wa Madini Adimu Dodoma;

(v) Kiwanda cha Kuchakata Gesi asilia ya Kimiminika Lindi;

(vi) Kitovu cha Kisasa cha Viwanda na Uchumi wa Buluu katika Ukanda wa Ziwa Makuu; na

(vii) Programu Shirikishi ya Uendelezaji wa Miji Nchini.

Afua mahususi za utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele katika mwaka 2027/28 zimeainishwa katika **kiambatisho Na. I**. Vile vile maelezo ya kina yanayohusu programu za kielelezo yameainishwa katika **kiambatisho Na.II.**

SURA YA TANO

SEKTA BINAFSI

5.1 Utangulizi

Sekta binafsi ni mhimili muhimu wa utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV) katika kufikia malengo ya Dira 2050. Sekta hii ni kichocheo cha uwekezaji, uongezaji wa thamani katika bidhaa na huduma, matumizi ya teknolojia na ubunifu, uzalishaji wa ajira, pamoja na kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika minyororo ya thamani ya kikanda na kimataifa. Serikali inalenga kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika maendeleo na utekelezaji wa FYDP IV kupitia uwekezaji, biashara, ubunifu, ugharamiaji na utekelezaji wa miradi ya kimkakati.

Aidha, sura hii imeainisha mchango wa sekta binafsi katika uchumi, mazingira ya biashara na uwekezaji, na maeneo ya kipaumbele kwa uwekezaji. Aidha, inafafanua ushiriki wa sekta binafsi katika programu za kielelezo na miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP); hatua za kuwezesha biashara za ndani; viashiria na mfumo wa kufuatilia uwekezaji halisi; pamoja na mikakati ya ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28.

5.2 Mwenendo wa Mchango wa Sekta Binafsi

Shughuli za sekta binafsi zimeendelea kukua ambapo jumla ya shughuli 257,405 zilisajiliwa mwaka 2024 ikilinganishwa na shughuli 219,371 mwaka 2023. Ongezeko hili liliongozwa na sekta ya viwanda kutoka asilimia 8.3 mwaka 2023 kufikia asilimia 14.3 mwaka 2024; sekta ya kilimo kutoka asilimia 0.2 mwaka 2023 kufikia asilimia 0.5 mwaka 2024; na sekta ya huduma kutoka asilimia 91.5 mwaka 2023 kufikia asilimia 85.1 mwaka 2024. Aidha, katika mwaka 2025, mikopo iliyotolewa na benki za biashara kwa sekta binafsi iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 44,603.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 36,097.4 mwaka 2024. Hali hii inaakisi kuongezeka kwa uwekezaji wa sekta binafsi katika shughuli za uchumi. Vilevile, kiwango cha ajira katika sekta isiyo rasmi kimeongezeka kutoka asilimia 27.3 mwaka 2024 hadi asilimia 28.2 mwaka 2025.


Aidha, kiwango cha ukuzaji wa rasilimali kilichofanywa na sekta binafsi kiliongezeka kutoka shilingi milioni 50,244,050 mwaka 2024 kufikia milioni 52,547,201 mwaka 2025; mikopo kwa sekta binafsi ilikua kutoka asilimia 12.4 mwaka 2024 kufikia asilimia 23.6 mwaka 2025; na kiwango cha amana katika benki za biashara kimeongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 40.05 mwaka 2024 kufikia dola za Marekani bilioni 53.03 mwaka 2025.

Sekta za uzalishaji na utoaji wa huduma zimeendelea kunufaika na mchango wa sekta binafsi kupitia uwekezaji na shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Miongoni mwa matokeo yaliyopatikana ni uzalishaji wa tani 50.88 za mbegu; kuongezeka kwa vituo vya huduma za afya vinavyomilikiwa na sekta binafsi kutoka vituo 4,123 mwaka 2024 hadi vituo 4,368 mwaka 2025, ambapo ongezeko kubwa lilijitokeza katika polyclinic, zahanati na hospitali; pamoja na kuongezeka kwa idadi ya shule zinazomilikiwa na sekta binafsi kutoka shule 314,668 mwaka 2024 hadi shule 335,131 mwaka 2025.

5.2.1 Mchango katika Uwekezaji

Uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje uliongezeka kwa asilimia 12.1 na kufikia dola za Marekani milioni 24,754.1 mwaka 2024 kutoka dola za Marekani milioni 22,074.4 mwaka 2023. Kati ya kiasi hicho, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ulifikia dola za Marekani milioni 21,698.9, sawa na asilimia 87.7, uwekezaji wa hisa ulifikia dola za Marekani milioni 272.7 (asilimia 1.1) na uwekezaji wa mwingine ulifikia dola za Marekani milioni 2,782.5 (asilimia 11.2). Uwekezaji huo ulielekezwa zaidi katika uchimbaji wa madini, huduma za fedha na bima, uchakataji wa bidhaa, na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Mwaka 2025, jumla ya miradi 956 yenye thamani ya dola za Marekani milioni 11,429.8 ilisajiliwa ikilinganishwa na miradi 901 yenye thamani ya dola za Marekani milioni 9,312.7 iliyosajiliwa mwaka 2024. Kati ya hiyo, miradi 297 ilikuwa ya wawekezaji wa ndani, miradi 473 ya uwekezaji wa nje na miradi 185 ya ubia kati ya wawekezaji wa ndani na wageni. Kielelezo Na. 1 kinatoa takwimu kwa asilimia ya miradi iliyowekezwa kwa mwaka 2025/2026.



Kielelezo Na. 1: Miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa kwa mwaka 2025/26

.

5.2.2 Mchango katika Uzalishaji

Kwa mujibu wa Sensa ya Uzalishaji Viwandani ya Mwaka 2023, sekta binafsi inamiliki asilimia 92.6 ya shughuli za uzalishaji viwandani na asilimia 99 ya shughuli ndogo za uzalishaji viwandani. Hali inaakisi mchango mkubwa wa sekta binafsi katika umiliki na uendeshaji wa shughuli za uzalishaji viwandani. Aidha, sehemu kubwa ya uzalishaji wa sekta binafsi umeelekezwa katika uchimbaji wa madini na uzalishaji viwandani, huku shughuli zinazofanywa kwa ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ni asilimia 0.4. Takwimu hizi zinaonesha ushirikiano hafifu katika uwekezaji wa ubia wa sekta ya umma na sekta binfasi.


5.2.3 Mchango katika Ajira

Kwa mujibu wa NBS, takribani asilimia 90 ya nguvu kazi ilijishughulisha na shughuli za sekta binafsi. Aidha, kwa mujibu wa *Tanzania Informal Sector Employment and Earning Survey* 2024/25, sekta binafsi imeajiri watu 3,185,947, sawa na asilimia 71 ya walioajiriwa katika sekta rasmi, ambapo asilimia 89 walikuwa katika

taasisi zinazolenga kupata faida, asilimia 10 katika taasisi za utoaji huduma, na asilimia 1 katika vyama vya ushirika.

5.2.4 Mchango katika Mauzo ya Nje

Mchango wa sekta binafsi katika mauzo ya nje ulifikia takribani dola za Marekani bilioni 17.6 mwaka 2025/26 kutoka dola za Marekani bilioni 16.0 mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 10.2. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani, tumbaku na kahawa, pamoja na mapato yatokanayo na huduma za usafiri na utalii.



5.3 Maeneo ya Kipaumbele ya Uwekezaji

Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano umebainisha na kufungamanisha minyororo ya thamani katika programu za kielelezo ili kuhakikisha zinakuwa na manufaa kwa biashara, uzalishaji, kukuza ushindani, kupanua wigo wa mapato, mauzo nje na kuongeza ajira. Kwa msingi huo, katika mwaka 2027/28, Sekta binafsi ina fursa ya kuwekeza na kushiriki katika hatua mbalimbali za minyororo ya thamani inayolenga kuharakisha maendeleo na ukuaji wa uchumi. Maeneo yatakayohusika katika kila mnyororo wa thamani ni kama ifuatavyo:

(a) **Kilimo cha maua na mazao ya bustani**: Eneo hili linahusisha matunda, mbogamboga, maua na viungo.

Fursa za uwekezaji zinapatikana katika hatua zote za mnyororo wa thamani, kuanzia utafiti na upatikanaji wa pembejeo, uzalishaji, uhifadhi na uchakataji, hadi usambazaji, usafirishaji na uuzaji katika masoko ya nje.

(b) **Ufugaji wa viumbe maji**: vipaumbele vya uwekezaji katika eneo hili vinahusisha uzalishaji wa mbegu na chakula cha viumbe maji; utengenezaji na usambazaji wa vifaa vya ufugaji; huduma za ugani; pamoja na ufugaji katika mabwawa na vizimba. Aidha, eneo hili linajumuisha uchakataji wa mazao, ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ya uhifadhi na usafirishaji wa bidhaa katika hali ya ubaridi, ubunifu katika matumizi ya mifumo ya kidijitali katika usimamizi wa shughuli za ufugaji, na uendelezaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi.

(c) **Uchimbaji na uongezaji thamani wa madini**: Fursa za uwekezaji katika eneo hili zinahusisha matumizi ya teknolojia na ubunifu katika uchimbaji, uendelezaji wa migodi, uchakataji na uthibitishaji wa ubora wa madini. Kipaumbele pia kitawekwa katika utengenezaji wa bidhaa zitokanazo na madini, usafirishaji, na upanuzi wa masoko ya nje, ili kuongeza thamani inayobaki nchini.

(d) **Uzalishaji wa mafuta ya kula**: Katika eneo hili fursa zipo katika utafiti, uzalishaji wa mbegu bora, kilimo cha kibiashara na uendelezaji wa viwanda vya uchakataji.


(e) **Uzalishaji wa Nguo na Mavazi**: Katika eneo hili fursa zipo katika kuendeleza viwanda vinavyounganisha uzalishaji wa pamba na hatua zinazofuata za uchakataji, utengenezaji wa nguo na mavazi, hadi mauzo ya nje. Mnyororo huu wa kimkakati unaunganisha shughuli za kilimo na viwanda.

Aidha, Serikali itakuwa na jukumu la kuweka mazingira wezeshi ya kufungua fursa katika minyororo ya thamani kimkakati.

5.4 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)

Sekta binafsi itashirikishwa katika mchakato wa upangaji, utekelezaji, uendeshaji na utoaji wa bidhaa na huduma katika programu na miradi ya maendeleo. Aidha, kwa mwaka 2027/28, ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi utajielekeza katika ukamilishaji wa maandalizi ili kufikia hatua ya utekelezaji wa miradi 121 iliyopo katika hatua mbalimbali za maandalizi kama ilivyoainishwa katika Kielelezo Na. 2.

Kielelezo Na.2: Miradi na Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi



5.5 Mkakati wa Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Utekelezaji wa Mpango

Kwa kuzingatia nafasi ya sekta binafsi, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV) umeainisha umuhimu wa kuimarisha makubaliano na ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika maeneo mbalimbali. Haya yanajumuisha ushiriki wa sekta binafsi katika programu za kielelezo ili kuwezesha upatikanaji wa matokeo endelevu, pamoja na kutumia njia mbadala za ugharamiaji wa uwekezaji.

Katika mwaka wa fedha 2027/28, Serikali itaimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango kwa kuelekeza juhudi katika kubadili fursa zilizoainishwa kwenye minyororo ya thamani kuwa miradi ya uwekezaji inayotekelezwa. Kipaumbele kitatolewa katika kupunguza vihatarishi na kuboresha mazingira ya

uwekezaji, kuboresha upatikanaji wa taarifa kuhusu fursa zilizopo, kuharakisha maamuzi yanayohitajika na kuimarisha uratibu kati ya taasisi za Serikali na wawekezaji. Aidha, sekta binafsi itaeendelea kushirikishwa kupitia majadiliano, mashauriano na vikao kazi katika maandalizi ya mipango ya kisekta, utekelezaji, utatuzi wa changamoto na tathmini ya miradi ya maendeleo.

5.6 Mfumo wa Ufuatiliaji wa Uwekezaji

Katika mwaka wa fedha 2027/28, Serikali itaimarisha mfumo wa kufuatilia uwekezaji halisi wa sekta binafsi katika minyororo ya thamani zilizopewa kipaumbele. Mfumo huo utatumia viashiria vya sekta binafsi vilivyoainishwa katika FYDP IV, pamoja na viashiria mahsusi vya kupima maendeleo ya uwekezaji katika kila mnyororo wa thamani. Ufuatiliaji utahusisha hatua mbalimbali za mradi, kuanzia maandalizi na upatikanaji wa rasilimali hadi utekelezaji na kuanza kwa uzalishaji. Taarifa zitakazopatikana zitatumika kubaini vikwazo na kuelekeza hatua za Serikali zinazohitajika ili kuharakisha utekelezaji wa uwekezaji.

Taarifa za ufuatiliaji zitakusanywa na kuhakikiwa na taasisi zinazowajibika katika kila mnyororo wa thamani. Taarifa hizo zitatumika kufanya maamuzi na kushughulikia vikwazo vinavyoweza kuchelewesha uwekezaji. Utekelezaji unapohusisha taasisi zaidi ya moja, taasisi hizo zitaratibu hatua zao na kufuatilia utekelezaji wake ili miradi ya uwekezaji ifikie hatua zilizokusudiwa ndani ya muda uliopangwa. Matokeo ya ufuatiliaji yatazingatiwa katika maandalizi na utekelezaji wa mipango na bajeti za taasisi husika.

SURA YA SITA

UGHARAMIAJI WA MPANGO

6.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza mwelekeo wa ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2027/28 ambao ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 (Mpango wa IV). Aidha, kwa mwaka 2027/28, ugharamiaji wa Mpango unalenga kuongeza uwekezaji katika sekta za kimageuzi, kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi, kuongeza uwekezaji na kukuza uzalishaji wa ajira. Hatua hizi zitachangia kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani.

6.2 Mahitaji ya Rasilimali Fedha kwa Mwaka 2027/28

Mahitaji ya rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2027/28 yanakadiriwa kufikia kiasi cha shilingi trilioni 89.3 kama ilivyoainishwa katika Mpango wa IV. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 20.7 zinatarajiwa kutoka kwenye bajeti ya Serikali, sawa na asilimia 30.2 ya bajeti kuu ya Serikali. Shilingi trilioni 6.3 uwekezaji unaotarajiwa kutoka katika mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara, na shilingi trilioni 62.3 ni uwekezaji kutoka sekta binafsi. Kiasi hicho ni makadirio ya uwekezaji wa sekta binafsi kitakachotengenezwa katika ukuzaji wa mitaji.

6.2.1 Vyanzo vya Mapato ya Serikali kwa Mwaka 2027/28

Mapato yanayotarajiwa kugharamia utekelezaji wa Mpango 2027/28 yatatokana na vyanzo vitatu (3) vikuu kama ifuatavyo:

(i) Mapato ya ndani: kodi, mapato yasiyo ya kodi, gawio kutoka kwa mashirika ya umma na mapato ya halmashauri;

(ii) Rasilimali fedha za Nje: mikopo nafuu, misaada, na mikopo isiyo nafuu kwa miradi ya kibiashara; na

(iii) Mbinu bunifu ya ufadhili: ikijumuisha hati fungani za kijani, za miundombinu, na za halmashauri.

6.2.2 Uwekezaji wa Mashirika ya Umma

Mashirika ya Umma yanayojiendesha kibiashara yataendelea kuwa chanzo muhimu cha rasilimali za ugharamiaji wa maendeleo, kuboresha ufanisi na kuongeza mapato na faida. Lengo ni kufikisha mchango wa mashirika hayo katika mapato ya serikali hadi asilimia 10 ifikapo Juni 2028. Kadhalika, kupunguza utegemezi wa ruzuku na kuongeza matumizi yenye tija ya rasilimali. Mikakati ya kufikia malengo ya mwaka 2027/28 ni kama ifuatavyo:

(i) Kuimarisha utawala, usimamizi wa mapato na matumizi pamoja na kuhakikisha uwajibikaji wa mashirika ya umma;

(ii) Kuongeza matumizi ya masoko ya mitaji, hatifungani, ufadhili mchanganyiko, dhamana na ubia wa kimkakati katika kugharamia uwekezaji;

(iii) Kuimarisha ushirikiano na uunganishaji wa rasilimali miongoni mwa mashirika ya umma ili kuongeza uwezo wa kugharamia na kutekeleza miradi mikubwa; na

(iv) Kuongeza matumizi yenye tija ya rasilimali na mali zisizotumika kikamilifu kupitia ukodishaji, ubia au ubinafsishaji wenye faida.

6.2.3 Uwekezaji wa Sekta Binafsi

Sekta binafsi itaendelea kuwa chanzo muhimu cha ugharamiaji wa maendeleo kwa mwaka 2027/28. Mpango unalenga kuimarisha uwekezaji wa ndani na nje, kukuza masoko ya mitaji, kuimarisha ubia kati ya serikali na sekta binafsi, pamoja na kuboresha upatikanaji wa mikopo. Uwekezaji utakaofanywa na sekta binafsi kufikia malengo ya Mpango wa IV ya kuongeza uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje hadi kufikia asilimia 10 ya Pato la Taifa ifikapo 2030 na uwekezaji wa ndani wa sekta binafsi hadi asilimia 25–30 ya pato la taifa. Mikakati ya 2027/28 ya kufikia malengo yaliyoanishwa ni kama ifuatavyo:

(i) Kuendeleza ufunguaji na uunganishaji wa soko la mitaji na masoko ya kimataifa;

(ii) Kuimarisha maandalizi, uchakataji na ugharamiaji wa miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi;

(iii) Kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje katika sekta za kimkakati;

(iv) Kuimarisha mifumo ya dhamana na vyanzo bunifu vya ugharamiaji wa miradi; na

(v) Kuboresha upatikanaji na ubora wa mikopo kwa sekta binafsi kupitia maboresho ya sekta ndogo ya fedha, kupunguza mikopo chechefu na kuimarisha mitaji na ukwasi wa taasisi za fedha.

6.3 Vyanzo Bunifu na Mbadala

Serikali itaendelea kuimarisha matumizi ya vyanzo bunifu na mbadala vya fedha katika mwaka 2027/28 ili kuongeza rasilimali za kugharamia maendeleo, kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi na kuvutia mitaji ya muda mrefu. Vyanzo hivyo vitajumuisha hatifungani za kijani, hatifungani za Watanzania waishio ughaibuni, vyanzo mseto vya fedha, biashara ya kaboni, masoko ya mitaji, pamoja na uzalishaji wa mapato kutokana na mali zilizopo Pamoja na upatikanaji wa mapato kutokana na sehemu ya ongezeko la thamani ya ardhi (Asset Monetisation na Land Value Capture). Kwa ujumla, vyanzo bunifu na mbadala vinatarajiwa kuchangia kati ya shilingi trilioni 42–62, sawa na asilimia 9–13 ya rasilimali zinazohitajika kutekeleza Mpango wa IV. Mikakati ya 2027/28 ya kufikia malengo yaliyoanishwa ni kama ifuatavyo:

(i) Kuendeleza uandaaji na uuzaji wa hatifungani za kijani, hati fungani za Watanzania waishio ughaibuni na hatifungani za maendeleo na miundombinu;

(ii) Kupanua matumizi ya vyanzo mseto vya fedha, ikiwemo mikopo yenye masharti nafuu na fedha za mazingira, katika miradi na sekta za kimkakati;

(iii) Kuimarisha utekelezaji wa mfumo wa biashara ya kaboni na kuongeza uwezo wa Tanzania kunufaika na soko la kaboni;

(iv) Kuongeza mapato kwa kutekeleza Mkakati wa uzalishaji wa mapato kutokana na taarifa (Data Monetisation) kwa kutumia taarifa za Serikali zisizo za watu binafsi, kwa kuzingatia usalama wa taarifa; na

(v) Kuongeza matumizi yenye tija yarasilimali zisizotumika kikamilifu kupitia uzalishaji wa mapato kutokana na mali zilizopo na patikanaji wa mapato kutokana na sehemu ya ongezeko la thamani ya ardhi (Asset Monetisation na Land Value Capture.

SURA YA SABA

USIMAMIZI WA UTELEKEZAJI NA UFUATILIAJI WA MATOKEO YA MPANGO

7.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza mfumo wa uratibu wa kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2027/28. Mfumo huu unalenga kuhakikisha utekelezaji wa vipaumbele, programu za kielelezo, miradi shikizi na miradi ya kimkakati inatelekezwa kwa ufanisi ili kufikia matokeo yaliyokusudiwa, pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa taarifa za utekelezaji kwa wakati, ubainishaji wa changamoto na hatua stahiki zakuchukuliwa.

Utekelezaji wa mfumo wa ufuatiliaji na upimaji wa matokeo utazingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Uidhinishaji wa Miradi ya Maendeleo (National Development Plan and Approval Guideline - NDPAG) na Mwongozo wa Kitaifa wa Upimaji Matokeo na Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo. Aidha, mfumo wa e-Delivery utatumika kama nyenzo kuu ya kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji. Kadhalika, utatumika kufuatilia na kutathmini matokeo ya Mpango, programu na miradi ya maendeleo na kuainisha viashiria vya hatari. Vile vile, utabainisha changamoto za

utekelezaji kwa wakati, kuthibitisha taarifa na matokeo, na kuimarisha uwajibikaji wa taasisi zinazotekeleza Mpango pamoja na kuwezesha matumizi ya taarifa katika kufanya maamuzi na kufanya marekebisho.

7.2 Ufuatiliaji, Tathmini na Matumizi ya Mfumo wa e-Delivery

Ufuatiliaji na tathmini ya matokeo ya utekelezaji wa Mpango utafanyika kwa kuzingatia taratibu na miongozo mbalimbali ikiwemo mpango wa ufuatiliaji na tathmini ya kila miradi pamoja na viashiria vya Mpango. Mfumo wa kidijitali wa ufuatiliaji wa matokeo utatumika kufungamanisha vipaumbele vya Mpango na taarifa za programu na miradi. Pia, utawezesha uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji zitakazooainishwa kwa kuzingatia malengo na viashiria vya Mpango IV. Aidha, mfumo huo utawezesha: kufuatilia utekelezaji wa Mpango kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa; kuhuisha na kupata taarifa za utekelezaji kwa wakati; kubaini miradi na programu zilizo nyuma ya ratiba; kubaini changamoto na hatua za maboresho; na kuzalisha taarifa na dashibodi kwa ajili ya maamuzi.

7.3 Utoaji na Matumizi ya Taarifa

Taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na viashiria vya Mpango zitaandaliwa na kuwasilishwa kila robo mwaka au kwa kuzingatia utaratibu wa utoaji wa taarifa wa mradi husika. Taarifa hizo zitawazesha kupima utekelezaji wa ADP, Mpango wa IV na Dira 2050, kubaini maeneo yenye changamoto na kuchukua hatua stahiki kwa lengo la kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mgawanyo wa Majukumu ya Ufuatiliaji na Uwasilishaji wa Taarifa

Na.	Shughuli	Muda	Mhusika	Matokeo
1.	Uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mfumoo wa e-Delivery	Kila robo mwaka au kulingana na mpango kazi wa mradi husika	Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala na Mashirika ya Umma	Taarifa za utekelezaji
2.	Ufuatiliaji wa utekelezaji wa viashiria vya Mpango	Kila robo mwaka au kulingana na ratiba ya muda wa ufuatiliaji wa viashiria	Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala na Mashirika ya Umma	Taarifa za ufuatiliaji wa utekelezaji wa viashiria vya Mpango
3.	Vikao vya wadau kwa ajili ya kujadili taarifa za ufuatiliaji	Kila robo mwaka	Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala na Mashirika ya Umma	Hatua za kutatua changamoto zilizobainika katika taarifa za utekelezaji.
4.	Tathmini maalum	Inapohitajika	Tume ya Taifa ya Mipango/ Taasisi husika	Taarifa ya tathmini
5.	Taarifa ya mwaka ya utekelezaji	Juni 2027	Tume ya Taifa ya Mipango	Taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mpango

Taasisi zinazotekeleza Mpango zitawajibika kuandaa na kuwasilisha taarifa kwa kupitia mfumo wa e-Delivery. Tume ya Taifa ya Mipango itaratibu ufuatiliaji, uhakiki na uchambuzi wa taarifa, pamoja na kuwasilisha masuala yanayohitaji hatua au maamuzi katika ngazi husika. Aidha, kwa kushikiriana na wadau mbalimbali, Tume Tume ya Taifa ya Mipango itafanya ziara za ukaguzi itakapohitajika.

Kwa upande wa utekelezaji wa miradi na programu unaohusisha taasisi zaidi ya moja, wizara inayoratibu utekelezaji itawajibika kuwasilisha taarifa za matokeo ya pamoja, kwa kushirikiana na taasisi wezeshi. Jedwali 7.0 linaainisha shughuli, muda, mhusika na matokeo tarajiwa ya ufuatiliaji na tathmini.

Jedwali 7.0: Ratiba na Mgawanyo wa Majukumu ya Ufuatiliaji na Uwasilishaji wa Taarifa

SURA YA NANE

VIHATARISHI VYA MPANGO KWA MWAKA 2027/28 NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO

8.1 Utangulizi

Sura hii inaainisha vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 pamoja na mikakati ya kukabiliana navyo. Utekelezaji wa Mpango unafanyika katika mazingira ya kiuchumi, kifedha, kijamii, kiteknolojia na kimazingira yanayobadilika. Hivyo, utambuzi wa mapema wa vihatarishi na kuweka mikakati na hatua stahiki za kukabiliana navyo ni muhimu ili kuhakikisha malengo ya Mpango yanafikiwa. Usimamizi wa vihatarishi unalenga kulinda utekelezaji wa vipaumbele na programu za kimkakati, Programu za Kielelezo na minyororo ya thamani ya kipaumbele, pamoja na kuhakikisha uwekezaji wa Serikali na sekta binafsi unaleta matokeo yaliyokusudiwa. Usimamizi huo utafungamanishwa na mifumo iliyopo ya utekelezaji (ufuatiliaji na tathmini, bajeti ya muda wa kati, mikataba ya utendaji na Mfumo wa E-Delivery) na utafuata mzunguko wa hatua tano za: kubaini vihatarishi; kutathmini uwezekano na athari; kuweka mikakati ya kudhibiti; kufuatilia na kutoa tahadhari ya mapema; kutoa taarifa na kuwasilisha maamuzi. Kanuni zinazoongoza hatua hizo ni uwajibikaji, uwazi, matumizi ya ushahidi, na ushirikiano wa kisekta.

8.2 Maeneo ya Vihatarishi na Mikakati ya Kukabiliana navyo

Vihatarishi vimegawanywa katika maeneo makuu matano: fedha, uchumi, taasisi, mazingira na mabadiliko ya tabianchi, na teknolojia. Mikakati ya kukabiliana navyo inajumuisha kuepuka vihatarishi, kupunguza uwezekano wa kutokea au ukubwa wa athari zake, kuhamisha sehemu ya athari kwa wahusika wengine na kukubali vihatarishi vinavyoweza kudhibitiwa kwa ufuatiliaji wa karibu. Jedwali Na. 8.1 linaonesha vihatarishi, athari zinazoweza kujitokeza, mikakati ya kukabiliana navyo pamoja na taasisi zinazowajibika na vipindi vya ufuatiliaji.

Jedwali 8.1: Vihatarishi na mikakati ya kukabiliana Navyo.

Eneo la Kihatarishi	Kihatarishi – Athari	Mikakati ya Kukabiliana navyo	Taasisi – Muda
Fedha	Kutopatikana kwa fedha kwa wakati — miradi kusimama; malipo ya wakandarasi kuchelewa.	Kuzingatia kalenda ya utoaji wa fedha kwa robo mwaka; kutoa kipaumbele kwa miradi inayoendelea; malipo kulipwa kulingana na matokeo.	MoF; MDAs; TAMISEMI – Kila robo mwaka
	Kuongezeka kwa gharama za hudumia deni — nafasi ya kifedha kupungua; mzigo wa deni kuongezeka.	Kutekeleza Mkakati wa usimamizi wa deni; Kukopa mikopo ya masharti nafuu; mikopo kuelekezwa kwenye miradi inayozalisha mapato.	MoF; Benki Kuu – kila robo mwaka
Uchumi	Mfumuko wa bei na gharama za maisha kupanda — bajeti kuvuka mipango.	Kutekeleza sera ya fedha inayolinda utulivu wa bei; Kuongeza akiba ya chakula na mafuta; na kuongeza uzalishaji wa ndani.	Benki Kuu; MoF; MIT – kila mwezi
	Thamani ya shilingi kushuka — gharama za uagizaji na deni la nje kuongezeka.	Kuimarisha akiba ya fedha za kigeni; kuongeza mauzo ya nje na utalii; na kuhimiza uzalishaji wa ndani.	Benki Kuu; MoF – kila mwezi
	Bei za bidhaa duniani kubadilika — mauzo ya nje na uwekezaji wa nje kupungua.	Kuongeza wigo wa masoko na bidhaa zinazouzwa nje ya nchi; na kuongeza thamani ya bidhaa za ndani.	MoF; Benki Kuu; MIT – kila robo mwaka
	Ukuaji mdogo wa sekta binafsi — mwitikio wa uwekezaji na ajira kupungua.	Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuimarisha huduma za upatikanaji wa umeme na usafirishaji; kuongeza	MoF; TISEZA; MIT; Halmashauri – kila robo mwaka

		upatikanaji wa mikopo kwa biashara ndogo na za kati.	
	Mivutano ya kisiasa na kiuchumi ya kikanda na kimataifa — minyororo ya ugavi kuvurugika.	Kutofautisha masoko na vyanzo vya ugavi; kuimarisha ushirikiano wa kikanda; kuimarisha akiba ya kimkakati ya bidhaa muhimu.	MoFA; MIT; Benki Kuu – endelevu
Taasisi	Udhaifu wa uratibu na mgawanyiko wa majukumu — kurudiwa kwa kazi; umiliki wa matokeo kutosemekana.	Kufafanua majukumu kwa miongozo na mikataba ya utendaji; kuboresha mikutano ya uratibu.	ORMU, NPC; Ofisi ya Waziri Mkuu - Uratibu – kila robo mwaka
	Kutopatikana kwa mwitikio wa uwekezaji binafsi — pengo la ufadhili; malengo ya uzalishaji kukosa.	Kuandaa miradi tayari kwa uwekezaji; kuimarsiha ushirikiano na sekta binafsi; na kuongeza majukwaa ya wawekezaji.	TIC; ORMU, NPC– kila robo mwaka
Mazingira na mabadiliko ya Tabianchi	Ukame, El- Nino, mafuriko na mabadiliko ya msimu — uzalishaji wa kilimo na nishati kupungua; miundombinu kuharibika.	Kuimarisha miundombinu inayohimili mabadiliko ya tabianchi; kuongeza eneo la umwagiliaji; kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora; kutekeleza tahadhari ya mapema; na kuimarisha upatikanaji wa bima ya mazao.	Mazingira; Kilimo; TMA – msimu/mwaka
	Maafa ya asili na dharura za afya — miundombinu kuharibika; fedha za dharura.	Kuboresha mifumo ya tahadhari ya mapema; Kuimarisha akiba ya dharura; Kutekeleza mipango miji inayohimili	Waziri Mkuu (Maafa); Afya – endelevu

		majanga; na kuimarisha uhamasishaji wa jamii.	
Teknolojia	Vitisho vya usalama wa mtandao — data kupotea; huduma kuvurugika; imani kupungua.	Kutekeleza sera ya usalama wa mtandao; kuimarisha ukaguzi wa mifumo; kutoa mafunzo kwa watumishi; na kutelekeza mipango ya matukio.	MCIT; TCRA; MDAs – endelevu
	Upungufu wa ujuzi wa kidijitali — mifumo kutotumika kikamilifu; pengo la kidijitali kuongezeka.	Kutoa mafunzo ya kidijitali; kuimarisha vituo vya ubunifu; kuwekeza katika upatikanaji wa huduma rahisi kwa watumiaji; na utoaji wa elimu ya teknolojia shuleni na vyuoni.	Mawasiliano; COSTECH; Elimu – mwaka

8.2.1 Ufungamanishaji wa Vihatarishi na Mfumo wa e-Delivery

Vihatarishi na vikwazo muhimu vinavyohusiana na programu za kimkakati, Programu za Kielelezo na minyororo ya thamani ya kipaumbele vitaingizwa katika mfumo wa e-Delivery. Mfumo huo utatunza taarifa kuhusu kila kihatarishi, kiwango chake, taasisi inayowajibika, hatua za kukabiliana nacho na muda wa kukamilisha hatua hizo. Aidha, utawezesha kufuatilia hali ya utekelezaji kwa kutumia alama za rangi (kijani, njano na nyekundu), kuwasilisha changamoto zinazohitaji maamuzi katika ngazi za juu na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi katika ngazi za sekta na Baraza la Mawaziri.

8.3 Ufuatiliaji na Udhibiti wa Vihatarishi

Kila taasisi itaandaa na kuhuisha daftari la vihatarishi likionesha aina ya kihatarishi, uwezekano wa kutokea, ukubwa wa athari zake, viashiria vya tahadhari za mapema na hatua za

kukidhibiti. Taarifa kutoka katika madaftari ya vihatarishi ya sekta, mikoa na halmashauri zitaunganishwa katika daftari la kitaifa. Mapitio ya vihatarishi yatafanyika kila robo mwaka na kila mwaka. Aidha, taarifa kuhusu hali ya vihatarishi na hatua zilizochukuliwa zitajumuishwa katika taarifa za utekelezaji wa Mpango za kila robo mwaka.

8.3.1 Viwango vya Uwezekano na Athari

Kiwango	Uwezekano wa Kutokea	Ukubwa wa Athari
Juu	Inawezekana sana kutokea katika kipindi cha utekelezaji; mwenendo unaonyesha hali inajirudia.	Kuchelewesha au kutokamilika kwa programu nzima; upotevu mkubwa wa fedha; kushindwa kufikia malengo makuu.
Kati	Inawezekana kutokea; hali zinazosababisha kihatarishi zinaweza kujitokeza katika kipindi cha utekelezaji.	Kuchelewesha sehemu ya utekelezaji; kuongeza gharama; kupunguza ubora wa matokeo.
Chini	Uwezekano mdogo; hali hazijitokezi mara kwa mara.	Athari ndogo zinazoweza kudhibitiwa kwa urahisi ndani ya taasisi.

Jedwali 8.2: Uainishaji wa viwango vya uwezekano na Athari

Kiwango cha jumla cha kihatarishi kitaamua mara ambazo ufuatiliaji utafanyika. Vihatarishi vya kiwango cha juu sana — vitahitaji hatua za haraka na uangalizi wa ngazi za juu za maamuzi, pamoja na ufuatiliaji wa kila mwezi. Vihatarishi vya kiwango cha juu — vitafuatiliwa kila mwezi au kila robo mwaka; vya kiwango cha kati kila robo mwaka; na vya kiwango cha chini — kila mwaka.

8.3.2 Mzunguko wa Ufuatiliaji, Utoaji Taarifa na Kuwasilisha Maamuzi

Uwasilishaji wa masuala yanayohitaji maamuzi utakuwa katika ngazi tatu: taasisi inayowajibika (hatua ya kwanza); kamati ya uratibu ya sekta na Tume ya Taifa ya Mipango (maamuzi ya kisekta); na Baraza la Mawaziri na Wizara ya Fedha kwa masuala yenye athari za kibajeti. Kuwasilishwa kwa ngazi ya juu hakuzui hatua za haraka za taasisi. Usimamizi madhubuti wa vihatarishi ni nguzo ya kulinda vipaumbele vya Mpango na kufanya maamuzi ya marekebisho kwa wakati.

Kalenda ya ufuatiliaji na utoaji wa taarifa itahusisha: (i) ufuatiliaji wa kila mwezi wa viashiria vya tahadhari za mapema unaofanywa na taasisi inayowajibika kwa kihatarishi husika; (ii) uhuishaji wa madaftari ya unaofanywa na wizara, idara na wakala wa Serikali, mikoa na halmashauri; (iii) mapitio ya kitaifa ya vihatarishi na uwasilishaji wa masuala yanayohitaji maamuzi kila robo mwaka au inapohitajika, chini ya uratibu wa NPC na MoF;

(iv) mapitio ya mwaka ya vihatarishi yanayofanywa na NPC na MoF ili kutoa mapendekezo yatakayozingatiwa katika maandalizi ya bajeti ya mwaka unaofuata; na (v) ukaguzi wa kila mwaka wa ufanisi wa usimamizi wa vihatarishi unaofanywa na CAG na Mkaguzi Mkuu wa Ndani, pamoja na kuwasilisha taarifa za ukaguzi na mapendekezo ya maboresho.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Profesa Kitila, kwa kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango kwa mwaka wa fedha 2027/2028.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi inafuata sasa taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambayo pia itawasilishwa na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kwa Niaba ya Waziri wa Fedha. Mheshimiwa Waziri, karibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI K.n.y WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ninaomba kuwasilisha maelezo ya Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati yaani 2026/2027 hadi 2028/2029.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliandaa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Muda wa Kati 2026/2027 hadi 2028/2029 ambapo uliidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Februari, 2026. Mwongozo huo

ulilenga kuimarisha usimamizi, uandaaji na utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Serikali na kubainisha vipaumbele vya mpango na bajeti na maelekezo kwa maafisa masuuli kwa kipindi cha muda wa kati. Mwongozo wa muda wa kati ulianza kutumika katika maandalizi ya bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2026/2027 na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Kanuni ya 116(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 21(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439, mwongozo wa mpango wa bajeti unapaswa kuwasilishwa Bungeni kila mwaka mwezi Oktoba au Novemba. Kwa kuwa Serikali iliandaa mwongozo wa muda wa kati unaoanzia mwaka 2026/2027 hadi 2028/2029 ambapo mwaka 2027/2028 umejumuishwa katika kipindi hicho, Serikali inapendekeza mwongozo huo uendelee kutumika katika maandalizi ya mpango na bajeti ya mwaka 2027/2028 badala ya kuandaa mwongozo mwingine unaojitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pendekezo ya kuendelea kutumia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti wa Serikali katika Muda wa Kati, Serikali inatarajia kufanya mapitio ya mwongozo huo ili kuhuisha baadhi ya taarifa ambazo ni muhimu na mahususi kwa ajili ya maandalizi ya mpango wa bajeti kwa mwaka 2027/2028. Mapitio hayo yatajumuisha uchumi jumla, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2026/2027, vipaumbele vya kibajeti, makadirio ya mfumo wa bajeti katika kipindi cha muda wa kati na utekelezaji wa maelekezo ya kimkakati ya mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatarajia pia kufanya mapitio katika maeneo yafuatayo; muundo wa gharama za uendeshaji wa shughuli za Serikali na usimamizi wa mikataba ya umma na ushiriki wa wazawa katika zabuni. Matokeo ya mapitio haya yanatarajiwa kuboresha maandalizi ya vipaumbele vya bajeti ya Serikali na utekelezaji wake ili kuongeza ufanisi wa matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilisha mapitio katika maeneo yaliyobainishwa, Serikali inapendekeza kuwasilisha maboresho ya mwongozo pamoja na mapendekezo ya ukomo wa

bajeti ya Serikali mwaka wa fedha 2027/2028 mwezi Februari, 2027 kwa mujibu wa Ibara ya 131(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kifungu cha 23 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni ya 119(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la Mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu utasaidia kuimarisha dhana ya *Medium Term Expenditure Framework (MTF)* pamoja na kuwezesha Serikali kuanza maboresho ya maandalizi ya bajeti Serikali katika mfumo wa programu yaani *Programme Based Budgeting (PBB*) kama ilivyoainishwa katika *LTPP* na katika *FYDP IV*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, utaratibu huu utaipa Serikali fursa ya kuandaa vikao vya usikilizaji wa maoni kutoka kwa wananchi na wadau wa bajeti ya Serikali yaani *public hearing* kwa lengo la kuboresha mchakato wa maandalizi ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; Serikali itahakikisha kuwa mapitio ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti katika Muda wa Kati 2026/2027 hadi 2024/2029 yanafanyika ili kuhuisha taarifa za mfumo na shabaha za uchumi jumla, ukomo wa bajeti katika kipindi cha muda wa kati, vipaumbele vya bajeti na mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 kwa ajili ya maandalizi na utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2027/2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ninaomba kuwasilisha. Ahsante sana.

MAELEZO YA WAZIRI WA FEDHA, MHE. BALOZI KHAMIS MUSSA OMAR (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KATIKA MUDA WA KATI (2026/27 – 2028/29) KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Serikali iliandaa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Muda wa Kati (2026/27–2028/29)

ambapo uliidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Februari 2026. Mwongozo huo ulilenga kuimarisha usimamizi, uandaaji na utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali pamoja na kubainisha vipaumbele vya Mpango na Bajeti na maelekezo kwa Maafisa Masuuli kwa kipindi cha muda wa kati. Mwongozo wa muda wa kati ulianza kutumika katika maandalizi ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2026/27 na utekelezaji wake.

2. MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2027/28

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni 116(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 21(2) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439, Mwongozo wa Mpango na Bajeti unapaswa kuwasilishwa Bungeni kila mwaka mwezi Oktoba au Novemba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali iliandaa Mwongozo wa Muda wa Kati unaoanzia mwaka 2026/27 hadi 2028/29 ambapo mwaka 2027/28 umejumuishwa katika kipindi hicho, Serikali inapendekeza Mwongozo huo uendelee kutumika katika maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2027/28 badala ya kuandaa mwongozo mwingine unaojitegemea.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pendekezo la kuendelea kutumia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati (2026/27 – 2028/29), Serikali inatarajia kufanya mapitio ya Mwongozo huo ili kuhuisha baadhi ya taarifa ambazo ni muhimu na mahsusi kwa ajili ya maandalizi ya mpango na bajeti kwa mwaka 2027/28. Mapitio hayo yatajumuisha: uchumi jumla; utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2026/27; vipaumbele vya kibajeti; makadirio ya mfumo wa bajeti katika kipindi cha muda wa kati (2027/28 - 2029/30); na utekelezaji wa maelekezo ya kimkakati ya mwongozo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia pia kufanya mapitio katika maeneo yafuatayo: muundo wa gharama za uendeshaji wa shughuli za Serikali, usimamizi wa mikataba ya umma na ushiriki wa wazawa katika zabuni. Matokeo ya mapitio haya yanatarajiwa kuboresha

maandalizi ya vipaumbele vya bajeti ya Serikali na utekelezaji wake ili kuongeza ufanisi wa matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha mapitio katika maeneo yaliyobainishwa, Serikali inapendekeza kuwasilisha maboresho ya Mwongozo pamoja na Mapendekezo ya Ukomo wa Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2027/28 mwezi Februari 2027 kwa mujibu wa Ibara ya 137(1) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 23 cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 na Kanuni ya 119(2) ya Kanuni za kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Toleo la mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu utasaidia kuimarisha dhana ya Medium Term Expenditure Framework (MTEF) pamoja na kuwezesha Serikali kuanza maboresho ya maandalizi ya bajeti ya Serikali katika mfumo wa programu (Programme Based Budgeting - PBB). Aidha, utaratibu huu utaipa Serikali fursa ya kuandaa vikao vya usikilizaji wa maoni kutoka kwa wananchi na wadau wa Bajeti ya Serikali (Public Hearing) kwa lengo la kuboresha mchakato wa maandalizi ya bajeti ya Serikali.

3. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Serikali itahakikisha kuwa mapitio ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti katika Muda wa Kati (2026/27 – 2028/29) yanafanyika ili kuhuisha taarifa za mfumo na shabaha za uchumi jumla, ukomo wa bajeti katika kipindi cha muda wa kati, vipaumbele vya bajeti na mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2026/27 kwa ajili ya maandalizi na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2027/28.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Balozi Khamis Mussa Omar (Mb.)
WAZIRI WA FEDHA
27 Oktoba, 2026

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, kwa kuwasilisha maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Tunakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa kanuni zetu baada ya taarifa zote za Serikali sasa tunapata maoni ya Bunge kupitia Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Mwenyekiti wa Kamati, karibu kwa ajili ya maoni yetu kama Wabunge.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka wa fedha 2027/2028 pamoja na Mapitio ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha Muda wa Kati 2026/2027 na 2028/2029.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(C) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikisomwa pamoja na Kanuni ya 116(2) na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2025 kwa pamoja vinalipa Bunge jukumu la kukaa kujadili na kuidhinisha mipango na mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya Serikali. Aidha, vifungu vya 8(1)(b), 9(1)(a), 21(1), (2) na (5) vya Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 vinabainisha majukumu ya Bunge pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti katika kuchambua na kuidhinisha mpango na mwongozo wa maandalizi ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka wa fedha 2027/2028 pamoja na Mapitio ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Muda wa Kati kama ilivyowasilishwa na Serikali na kutoa ushauri wake. Uchambuzi wa Kamati ulifanyika kwa kurejea nyaraka mbalimbali kama zinavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu sita kama inavyooneshwa kwenye taarifa ya Kamati. Tathmini ya mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla na kubaini masuala yafuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2021 – 2025 ukuaji wa uchumi umekuwa kwa wastani wa 5.2% ikilinganishwa na lengo la kukua kwa 6% kwa mwaka. Serikali imekuwa haifikii malengo ya ukuaji wa uchumi kutokana na uandaaji wa makisio au *data* yaani *assumptions* kutokuwa halisia na halisi na hali halisi ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, shughuli zote zilizokuwa kwa kasi zina uhusiano na uwekezaji wa moja kwa moja wa Serikali. Aidha, mwelekeo wa Dira 2050 ni sekta binafsi kuwa *engine* ya uchumi kwa uwiano wa 70% kwa 30%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ongezeko la watu nchini ni 2.8%. Kiwango hiki ni kikubwa kuliko kiwango kinachokubalika kwa nchi zinazoendelea cha 1.5% hadi 2.5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia uchambuzi huo Kamati inashauri mambo yafuatayo kwa Serikali: Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji kwa kutatua changamoto zilizopo ikiwemo malipo ya madeni ya wakandarasi, ukarabati wa miundombinu iliyoharibika kwa wakati na ujenzi wa miundombinu yenye ubora inayoweza kudumu kwa muda mrefu. Hatua hii itaongeza mchango wa miundombinu katika ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, Serikali kuweka mikakati ili kuhakikisha ukuaji wa sekta ya huduma unafungamanishwa na sekta nyingine za uchumi kama vile kilimo, misitu, uvuvi, viwanda na ujenzi. Tatu, kufanya tathmini ya ufanisi wa mfumo wa riba ya Benki Kuu ili kubaini ni kwa kiasi gani mfumo huu umesaidia kupunguza viwango vya riba na mfumuko wa bei nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa mpango wa mwaka 2025/2026 pamoja na robo ya kwanza ya mwaka 2026/2027. Kamati ilichambua utekelezaji wa Mpango wa

Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/2026 pamoja na robo ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/2027 na kubaini masuala yafuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ni kuhusu miradi ya kimkakati kuchelewa kuanza utekelezaji kwa muda mrefu. Baadhi ya miradi ya kimkakati imekuwa haitekelezwi kwa muda mrefu na imebaki katika hatua za awali kama vile majadiliano au upembuzi yakinifu. Mfano wa miradi hiyo ni Mradi wa Umeme wa Ruhudji, Rumakali, Chuma Liganga, Makaa ya Mawe Mchuchuma, Mradi wa Magadi Soda Engaruka, pamoja na miradi ya usindikaji gesi asilia na utafutaji wa mafuta. Hali hii imepelekea kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi kutokana na tathmini za awali kupitwa na wakati na hivyo kulazimika kufanya tathmini upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta za kilimo, mifugo na uvuvi; pamoja na kwamba bajeti ya sekta ya kilimo ilipungua kutoka shilingi trilioni 1.243 mwaka wa fedha 2025/2026 hadi shilingi trilioni 1.105 mwaka wa fedha 2026/2027 sawa na kupungua kwa 11.1%, bado sekta hii ina umuhimu mkubwa katika kuchangia uchumi wa Taifa. Kamati ilifanya uchambuzi wa utekelezaji wa miradi iliyopo katika sekta hizi na kubaini kuwa sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi zinakabiliwa na changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri masuala yafuatayo kwa Serikali: Moja, kuhakikisha ruzuku ya mbolea inawafikia wakulima kwa wakati ili kuboresha kilimo kiwe na tija na hivyo kufikia malengo ya maendeleo ya sekta hizo. Mbili, kuongeza uwekezaji katika upatikanaji wa malisho na maji ya mifugo, kuharakisha uhimilishaji wa mifugo pamoja na kuimarisha miundombinu ya usindikaji wa nyama na maziwa ili kuongeza thamani ya bidhaa za mifugo. Tatu, kuvutia uwekezaji katika ufugaji wa samaki, ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi na kusafirisha mazao ya uvuvi pamoja na kuboresha mnyororo wa thamani wa bidhaa za uvuvi ili kuongeza mauzo nje na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya viwanda, Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kwamba mchango wa sekta ya viwanda kwenye pato la Taifa ulishuka kutoka asilimia 6.8 mwaka 2024 hadi asilimia 5.9 mwaka 2025 sawa na kupungua kwa asilimia

0.9. Pamoja na kwamba mchango wa sekta hii katika pato la Taifa ulipungua, ajira zinazotokana na sekta hii ziliongezeka kwa asilimia 1.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado sekta hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali na hivyo Kamati ina ushauri ufuatao kwa Serikali: Moja, kuandaa mikakati ya kuendeleza uzalishaji wa ndani wa malighafi na bidhaa za kati hasa katika sekta zenye uwezekano wa kutumia rasilimali zilizopo nchini. Mbili, kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa nishati ya umeme viwandani na kwa bei nafuu. Tatu, kuimarisha mifumo ya mikopo ya muda mrefu pamoja na kuweka mifumo ya udhamini wa mikopo kwa biashara zinazokidhi vigezo. Nne, Serikali kuweka vivutio kwa viwanda vinavyoongeza thamani kwa kutumia malighafi za ndani husuan katika kilimo, mifugo, uvuvi na madini ili kuongeza fursa za ajira, mapato ya mauzo ya nje na wigo wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya ujenzi kuhusu miundombinu ya barabara, Kamati ilibaini miundombinu ya barabara nchini inakabiliwa na changamoto zifuatazo; Moja, barabara kujengwa chini ya viwango na hivyo kuharibika ndani ya muda mfupi. Mbili, miradi ya barabara kutokukamilika kwa wakati kutokana na ucheleweshaji wa malipo na madeni ya wakandarasi; jambo linalosababisha wakandarasi kuondoka eneo la miradi. Tatu, kuongezeka kwa gharama za miradi ya barabara kutokana na ucheleweshaji wa malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia changamoto hizo Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo: Moja, kuhakikisha barabara zinajengwa kwenye ubora ili ziweze kudumu kwa muda mrefu. Mbili, kuendelea kutoa kupaumbele cha ulipaji wa madeni ya wakandarasi ili kuhakikisha miradi inatekelezwa na inakamilika ndani ya muda uliopangwa. Tatu, kuimarisha udhibiti wa magari yanayotumia barabara ili kupunguza athari za kuzidisha mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na miundombinu ya bandari, shehena ya mizigo inayopokelewa bandarini

imeongezeka kutoka tani 32,000,000.753 mwaka wa fedha 2024/2025 hadi tani 39,000,000.899 mwaka wa fedha 2025/2026, sawa na ongezeko la 21%. Tunaipongeza Serikali kwa ongezeko hili. Ongezeko hili linaashiria kuimarika kwa shughuli za biashara, usafirishaji na ushindani wa bandari za Tanzania katika ukanda huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ongezeko la shehena bado bandari inakabiliwa na changamoto mbalimbali; na Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo: Moja, kudhibiti uanzishwaji wa *ICD* katikati ya mji na kuhakikisha zinajengwa nje ya mji. Mbili, kipande cha reli kinachounganisha Bandari ya Dar es Salaam na Bandari Kavu ya Kwala kianze kutumika ili kupunguza msongamano wa magari bandarini na katikati ya Jiji la Dar es Salaam. Tatu, uendelezaji wa bandari uende sambamba na uendelezaji wa miundombinu ya usafiri pamoja na upanuzi na ujenzi wa gati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya utalii. Sekta ya utalii iliendelea kuimarika mwaka 2025 ambapo mapato yaliongezeka kwa 13% na kufikia Dola za Marekani milioni 4,410.6 kutoka Dola za Marekani milioni 3,903.1 mwaka 2024. Aidha, idadi ya watalii wa kimataifa walioingia nchini iliongezeka kwa asilimia 6.7 kutoka watalii 2,141,895 mwaka 2024 hadi watalii 2,294,495 mwaka 2025. Takwimu hizo zinaonesha kuwa utalii wa mapumziko uliendelea kuwa chanzo kikuu cha wageni ukiwa na 64% ya watalii wote nchini Tanzania Bara na 92.9% kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Kamati ilibaini kuwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana, sekta inakabiliwa na changamoto zifuatazo: Moja, miundombinu hafifu ya kuwezesha shughuli za utalii kama vile ukosefu wa njia za kutua na kupaa kwa ndege kwenye maeneo ya vivutio; huduma za malazi na barabara kwenye maeneo ya mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia lengo, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo: Moja, kuendelea kuboresha miundombinu katika maeneo yenye vivutio vya utalii; mbili, kulinda maeneo ya utalii na kudhibiti uvamizi kwa ajili ya shughuli za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala haya yakitekelezwa yatasaidia kukuza sekta ya utalii na kufikia malengo ya kuvutia watalii wengi zaidi kutoka ndani na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na maji na usafi wa mazingira, takwimu zinaonesha kwamba upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa vijijini umeongezeka kutoka 83.1% mwaka wa fedha 2024/2025 hadi 85.2% mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, upatikanaji wa maji katika makao makuu ya mikoa uliongezeka kutoka 90.6% hadi 92.5%, huku kaya za vijijini zenye miundombinu bora ya usafi wa mazingira zikiongezeka kutoka 72% hadi 78.5% katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya sekta bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali na Kamati ina ushauri ufuatao; Moja, Serikali kufanya marejeo ya namna inavyokusanya takwimu za upatikanaji wa maji, kwa sababu hazioneshi hali halisi ya upatikanaji wa maji mijini na vijijini kwa sababu baadhi ya miradi iliyotumika katika kukusanya takwimu haifanyi kazi wakati huu. Mbili, kabla ya kuanza kutekeleza mradi wowote ule Serikali ijiridhishe na uendelevu wa chanzo cha maji. Tatu, kulipa madeni ya wakandarasi ili kuhakikisha kwamba miradi iliyoanza inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya nishati, uzalishaji wa umeme umefikia megawati 4,648.69 mwezi Juni, 2026 sawa na 94.6% ya lengo la mwaka la megawati 4,915. Aidha, wananchi waliounganishwa na huduma ya umme walifikia 52.1% mwaka wa fedha 2024/2025 ilihali upatikanaji wa huduma ya umeme ukifikia 85.5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi wa mwenendo wa sekta hii na changamoto mbalimbali zilibainishwa na Kamati ina ushauri ufuatao: Moja, kufanya mapitio ya Shirika la *TANESCO* ili kuangalia uwezekano wa kuwa na shirika moja linalomiliki kampuni tatu; kampuni ya uzalishaji, usafirishaji, na usambazaji. Hatua hii italeta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya shirika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, kuhakikisha miradi yote ya kuboresha miundombinu ya umeme, hasa ya usafirishaji,

inakamilika ili umeme uliopo upatikane kwa wakati na kupunguza upotevu ambao upo kati ya 14% na 15% ilihali kiwango kinachokubaliwa kimataifa ni asilimia tano hadi asilimia nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/2028. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/2028 ni mpango wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao unatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi trilioni 20.89, sawa na 30.2% ya bajeti yote ya mwaka 2027/2028. Mpango huu umeweka mkazo katika kuongeza tija, thamani ya uzalishaji, kuimarisha ushindani wa bidhaa na huduma, kuchochea uwekezaji wa ndani na nje, kuongeza ushiriki wa sekta binafsi na kuboresha huduma za kijamii pamoja na ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2027/2028 una malengo mahususi saba, kama yanavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya mpango kwa mwaka 2027/2028 yamejikita katika maeneo sita ya kimkakati yaliyoainishwa katika *FIDP* 4 kama yanavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati. Kamati ilifanya uchambuzi wa vipaumbele na kubaini yafuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, vipaumbele ni vingi na hakuna msisitizo katika eneo moja ambalo linaweza kuleta matokeo yaliyotarajiwa; mbili, rasilimali fedha zilizotengwa na Serikali endapo kutakuwa na ushiriki hafifu wa sekta binafsi kama ilivyojitokeza katika Mpango wa Mwaka wa fedha 2024/2025 itakuwa ni vigumu vipaumbele kufikiwa. Tatu, tulichokiona ni kwamba, mageuzi katika sekta za kimkakati yanahitaji ushirikiano wa taasisi zote za umma ili yaweze kufikiwa. Nne, sekta za msingi kama vile kilimo, miundombinu, ardhi, viwanda pamoja na maliasili na utalii hazijapewa kipaumbele cha pekee, ikiwa ndiyo sekta za msingi ili kuwezesha utekelezaji wa vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kufikia malengo na shabaha Kamati inashauri yafuatayo: Moja, Serikali kuwekeza zaidi

kwenye miundombinu ya usafiri na usafirishaji pamoja na upatikanaji wa umeme wa uhakika, ili iwe kichocheo cha ukuaji wa sekta zingine. Serikali kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara ili kuvutia uwekezaji na sekta binafsi kutoka ndani na nje ya nchi katika kutekeleza mpango. Hatua hii itasaidia uzalishaji wa ajira, uhamishaji wa teknolojia, kuongeza ufanisi katika uzalishaji na kukuza sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iimarishe miundombinu ya utalii kama vile barabara kwenye mbuga, uboreshaji wa viwanja vya ndege, pamoja na kuweka vivutio katika sekta ya hoteli ili kuongeza idadi ya watalii na hatimaye kuongeza mapato ya kigeni. Serikali iupe kipaumbele mpango wake wa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Serikali kuwekeza kwenye sekta ya kilimo ili kuongeza tija sambamba na kutafuta masoko ya uhakika ya kimataifa. Serikali ifungue soko la mitaji ili kuwezesha upatikanaji wa mitaji na kwa gharama nafuu. Serikali iimarishe huduma kama vile afya na elimu ili kuwe na jamii bora na iliyoelimika na yenye afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo na shabaha za uchumi jumla ni kama inavyoonekana kwenye majedwali kwenye taarifa yetu, pamoja na afua za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka wa fedha 2027/2028 zilizoainishwa kwenye mapendekezo ya mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri masuala yafuatayo: Moja, Serikali kuwekeza na kuimarisha upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi na kwa wakati ili ziweze kutumika katika matumizi mbalimbali kama vile akili unde. Vilevile, iwekeze kwenye vituo vya kutunza takwimu *(data center)* ambapo hivi sasa nchini vipo viwili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuliko kuendelea kutegemea fedha za wafadhili katika kukusanya takwimu muhimu. Serikali ipunguze matumizi yasiyo ya lazima, hatua itakayosaidia kupunguza kasi ya ukuaji wa matumizi na hivyo kupunguza nakisi ya bajeti. Kingine, Serikali kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija

kwa kufanya tathmini ya misamaha ya kodi inayotolewa hivi sasa kwa makampuni na taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na demografia na maendeleo ya watu, hali ya umasikini kwa mujibu wa Taarifa ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Tanzania Mwaka 2025 kuna masuala yafuatayo: Kwanza, kiwango cha umasikini kimepungua kutoka 34.4% mwaka 2007 hadi 25.1% mwaka 2025, ambapo kwa kipindi cha miaka 18 Serikali imeweza kupunguza umasikini kwa asilimia 9.3. Pili, kiwango cha umaskini ni kikubwa zaidi vijijini kuliko mijini, ambapo 30.7% ya Watanzania waishio bara wanaishi katika umasikini wa mahitaji ya msingi ikilinganishwa na 14.8% ya wananchi wanaoishi mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utofauti wa umasikini *(povert gape)* nchini ni asilimia 6.2 na umaskini uliokithiri ni asilimia 2.2. Baadhi ya sababu zinazochangia kasi ndogo ya kupungua kwa umasikini; moja, hali ya utegemezi nchini ambapo uwiano ni 100:87 maana yake ni katika kila watu 100, watu 87 ni tegemezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ni utofauti wa kipato na matumizi nchini umeongezeka kutoka kiwango cha 0.38 mwaka wa fedha 2017/2018 hadi kufikia kiwango cha 0.42 mwaka 2025. Kiwango kinachokubalika ni chini ya 0.39, kiwango chochote kinachovuka 0.4 kinahesabika kwamba kuna utofauti mkubwa wa kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kiwango cha umasikini kinapungua na kufikia lengo la chini ya 15% ifikapo wa fedha 2030/2031, Kamati inashauri masuala yafuatayo: Moja, kupunguza kasi ya ongezeko la watu; pili, kuongeza tija ya sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuongeza uzalishaji; tatu, kupunguza tofauti za maendeleo kati ya mijini na vijijini kwa kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya barabara, umeme, maji, mawasiliano na masoko katika maeneo ya vijijini ili kuchochea shughuli za kiuchumi kwa kuongeza fursa za ajira; na nne, kuimarisha ufuatiliaji na tathmini wa programu za kupunguza umasikini ili kubaini endapo zinaleta tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la ajira, Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa ya utafiti wa watu wenye uwezo wa

kufanya kazi na masuala yafuatayo yalibainika: Moja, kiwango cha ushiriki wa nguvu kazi *(labour force participation rate)* kimeongezeka kutoka 73.2% mwaka 2024 hadi 75.9% mwaka 2025. Hali hii inaashiria kuwa kiwango cha watu wenye umri wa kufanya kazi kinachojishughulisha kwenye shughuli za uzalishaji kimeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, 51.5% ya nguvu kazi imeajiriwa kwa masharti ya muda na 13.2% ya nguvu kazi ina ajira ya kulipwa mishahara. Tatu, sekta ya kilimo imeendelea kuajiri takribani 54.4% ya nguvu kazi mwaka 2025 ikifuatiwa na sekta ya huduma kwa 35.5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; sekta ya kilimo imeendelea kuajiri takribani 54.4% ya nguvu kazi mwaka 2025, ikifuatiwa na sekta ya huduma 35.5% na kiwango cha nguvukazi kilichoajiriwa katika sekta ya viwanda ni 10.1% mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne; kiwango cha ukosefu wa ajira kimepungua na kufikia asilimia 5.9 mwaka 2025, ikilinganishwa na 6.2% mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano; kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana wenye miaka kati ya 15 hadi 35 kimepungua hadi asilimia 7.5 mwaka 2025 kutoka asilimia 8.1mwaka 2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendelea kuongeza fursa za ajira Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali kuendelea na mikakati ya kufanya mageuzi katika sekta ya kilimo kuhakikisha kinakuwa cha kisasa na chenye tija ili kuongeza uzalishaji utakaochochea maendeleo ya viwanda ambayo yatatoa fursa ya ajira;

(ii) Kuendelea kuwekeza kwenye Elimu ya Ujuzi na Ufundi Stadi, hatua hii itawawezesha wananchi kujiajiri na kuendana na mahitaji ya soko la ajira ndani na nje ya nchi; na

(iii) Kuendelea kuhamasisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika ujenzi na uendelezaji wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa Sekta Binafsi. Sekta Binafsi itaendelea kuwa chanzo muhimu cha ugharimiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka wa fedha 2027/2028. Aidha, mpango unapendekeza kuongeza mchango wa uwekezaji wa Sekta Binafsi kwenye rasilimali za kudumu kufikia 77% ambapo kwa sasa Sekta Binafsi inatarajiwa kuchangia 70% tu. Pia, Sekta Binafsi inatarajiwa kuchangia shilingi trilioni 62.3. Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini yafuatayo:-

(i) Tangu kutungwa kwa Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi sura ya 103 mwaka 2010 pamoja na marekebisho yake, bado Tanzania haijaweza kunufaika na utekelezaji wa miradi kwa njia hii ya ubia; na

(ii) Maafisa Masuuli kutokutekeleza Kifungu 4(6) cha Sheria ya *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha miradi ya *PPP* inatekelezeka kikamilifu, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Maafisa Masuuli kutangaza fursa za miradi iliyopo katika maeneo yao;

(ii) Serikali kufanya maboresho ya Sheria ya *PPP* pamoja na Kanuni zake ili kurahisisha hatua za uandaaji, uidhinishaji na utekelezaji wa miradi ya *PPP*. Mwaka wa Fedha 2027 miradi yote ambayo Serikali ina nia ya kuitekeleza kwa njia ya *PPP* basi itangaze ili Sekta Binafsi iweze kushindana;

(iii) Kufanya maboresho ya Kifungu 4(6) cha Sheria ya *PPP* ili kuweka adhabu kwa Maafisa Masuuli ambao hawatekelezi; na

(iv) Kuweka masharti katika Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti katika Sheria ya Tume ya Mipango ili

kuweka sharti la lazima kwa miradi yote ya Serikali yenye sura ya kibiashara kutoingizwa kwenye orodha ya miradi inayotegemea bajeti ya Serikali na badala yake itekelezwe kwa mfumo wa *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugharimiaji wa mpango; Kamati ilifanya uchambuzi na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka wa fedha 2027/2028 utagharimu shilingi trilioni 89.3 kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano. Kiasi hicho shilingi trilioni 20.89 kutoka kwenye bajeti ya Serikali na trilioni 6.3 ni uwekezaji unaotarajiwa kutoka katika Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi huo Kamati inashauri:-

(i) Ili Sekta Binafsi iweze kuchangia rasimali fedha kwenye utekelezaji wa mpango ni vyema Serikali ikaweka kipaumbele katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji wa biashara, sambamba na kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI) kwa ukamilifu wake; na

(ii) Serikali kutekeleza sera ya kubana matumizi ili kupata ahueni kwenye bajeti ya kugharimia shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu biashara ya kaboni; Kamati ilifanya uchambuzi wa biashara ya kaboni nchini na kubaini masuala yafuatayo:-

(i) Mapato yanayotokana na mauzo ya viwango vya kaboni yamefikia dola za Marekani 2,000,000; na

(ii) Mfumo wa kitaifa wa uhakiki haujaanza kazi kikamilifu, hivyo Serikali kutegemea taarifa za waendelezaji bila uwezo wa kujiridhisha kwa uhuru kuhusu idadi ya hali ya kaboni zinazouzwa na bei yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uchambuzi huo, Kamati inaishauri Serikali kwamba, kutokana na mapato yanayotokana na

biashara ya kaboni dola za Marekani 2,000,000 ni kidogo ikilinganishwa na fursa zilizopo kwenye sensa za misitu, kilimo, nishati safi, uhifadhi wa mazingira, matumizi ya teknolojia za kupunguza utoaji wa hewa ukaa, kuna haja ya kuongeza kasi ya kutumia chanzo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu mwongozo, maandalizi na bajeti ya Serikali. Utekelezaji wa bajeti ya Serikali mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 56.49. Fedha hizo shilingi 39,000,000,000,000 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 17.49 zilikuwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji wa mapato. Mapato ya kodi; mapato halisi ya kodi yalikuwa ni shilingi trilioni 34.8 sawa na 107.7% ya lengo la kipindi hicho ya 14.3% ya pato la Taifa. Aidha, mapato hayo ni sawa na ukuaji wa 20.6% ikilinganishwa na mapato ya shilingi trilioni 28.9 ya mwaka 2024/2025. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarishwa kwa ufuatiliaji, usimamizi wa kodi pamoja na ulipaji kodi kwa hiari. Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uhamasishaji wa walipakodi na kulipa kodi kwa hiari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo ya ukusanyaji na kuimarika kwa makusanyo, Kamati inashauri:-

(i) Mamlaka ya Mapato Tanzania kuhakikisha kwamba mapato ya tozo ya huduma ya ushuru wa forodha yanatumika kikamilifu kukamilisha mfumo wa *IDRAS* na mifumo mingine;

(ii) Serikali kuhakikisha kwamba kila kunapokuwa na mabadiliko ya sheria inayolenga ama kupanua wigo wa mapato au kudhibiti upotevu wa mapato, maandalizi ya utekelezaji wake yanakamilika; na

(iii) Kuimarisha timu ya wataalamu ya kuzuia magendo na kuhusisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa matumizi. Mwenendo wa matumizi unaonyesha kuwa katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali ilitoa idhini ya matumizi ya shilingi 55,000,000,000,000 ikiwa ni zaidi kwa shilingi 33,000,000,000 ya mapato yote yaliyokusanywa ya shilingi trilioni 55.5 iliyogharimiwa na mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu. Pamoja na ufanisi huu, Kamati ilibaini kuwa matumizi hayaendani na utolewaji wa fedha kwenye mafungu kama ilivyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapitio ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti katika muda wa kati utakaotumika katika kipindi cha kati, Kamati ilichambua na kubaini kwamba unahitaji kufanyiwa marejeo kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kama hakutakuwa na hatua zozote za kupunguza matumizi ya Serikali katika mwaka wa fedha 2027/2028, makisio ya kutumia shilingi trilioni 69.16 itakuwa vigumu kufikiwa kwa kuangalia makusanyo halisi yaliyokusanywa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maelekezo mbalimbali yaliyobadilishwa katika Mwongozo wa Maandalizi. Kuna maelekezo ambayo yalitolewa kwenye maandalizi, lakini hayakutekelezwa. Moja ni ile kubuni na kutekeleza mikakati ya kuongeza mapato kwa ajili ya kugharimia miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya kimkakati. Suala hili lilielekezwa kwenye Mwongozo wa Mapendekezo ya Bajeti, halikutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo kuhusu kuimarisha usimamizi kwa Mashirika ya Umma kufanya biashara ili kuongeza uchangiaji wa mapato kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali halikutekelezwa sawasawa, kubana matumizi ya Serikali halikutekelezwa sawasawa, kupunguza gharama za ununuzi wa shajara halikutekelezwa sawasawa na kufuta ama kusitisha matumizi yote halikutekelezwa sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ulipaji na malimbikizo ya madeni ya wazabuni, wakandarasi, watumishi na watoa huduma. Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kwamba mwezi Juni, 2022, Serikali iliandaa mkakati wa kudhibiti ongezeko la

madeni iliyokuwa ikidaiwa na wazabuni, wakandarasi na watoa huduma shilingi trilioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia iligundua kwamba Serikali ilikuwa inadaiwa kiasi cha shilingi trilioni 6.58 sawa na ongezeko la 103% mpaka Juni, 2025. Kiwango cha malimbikizo ya madeni ni asilimia 9.8 na Kamati ilikuwa inashauri masuala yafuatayo:-

(i) Kuwachukulia hatua Maafisa Masuuli wote ambao hawatekelezi Waraka Na.1 wa Hazina wa Mwaka 2018; na

(ii) Kuboresha utaratibu wa uhakiki wa madeni ili yalipwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapendekeza Serikali kufanya mapitio ya viwango vinavyoruhusiwa kufanya uhamisho pamoja na kuangalia maeneo ambayo kila mwaka fedha huelekezwa. Aidha, kabla ya uhamisho kufanyika tathmini ya kina ifanyike kuhakikisha kama shughuli inayohamishiwa fedha ama siyo shughuli ambayo ilipaswa iwe imetengewa fedha, lakini haikutengewa au ni shughuli ambayo imetokana na dharura isiyokwepeka na ambayo haikutarajiwa. Kamati ilikuwa na maoni ya jumla kama yanavyoonekana kwenye taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nihitimishe kwa kukushukuru wewe, kumshukuru sana Mheshimiwa Spika wetu Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutuongoza vyema kama Bunge lake Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuwashukuru Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Mipango na Uwekezaji; na Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar, , Waziri wa Fedha pamoja na Naibu Mawaziri wa Fedha Mheshimiwa Mhandisi Mshamu Ali Munde, na Mheshimiwa Laurent Deogratius Luswetula, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, Naibu Waziri, Mipango na Uwekezaji kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kujadili Mpango na Mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru pia Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali; Dkt. Tausi Mbaga Kida, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Mipango pamoja na Dkt. Fred Msemwa, Katibu Mkuu Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru vilevile Naibu Makatibu Wakuu wa Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Makamishna, Wakuu wa Taasisi na wataalamu wote kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha uchambuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upendo wa dhati ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Ali Hassan King, Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kunisaidia wakati wote wa shughuli za Kamati. Pia, nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa umahiri wao katika kuchambua Mpango na Mwongozo uliowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ila si kwa umuhimu nimshukuru sana Ndugu Baraka Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2027/28 PAMOJA NA MAPITIO YA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KATIKA KIPINDI CHA MUDA WA KATI (2026/27 – 2028/29) KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ibara ya 63(3) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikisomwa pamoja na Kanuni ya 116 (2) na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, kwa pamoja vinalipa Bunge jukumu la kukaa, kujadili na kuidhinisha Mipango na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali. Aidha, vifungu vya 8(1)(b), 9(1)(a), 21(1), (2) na (5) vya Sheria ya Bajeti Sura ya 439 vinabainisha majukumu ya Bunge pamoja na Kamati ya Bajeti katika kuchambua na kuidhinisha Mpango na Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2027/28 pamoja na mapitio ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa muda wa kati (2026/27-2028/29) kama ilivyowasilishwa na Serikali na kutoa ushauri wake. Uchambuzi wa Kamati ulifanyika kwa kurejea nyaraka zifuatazo:-

i. Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050;

ii. Mpango wa Maendeleo wa Muda Mrefu wa Miaka 25 (2026/27 – 2050/51);

iii. Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27-2030/31);

iv. Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025;

v. Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26, Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/26 pamoja na robo ya kwanza ya mwaka 2026/27; na

vi. Taarifa, maandiko na machapisho ya Taasisi za utafiti pamoja na za kimataifa.

1.1. Mgawanyo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tisa (09) kama ifuatavyo, Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Tathmini ya Mwenendo wa Viashiria vya Uchumi jumla kwa Mwaka 2025/26; Sehemu ya tatu ni Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2025/26 pamoja na Robo ya Kwanza ya Mwaka 2026/27; Sehemu ya nne ni Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 kwa kipindi cha Robo ya Kwanza; Sehemu ya tano ni Uchambuzi wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28; Sehemu ya sita ni Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali; Sehemu ya saba ni Uchambuzi wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti katika Muda wa Kati (2026/27–2028/29); sehemu ya nane ni Maoni na Mapendekezo ya Ujumla na Sehemu ya tisa ni Hitimisho.

SEHEMU YA PILI

2.0. TATHMINI YA MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI JUMLA KWA MWAKA 2025/26

2.1. Mapitio ya hali ya uchumi wa dunia

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla wa Dunia kwa kuzingatia Taarifa ya Mwenendo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa Mwezi Julai, 2026 (World Economic Outlook Report, July 2026) na kubaini masuala yafuatayo:-

i. Uchumi wa dunia ulikua na kufikia **asilimia 3.5** mwaka 2025 ikilinganishwa na **asilimia 3.4** ya mwaka 2024. Aidha, ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kushuka na

kufikia **asilimia 3.0** mwaka 2026. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia kulichangiwa na athari za migogoro inayoendelea Mashariki ya Kati, ambayo imeongeza shinikizo katika bei za nishati, kuathiri mnyororo wa ugavi na kudhoofisha mazingira ya biashara na uwekezaji duniani;

ii. Ukuaji wa uchumi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ulifikia **asilimia 4.5** mwaka 2025. Aidha, ukuaji unatarajiwa kupungua hadi **asilimia 4.3** mwaka 2026 kabla ya kurejea katika kiwango cha **asilimia 4.5** mwaka 2027; na

iii. Uchumi wa nchi zinazoagiza mafuta na zile ambazo uchumi wake hautegemei kwa kiasi kikubwa rasilimali asilia zinatarajiwa kuathiriwa zaidi na ongezeko la bei za nishati na chakula, kupungua kwa misaada rasmi ya maendeleo (Official Development Assistance - ODA) pamoja na kasi ndogo ya matumizi ya teknolojia ya akili unde (Artificial Intelligence – AI).

Mheshimiwa Spika, jedwali na. 1 linaonyesha mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa dunia kuanzia mwaka 2022 hadi 2025 na maoteo ya mwaka 2026.

Jedwali Na. 1: Mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa dunia kuanzia mwaka 2022 hadi 2025 na maoteo ya mwaka 2026

KUNDI/MWAKA	UKUAJI HALISI NA MAOTEO(ASILIMIA)				
	022	2023	2024	2025	2026 (Maoteo)
Dunia	.8	3.3	3.4	3.5	3.0
Nchi zinazoendelea	.1	1.7	1.9	1.9	1.7
Nchi zinazoibukia na zinaendelea	.3	4.4	4.5	4.5	3.8
Nchi za Kusini Mwa Jangwa la Sahara	.4	3.8	4.2	4.5	4.3

Chanzo: *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF-WEO) Julai, 2026*

Mheshimiwa Spika, kufuatia ongezeko la bei za mafuta katika soko la Dunia na kwa kuzingatia mafanikio yaliyopatikana katika matumizi ya gesi asilia nchini ambapo kati ya mwaka 2024 hadi Desemba 2025, nyumba zilizounganishwa na mtandao wa gesi zimeongezeka kutoka nyumba **1,514** hadi **2,515,** viwanda vilivyounganishwa kwenye mtandao wa gesi vimeongezeka kutoka viwanda **14** hadi **59,** Taasisi zimeongezeka kutoka **6** hadi **26,** magari yanayotumia gesi asilia yameongezeka kutoka **5,000** hadi **7,000** na vituo vya kujazia gesi vimeongezeka kutoka **6** hadi **13**. Hivyo, mafanikio hayo yanaonyesha bado kuna fursa ya kuongeza kasi ya usambazaji wa mtandao wa gesi asilia pamoja na kuhamasisha matumizi ya nishati hiyo ili kupunguza madhara ya upandaji wa bei ya nishati ya mafuta katika soko la dunia;

2.2. Mwenendo wa uchumi wa Taifa

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla wa Taifa ni kama ifuatavyo:-

i. Pato halisi la Taifa lilifikia **shilingi trilioni 186.1** mwaka 2025 ikilinganishwa na **shilingi trilioni 175.7** mwaka 2024, sawa na ukuaji wa **asilimia 5.9** ikilinganishwa na ukuaji wa **asilimia 5.6** mwaka 2024;

ii. Wastani wa Pato kwa mtu lilifikia **dola za Marekani 1,390** sawa na **shilingi 3,544,124** mwaka 2025 ikilinganishwa na **dola za Marekani 1,264** sawa na **shilingi 3,299,637** mwaka 2024;

iii. Mwaka 2025/26, mfumuko wa bei ilifikia wastani wa **asilimia 3.6** ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 3.1** mwaka 2024/25. Aidha, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa **asilimia 4.0** Juni 2026 ikilinganishwa na **asilimia 3.3** katika kipindi kama hicho mwaka 2025 kutokana na kuongezeka kwa bei ya nishati.

iv. Urari wa malipo ya kawaida uliongezeka kwa **asilimia 8.8** na kufikia **dola za Marekani milioni 2,370.4** mwaka 2025/26 kutoka **dola za Marekani milioni 2,178.9** mwaka 2024/25. Aidha, katika mwaka 2026/27 nakisi ya urari wa

malipo ya kawaida inatarijwa kupungua hadi **asilimia 2.4** ya Pato la Taifa kutoka **asilimia 2.5** mwaka 2025/26 na **asilimia 2.3** katika kipindi cha muda wa kati;

v. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia **dola za Marekani milioni 5,888.2** sawa na **shilingi trilioni 15.5** kiasi hicho kinatosheleza kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha **miezi 4.2** juu ya lengo la nchi la kuwa na akiba inayotosheleza uagizaji kwa angalau **miezi 4**;

vi. Hadi kufikia Juni 2026, deni la Serikali lilifikia **shilingi trilioni 117.4** sawa na ongezeko la **asilimia 7.26** ikilinganishwa na **shilingi trilioni 109.4** Juni 2025;

vii. Thamani ya shilingi imeendelea kuimarika ambapo mwaka 2025/26 **dola moja ya Marekani** ilibadilishwa kwa wastani wa **shilingi 2,540.1** ikilinganishwa na **shilingi 2,624.66** mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la thamani ya **shilingi** kwa **asilimia 3.2**.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla na kubaini masuala yafuatayo:-

i. Moja ya sababu iliyochangia ukuaji wa uchumi wa Taifa ni miundombinu ya usafiri na usafirishaji. Hata hivyo, sekta ya miundombinu inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile barabara kuharibika, utekelezaji wa miradi ya barabara kuchukua muda mrefu kukamilika, barabara kujengwa chini ya kiwango na wakandarasi kuondoka maeneo ya miradi kutokana na kutolipwa kwa wakati;

ii. Katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2021 hadi 2025 ukuaji wa uchumi umekuwa kwa wastani wa **asilimia 5.2** ikilinganishwa na lengo la kukua kwa **asilimia 6.0** kwa mwaka Serikali imekuwa haifikii malengo ya ukuaji wa uchumi kutokana na uuandaaji wa makisio au dhana (assumptions) kutokuwa halisia na hali ya uchumi;

iii. Shughuli zote zilizokuwa kwa kasi zina uhusiano na uwekezaji wa moja kwa moja wa Serikali. Aidha mwelekeo wa Dira 2050 ni Sekta Binafsi kuwa injini ya uchumi kwa uwiano wa **asilimia 70** kwa 30. Hivyo ni wazi kwamba malengo ya Dira hayatafikiwa endapo mwelekeo huu utaendelea kwa kipindi kirefu;

iv. Shughuli za kiuchumi za huduma imeendelea kukua kwa kiwango kikubwa kuliko shughuli za kiuchumi za kilimo, misitu, uvuvi, viwanda na ujenzi;

v. Ongezeko la watu nchini ni **asilimia 2.8**, kiwango hiki ni kikubwa kuliko kiwango kinachokubalika kwa nchi zinazoendelea cha **asilimia 1.5 hadi 2.5**; na

vi. Licha ya kuwa kiwango cha Riba ya Benki Kuu (Central Bank Rate - CBR) kilipunguzwa kutoka **asilimia 6** hadi **asilimia 5.75** katika kipindi Julai 2025 ili kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo la muda wa kati la **asilimia 3** hadi **5**, mfumuko wa bei umeendelea kuongezeka hadi kufika **asilimia 4** Juni 2026. Mwenendo huu unaashiria kuwa kupunguza riba ya Benki Kuu pekee hakuzuii ongezeko la mfumuko wa bei. Hali hii inaweza kusababishwa na changamoto za uzalishaji na ugavi (supply- side shocks) kama vile kupanda kwa bei ya mafuta duniani, uhaba wa chakula kutokana na ukame pamoja na kupanda kwa gharama za usafirishaji. Aidha, inaweza kuashiria kwamba sera za fedha nchini zina athari ndogo katika mwenendo wa mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, kufuatia uchambuzi huo Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji kwa kutatua changamoto zilizopo zikiwemo malipo ya madeni ya wakandarasi, ukarabati wa miundombinu iliyoharibika kwa wakati na ujenzi wa miundombinu yenye ubora inayoweza kudumu kwa muda mrefu. Hatua hii itaongeza mchango wa miundombinu katika ukuaji wa uchumi;

ii. Serikali kuandaa maoteo kwa kutumia dhana (assumptions) zenye uhalisia na hali ya mwenendo wa uchumi ili kuongeza usahihi wa maoteo ili kupanga mipango na bajeti zinazoendana na hali halisi;

iii. Serikali kuweka mikakati ili kuhakikisha ukuaji wa sekta ya huduma unafungamanishwa na sekta zingine za uchumi kama vile kilimo, misitu, uvuvi, viwanda na ujenzi; na

iv. Kufanya tathmini ya ufanisi wa mfumo wa riba ya Benki Kuu (Central Bank Rate - CBR) ili kubaini ni kwa kiasi gani mfumo huu umesaidia kupunguza viwango vya riba na mfumuko wa bei nchini kwa kipindi chote ambacho umetumika kuanzia mwaka 2024.

SEHEMU YA TATU

3.0. UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA 2025/26 PAMOJA NA ROBO YA KWANZA YA MWAKA 2026/27

Mheshimiwa Spika, Kamati imechambua utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/26 pamoja na robo ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/27 na kubaini masuala yafuatayo:-

i. **Taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Mwaka mmoja kujumuisha utekelezaji wa miradi iliyokwisha kukamilika katika Mpango wa tatu wa Maendeleo wa miaka mitano**

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2025/26, Serikali ilitekeleza miradi kama vile ujenzi wa Bwawa la Julius Nyerere lenye uwezo wa kuzalisha umeme wa **MW 2,115**; mradi wa kuunganisha umeme katika Gridi ya Taifa katika Mikoa 24; miradi ya madaraja ya JPM (Kigongo–Busisi) na Tanzanite, ujenzi wa barabara za juu za Uhasibu na Chang'ombe; ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) katika vipande vya Dar es Salaam–Morogoro (km 300) na Morogoro–Makutupora (km 422); na ujenzi wa Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi. Kamati inapendekeza Tume kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ili utoaji wa taarifa

uzingatie miradi iliyokamilika katika mwaka husika wa fedha na ile inayotekelezwa kwa mwaka zaidi ya mmoja.

ii. **Tume kutoa Mafunzo kwa Wizara, Idara, Mamlaka na Taasisi mbalimbali za Umma kuhusu mfumo wa e-Delivery**

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Mipango ihakikishe inatoa mafunzo elekezi ya jinsi ya kutumia mfumo wa tathmini na ufuatiliaji wa e-Delivery kwa taasisi zinazotekeleza mpango ili watumishi wanaopaswa kutoa taarifa za utekelezaji wa miradi waweze kutoa taarifa hizo kwa usahihi na kwa wakati.

iii. **Miradi ya kimkakati kuchelewa kuanza utekelezaji kwa muda mrefu**

Mheshimiwa Spika, baadhi ya miradi ya kimkakati imekuwa haitekelezwi kwa muda mrefu na imebaki katika hatua za awali kama vile majadiliano au upembuzi yakinifu. Miradi hiyo ni miradi ya umeme ya Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222), mradi wa chuma Liganga na makaa ya mawe Mchuchuma, mradi wa Magadi Soda Engaruka pamoja na miradi ya usindikaji gesi asilia na utafutaji wa mafuta. Hali hii imepelekea kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi kutokana na tathmini za awali kupitwa na wakati na hivyo kulazimika kufanya tathmini upya, jambo linaloongeza gharama na kuchelewesha upatikanaji wa manufaa ya kiuchumi yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa spika, Kamati inaishauri Serikali, kuharakisha ufanyaji wa maamuzi ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa wakati na kupunguza gharama ya utekelezaji.

3.1. Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba bajeti ya Sekta ya Kilimo ilipungua kutoka **shilingi trilioni 1.243** mwaka 2025/26 hadi **shilingi trilioni 1.105** mwaka 2026/27, sawa na kupungua kwa **asilimia 11.1**, bado sekta hii ina umuhimu mkubwa katika kuchangia uchumi wa Taifa. Kamati imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa miradi iliyopo katika sekta hizi na kubaini inakabiliwa na changamoto zifuatayo:-

i. Kilimo kilikua hadi kufikia **asilimia 5.5** mwaka 2025 ikilinganishwa na **asilimia 5.1** mwaka 2024;

ii. Thamani ya mauzo ya mazao ya kilimo nje ilifikia **Dola za Marekani bilioni 3.73** mwaka 2025, ikilinganishwa na **Dola za Marekani bilioni 3.54** mwaka 2024;

iii. Mchango wa sekta ya kilimo katika Pato la Taifa ulipungua hadi **asilimia 24.3** mwaka 2025 kutoka **asilimia 24.9** mwaka 2024. Hatua hii inaweza kuashiria kwamba kuna mabadiliko katika muundo wa uchumi (structual changes);

iv. Mauzo ya nyama nje ya nchi yamepungua kutoka **tani 13,112.44** mwaka 2024/25 hadi **tani 12,763.77** mwaka 2025/26, jambo linaloweza kusababishwa na ushindani wa bidhaa ya nyama katika masoko ya kimataifa au nyama inayozalishwa nchini kukosa ithibati;

v. Sekta ya Uvuvi imeendelea kukua na kufikia **asilimia 6.3** mwaka 2025 kutoka **asilimia 6.0** mwaka 2024;

vi. Uzalishaji wa mazao ya uvuvi umeongezeka kutoka tani **575,000** mwaka 2024/25 hadi tani **659,242.69** mwaka 2025/26; na

vii. Mchango wa sekta ya uvuvi katika Pato la Taifa umepungua kutoka **asilimia 2.3** mwaka 2024/25 hadi **asilimia 2.0** mwaka 2025/26.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi inakabiriwa na changamoto zifuatazo:-

i. Kwa kiasi kikubwa kilimo bado kinategemea mvua za msimu na si umwagiliaji;

ii. Uhaba wa malisho na maji kwa mifugo hasa wakati wa ukame unaochangiwa na mabadiliko ya tabianchi;

iii. Migogoro ya ardhi kati ya wafugaji, wakulima na watumiaji wengine wa ardhi;

iv. Ukosefu wa miundombinu ya kisasa ya mifugo kama vile majosho, machinjio, minada na vituo vya kukusanyia maziwa;

v. Uhaba wa miundombinu ya kisasa ya kuhifadhi samaki, ikiwemo vyumba vya baridi, vituo vya kupokelea na usafirishaji;

vi. Mazao ya samaki, mifugo na kilimo kuuzwa bila kuongezwa thamani;

vii. Athari za mabadiliko ya tabianchi zinazoathiri mazingira ya uzalishaji na upatikanaji wa samaki; na

viii. Uvuvi haramu na matumizi ya zana zisizoruhusiwa zinazopunguza rasilimali za samaki.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. Kuhakikisha ruzuku ya mbolea inawafikia wakulima kwa wakati ili kuboresha kilimo kiwe na tija na hivyo kufikia malengo ya maendeleo ya sekta hiyo;

ii. Kuongeza uwekezaji katika upatikanaji wa malisho na maji ya mifugo, kuharakisha uhimilishaji wa mifugo pamoja na kuimarisha miundombinu ya usindikaji wa nyama na maziwa ili kuongeza thamani ya bidhaa za mifugo; na

iii. Kuvutia uwekezaji katika ufugaji samaki, ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi na kusafirisha mazao ya uvuvi pamoja na kuboresha mnyororo wa thamani wa bidhaa za uvuvi ili kuongeza mauzo ya nje na ajira.

3.2. Sekta ya Viwanda

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba mchango wa sekta ya viwanda kwenye pato la taifa ulishuka kutoka **asilimia 6.8** mwaka 2024 hadi **asilimia 5.9** mwaka 2025 sawa na kupungua kwa **asilimia 0.9**. Pamoja na kwamba mchango wa sekta hii katika pato la taifa umepungua, ajira zinazotokana na sekta hii zimeongezeka kwa **asilimia 1.7.**

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, sekta hii bado inakumbwa na changamoto zifuatazo:-

i. Kukosekana kwa nishati ya umeme ya uhakika na gharama nafuu;
ii. Matumizi ya teknolojia duni na iliyopitwa na wakati pamoja na utegemezi wa mitambo na teknolojia kutoka nje;

iii. Kukosekana kwa mitaji na mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda;

iv. Matumizi hafifu ya malighafi zinazopatikana nchini;
v. Kukosekana kwa miundombinu wezeshi ya usafiri na usafirishaji;

vi. Wingi wa mamlaka za udhibiti zinazotekeleza majukumu yanayofanana hali inayopelekea ongezeko la gharama za ufanyaji biashara;

vii. Kukosekana kwa ujuzi unaohitajika viwandani; na

viii. Ukosefu wa ithibati kwa bidhaa zinazozalishwa nchini na hivyo kusababisha ukosefu wa masoko ya nje.

Mheshimiwa spika, Kamati ina ushauri ufuatao kwa Serikali:

i. Kuandaa mikakati ya kuendeleza uzalishaji wa ndani wa malighafi na bidhaa za kati hasa katika sekta zenye uwezekano wa kutumia rasilimali zilizopo nchini;

ii. Kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa nishati ya umeme viwandani na kwa bei nafuu;

iii. Kuimarisha mifumo ya mikopo ya muda mrefu pamoja na kuweka mifumo ya udhamini wa mikopo (guarantee schemes) kwa biashara zinazokidhi vigezo;

iv. Kudhibiti ubora wa bidhaa pamoja na kupatikana kwa ithibati kwa bidhaa zinazozalishwa nchini; na

v. Serikali kuweka vivutio kwa viwanda vinavyoongeza thamani kwa kutumia malighafi za ndani, hususan katika kilimo, mifugo, uvuvi na madini ili kuongeza fursa za ajira, mapato ya mauzo ya nje na wigo wa mapato ya Serikali.

3.3. Sekta ya Ujenzi

3.3.1. Miundombinu ya barabara

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa licha ya ongezeko la mtandao wa barabara kuu na za Mikoa kufikia kilometa **37,734.41** na kuongezeka kwa ushiriki wa kampuni za ndani kwa **asilimia 60** katika miradi ya ujenzi mchango wa sekta katika Pato la Taifa umepungua kutoka **asilimia 12.5** mwaka 2024 hadi **asilimia 11.9** mwaka 2025. Kutokana na kushuka kwa mchango wa sekta hii kwenye Pato la Taifa, ajira katika sekta ya ujenzi zimepungua kutoka **21,527** hadi **18,988**. Pamoja na masuala hayo, Kamati imebaini sekta hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Barabara kujengwa chini ya viwango na hivyo kuharibika ndani ya muda mfupi;

ii. Miradi ya barabara kutokamilika kwa wakati kutokana na ucheleweshaji wa malipo na madeni ya wakandarasi jambo linalosababisha wakandarasi kuondoka eneo la miradi. Hadi kufikia mwaka 2025 madeni ya wakandarasi yalifikia **trilioni 1.299**;

iii. Malipo ya awali kutolewa kwenye miradi ya barabara ambayo Serikali haina uhakika wa fedha za uendelezaji wake na hivyo kuzalisha madeni;

iv. Kuongezeka kwa gharama za miradi ya barabara kutokana na ucheleweshaji wa malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha miradi hiyo; na

v. Magari kuzidisha uzito kuliko uwezo wa barabara kuhimili.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto hizo Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. Kuhakikisha barabara zinajengwa kwenye ubora ili ziweze kudumu kwa muda mrefu;

ii. Kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa kampuni za ndani ili kuongeza ushiriki wao katika miradi ya ujenzi wa barabara ili kukuza uhamishaji wa teknolojia na ujuzi;

iii. Kuendelea kutoa kipaumbele cha ulipaji wa madeni ya wakandarasi ili kuhakikisha miradi inatekelezwa na inakamilika ndani ya muda uliopangwa;

iv. Kuimarisha udhibiti wa magari yanayotumia barabara ili kupunguza athari za kuzidisha uzito; na

v. Kutumia vyanzo bunifu vya fedha kutekeleza miradi ya barabara (innovative financing), mfano ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya barabara na kupunguza mahitaji ya fedha kwenye bajeti ya Serikali.

3.3.2. Miundombinu ya Reli

Mheshimiwa Spika, huduma za usafiri wa reli ya SGR ziliendelea kutolewa katika vipande vya Dar es Salaam–Morogoro (km 300 – **asilimia 100**) na Morogoro–Makutupora (km 422 – **asilimia 98.79**), huku urefu wa reli iliyokamilika ukiongezeka kutoka kilometa 680.38 mwaka 2024/25 hadi kilometa 749 mwaka 2025/26. Hata

hivyo, Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa baadi ya vipande ulikumbwa na changamoto za upatikanaji wa fedha kwa wakati, hali iliyosababisha kuchelewa kwa ujenzi wa vipande hivyo. Vipande hivyo ni Lot 3 Makutupora–Tabora (km 368 – **asilimia 15.54**) na Lot 4 Tabora–Isaka (km 165 - **asilimia 9.12**), Isaka – Mwanza (km 341 **asilimia 69.31**), Tabora – Kigoma (km 506 - **asilimia 11.35**), Uvinza – Msongati (km 282 - **asilimia 0.62**).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaarifiwa kwamba fedha za utekelezaji wa vipande vilivyosalia zimepatikana na hivyo kipande cha Dar es Salaam–Mwanza kinatarajiwa kukamilika mwaka 2029, huku kipande cha Dar es Salaam–Kigoma kikitarajiwa kukamilika mwaka 2030. Vilevile, Kamati ilitaarifiwa kwamba maandalizi ya utekelezaji wa reli ya Mtwara–Mbamba Bay yameanza.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ukamilishaji wa miundombinu saidizi, kuimarisha muunganiko wa reli na bandari pamoja na maeneo ya uzalishaji na kuhakikisha upatikanaji endelevu wa fedha ili kuongeza tija ya uwekezaji huo na kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kitovu cha usafirishaji na biashara katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

3.3.3. Miundombinu ya Bandari

Mheshimiwa Spika, shehena ya mizigo inayopokelewa bandarini imeongezeka kutoka **tani milioni 32.753** mwaka 2024/25 hadi **tani milioni 39.899** mwaka 2025/26, sawa na ongezeko la **asilimia 21.8**. Ongezeko hili linaashiria kuimarika kwa shughuli za biashara, usafirishaji na ushindani wa bandari za Tanzania katika ukanda huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ongezeko la shehena bado bandari inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Ukuaji wa shehena usioambatana na upangaji bora wa miundombinu ya usafirishaji na uhifadhi wa mizigo;

ii. Kuongeza gharama za usafirishaji na kupunguza ufanisi wa mnyororo wa ugavi; na

iii. Uwepo wa bandari kavu za kuhifadhia makasha nje ya bandari (ICDs) bila bila mpango shirikishi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. Kudhibiti uanzishwaji wa ICDs katikati ya mji na kuhakikisha zinajengwa nje ya mji;

ii. Kipande cha reli kinachounganisha bandari ya Dar es Salaam na bandari kavu ya Kwala kianze kutumika ili kupunguza msongamano wa magari bandarini na katikati ya Jiji la Dar es Salaam;

iii. Uendelezaji wa bandari uende sambamba na uendelezaji wa miundombinu ya usafiri pamoja na upanuzi na ujenzi wa gati.

3.4. Sekta ya Madini na Uchimbaji

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa Sekta ya Madini umeongezeka kutoka **asilimia 8.1** mwaka 2024 hadi **asilimia 9.4** mwaka 2025 na mchango wake katika Pato la Taifa ukiongezeka kutoka **asilimia 7.8** mwaka 2024 hadi **asilimia 10.3** mwaka 2025. Aidha, thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi imeongezeka na kufikia **dola za Marekani bilioni 5.4** mwaka 2025 kutoka **dola za Marekani bilioni 3.1** mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Utoroshwaji wa madini nje ya nchi;

ii. Ukosefu wa mitaji kwa wachimbaji wadogo na wa kati wa madini;

iii. Uongezaji mdogo wa thamani ya madini ndani ya nchi na ukosefu wa ithibati kwa madini ya dhahabu; na

iv. Utegemezi mkubwa wa madini ya dhahabu na Tanzanite ikiwa nchi ina fursa madini adimu kama vile nickel,

graphite na kobalt ambayo bado hayajaanza kuchimbwa na yanahitajika kwa wingi katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuikuza Sekta ya Madini na kuongeza mchango wake katika uchumi wa Taifa, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. Kuweka vivutio ili kuvutia wawekezaji katika uongezaji thamani wa madini nchini;

ii. Kuvutia uwekezaji katika utafiti na uchimbaji wa madini adimu, mafuta na gesi;

iii. Kuboresha miundombinu muhimu kwenye maeneo ya migodi kama vile umeme, barabara na viwanja vya ndege; na

iv. Kuwawezesha wachimbaji wadogo mitaji na teknolojia ili kuongeza tija, ajira, mapato ya Serikali na fedha za kigeni.

Jedwali Na.2 utekelezaji Sekta ya Madini mwaka 2025/26

Na.	Kigezo	Hali halisi 2025/26 (%)	Lengo 2030/31 (%)
1.	Mchango wa Madini kwenye Pato la Taifa	10.3	12.5
2.	Ukuaji	9.4	9
3.	Mauzo nje (USD milioni)	5,401.9	

Chanzo: Mapendekezo ya Mpango 2027/28

3.5. Sekta ya Utalii

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii iliendelea kuimarika mwaka 2025, ambapo mapato yaliongezeka kwa **asilimia 13** na kufikia **dola za Marekani milioni 4,410.6** kutoka **dola za Marekani milioni 3,903.1** mwaka 2024. Aidha, idadi ya watalii wa kimataifa walioingia nchini iliongezeka kwa **asilimia 6.7** kutoka watalii **2,141,895** mwaka 2024 hadi watalii **2,294,495** mwaka 2025. Takwimu hizo zinaonesha kuwa utalii wa mapumziko (leisure tourism)

uliendelea kuwa chanzo kikuu cha wageni, ukiwa na **asilimia 64.6** ya watalii wote nchini Tanzania Bara na **asilimia 92.9** kwa upande wa Zanzibar. Kwa upande mwingine, watalii waliokuja kwa madhumuni ya biashara ni **asilimia 12.5** nchini Tanzania na **asilimia 0.4** Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati imebaini kuwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii, bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Miundombinu hafifu ya kuwezesha shughuli za utalii kama vile ukosefu wa njia za kutua na kupaa kwa ndege kwenye maeneo ya vivutio, huduma za malazi na barabara kwenye maeneo ya mbuga za wanyama;

ii. Baadhi ya vivutio vya utalii vilivyopo nchini havijaweza kutangazwa ili kuvutia watalii na hivyo kuikosesha Serikali mapato stahiki; na

iii. Kuvamiwa kwa maeneo ya hifadhi za Taifa na mapori tengefu kwa ajili ya shughuli za kibinadamu.

Mheshimiwa Spika, moja ya afua zilizobainishwa na Serikali katika kuimarisha Sekta ya Utalii ni kuhakikisha angalau **asilimia 40** ya biashara za utalii zinaendeshwa kwa kutumia mifumo ya kidijitali. Utekelezaji wa azma hii unatarajiwa kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma, kupunguza gharama za uendeshaji na kuimarisha uwezo wa kuitangaza Tanzania katika masoko ya kimataifa kupitia majukwaa ya kidijitali. Hivyo, ili kufikia lengo, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. Kuendelea kuboresha miundombinu katika maeneo yenye vivutio vya utalii;

ii. Kuendelea kutangaza vivutio ambavyo bado havijatangazwa kikamilifu hasa vivutio vilivyopo ukanda wa kusini; na

iii. Kulinda maeneo ya utalii na kudhibiti uvamizi kwa ajili ya shughuli za kijamii kwenye maeneo ya hifadhi na mapori tengefu.

Mheshimiwa Spika, masuala haya yakitekelezwa yatasaidia kukuza Sekta ya Utalii na kufikia malengo ya kuvutia watalii wengi zaidi kutoka ndani na nje ya nchi hadi kufikia **asilimia 8** na hatimaye kuongeza mapato ya fedha za kigeni pamoja na mchango wa sekta hiyo katika ukuaji wa uchumi wa Taifa.

3.6. Maji na Usafi wa Mazingira

Mheshimiwa Spika, Takwimu zinaonyesha kwamba upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa vijijini umeongezeka kutoka **asilimia 83.1** mwaka 2024/25 hadi **asilimia 85.2** mwaka 2025/26. Aidha, upatikanaji wa maji katika Makao Makuu ya Mikoa uliongezeka kutoka **asilimia 90.6** hadi **asilimia 92.5**, ilhali kaya za vijijini zenye miundombinu bora ya usafi wa mazingira zikiongezeka kutoka **asilimia 72.0** hadi **asilimia 78.5** katika kipindi hicho. Pamoja na mafanikio hayo bado sekta hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Licha ya ongezeko la uwekezaji katika Sekta ya Maji ikiwa ni pamoja na ununuzi wa mitambo ya kuchimba visima katika Wilaya mbalimbali, changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama bado inaendelea kujitokeza, hasa katika maeneo ya vijijini;

ii. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) imeonesha kwamba Mabwawa **145** yanayomilikiwa na Taasisi za Serikali bado hayajasajiliwa na Wizara husika. Kwa kutokusajiliwa kwa mabwawa hayo kunaweza kusababisha kutokuwepo kwa usimamizi na ufuatiliaji madhubuti, hatari ya kutofanyiwa ukaguzi wa usalama kwa wakati, ugumu wa kupanga matumizi ya rasilimali za maji na uwezekano wa Serikali kukosa takwimu sahihi kwa ajili ya mipango na uwekezaji katika Sekta ya Maji.

iii. Kuvamiwa na kukauka kwa baadhi ya vyanzo vya maji;

iv. Miradi ya maji kutokamilika kwa wakati kutokana na madeni ya wakandarasi kutolipwa; na

v. Miradi ya maji kujengwa kwenye vyanzo vya maji visivyo vya uhakika na hivyo kukauka ndani ya muda mfupi na kuleta hasara ya uwekezaji kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua changamoto hizo Kamati inashauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. Kuhakikisha mabwawa yote yanatambuliwa na kusajiliwa kwenye daftari la kitaifa la mabwawa. Hatua hii itasaidia kuimarisha ufuatiliaji, usalama na usimamizi wa rasilimali za maji;

ii. Serikali kufanya marejeo ya namna inavyokusanya takwimu za upatikanaji wa maji kwa sababu hazionyeshi hali halisi ya upatikanaji wa maji mijini na vijijini kwa sababu baadhi ya miradi iliyotumika katika kukusanya takwimu haifanyi kazi;

iii. Kabla ya kuanza kutekeleza mradi wowote wa maji, Serikali ijiridhishe na uendelevu wa chanzo cha maji;

iv. Kulipa madeni ya wakarandasi ili kuhakikisha kwamba miradi iliyoanza inakamilika kwa wakati;

v. Kuongeza uwekezaji katika miradi ya maji vijijini, umwagiliaji na mabwawa ya kunyweshea mifugo ili kuhakikisha fedha zinazotengwa katika Sekta ya Maji zinaleta matokeo yanayoonekana katika uzalishaji na ustawi wa wananchi;

vi. Serikali iharakishe ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kuhifadhi na kusambaza maji pamoja na kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya maji ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; na

vii. Serikali ikamilishe ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji ili wakulima wasiwe wanategemea mvua kwenye kilimo.

Jedwali na.3 Utekelezaji wa miradi ya maji kwa mwaka 2025/26

Na.	Kigezo	Hali halisi 2025/26(%)	Lengo 2030/31(%)
1.	Watu vijijini wanaopata maji ya bomba/salama	85.2	87.9
2.	Kaya zenye miundombinu bora ya usafi wa mazingira	76.4	100
3.	Watu Dar es salaam wanaopata maji ya bomba/salama	91.6	100
4.	Watu kwenye Makao Makuu ya Mikoa wanaopata maji ya bomba/salama	92.5	98.4
5.	Kaya za Makao Makuu ya Mikoa zenye mfumo rasmi wa maji taka	24.0	60

Chanzo: *Taarifa ya mapendekezo ya Mpango wa mwaka 2027/28*

3.7. Ardhi na Maendeleo ya Makazi

Mheshimiwa Spika, viwanja na mashamba yaliyopimwa vilifikia **3,079,886** mwaka 2025/26 kutoka **2,857,349** mwaka 2024/25; hati zilizotolewa zilifikia **2,675,848** mwaka 2025/26 kutoka **2,573,849** mwaka 2024/25 na vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi vilifikia **4,953** sawa na **asilimia 40.47** kutoka vijiji **4,672** sawa na **asilimia 37.76** mwaka 2024/25. Aidha, Mpango unapendekeza kupunguza kiwango cha ardhi yenye makazi yasiyo rasmi kufikia **asilimia 45.4** na kuongeza Mikoa yenye mipango kabambe na mipango miji kufikia **asilimia 88.6**.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mwenendo huo, uchambuzi wa Kamati umebaini Sekta ya Ardhi bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Kuongezeka kwa makazi holela;

ii. Wananchi kushindwa kutumia ardhi kama dhamana ya kuchukulia mikopo kwenye taasisi za kifedha;

iii. Kukosekana kwa maeneo ya ardhi yaliyopimwa kwa ajili ya uwekezaji mfano mashamba, viwanda na ufugaji;

iv. Urasimu katika utoaji wa vibali vya ujenzi;

v. Ardhi ya kilimo kubadilishwa kwa ajili ya matumizi ya makazi; na

vi. Kuendelea kuwepo kwa migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi za Serikali katika utekelezaji wa Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK). Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mpango wa KKK ambao utasaidia kupunguza na kuondokana na changamoto zote za ardhi. Vilevile, Serikali ihakikishe inatoa hati miliki kwa wakati ili wananchi waweze kuzitumia kwa ajili ya kupata mitaji na kuendeleza shughuli za kiuchumi.

3.8. Sekta ya Nishati

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa umeme umefikia **MW 4,648.69** mwezi Juni 2026 sawa na **asilimia 94.6** ya lengo la mwaka la **MW 4,915**. Aidha, mahitaji ya juu ya umeme (peak demand) mwaka 2025/26 kwenye grid ya Taifa ni **MW 2,505.86** hii inamaanisha kwamba kuna ziada ya **MW 2,142.83** juu ya mahitaji ya umeme ya nchi. Aidha, wananchi waliounganishwa na huduma ya umeme walifikia **asilimia 52.1** mwaka 2024/25, ilhali upatikanaji wa huduma ya umeme ukifikia **asilimia 85.5**

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa mwenendo wa Sekta hii na kubaini masuala yafuatayo:-

i. Matumizi ya umeme kwa mtu yaliongezeka na kufikia **kWh 243** mwaka 2025/26 kiwango ambacho ni chini ya

kiwango cha nchi za uchumi wa kati cha **kWh 928** kwa mtu;

ii. Takwimu zinaonyesha kwamba kuna umeme wa ziada wa **MW 2,375**. Hata, hivyo ziada hii inakadiriwa kwa kuangalia waliounganishwa na sio mahitaji ya wananchi, viwanda, migodi na maeneo mengine ambayo yanahitaji huduma hiyo na hayajaunganishwa;

iii. Kampuni ya umeme ya Taifa (TANESCO) ni shirika hodhi kwenye biashara ya uzalishaji na usambazaji wa nishati ya umeme jambo ambalo linaathiri ufanisi katika utoaji wa huduma wa shirika hilo; na

iv. Pamoja na jitihada za Serikali za kuboresha miundombinu ya Kusafirishia umeme bado kuna changamoto kubwa inayosababisha kukatika kwa umeme mara kwa mara. Aidha, miradi ya gridi imara imekuwa ikitekelezwa kwa kusuasua kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto hizo kamati inashauri masuala yafuatayo:-

i. Kufanya mapitio ya shirika la TANESCO ili kuangalia uwezekano wa kuwa na Shirika moja linalomiliki kampuni tatu (Holding Company) Kampuni ya Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji. Hatua hii italeta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya shirika hilo;

ii. Kuhakikisha miradi yote ya kuboresha Miundombinu ya Umeme hasa ya usafirishaji inakamilika ili umeme uliopo upatikane kwa wakati na kupunguza upotevu ambao upo kati ya **asilimia 14** na **asilimia 15** wakati kiwango kinachokubaliwa kimataifa ni kati ya **asilimia 5** hadi **asilimia 8**;

iii. Kampuni ya umeme ya TANESCO kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya umeme mfano miradi ya Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba utekelezaji wa miradi hii utasaidia sana upatikanaji wa umeme na kufikia malengo ya Dira 2050.

SEHEMU YA NNE

4.0. UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2026/27 KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa mpango kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2026/27 na kubaini masuala yafuatayo:-

i. Kiasi cha fedha kilichotumika katika robo ya kwanza ya mwaka hakikubainishwa;

ii. Taarifa ya utekelezaji wa miradi imejumuisha na miradi ya mwaka uliotangulia hivyo ni vigumu kupima ufanisi; na

iii. Hakuna vigezo vya wazi vinavyopimika vilivyotarajiwa kufikiwa katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka kwa kila programu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza Serikali kuhakikisha kwamba Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango kwa robo mwaka inaainisha kiwango cha fedha kilichotumika, malengo yaliyokusudiwa kufikiwa katika muda huo ili Kamati ifanye ufuatiliaji wenye tija.

SEHEMU YA TANO

5.0. UCHAMBUZI WA MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA MWAKA 2027/28

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2027/28 ni mpango wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27-2030/31) ambao unatarajiwa kugharimu kiasi cha **Shilingi trilioni 20.89** sawa na **asilimia 30.2** ya bajeti yote ya mwaka 2027/28. Mpango huu umeweka mkazo katika kuongeza tija na thamani ya

uzalishaji, kuimarisha ushindani wa bidhaa na huduma, kuchochea uwekezaji wa ndani na nje, kuongeza ushiriki wa sekta binafsi na kuboresha huduma za kijamii pamoja na ustawi wa wananchi. Aidha, lengo kuu la Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2027/28 ni kuendelea kutekeleza afua za kimkakati ili kuleta mageuzi kwa ajili ya ukuaji jumuishi wa uchumi na uzalishaji wa ajira.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2027/28 una malengo mahsusi 7 ambayo ni:-

i. Kuimarisha ukuaji wa uchumi, mazingira ya biashara na uwekezaji;

ii. Kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi;

iii. Kuongeza fursa za ajira na kipato;

iv. Kuchochea maendeleo ya watu na ustawi wa jamii;

v. Kuboresha miundombinu na kuendeleza vichocheo vya mageuzi;

vi. Kuimarisha uhimilivu wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi; na

vii. Kuimarisha utawala, uratibu na utekelezaji wa Mpango.

5.1. Vipaumbele vya mpango

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango kwa mwaka 2027/28 yamejikita katika maeneo sita (6) ya kimkakati yaliyoainishwa katika FYDP IV ambayo ni:

i. Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani;

ii. Kujenga Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii;

iii. Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi;

iv. Vichocheo vya maendeleo;

v. Mageuzi katika Sekta za Kimkakati; na

vi. Kuimarisha Misingi ya Uendelevu wa Taifa.

Mheshimiwa spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2027/28 na kubaini yafuatayo:-

i. Vipaumbele ni vingi na hakuna msisitizo katika eneo moja ambalo linaweza kuleta matokeo yaliyotarajiwa;

ii. Rasilimali fedha zilizotengwa na Serikali endapo kutakuwa na ushiriki hafifu wa sekta binafsi kama ilivyojitokeza katika mpango wa mwaka 2024/25 itakuwa ni vigumu vipaumbele kufikiwa;

iii. Mageuzi katika Sekta za Kimkakati yanahitaji ushirikiano wa Taasisi zote za umma ili yaweze kufikiwa;

iv. Sekta za msingi kama vile kilimo, miundombinu, ardhi, viwanda pamoja na maliasili na utalii na hazijapewa kipaumbele cha pekee ikiwa ndio sekta za msingi ili kuwezesha utekelezaji wa vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kufikia malengo na Shabaha zilizokusudiwa, Kamati inashauri masuala yafuatayo:-

i. Serikali kuwekeza zaidi kwenye miundombinu ya usafiri na usafirishaji pamoja na upatikanaji wa umeme wa uhakika ili iwe kichocheo cha ukuaji wa sekta nyingine;

ii. Serikali kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara ili kuvutia wawekezaji na sekta binafsi kutoka ndani na nje ya nchi katika kutekeleza mpango. Hatua hii itasaidia uzalishaji wa ajira, uhamishaji wa teknolojia, kuongeza ufanisi katika uzalishaji na kukuza Sekta ya Viwanda;

iii. Serikali kuimarisha miundombinu ya utalii kama vile barabara kwenye mbuga, uboreshaji wa viwanda vya ndege pamoja na kuweka vivutio katika sekta ya hoteli ili kuongeza idadi ya watalii na hatimaye kuongeza mapato ya kigeni;

iv. Serikali iupe kipaumbele mpango wake wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK) ambao utasaidia kuondoa migogoro ya ardhi iliyopo, kuondokana na uwezekano wa kulipa fidia, kutenga eneo kwa ajili ya uwekezaji na kuongeza mapato ya Serikali;

v. Serikali kuwekeza kwenye Sekta ya Kilimo ili kuongeza tija sambamba na kutafuta masoko ya uhakika ya kimataifa;

vi. Serikali kufungua soko la mitaji ili kuwezesha upatikanaji wa mitaji na kwa gharama nafuu; na

vii. Serikali kuimarisha huduma kama vile Afya na Elimu ili kuwa na jamii bora na iliyo elimika na yenye afya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini vipaumbele hivi sita vikizingatiwa na kupewa kipaumbele katika mwaka 2027/28 vitajenga msingi mzuri wa kufikia malengo na shabaha zilizowekwa.

5.2. Malengo na Shabaha za Mpango wa Mwaka 2027/28

Mheshimiwa Spika, Malengo na shabaha za uchumi jumla ni kama inavyoonekana kwenye jedwali Na.1.

Jedwali Na. 4 Malengo na Shabaha za uchumi jumla za mwaka 2026/27

Na.	Viashiria	Malengo(2027)%
1.	Pato halisi la Taifa	6.6
2.	Mfumuko wa bei	3.0-5.0
3.	Mapato ya ndani kwa Pato la Taifa	17.1
4.	Mapato ya kodi kwa Pato la Taifa	13.8
5.	Nakisi ya Bajeti kwa Pato la Taifa	3.0
6.	Kiwango cha akiba ya fedha za kigeni	Miezi minne (4)
7.	Ajira	1,700,000

Chanzo: *Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2027/28*

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa malengo na shabaha za Mpango za mwaka 2027/28 na kubaini masuala yafuatayo:-

i. Moja ya kichocheo cha ukuaji wa uchumi wa Dunia katika mwaka 2027/28 kinatarajiwa kuwa ni matumizi ya akili unde (AI). Hata hivyo, Kamati imebaini nchi nyingi za Afrika, ikiwemo Tanzania bado zipo kwenye hatua za awali katika matumizi ya teknolojia hiyo. Hii ni kutokana na changamoto ya upatikanaji wa takwimu na Taarifa sahihi zinazowezesha akili unde kufanya kazi vizuri na kwa ufanisi. Hivyo, ni wazi kwamba bado Taifa linaweza lisinufaike kikamilifu na teknolojia hiyo;

ii. Usafiri katika kapu la bidhaa ina uzito wa **asilimia 14.1** kutokana na kuongezeka kwa bei ya mafuta katika Soko la Dunia liliathiri ongezeko la bei za usafiri na hivyo kuongeza mfumuko wa bei kufikia **asilimia 4.3** mwezi Septemba, 2026 kutoka **asilimia 3.4** katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Kwa kuwa vita ya Marekani na Israel dhidi ya Iran inaendelea inaweza kusababisha bei za mafuta kuendelea kupanda kwenye Soko la Dunia na hivyo inaweza kuwa ni vigumu kubaki ndani ya lengo lililowekwa la mfumuko wa bei kuwa katika wigo wa **asilimia 3** hadi **5.**

iii. Serikali imeweka lengo la uwiano wa mapato ya kodi kwa pato la taifa kufikia **asilimia 13.8** kiwango hiki ni chini ya makusanyo halisi yaliyofikiwa mwaka 2025/26. Hata hivyo, imebainika kwamba kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), katika kipindi cha 2019/20 hadi 2024/25, idadi ya mashauri ya kila mwaka katika migogoro ya kodi ambayo haijatatuliwa pamoja na thamani ya mapato yanayobishaniwa mbele ya Mahakama ya Rufaa ya Kodi ya Tanzania (Tax Revenue Appeals Tribunal -TRAT) na Bodi ya Rufaa ya Kodi (Tax Revenue Appeals Board - TRAB) iliongezeka kutoka mashauri 7 hadi 1,223 yenye thamani ya kodi ya **shilingi trilioni 10.75** kwa Tanzania Bara. Hivyo, endapo kasi ya kutatua mashauri ya kodi inaongezeka ni wazi kwamba tunaweza kufikia ukusanyaji wa mapato ya kodi wa **asilimia 15** ya Pato la Taifa ambao ni wastani wa nchi Kusini mwa Jangwa la Sahara;

iv. Serikali imeweka lengo la nakisi ya bajeti kwa Pato la Taifa kuwa chini ya **asilimia 3**, hata hivyo Kamati imebaini kwamba kasi ya ongezeko la matumizi ya Serikali ni kubwa kuliko kasi ya ongezeko la mapato. Mfano katika kipindi cha miaka 4 kuanzia mwaka 2020/21 hadi 2023/24 mapato yalikua kwa wastani wa **asilimia 8.9** wakati matumizi yaliongezeka kwa wastani wa **asilimia 10.2**, jambo linalopelekea kuongezeka kwa nakisi ya bajeti; na

v. Serikali imekusudia kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa ajili ya kugharamia uagizaji wa huduma na bidhaa kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 4, Kamati imebaini kwamba mapato yatokanayo na mauzo ya nje yalikuwa kwa **asilimia 12.2** ikilinganishwa na ukomo wa **asilimia 15**. Hivyo, mwenendo huo unaweza kusababisha Serikali kuanza kutumia akiba yake kuhudumia deni endapo ukomo wa **asilimia 15** utafikiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na afua za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 zilizoainishwa kwenye mapendekezo ya Mpango, Kamati ina ushauri ufuatao:-

i. Serikali kuwekeza na kuimarisha upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi na kwa wakati ili ziweze kutumika katika matumizi ya akili unde (AI). Vilevile, iwekeze kwenye vituo vya kutunza takwimu (data centre), ambavyo hivi sasa nchini vipo viwili tu. Aidha, Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuliko kuendelea kutegemea fedha za wafadhili katika kukusanya takwimu muhimu;

ii. Serikali kujenga na kuboresha mifumo ya kidijiti ya usimamizi wa mashauri ya kodi ili kuhakikisha yanatatuliwa kwa wakati. Hatua hii itawezesha Serikali kupata mapato yake stahiki. Aidha, Serikali iziwezeshe kibajeti TRAB na TRAT ili ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu;

iii. Serikali kupunguza matumizi yasiyo ya lazima hatua itakayosaidia kupunguza kasi ya ukuaji wa matumizi na hivyo kupunguza nakisi ya bajeti;

iv. Serikali kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija kwa kufanya tathmini ya misamaha ya kodi inayotolewa hivi sasa kwa makampuni na taasisi mbalimbali; na

v. Kuimarishwa mifumo ya kodi na taratibu za urasimishaji wa shughuli za sekta isiyo rasmi ili kupanua wigo wa ulipaji wa kodi.

5.3. Demografia na Maendeleo ya Watu

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa baadhi ya viashiria vya demografia na maendeleo ya watu kama ifuatavyo:-

5.3.1. Hali ya umaskini

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya binafsi Tanzania wa mwaka 2025 na kubaini masuala yafuatayo:-

i. Kiwango cha umaskini kimepungua kutoka **asilimia 34.4** mwaka 2007 hadi **asilimia 25.1** mwaka 2025 ambapo kwa kipindi cha miaka 18 Serikali imeweza kupunguza umasikini kwa **asilimia 9.3**;

ii. Kiwango cha umaskini ni kikubwa zaidi vijijini kuliko mijini ambapo **asilimia 30.7** ya watanzania waishio Bara wanaishi katika umaskini wa mahitaji ya msingi, ikilinganishwa na **asilimia 14.8** mijini;

iii. Utofauti wa umaskini (poverty gap) nchini ni **asilimia 6.2** na umasikini uliokithiri (poverty severity) ni **asilimia 2.2.**

Mheshimiwa Spika, baadhi ya sababu zinazochangia kasi ndogo ya kupunguza umaskini ni pamoja na:-

i. Hali ya utegemezi nchini ambapo uwiano ni **100:87** maana yake ni katika kila watu **100**, watu **87** ni tegemezi;

ii. Ongezeko kubwa la idadi ya watu lisiloendana na kasi ya ukuaji wa uchumi ambapo mwenendo wa ongezeko la watu ni **asilimia 2.8**, kiwango ambacho ni kikubwa kuliko kiwango kinachokubalika cha **asilimia 1.5** hadi **2.5;**

iii. Utofauti wa kipato na matumizi nchini umeongezeka kutoka kiwango cha **0.38** mwaka 2017/18 hadi kufikia kiwango cha **0.42** mwaka 2025, kiwango kinachokubalika ni chini ya **0.39**. Kiwango chochote kinachovuka **0.4** kinahesabika kwamba kuna utofauti mkubwa wa kipato.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kiwango cha umaskini kinapungua na kufikia lengo la chini ya **asilimia 15** ifikapo mwaka 2030/31, Kamati inashauri masuala yafuatayo:-

i. Kupunguza kasi ya ongezeko la watu kutoka **asilimia 2.8** hadi ongezeko la kati ya **asilimi 1.5** hadi **2.5**;

ii. Kuongeza tija ya sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuongeza uzalishaji;

iii. Kupunguza tofauti za maendeleo kati ya mijini na vijijini kwa kuongeza uwekezaji katika miundombinua ya barabara, umeme, maji, mawasiliano na masoko katika maeneo ya vijijini ili kuchochea shughuli za kiuchumi na kuongeza fursa za ajira; na

iv. Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini wa programu za kupunguza umaskini ili kubaini endapo zinaleta tija iliyokusudiwa.

5.3.2. Ajira

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa Taarifa ya Utafiti wa Watu wenye Uwezo wa Kufanya Kazi (Integrated Labour Force Survey– ILFS) wa mwaka 2025 na kubaini masuala yafuatayo:-

i. Kiwango cha ushiriki wa nguvu kazi (Labour Force Participation Rate) kimeongezeka kutoka **asilimia 73.2** mwaka 2024 hadi **asilimia 75.9** mwaka 2025. Hali hii inaashiria kuwa kiwango cha watu wenye umri wa kufanya kazi kinachojishughulisha kwenye shughuli za uzalishaji kimeongezeka;

ii. **Asilimia 51.5** ya nguvu kazi imeajiriwa kwa masharti ya muda na **asilimia 13.2** ya nguvu kazi ina ajira ya kulipwa mishahara;

iii. Sekta ya Kilimo imeendelea kuajiri takriban **asilimia 54.4** ya nguvu kazi mwaka 2025 ikifuatiwa na sekta ya huduma **asilimia 35.5** na kiwango cha nguvu kazi kilichoajiriwa katika sekta ya viwanda ni **asilimia 10.1** mwaka 2025;

iv. Kiwango cha ukosefu wa ajira kimepungua na kufikia **asilimia 5.9** mwaka 2025 ukilinganisha na **asilimia 6.2** mwaka 2024;

v. Kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana wenye miaka kati ya 15 hadi 35 kimepungua hadi **asilimia 7.5** mwaka 2025 kutoka **asilimia 8.1** mwaka 2024**;** na

vi. **Asilimia 10.1** ya nguvu kazi imeajiriwa kwenye sekta ya viwanda licha ya kuwa sekta hii inauwezo wa kuajiri watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuongeza fursa za ajira nchini, Kamati inaushauri ufuatao:-

i. Serikali kuendelea na mikakati ya kufanya mageuzi katika Sekta ya Kilimo kuhakikisha kinakuwa cha kisasa na chenye tija ili kuongeza uzalishaji utakaochochea maendeleo ya viwanda ambayo yatatoa fursa ya ajira; na

ii. Kuendelea kuwekeza kwenye elimu ya ujuzi na ufundi stadi. Hatua hii itawezesha wananchi kujiari na kuendana na mahitaji ya soko la ajira ndani na nje ya nchi; na

iii. Kuendelea kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika ujenzi na uendelezaji wa viwanda.

5.4. Ushiriki wa Sekta Binafsi

Mheshimiwa Spika, Sekta binafsi itaendelea kuwa chanzo muhimu cha ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2027/28. Aidha, Mpango unapendekeza kuongeza mchango wa uwekezaji wa sekta binafsi kwenye rasilimali za kudumu kufikia **asilimia 77** ambapo kwa sasa Sekta Binafsi inatarajiwa kuchangia **asilimia 70** tu. Katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP - IV) Sekta Binafsi inatarajiwa kuchangia **shilingi trilioni 62.3**. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini masuala yafuatayo:-

i. Tangu kutungwa kwa Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Sura ya 103 mwaka 2010 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2014, 2018 na 2023 bado Tanzania haijaweza kunufaika na utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia;

ii. Kutokuwepo na taarifa kamili ya kiasi kilichotumiwa na Sekta Binafsi katika kutekeleza Mpango;

iii. Maafisa Masuuli kutokutekeleza kifungu cha 4(6) cha sheria ya PPP kinachowataka kila mwanzo wa mzunguko wa bajeti wawasilishe andiko dhana na upembuzi wa awali wa miradi inayoweza kutekelezwa kwa njia ya ubia baina ya Sekta ya umma na Sekta Binafsi;

iv. Maafisa Masuuli kutotenga fedha za kutosha katika bajeti kwa ajili ya maandalizi ya miradi ya PPP;

v. Mfuko wa uwezeshaji wa miradi ya PPP (PPP facilitation fund) kutokuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia maandalizi ya miradi ya PPP;

vi. Uwepo wa dhana kwa watumishi wa umma kwamba Serikali ina fedha za kutosha kutekeleza miradi hata ile ambayo inaweza kutekelezwa na sekta binafsi. Hali inayosababisha Maafisa Masuuli kutoibua miradi ya PPP;

vii. Bado kuna dhana iliyojengeka miongoni mwa wadau kuwa miradi ya PPP inatakiwa kuibuliwa na kuandaliwa na kituo cha ubia (PPP centre); na

viii. Watumishi wa umma kuwa na fikra potofu dhidi ya kushirikisha sekta binafsi katika kutekeleza miradi ya umma yenye sura ya kibiashara;

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha miradi ya PPP inatekelezeka kikamilifu, Kamati ina ushauri ufuatao kwa Serikali:-

i. Maafisa Masuuli kutangaza fursa za miradi iliyopo katika maeneo yao ili kuvutia sekta binafsi kutekeleza miradi hiyo;

ii. Serikali kufanya maboresho ya Sheria ya PPP pamoja na Kanuni zake ili kurahisisha hatua uandaaji, uidhinishaji na utekelezaji wa miradi kwa njia ya PPP;

iii. Katika mwaka wa fedha 2027/28 miradi yote ambayo Serikali ina nia ya kuitekeleza kwa njia ya PPP itangazwe ili Sekta Binafsi ishindanie kuitekeleza;

iv. Kati ya mwezi Novemba na Januari Serikali ifanye mapitio ya utaratibu wa udhinishaji wa miradi ya Ubia na kubainisha mfumo wenye tija, ufanisi na unaolinda maslahi ya Serikali katika utekelezaji wa miradi. Aidha, mfumo huo uzingatiwe katika ngazi zote za Serikali kama vile Mamlaka ya Serikali za mitaa, Wizara, Taasisi za Umma na Mamlaka mbalimbali;

v. Kituo cha Ubia pamoja na Wizara ya Fedha kuandaa Mkataba Sanifu wa Mfumo wa Makubaliano (Framework agreement) ambao utatumika na Taasisi za Serikali zinapotaka kutekeleza miradi kwa njia ya Ubia;

vi. Kufanya maboresho ya kifungu cha 4(6) cha Sheria ya PPP ili kuweka adhabu kwa Afisa Masuuli ambae hatakitekeleza; na

vii. Kuweka masharti katika mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti na katika Sheria ya Tume ya Mipango ili kuweka sharti la lazima kwa miradi yote ya Serikali yenye sura ya Kibiashara kutoingizwa kwenye orodha ya miradi inayotegemea Bajeti ya Serikali na badala yake itekelezwe kwa mfumo wa PPP.

5.5. Ugharamiaji wa Mpango

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa vyanzo vya ugharamiaji wa Mpango na kubaini masuala yafuatayo:-

i. Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2027/28 unakadiriwa kugharimu kiasi cha **shilingi trilioni 89.3** kama ilivyoainishwa katika Mpango wa IV wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27-2030/31). Kati ya kiasi hicho, **shilingi trilioni 20.89** zinatarajiwa kutoka kwenye bajeti ya Serikali, sawa na **asilimia 30.2** ya bajeti ya Serikali;

ii. Serikali imepanga kutumia vyanzo bunifu na mbadala vya mapato kama vile hatifungani za kijani, hatifungani za Watanzania waishio ughaibuni, vyanzo mseto vya fedha, biashara ya kaboni na masoko ya mitaji; na

iii. **Shilingi trilioni 6.3** ni uwekezaji unaotarajiwa kutoka katika mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara ambapo Mashirika hayo yanatarajiwa kuchangia **asilimia 10** katika mapato ya Serikali ifikapo mwaka 2028. Jedwali Na. 1 linaonyesha Rasilimali za Mashirika ya Umma na Ongezeko la Thamani;

Jedwali: Na. 5 Rasilimali za Mashirika ya Umma na Ongezeko la Thamani

Mwaka	Rasilimali za mashirika ya umma (Shilingi milioni)	Ongezeko la thamani (Shilingi milioni)	Ongezeko (%)
2019	1,032,648	-	-
2020	1,216,944	184,296	17.85
2021	1,358,470	141,526	11.63
2022	1,674,126	315,656	23.25
2023	1,780,949	106,823	6.38
2024	1,887,044	106,095	5.96
2025	1,963,597	76,553	4.06
Jumla ya ongezeko	-	**930,949**	**90.14**

Chanzo: *Taarifa ya Hali ya Uchumi mwaka 2025*

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo Kamati ina ushauri ufuatao kwa Serikali:

i. Ili Sekta binafsi iweze kuchangia rasilimali fedha kwenye utekelezaji wa Mpango ni vema Serikali ikaweka kipaumbele katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara sambamba na kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI) kwa ukamilifu wake;

ii. Serikali kutekeleza sera ya kubana matumizi (austerity measures) ili kupata ahueni kwenye bajeti na kugharamia shughuli zake;

iii. Kuongeza ufanisi kwenye mashirika ya umma ili yaweze kuchangia kwenye utekelezaji wa mpango;

iv. Ofisi ya Msajili wa Hazina kufanya uchambuzi na marejeo ya muundo na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya mashirika ya umma ili yaweze kuchangia kiasi kinachotarajiwa kutoka kwao; na

v. Serikali kuruhusu mashirika yanayojiendesha kibiashara kwenda kwenye soko la hisa ili kupata mitaji kuliko kutegemea ruzuku ya Serikali.

5.5.1. Biashara ya Kaboni

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa biashara ya Kaboni nchini na kubaini masuala yafuatayo:-

i. mapato yatokanayo na mauzo ya viwango vya kaboni yamefikia **Dola za Marekani milioni 2**;

ii. Serikali imeendelea kuimarisha mfumo wa usimamizi wa biashara ya kaboni kupitia kituo cha Taifa cha kuratibu kaboni (National Carbon Monitoring Centre - NCMC), taasisi iliyoundwa kusimamia usajili, ufuatiliaji na uthibitishaji wa miradi ya kaboni nchini;

iii. Hadi Julai 2026, kituo cha Kaboni kilikuwa kimesajili miradi 117 ya kaboni, huku Serikali ikiidhinisha miradi mipya yenye thamani ya zaidi ya **Dola za Marekani milioni 52.1** inayotarajiwa kuzalisha tani **milioni 4.2** za kaboni kwa ajili ya biashara katika soko la kimataifa;

iv. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka wa fedha 2024/25 ilibaini kutotumika kikamilifu kwa fursa za mapato ya biashara ya Kaboni. Ambapo ilibaini **asilimia 70** ya miradi iliyosajiliwa haijaanza kutekelezwa na baadhi ilikuwa imekwama kwa zaidi ya miaka miwili. Aidha, TFS haikuwa imeripoti mapato ya kaboni licha ya kusimamia zaidi ya hekta **milioni 14.5** za misitu. Vilevile, Mikataba yenye muda wa hadi miaka 40

haijaweka tarehe mahsusi za kuanza utekelezaji, malengo yanayopimika na ratiba wazi za malipo; na

v. Mfumo wa kitaifa wa uhakiki haujafanya kazi kikamilifu, hivyo Serikali kutegemea taarifa za waendelezaji bila uwezo wa kujiridhisha kwa uhuru kuhusu idadi ya hati za kaboni zilizouzwa na bei zake.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi huo, Kamati inaishauri Serikali kwamba kutokana na mapato yanayotokana na biashara ya kaboni ya **Dola za Marekani milioni 2** ni kidogo ukilinganishwa na fursa zilizopo kwenye sekta za misitu, kilimo, nishati safi, uhifadhi wa mazingira na matumizi ya teknolojia za kupunguza utoaji wa hewa ukaa. Hivyo, kuna haja ya kuongeza kasi ya kutumia chanzo hiki ili kuongeza mapato ya Serikali na kugharamia utekelezaji wa mpango.

SEHEMU YA SITA

6.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI

6.1. Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/26

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/26 Serikali ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya **shilingi trilioni 56.49**. Kati ya fedha hizo **shilingi trilioni 39** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na **shilingi trilioni 17.49** zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika utekelezaji wa bajeti wa mwaka 2025/26, makusanyo halisi kutoka vyanzo vya ndani na nje yalifikia jumla ya **shilingi trilioni 55.5** sawa na **asilimia 98.3** ya bajeti ya **shilingi trilioni 56.49**. Kwa upande mwingine, matumizi ikijumuisha malipo ya mtaji wa deni la Serikali yalikuwa jumla ya **shilingi trilioni 55.6**, sawa na **asilimia 98.3** ya bajeti.

6.1.1. Ukusanyaji wa Mapato

6.1.1.1. Mapato ya Kodi

Mheshimiwa Spika, Mapato halisi ya kodi yalikuwa **shilingi trilioni 34.8** sawa na **asilimia 107.7** ya lengo la kipindi hicho la **asilimia 14.3** ya Pato la Taifa. Aidha, mapato hayo ni sawa na ukuaji wa **asilimia 20.6** ikilinganishwa na mapato ya **shilingi trilioni 28.9** mwaka 2024/25. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarishwa kwa ufuatiliaji, usimamizi wa kodi pamoja na ulipaji kodi kwa hiari. Kamati inampongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuhamasisha walipa kodi kulipa kodi kwa hiari.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo Kamati imebaini masuala yafuatayo:-

i. Moja ya sababu ya mafanikio ya ukusanyaji wa mapato ni matumizi ya mfumo wa IDRAS (Integrated Domestic Revenue Administration System), hata hivyo awamu ya pili ya ujenzi wa mfumo huo haijakamilika na hivyo kupunguza ufanisi wake;

ii. Kiwango cha mapato ya kodi kilichokusanywa kinajumuisha makusanyo ya malimbikizo ya kodi ya miaka iliyopita hivyo ni vigumu kupima ufanisi wa makusanyo ya kodi katika mwaka husika;

iii. Bado kuna changamoto ya baadhi ya wafanyabiashara kutotumia mashine za EFD katika mauzo na hivyo kuikosesha Serikali kodi stahiki;

iv. Baadhi ya maboresho ya kodi mbalimbali yanayofanyika kupitia Sheria ya Fedha, kutoanza utekelezaji wake mwaka wa fedha mpya unapoanza kutokana na maandalizi hafifu ya ukusanyaji wake. Mfano katika mwaka wa fedha 2026/27 Serikali ilifanya mabadiliko kwenye Sheria ya Malipo ya Taifa sura ili kusitisha malipo kwa kutumia fedha taslimu kwenye maduka makubwa lakini hadi hivi sasa utekelezaji wake haujaanza; na

v. Kushamiri kwa biashara za magendo mipakani.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato sambamba na kuondokana na changamoto hizo, Kamati ina ushauri ufuatao:-

i. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhakikisha kwamba mapato ya tozo ya huduma ya ushuru wa Forodha (Customs Processing Fee-CPT) yanatumika kikamilifu kukamilisha mfumo wa IDRAS na Mifumo mingine;

ii. Serikali kuhakikisha kwamba kila kunapokuwa na mabadiliko ya Sheria inayolenga ama kupanua wigo wa mapato au kudhibiti upotevu wa mapato maandalizi ya utekelezaji wake yanakamilika sambamba na kupitishwa kwakwe na Bunge;

iii. Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato kuweka utaratibu utakaotofautisha mapato yanayotokana na malimbikizo ya madeni na kutotambua marejesho ya kodi kama mapato ya Serikali; na

iv. Kuimarisha Timu ya Watalaamu ya kuzuia magendo kwa kuhusisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama kwa sababu suala la magendo sio tu ni tishio katika uchumi bali katika usalama wa raia kwa bidhaa zinazoingia nchini bila kufuata utaratibu.

6.1.1.2. Mapato yasiyo ya Kodi

Mheshimiwa Spika, mapato yasiyo ya kodi yanayojumuisha mapato yaliyokusanywa na Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Taasisi za Serikali, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalifikia jumla **shilingi trilioni 5.8** sawa na **asilimia 71.3** ya lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi trilliioni 8.1**.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini sababu zilizosababisha kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato kama ifuatavyo:-

i. Baadhi ya mashirika, Taasisi na Mamlaka za umma zinazotakiwa kutoa mchango wa **asilimia 15** au zaidi wa mapato ghafi kutokufanya hivyo kwa wakati;

ii. Baadhi Wizara, Idara na Mamlaka za Serikali za mitaa kuendelea kukusanya mapato ya Serikali nje ya mfumo wa GePG na GoTHOMIS; na

iii. Uwekaji wa makadirio makubwa kuliko uwezo wa ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto hizo Kamati inashauri masuala yafuatayo:-

i. Kuhakikisha Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Taasisi za Serikali zote zimeunganishwa na kutumia mifumo ya ukusanyaji wa mapato;
ii. Taasisi na Mashirika ya Umma kuwasilisha gawio na michango ya Serikali kama inavyotakiwa kisheria sanjari na kuwachukulia hatua wanaochelewesha kuwasilisha michango bila sababu za msingi; na

iii. Makadirio ya makusanyo ya mapato katika mwaka wa fedha 2027/28 yazingatie hali halisi ya uchumi wa eneo husika na uwezo wa ukusanyaji wa mapato.

6.2. Deni la Serikali

Viashiria vya Uhimilivu	Ukomo	2025/26	2026/27	2027/28	2028/29	2029/30	2030/31
Deni la Nje							
(PV)/pato la taifa	**40**	24.4	23.6	22.4	21.1	20	19.5
Deni (PV)/uuzaji wa bidhaa nje	**180**	123.1	123.8	119.3	114.3	110.4	108.2
Ulipaji wa deni la nje/Uuzaji wa bidhaa nje	**15**	12.8	12.2	13.7	13.3	13.1	12

Ulipaji wa deni/ Mapato ya ndani	**18**	15.4	13.8	15.1	14.3	13.9	12.9
Deni la Serikali (Ndani na Nje)							
Deni (PV)/ Pato la Taifa	**55**	39.6	38.6	36.9	35.9	34.8	34.6
Deni (PV)/ Mapato ya ndani	**N/A**	233.4	225.6	214.8	208.2	202.8	205.6
Ulipaji wa deni/ Mapato ya ndani	**N/A**	45.2	32.9	34.1	30.8	31.4	32.9

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa ya tathmini ya uhimilivu wa deni, moja ya kiashiria kinachoangaliwa ni uwiano wa ulipaji wa deni kwa mapato ya ndani. Hivi sasa uwiano wa ulipaji wa deni kwa mapato ya ndani umefikia **asilimia 14.5** dhidi ya ukomo wa **asilimia 18**, inatarajiwa kwamba ifikapo 2027 uwiano huo utakuwa **asilimia 17.2** dhidi ya ukomo wa **asilimia 18.** Pamoja na kwamba hatujafika ukomo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaweka vigezo vya ndani vya upimaji wa uhimilivu wa Deni kwa sababu mfumo wa kutathmini Deni unaotumika umeandaliwa na Benki ya Dunia (World Bank-WB) na Shirika la Fedha la Kimataifa (International Monetary Fund- IMF) ambao kimsingi unayahakikishia mashirika hayo kwamba deni la nje (External Debt) linalipwa bila kuangalia shinikizo kwenye mapato na matumizi ya Serikali.

Jedwali Na. 6: Mwenendo wa Tathmini ya Uhimilivu wa Deni

6.2.1.Mwenendo wa Matumizi

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa matumizi unaonyesha kuwa katika mwaka wa fedha 2025/26 Serikali ilitoa idhini ya matumizi ya **shilingi trilioni 55.6** ikiwa ni zaidi kwa **shilingi bilioni 33** ya mapato yote yaliyokusanywa ya **shilingi trilioni 55.5** iliyogharimiwa na mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu**.** Pamoja na ufanisi huu, Kamati imebaini kuwa matumizi hayaendani na utolewaji wa fedha kwenye mafungu kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini masuala yafuatayo:-

i. Pamoja na kwamba ukusanyaji wa mapato ya Serikali umefikia **asilimia 98.4** ya lengo, utolewaji wa fedha kwa mafungu mbalimbali si sawa na makusanyo ya mapato;

ii. Miradi ya maendeleo ya mwaka 2025/26 haikutekelezwa kwa kiasi kinacholingana na makusanyo ya mapato; na

iii. Bado kuna malimbikizo ya madeni ya wakandarasi, wazabuni, Watoa huduma na Watumishi.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizo zinaweza kuashiria masuala makuu mawili, Mosi ni kutokuwepo kwa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na Pili ni uwepo wa madeni ya watumishi, wazabauni, wakandarasi na watoa huduma yanayohama kutoka mwaka mmoja wa fedha na kwenda mwaka unafuata na hivyo kuathiri utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka husika. Hivyo, suluhisho la muda mfupi linaloweza kuondoa changamoto hii ni kuchukua hatua za kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kuleta ahueni kwenye mfuko mkuu wa Hazina na kuwezesha Bajeti za miaka inayofuata kutekelezwa kama ilivyopangwa.

SEHEMU YA SABA

7.0. UCHAMBUZI WA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KATIKA MUDA WA KATI (2026/27 – 2028/29)

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa mwezi Februari, 2026 Bunge lako tukufu liliidhinisha Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa kipindi cha muda wa kati (2026/27 – 2028/29). Hivyo, naomba kulitaarifu Bunge lako kwamba Mwongozo huo ndio utakaotumika katika maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2027/28.

Mheshimiwa Spika, katika mapitio ya Mwongozo huo utakaotumika katika kipindi cha kati, Kamati imechambua na kubaini kwamba unahitaji kufanyiwa marejeo kwa sababu zifuatazo:-

i. Ilitarajiwa katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mwongozo huo, Bajeti yote ya Serikali ingekuwa jumla ya **shilingi trilioni 61.934**. Hata hivyo, Bajeti iliyopitishwa na Bunge ilikuwa **shilingi trilioni 62.333** sawa na tofauti ya **shilingi bilioni 400**; na

ii. Kama hakutakuwa na hatua zozote za kupunguza matumizi ya Serikali katika mwaka 2027/28, makisio ya kutumia **shilingi trilioni 69.16** itakuwa vigumu kufikiwa kwa kuangalia makusanyo halisi yaliyokusanywa mwaka 2025/26 ya **shilingi bilioni 55.6.**

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hizo, Kamati imeona ni vyema kuwasilisha mapendekezo yake kwa Serikali ili wakati wa kufanya marejeo ya Mwongozo huo yazingatiwe kwa ukamilifu.

7.1. Misingi ya Uchambuzi wa Mwongozo

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati inafanya uchambuzi wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali ya kipindi cha muda wa kati ilijikita katika kubainisha maeneo yaliyotolewa maelekezo kwa Maafisa Masuuli na changamoto zilizopo katika uchumi na utatuzi wake. Maeneo yatakayotolewa mapendekezo ni:-

(i) Utekelezaji wa Hatua mbalimbali zilizobainishwa katika Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali ya kipindi cha muda wa kati;

(ii) Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Bajeti;

(iii) Kubana matumizi ya Serikali kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na yale ambayo yanaweza kuahirishwa kwa mwaka mmoja;

(iv) Ulipaji wa malimbikizo ya madai ya wazabuni, wakandarasi, watumishi na watoa huduma;

(v) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

(vi) Kudhibiti uhamisho wa Fedha ndani ya Fungu na kati ya Mafungu;

(vii) Utumiaji wa mifumo ya kukusanya mapato ya Serikali; na

(viii) Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

7.1.1. Utekelezaji wa Maelekezo mbalimbali yaliyobainishwa katika Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Maandaalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali pamoja na masuala mengine unatoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli wote kuhusu masuala ya kuzingatia wakati wa maandalizi na utekelezaji wa mpango na bajeti katika muda wa kati. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa pamoja na kwamba mwongozo unaojadiliwa ni wa miaka mitatu, uchambuzi uliofanyika uliangalia utaratibu uliokuwepo awali na utaratibu uliopo hivi sasa na utekelezaji wake kwa mwaka wa fedha unaoendelea ambapo ilibainika kuwa baadhi ya maelekezo ya Mwongozo yamekuwa hayafuatwi na Maafisa Masuuli. Maelekezo hayo ni:-

i. **Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuongeza mapato kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya kimkakati na kielelezo**

Mheshimiwa Spika, Taasisi na Mashirika ya Umma takribani 308 yamekuwa yanapokea ruzuku kutoka Serikalini licha ya kuwa baadhi ya Taasisi hizo zinauwezo wa kuzalisha mapato yake yenyewe, Taasisi kama TFS inasimamia zaidi ya Hekta **milioni 14.5** za misitu ambazo zingetumika katika Biashara ya Kaboni. Hadi hivi sasa hakuna mapato yoyote inayopata na badala yake inategemea Bajeti ya Serikali. Hii ilitokana na ukosefu wa mwongozo na uhamasishaji kuhusu namna bora ya kutumia fursa zilizopo katika biashara ya kaboni, jambo lililopelekea mapato yaliyokusanywa kuwa ni **shilingi bilioni 36** sawa na **asilimia 3** ya mapato yaliyotarajiwa ya **shilingi trilioni 1.26** katika kipindi cha Januari 2023 hadi Julai 2024.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulibaini kwamba katika kipindi cha Januari 2023 hadi Julai 2024, ni miradi **minne (4)** tu kati ya miradi **56** ya biashara ya kaboni iliyokuwa imesajiliwa nchini Tanzania iliyokuwa imefikia hatua ya utekelezaji, huku miradi **52** iliyobaki ikiwa bado katika hatua za maandalizi. Hivyo, Kamati inashauri kuwa Taasisi zote za Umma ambazo ama zina vyanzo na hazikusanyi au hazikusanyi mapato vizuri zipewe kipindi cha mpito cha mwaka mmoja kisha ziachwe zijiendeshe kwa mapato yake yenyewe.

ii. **Utekelezaji wa maelekezo kuhusu kuongeza matumizi ya magari yanayotumia nishati ya gesi na umeme, yakiwemo ya Serikali ili kupunguza matumizi ya mafuta na uchafuzi wa mazingira**

Mheshimiwa Spika, kimsingi agizo hili halitekelezwi kwa sababu kila mwaka Serikali huongeza Bajeti ya matumizi ya Mafuta kwenye Mafungu mbalimbali. Hivyo, Kamati ilikuwa na mapendekezo kuwa katika mwaka wa Fedha 2027/28 bajeti za mafuta katika mafungu yote zibaki kama zilivyo mwaka huu wa fedha kwa sababu bei imeongezeka, ni wazi yatanunuliwa mafuta kiasi kidogo na hivyo kuzifanya Taasisi za Umma kuhamasika kwenda kwenye nishati safi au kuweka kipindi cha mpito kwa Taasisi za Umma kuhamia kwenye teknolojia mbadala na zinazotumika nchini. Aidha, muongozo ubainishe mwelekeo wa Serikali wa kununua magari mapya yanayotumia nishati jadidifu na kupunguza magari yanayotumia mafuta ya petroli na dizeli;

iii. **Maelekezo kuhusu kuimarisha usimamizi kwa mashirika ya umma kufanya biashara ili kuongeza uchangiaji wa mapato kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kupunguza utegemezi kwa Serikali.**

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba Mashirika mengi ya Umma bado yanaendeshwa kwa hasara ikilinganishwa na makampuni binafsi yaliyo katika sekta hiyo ambayo yanafanya vizuri na mengine yanatengeneza faida au kupunguza kiwango cha hasara. Mfano Vodacom wanasambaza Mkongo kwenye nyumba za Watu binafsi kwa kasi kuliko mmiliki wa Mkongo ambaye ni Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina kufanya uchambuzi katika mwaka wa Fedha 2027/28 na kubaini mashirika ambayo yanatakiwa kuondoshwa kwenye utaratibu wa ruzuku ya Serikali hasa ya gharama za uendeshaji na Serikali ibakie na jukumu la kuyasaidia kwenye uwekezaji. Hatua hii iende sambamba na kubadili Sheria ya Msajili wa Hazina ili kuondoa vikwazo vya kiutendaji na kisheria vinavyofanya mashirika na kampuni za umma zisijiendeshe kwa faida na kwa ufanisi.

iv. **Changamoto ya Matumizi ya Mifumo ya Kieletroniki.**

Mheshimiwa Spika, Kamati kupitia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pia imebaini kuwa kuna baadhi ya Taasisi za Serikali hazizingatii maelekezo ya Serikali kuhusu Matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki. Aidha, ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulibaini jumla ya Taasisi **80** zilitumia mifumo mingine badala ya MUSE bila kibali, taasisi **59** zilifanya manunuzi ya **shilingi bilioni 9.90** nje ya NeST na Halmashauri **23** zilikusanya mapato ya afya ya **shilingi bilioni 6.65** nje ya GoTHOMIS. Hivyo, Kamati inapendekeza Serikali katika mwaka wa Fedha 2027/28 Afisa Masuuli yeyote atakae tumia mfumo ambao hauna kibali achukuliwe hatua za kinidhamu. Aidha, ifikapo mwaka 2028/29 wakati mwongozo huu unatamatika utekelezaji wake Taasisi zote za Umma zinazotakiwa kutumia mifumo shirikishi ziwe zimeunganishwa na zinaitumia mifumo ili kudhibiti ukusanyaji wa mapato na matumizi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mapungufu yaliyobainika, Kamati inapendekeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuhakikisha Mwongozo unapotolewa uwe na nguvu ya kisheria na hatua za kuchukua dhidi ya Maafisa Masuuli ambao ama hawafuati maelekezo ya mwongozo.

7.1.2. Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Bajeti;

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa changamoto zilizoainishwa katika mwongozo na kubaini kwamba

changamoto hizi zimekuwa zikijirudia kila mwaka na hakuna hatua za utatuzi zinazopendekezwa haziondoi changamoto hizo. Changamoto hizo ni:-

i. Ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika kutekeleza miradi ya maendeleo; na

ii. Mwitikio mdogo wa matumizi ya teknolojia kwenye kufanya malipo bila kutumia fedha taslimu.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba changamoto hizi zinaendelea kuwepo kwa sababu hakuna hatua zinazochukuliwa. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2027/28 Kamati inapendekeza kuwa Serikali itoe Tamko la Kisera ili kuzuia matumizi ya fedha taslimu.

Kubana matumizi ya Serikali

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba karibia kila mwaka kumekuwa na maelekezo kwa Maafisa Masuuli kupunguza matumizi, hata hivyo, uchambuzi wa Bajeti za mafungu hauoneshi utekelezaji wa maelekezo hayo. Hivyo, katika mwaka wa Fedha 2027/28, Kamati inapendekeza Serikali kutekeleza masuala yafuatayo:-

i. Taasisi zote za Serikali ambazo zilitakiwa kuhamia Dodoma hazijahamia na ofisi zote za Umma zenye ofisi mbili Dar es Salaam na Dodoma kuhamia Dodoma ili kupunguza matumizi ya uendeshaji wa Ofisi;

ii. Kusitisha ununuzi wa magari kwa mafungu yote isipokuwa yale tu yenye ulazima kwa mwaka mmoja;

iii. Kutekeleza kwa vitendo agizo la Serikali la kupunguza misafara ya viongozi na watumishi wa umma wanaposhiriki vikao na ziara mbalimbali;

iv. Kupunguza gharama za ununuzi wa shajala (Stationaries) kwa **asilimia 10** kwa mafungu yote na kuhimiza matumizi ya teknolojia;

v. Kufuta ama kusitisha matumizi yote ya warsha na semina na sherehe ambazo hazina tija kwa mwaka 2027/28;

vi. Kusimamisha michezo ya Taasisi za Umma walau kwa mwaka mmoja 2027/28;

vii. Serikali kufanya uchambuzi wa kina wa gharama na uwezo wa kugharamia mikutano ya Kimataifa inayopendekezwa kufanyika nchini kabla ya kukubali mikutano hiyo ifanyike nchini; na

viii. Serikali kufanya mabadiliko kwenye kifungu cha 80 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 ili kuwezesha Serikali kununua magari yaliyotumika si chini ya miaka 3. Aidha, Serikali ifanye mapitio ya Mwongozo wa ununuzi wa magari kwa viongozi mbalimbali wa Serikali ili kuhakikisha kwamba yanaendana na uwezo wa kifedha na wakati wa sasa.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo hayo ya Kamati yamezingatia kwamba matumizi ya Serikali katika kipindi cha muda wa kati, matumizi (bila kujumuisha malipo ya mtaji wa deni la Serikali) yalikadiriwa kuwa wastani wa **shilingi bilioni 59,250.1**.

7.1.2.1. Ulipaji wa malimbikizo ya madeni ya wazabuni, wakandarasi, watumishi na watoa huduma

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba Mwezi Juni, 2022 wakati Serikali inaandaa Mkakati wa kudhibiti ongezeko la Madeni ilikuwa ikidaiwa na Wazabuni, Wakandarasi na Watoa huduma jumla ya **Shilingi trilioni 3.228**. Hata hivyo, Taarifa ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali imeonesha hadi mwezi Juni, 2025 Serikali ilikuwa inadaiwa kiasi cha **shilingi trilioni 6.580** sawa na ongezeko la **asilimia 103** katika kipindi cha miaka minne.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha malimbikizo ya madeni ni **asilimia 9.8** zaidi ya kiwango kinachokubalika kimataifa cha uwiano wa malimbikizo ya deni kwa Bajeti cha **asilimia 2**. Endapo madeni haya yataendelea yataleta changamoto kwenye

utekelezaji wa Bajeti miaka ijayo. Hivyo basi, Kamati inapendekeza masuala yafuatayo:-

i. Kuwachukulia hatua Maafisa Masuuli wote ambao hawatekelezi waraka Na. 1 wa Hazina wa mwaka 2018 sambamba na kuuboresha waraka huo na kuutoa tena mwaka 2027;

ii. Kutotekeleza miradi mipya kabla ya kukamilisha miradi ya awali isipokuwa tu kwa miradi mipya inapoibuliwa katika maeneo yenye uhitaji maalumu;

iii. Serikali kuongeza kiwango kinacholipwa cha malimbilizo ya madeni kutoka **shilingi bilioni 100** za sasa hadi **shilingi bilioni 300** kwa mwezi;

iv. Kuangalia uwezekano wa kuanza majadiliano na wadeni ili wale ambao watakubali kuondosha faida zao walipwe mtaji tu; na

v. Kuboresha utaratibu wa uhakiki wa madeni ili yalipwe kwa wakati.

7.1.2.2. Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa Mapendekezo ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo yana lengo la kuimarisha ukusanyaji wa mapato na imebaini masuala yafuatayo:-

i. Kodi ya mapato ya ajira (PAYE) ya **shilingi bilioni 4.91** iliyokatwa kwa wafanyakazi katika mikoa miwili haikuwasilishwa TRA;

ii. Taasisi **17** hazikuwa zimekusanya madai ya mapato yasiyo ya kodi ya **shilingi bilioni 147.99** na **dola za Marekani milioni 24.3** hadi tarehe 30 Juni 2025;

iii. Ukusanyaji wa Mapato Nje ya Mfumo wa GePG yenye jumla ya **shilingi milioni 694.99**. Ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulibaini kuwa Kitengo cha Afya cha Polisi, Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi na TRITA Moshi zilikusanya jumla ya **shilingi milioni 694.99** nje ya mfumo wa GePG.

iv. Udhaifu Katika Usimamizi na Utekelezaji wa Bajeti. Kutokuzingatiwa kwa bajeti zilizoidhinishwa na maelekezo ya matumizi ya fedha kumejitokeza katika taasisi za Serikali na Halmashauri kama ifuatavyo:

a) Klabu za Pamba Jiji, Geita Gold na Dodoma Jiji zilipewa **shilingi bilioni 2.13** bila kutengewa bajeti au zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa;

b) Taasisi **36** zilitumia **shilingi bilioni 9.48** kwa shughuli zisizokuwa kwenye bajeti au zilihamisha fedha kati ya shughuli bila idhini; na

c) Halmashauri **102** hazikutenga **shilingi bilioni 36.92** kwa ajili ya maendeleo na sekta mahususi kama ilivyoelekezwa katika mwongozo wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mapungufu yaliyobainika, Kamati inapendekeza kuwa katika upangaji wa Bajeti ya Mwaka 2027/28 Serikali itoe maelekezo kwa Maafisa Masuuli kwamba hoja zote zinazohusu fedha kurejeshwa, ukusanyaji wa mapato na ubadhilifu zitakuwa ni msingi wa upangaji wa Bajeti.

7.1.2.3. Kudhibiti uhamisho wa Fedha ndani ya Fungu na kati ya Mafungu

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kifungu cha 14(3) pamoja na kifungu cha 41 cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 na kubaini kuwa pamoja na kwamba Sheria imeweka utaratibu mzuri wa uhamisho wa fedha, utaratibu huu umekuwa ukitumika vibaya kwa maeneo yafuatayo:-

i. Maafisa Masuuli kutopanga Bajeti kwa kazi za msingi ambazo wanatambua ni za lazima na baadae kuomba uhamisho wa kati ya mafungu. Mfano uhamisho kati ya mafungu kwa mwaka 2025/26 kwa Wizara **8** tu ilikuwa jumla ya **shilingi bilioni 255.508**;

ii. Fedha za mradi mmoja kuhamishwa kwenda kwenye mradi mwingine au kutumika kwa matumizi yasiyokusudiwa. Mfano Fedha za miradi yenye thamani ya **shilingi bilioni 6.94** zilitumika kinyume na madhumuni mwaka 2024/25; na

iii. Fedha kuhamishwa kutoka mradi mmoja kwa sababu zimepokelewa na hatua ya ulipaji haijafikiwa na kuhamishwa kwenda kwenye mradi mwingine ambao unahitaji fedha na matokeo yake ni kuzalisha madeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza Serikali kufanya mapitio ya viwango vinavyoruhusiwa kufanya uhamisho pamoja na kuangalia maeneo ambayo kila mwaka fedha huelekezwa. Aidha, kabla ya uhamisho kufanyika tathmini ya kina ifanyike kuhakikisha kama shughuli inayohamishiwa fedha, ama sio shughuli ambayo ilipaswa iwe imetengewa fedha lakini haikutengewa au ni shughuli ambayo imetokana na dharula isiyokwepeka na ambayo haikutarajiwa.

SEHEMU YA NANE

8.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA UJUMLA

8.1. Matumizi ya kadi za simu za kiganjani

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2025, kadi za simu za kiganjani zilifikia **106,823,601** kutoka kadi **86,769,161** mwaka 2024, sawa na ongezeko la **asilimia 23.1**. Hii ilitokana na kuongezeka kwa maeneo yaliyofikiwa na miundombinu ya mawasiliano pamoja na matumizi ya simu za kiganjani katika utoaji wa huduma mbalimbali. Aidha, kadi za simu za mezani ziliongezeka kwa **asilimia 42.5** na kufikia **111,600** mwaka 2025 kutoka kadi za simu za mezani **78,299** mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, licha ya mafanikio hayo, bado Kumekuwa na changamoto mbalimbali zinazotokana na matumizi ya kadi za simu kama ifuatavyo:

i. Kitambulisho cha mtu mmoja kutumika kusajili laini zinazotumiwa na watu wengine. Takwimu zinaonesha hadi kufikia Juni 2026 jumla ya watu **27,374,283** walikuwa wamesajiliwa na NIDA, hata hivyo simu za kiganjani zilizosajiliwa kipindi kama hicho ni **106,823,601.** Takwimu hizi zinaonesha kuwa kuna watu wamesajili laini kwa kutumia vitambulisho vya watu wengine;

ii. Kuongezeka kwa uhalifu wa kimtandao; na

iii. Mamlaka husika kuchelewa kuchukua hatua kwa namba ambazo zinatumika na wahalifu wa kimtandao ikiwa pamoja na kuzifungia.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na changamoto hizi, Kamati ina ushauri ufuatao kwa Serikali:

i. Mamlaka ya mawasiliano Tanzania kwa kushirikiana na makampuni ya simu kufanya tena uhakiki wa wamiliki wa kadi za simu na majina yaliyosajiliwa;

ii. Kuweka sharti la kusajili kadi katika duka la mtandao husika; na

iii. Kuboresha mifumo ya utambuzi wa matumizi ya kadi yasiyo ya kawaida na kuweka utaratibu rahisi wa kuripoti na kufungia kadi za simu zinazojihusisha na uhalifu wa kimtandao.

8.2. Kuweka utaratibu wa kisheria na kiutawala wa kudhibiti ufutwaji, uhamishaji au matumizi ya fedha za mikopo ya miradi kwa madhumuni tofauti na yale yaliyokubaliwa.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulibaini kutokuwepo kwa sera na miongozo kuhusu ufutwaji na ubadilishaji wa matumizi ya fedha za

mikopo za miradi. Aidha, changamoto hii pia inapelekea kutokutekelezwa kwa miradi iliyokusudiwa na hivyo kupunguza imani kwa wakopeshaji. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuandaa na kuidhinisha sera na miongozo mahsusi ya kusimamia ufutwaji, usitishaji na ubadilishaji wa matumizi ya fedha za mikopo ya miradi. Hii iende sambamba na kubainisha mazingira yanayoruhusu mabadiliko hayo, mamlaka ya uamuzi, taratibu za kupata idhini zinazohitajika na wajibu wa kuzingatia masharti ya mikataba ya mikopo. Vilevile, Serikali iweke utaratibu wa kutoa taarifa kwa Bunge kuhusu mabadiliko yoyote makubwa ya matumizi ya fedha hizo na hatua zilizochukuliwa kulinda maslahi ya Serikali na wananchi.

8.3. Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi

Mheshimiwa Spika, moja ya kihatarishi ambacho kimebainishwa katika Mpango wa mwaka 2027/28 ni Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabia nchi. Hata hivyo pamoja na kwamba baadhi ya madhara ya mabadiliko ya tabia nchi yameanza kuonekana bado Serikali haijatia mkazo katika kudhibi uharibifu wa mazingira. Mfano Baraza la Taifa la Mazingira na Wizara ya Afya walifanya Utafiti katika Mikoa ya Kanda ya ziwa na kukuta watu walio katika maeneo ya migodi wana kiwango kikubwa cha kemikali katika haja ndogo kuliko kinachokubalika na hivyo kusababisha miaka ya mbeleni kuwa na wagonjwa wengi wa figo. Aidha, Duniani suala la uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa ni moja ya janga linaloongeza umasikini kwa takribani watu milioni 26 kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba Baraza la Taifa la Mazingira halina uwezo wa kifedha wa kusimamia mazingira nchi nzima. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Baraza hilo linawezeshwa kifedha ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, inashauriwa kufuta kitengo cha mazingira kilichopo Wizara ya Madini na majukumu hayo yahamishiwe Baraza la Mazingira kwa sababu kimsingi hakitekelezi majukumu yake kikamilifu na kwa kujali mazingira.

8.4 Uanzishwaji wa Taasisi, Mamlaka na Mapitio ya Sera na Sheria Mbalimbali

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia afua mbalimbali za Serikali na kubaini **kwamba** zinaenda kuanzisha Mamlaka na Taasisi mbalimbali. Mfano sekta ya Utalii pekee inataka kuanzisha Taasisi ambapo moja ya Taasisi hiyo itasimamia utalii wa Fukwe. Aidha, Mamlaka ya Mapato inakusudia kuanzisha kitengo cha kusimamia wafanyabiashara wa kati. Afua hizo pia zinapendekeza kuanzisha mifumo mingi, mapitio ya sera, kuanzisha mikakati pamoja na kubadili sheria.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia afua hizi kwa pamoja zinaenda kuongeza gharama za uendeshaji wa Serikali. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuanza kwa kutumia mifumo na Taasisi zilizopo hivi sasa na pale ambapo Serikali itakuwa na uwezo wa kifedha inaweza kuanzisha Taasisi mpya au mifumo mipya.

SEHEMU YA TISA

9.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha kwa kukushukuru wewe Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb), Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza vema Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwashukuru Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb), Waziri wa Mipango na Uwekezaji na Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu Waziri wa Fedha Mhe. Mhandisi Mshamu Ali Munde (Mb) na Mhe. Laurent Deogratius Luswetula (Mb) pamoja na Dkt. Pius Chaya Naibu Waziri Mipango na Uwekezaji kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kujadili Mpango na Mwongozo.

1. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb — Mwenyekiti
2. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb — M/Mwenyekiti
3. Mhe. Bal. Dkt. Pindi Hazara Chana, Mb — Mjumbe

4. Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb Mjumbe
5. Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb Mjumbe
6. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb Mjumbe
7. Mhe. Amina Idd Mabrouk, Mb Mjumbe
8. Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb Mjumbe
9. Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb Mjumbe
10. Mhe. Bahati Kenneth Ndingo, Mb Mjumbe
11. Mhe. Ally Yahya Mhata, Mb Mjumbe
12. Mhe. Kakulu Buchard Kakulu, Mb Mjumbe
13. Mhe. Dkt. Catherine Canute Joachim, Mb Mjumbe
14. Mhe. Moses Charles Bujaga, Mb Mjumbe
15. Mhe. Asma Ali Mwinyi, Mb Mjumbe
16. Mhe. Haran Nyakisa Sanga, Mb Mjumbe
17. Mhe. Devotha Daniel Mburarugaba, Mb Mjumbe
18. Mhe. Thomas Mgonto Kitima, Mb Mjumbe
19. Mhe. Enock Zadock Koola, Mb Mjumbe
20. Mhe. Nancy Hassan Nyalusi, Mb Mjumbe

Mheshimiwa Spika, pia niwashukuru Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Tausi Mbaga Kida, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Mipango pamoja na Dkt. Fred Msemwa Katibu Mkuu Uwekezaji. Vilevile, niwashukuru Manaibu Katibu Wakuu wa Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Makamishna, Wakuu wa Taasisi na Wataalam wote kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa upendo wa dhati napenda kumshukuru Mhe. Ally Hassan King, (Mb) Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kunisaidia wakati wote wa shughuli za Kamati. Nitumie fursa hii pia kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa umahiri wao katika kuchambua Mpango na Mwongozo uliowasilishwa. Naomba niwatambue wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwisho ila si kwa umuhimu, nimshukuru Ndg. Baraka Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mashimba Mashauri Ndaki, (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI
27 Oktoba, 2026

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa kuwasilisha maoni ya Kamati yako ya Bajeti.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kupata maoni yetu kama Bunge, ninaomba sasa tuanze kuchangia na kwa kuwa muda umekimbia tutakuwa na mchangaji mmoja halafu tutaendelea jioni. Tutaanza na Mheshimiwa Kakulu Burchard Kakulu.

MHE. KAKULU B. KAKULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninashukuru kwa kupata nafasi na nichukue nafasi hii pamoja na mambo mengine kumpongeza Mwenyekiti wangu wa Kamati, Mheshimiwa Mashimba Ndaki kwa uwasilishaji mahiri na kwa kweli kwa kuzingatia maoni yetu kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nitachangia mambo machache na ninafanya hivyo kwa sababu ya kuweka *focus* katika jambo ambalo ninataka kulichangia na umuhimu wake kwa nchi. Mapema asubuhi ya leo wakati wa kipindi cha maswali na majibu tulimwona Waziri wetu wa Ujenzi akifafanua kuhusu hali ya barabara zetu na umuhimu wa kuweka kipaumbele katika uendelezaji wa miundombinu ya barabara. Kwa sababu hiyo nikamsikia akisisitiza kwamba ni lazima tubadili mwelekeo wa namna tunavyo-*finance* uendelezaji wa miundombinu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jambo lililoko mezani kwetu nitazungumzia kuhusu ushiriki wa Sekta Binafsi kwa kushirikiana na Sekta ya Umma kwa kutumia mfumo wa *PPP* kusaidia ujenzi wa miundombinu muhimu ya kiuchumi hasa miundombinu ya uchukuzi, usafirishaji na nishati. Kwa leo ninataka nitumie muda mrefu sana kuzungumzia hali ya barabara zetu na namna Sekta Binafsi inavyoweza kutusaidia kutoka hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa nini *PPP*? Kwa nini tunahangaika kutaka Sekta Binafsi itusaidie kujenga miundombinu? Kwanza ni sahihi kwamba kwa uwezo wetu wa kibajeti hatuwezi kuwa na pesa ya kutosheleza kujenga miundombinu yote kwa pamoja au kwa haraka. Katika miaka yetu ya Uhuru sasa miaka 65 bado hatujaweza kukamilisha shauku yetu ya kujenga miundombinu kwa ukamilifu katika maeneo yote. Kwa hiyo haja ya kuwa na Sekta Binafsi ni kwa sababu hiyo, nchi yetu bado hatujawa na uwezo wa kutosha kibajeti ku-*finance* uendelezaji au ujenzi wa miundombinu muhimu kama reli, barabara na miundombinu ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalau kwa sehemu ya nishati kwa sasa hivi kwa kweli hatua imepigwa kwa sehemu kubwa sana, lakini bado tuna shida kubwa kwenye barabara zetu. Barabara zinazotoka hasa zile zinazopita kwenye *corridor* muhimu sana za kiuchumi, Barabara kama ya *Tanzam Highway* kuanzia Morogoro – Iringa – Makambako – Igawa – Mbeya – Tunduma ambayo kwa sasa inasafirisha mizigo yetu ya kwenda nchi za ng'ambo *(transit cargo)* kwa wastani wa 80% ya mizigo yote inayoenda nchi za jirani. Kwa hiyo unaweza ukaona umuhimu wa barabara yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; kwa nini *PPP*? Tunataka tu-*exploit* ufanisi wa Sekta Binafsi kwa sababu, ninaamini kwamba leo kama ninataka kuwekeza katika kujenga Barabara ya Tanzam kuanzia Morogoro – Tunduma kwa vile ninataka niweke pesa yangu na niikusanye katika muda mfupi au nianze kupata mapato katika muda mfupi iwezekanavyo kwa vyovyote vile nitaweka bidii ya kuijenga hiyo barabara moja kwa haraka. Pili, katika viwango vinavyotakiwa ili nisilazimike kuweka gharama za kui-*maintain* katika muda mfupi ili pesa nitakayoipata inisaidie ku-*service* ama mkopo wangu au *equity* yangu niliyoiweka katika kujenga barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili la muhimu, Serikali tunaweza tukatumia pengine miaka kadhaa kujenga hiyo barabara kwa sababu ya uwezo wetu, lakini kama ninataka kuijenga na mmenipa mkataba nitahakikisha nimetenga *lot* nyingi iwezekanavyo ili barabara hiyo niweze kui-*deliver* katika muda mfupi, nianze kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiniuliza leo mimi sioni kwa kweli sababu ya kusita. Kama tunasema 80% ya *transit cargo* yote inapita hiyo barabara, kuna sababu gani ya kutokuialika Sekta Binafsi kushiriki kujenga hiyo barabara angalau kwa njia sita au njia nane ili moja, katika ujenzi wenyewe wa barabara utatusaidia kuchochea shughuli nyingi sana wakati wa ujenzi, lakini baada ya ujenzi kurahisisha *haulage* ya mizigo yetu ambayo kwa sasa inatumia muda mrefu kutoka Bandari ya Dar es Salaam mpaka Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ya uendelezaji wa bandari sasa hivi na ufanisi wa bandari. Mheshimiwa Waziri asubuhi alizungumza hapa kwa sasa hivi angalau kwa takwimu za mwaka unaoishia mwaka jana bandari imehudumia mizigo inayofikia tani 39,000,000. Makadirio yetu ni kwamba bandari itakuwa ina uwezo kuhudumia zaidi ya tani 60,000,000 ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ya uendelezaji wa bandari ukiitazama na kasi ya uendelezaji wa barabara haviendani. Kwa sisi tunaokaa Dar es Salaam uwezekano ni mkubwa kwamba kama *speed* ya ujenzi wa barabara haitaongezeka na kwa hiyo kutumia mbinu za sasa hivi za kutumia Sekta Binafsi, upo uwezekano utakuwa unatoka Dar es Salaam kuitafuta Mwanza au Tunduma kwa masaa pengine 48 au zaidi ya hapo. Kwa sababu barabara hizi zitakuwa *congested* kwa kiwango ambacho hakitaweza kuhimilika. Kwa hiyo, ninaona suala la miundombinu ni suala la dharura hasa ya barabara kwa sababu ya kuzingatia uendelezaji na *speed* ya uendelezaji wa bandari na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipendekeze kwamba suala la kuendeleza miundombinu ya bandari na barabara pamoja na reli liwe suala litakalofungamanishwa kwa pamoja (liwe *package* moja). Kwa hiyo tuzitake sekta zetu zinazohusika na uendelezaji wa sekta mbili: Uchukuzi na Ujenzi, zote zifungamane kwa pamoja kuandaa mkakati wa pamoja wa namna ya kuondoka hapo. Vinginevyo tukisubiri sana tutakuja ku-*deal* na *crisis* ambayo itatusumbua kwa muda mrefu na itatufanya tuwe *very unpopular* bila sababu wakati uwezo wa kutumia Sekta Binafsi upo na uwezo wa kufanya sekta binafsi upo tuipe nafasi ifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri nimepata nafasi ya kuzishuhudia Serikali kadhaa angalau nikiwa sasa nimekua, kuanzia angalau Serikali ya Rais Mwinyi nimeshakuwa mwanafunzi wa sekondari wakati huo ndiyo ninaanza sekondari. Serikali ya Mzee Mkapa, Serikali ya Rais Kikwete, Serikali ya Rais Magufuli na sasa Serikali ya Rais Samia. Katika kipindi chote hicho kama kuna wakati kumewahi kuwepo utashi wa kisiasa wa kutumia sekta binafsi kutusaidia ku-*deliver* miundombinu mikubwa ni wakati huu kuliko wakati wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wetu kama viongozi sasa kumbe tutumie *political will* iliyopo kutokea *the highest political office* ili ku-*deliver vision* ya Rais na *vision* ya nchi yetu. Kwa sababu tusipofanya hivi tunasubiri kutatua kwa zimamoto na barabara huwezi kuijenga kwa mwezi mmoja. Tujiandae leo ili ku-*deliver vision* ya nchi yetu, *vision* ya Mheshimiwa Rais. Tatizo hili baadaye pamoja na uoga uliopo kidogo kidogo siku moja tutakuja kumkumbuka Rais kwa hili. Hilo lilikuwa la kwanza kwenye *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko changamoto katika utekelezaji. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati wakati anawasilisha ripoti ya Kamati amesema kwa urefu, lakini ninataka niseme machache; Kwanza tunatakiwa kufanya *overhaul* ya mfumo wetu wa kisera na wa kisheria. Utaratibu mrefu mara *pre-feasibility study,* mara *feasibility study*, mara *detailed design* unatuchukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sekta zote zinazotokana na haya mambo zikutane zikubaliane kufanya marekebisho makubwa ya sheria yetu ili tuondoe mnyororo mrefu. Nimekuwepo Wizara ya Fedha wakati ninaondoka Wizara ya Fedha kwenda Wizara ya Kilimo mwaka 2016 tulishatunga sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo tunapozungumza miaka 10 *down the line* hakuna jambo kubwa sana unaweza ukalitetea angalau basi tuseme lile la *PPP* ya Daraja la Kigamboni, lakini mradi mwingine mkubwa tukiondoa ule wa Bandari ya Dar es Salaam ambao Mheshimiwa Rais alisimama nao na huu unaoendelea wa *BRT* sioni kingine kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninasema bado tuna nafasi ya kufanya vizuri tuitumie kwa kweli kuiepusha nchi yetu na tatizo ambalo tunaweza tukakabiliana nalo huko mbele. Nafasi iliyopo kwa sasa hivi kwa baadhi ya sekta kufanya kila mmoja kwa kipande chake, ni muhimu sana tukaunganisha nguvu ili utekelezaji wa miradi ya *PPP* uwe rahisi. Pengine *definition* ya *PPP* bado ninafikiri kuna shida. Tukienda hapa Congo kuna wakati tunasikiliza Wizara ya Uchukuzi wametupatia mfano mmoja mzuri sana wa namna ya kutekeleza *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwekezaji mmoja amewekeza mradi mkubwa sana wa madini kule Congo, amejenga barabara ya karibu kilometa 400 na anasaidia kujenga Bbandari ya Kalemie na ndiye anayejenga zile meli nne pale *Lake Tanganyika*. Kwa nini tusitumie njia rahisi ambazo wawekezaji wako tayari kufanya ili watusaidie kufanya badala ya kutumia ile *commercial definition* ambazo tunatumia kila siku *pre-feasibility study*, *what*. Hivi viingereza vikiwa vingi vitatukwamisha. Tunataka kuona mambo yanatokea ili sisi tunufaike na matunda ya matokeo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeweza kusema mengi pengine, lakini kwa kuhitimisha ninaomba kwa dhati kabisa ninarejea *statement* niliyoisema tutumie utashi wa Mheshimiwa Rais, tutumie utashi wa Serikali yetu wa kutaka kuona sekta binafsi inashiriki vya kutosha kutusaidia kuendeleza miundombinu yetu ya barabara ili safari yetu ya maendeleo iwe *speed* kubwa zaidi kuliko tunavyoitarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo machache ninakushukuru kwa kunipatia nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kakulu Burchard Kakulu kwa mchango wako mzuri.

Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirejea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa *session* hii ya asubuhi, hivyo basi ninasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 Jioni.

(Saa 7.03 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Katibu!

NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa Kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028

na

Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028.

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano, na kuishauri Serikali kuhusiana na mpango wa maendeleo unaopendekezwa kutekelezwa na Serikali, pamoja na mwongozo kwa Mwaka 2027/2028.

Tuna wachangiaji hapa; nitamwita mchangiaji wetu wa kwanza jioni hii, Mheshimiwa Devotha Daniel Mburarugaba, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata. Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, ajiandae.

MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ametupa uhai mpaka tumeweza kufika hapa siku ya leo. Pia, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anazozifanya; kweli tunaziona, anapambana na Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Mipango na Uwekezaji kwa mapendekezo ya mpango ambayo ameweza kuyasoma leo hapa, kweli amefanya kazi kubwa sana. Tunaona kwamba, ripoti iko *very detailed,* ameeleza mambo mengi ambayo tukilinganisha na ilani ya chama ambacho kiko madarakani, na tukalinganisha na dira pia, na mpango huu, tunaweza kufika mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, tunafahamu Dira ya Mwaka 2050 imeeleza kwamba, sekta binafsi itakwenda kuchangia 70%. Hili jambo ni kubwa sana kwa sababu, Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameonesha kwa kiasi kikubwa sana anashirikiana na sekta binafsi. Kwa hiyo, ningependa kutoa mapendekezo machache, ili tuweze kwenda na mpango huu, tuweze kufanikisha Dira yetu ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye huu mpango tumeona kuna sekta ambazo zimekuwa *identified* kwamba, ndiyo sekta za mageuzi. Leo hii nitakwenda kuzungumzia Sekta ya Kilimo kwa sababu, imebeba 75% ya Watanzania; yaani tukimaanisha ajira nyingi zinapatikana kwenye Sekta ya Kilimo. Hivyo basi, huu mpango bila ku-*accommodate* sekta binafsi, yaani nikimaanisha *PPP,* ambayo inaonekana iki-*intervene* kwa asilimia kubwa tutakwenda kufanikisha mpango huu. Kwenye Sekta ya Kilimo tuna sehemu mbalimbali ambazo ninaona zikiwa *intervened* na *PPP,* tutakwenda kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni miradi ya umwagiliaji. Tunafahamu kabisa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweka miradi mingi ya umwagiliaji. Miradi hiyo, tunafahamu tunazo fedha zinazotoka, lakini bado hatuwezi kujitosheleza kwa miradi yote hivyo basi, sekta binafsi kama *PPP* zikiweza kuingia kwenye miradi ya umwagiliaji; kama kule Mbarali kuna vijiji ambavyo vinashirikiana katika kilimo, vikipata mwekezaji

ambaye ataingia kwenye miradi ya umwagiliaji, aka-*invest* pale, tunaona kwamba, tutakwenda kwenye kilimo ambacho kitakwenda kuleta tija kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunafahamu kabisa kwamba, mvua zetu zinapatikana, lakini siyo kwa wakati wowote. Kwa hiyo, tukiwa na miradi ya umwagiliaji, ambayo iko *intervened* na sekta binafsi tutapiga hatua kubwa sana na tutakuwa na mafanikio makubwa kwenye Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapohapo kwenye Sekta ya Kilimo, naona *PPP* ikifanikiwa, tunaweza tukaenda kwenye *angle* ambayo; tunayo mazao mengi tunayozalisha, kwa mfano tuna mahindi mengi na mazao ya aina mbalimbali ambayo yanazalishwa, lakini hatimaye kuna mazao huwa yanapotea kwa sababu, hatuna maghala ya kutosha katika nchi yetu. Maghala yapo, lakini tunaona mikoa inazalisha aina mbalimbali za mazao kwa hiyo, ninaona *PPP* ikipewa kipaumbele kwenye uwekezaji huo wa maghala, tutaweza kukomboa mazao ya wananchi, na tutaweza kuhakikisha upotevu wa mazao unashuka kwa asilimia ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunazo *cooling system,* yaani *cold systems,* ambazo zinatakiwa kuwepo, ili hawa wakulima wanapolima matunda, wanapolima vitu mbalimbali, inakuwa yale matunda hatuwezi kuyatumia yote kwa wakati mmoja; kwa mfano kuna wakulima wa parachichi ambao wanahitaji kupata hizi *cold systems,* zikiwepo kila wilaya au kila mkoa tutahakikisha hayo matunda yanaweza kufika kwenye *airport* zetu na sehemu nyingine. Sekta binafsi, yaani *PPP*, itakuwa ni mchango mkubwa sana kuhakikisha hayo matunda yetu yanatumika vizuri, na pia mkulima anaiona faida ya kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni muhimu sana kwenye sekta ya kilimo, ni kuhusiana na mikopo nafuu. Wakulima wamekuwa wakipata mikopo, lakini mikopo hii inakuwa ni ya ghali sana. Tukiangalia *central bank rate, it's about* 6.25 ambayo tunaipata huko *central bank rate*. Benki zetu tunaona kwamba, *interest rate* ambazo zinatolewa ni kubwa sana kwa wakulima wetu na wawekezaji wa viwanda. Kwa hiyo, tukipata

interest rate ambazo zitakuwa *friendly* kwa wawekezaji, *especially* hawa watu wanaokuja kufanya hii *PPP,* itakuwa ni rahisi sana kwa wakulima kuweza kulima na kupata mikopo ya nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ninaweza kuongelea Mkoa wa Kagera. Kagera ni mkoa ambao tunajikita kwenye kilimo cha kahawa, lakini inaonekana kwamba, kuna kipindi cha mavuno ambapo wakulima wanahitaji *support* ya mikopo ya muda mfupi. Tunayo Benki yetu ya *TADB,* ingeweza kuwezeshwa ikatoa mikopo kwa *single digit,* wakulima hawa waweze kupata mikopo ya bei nafuu, ili tuweze ku-*intervene,* na kuhakikisha wakulima wanapata mikopo ambayo iko *affordable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni ushauri. Kwa sababu, *PPP* toka imeanza tumeona kuna sera na kanuni zipo pale *PPP center,* ambazo zinawafanya maafisa masuuli ambao wapo kwenye halmashauri zetu wanaibua miradi, lakini hatimaye miradi hiyo inashindwa kutekelezwa kwa sababu, kumekuwa kuna sheria nyingi, kanuni nyingi, na pia, kuna mlolongo mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *just imagine* mtu anaanza mradi kwenye halmashauri, lakini huo mradi anatakiwa aripoti kwenye *PPP center,* ili uweze kuwa *approved* na *procedure* ziweze kufuatwa. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba, hawa maafisa masuuli wapewe uwezo wa kupokea miradi na kuitangaza kwa umma, ili hawa sekta binafsi waweze kushindania miradi hiyo na kuhakikisha tunapata mwekezaji, ambaye ataendana na eneo lile ambalo linatakiwa kuwekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PPP* nyingi ambazo zinafanyika kwenye halmashauri zetu unakuta tunajenga soko, tunajenga stendi, zimekuwa ni *very common!* Kwa sababu, maisha ya Watanzania unakuta stendi imejengwa mbali na mji, sasa tukijenga ile stendi inakuwa *used,* lakini *not* 100% kwa matarajio ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninashauri miradi hii iweze kuibuliwa kuendana na maisha ya Watanzania. Baada ya kusema hayo nawashukuru sana, na pia, nampongeza Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga. Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, ajiandae.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, mchana huu au jioni hii, kuchangia mpango wa mapendekezo ulioletwa na Profesa Kitila Mkumbo. Awali ya yote nami namshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, ambaye ametuwezesha kuwepo hapa jioni hii. Pia, namshukuru sana Waziri na timu yake yote; Naibu Waziri na watendaji wote kwa kazi kubwa aliyoifanya katika maandalizi na mapendekezo ya mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze katika maeneo makubwa matatu; Moja, Dira ya Taifa. Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo alipokuwa anawasilisha asubuhi hapa suala la Dira ya Taifa ya Mwaka 2050 ameeleza mambo mengi sana ya msingi. Lengo kubwa ni kuigeuza nchi yetu kuwa Taifa kubwa linalojitegemea katika viwanda ambavyo vitahimili changamoto ya tabia ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ameeleza sana; katika *document* yake kuna mambo mengi, lakini kwa ufupi, ameeleza malengo ambayo Taifa letu tufikapo Mwaka 2050 tunategemea ku-*achieve* mambo gani! Kwanza, tunasema kwamba, pato letu lifike dola trilioni moja, pato la Mtanzania lifike *USD* 7,000, lakini pia, kutokomeza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi ameyaeleza ndani ya mpango ule kwenye Dira yetu ya Taifa. Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, anatambua kwamba, tunazo changamoto ambazo zitasababisha mpango wetu huu kutofanikiwa; kuna changamoto nyingi zipo, lakini mimi nimeiona moja ambayo, tusipoiangalia, inaweza ikatukwamisha tusifike malengo tunayokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni, kuna changamoto ya utawala bora, ukiritimba na rushwa. Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, hii ni changamoto kubwa sana, tusipoangalia na

kuichukulia hatua, kuanza kuweka mikakati ya kukabiliana nayo, nina imani kabisa hatutafika Mwaka 2050 na kutimiza malengo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu fikiria leo hii, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, yeye ndiye Waziri mwenye dhamana ya mipango na uwekezaji. Ana mipango mizuri ya kuleta maendeleo ya nchi yetu, lakini kesho na kesho kutwa yeye si Waziri wa Wizara hii! Je, anategemea mpango huu utatekelezeka? Kwa sababu, nimeisikiliza *document* yake yote, hakuna sheria ambayo ipo ya kuhakikisha kwamba, mpango huu unaoundiwa sheria yake! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo yeye ni shahidi, tena yeye ni Profesa! Amefanya kazi na viongozi wengi wa nchi hii tangu Mwalimu Nyerere, Mzee Mwinyi, Mzee Mkapa na wengine, na Marehemu Dktari Magufuli na mama yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Kitila atakubaliana na mimi, kila Rais anayekuja anakuja na mipango yake. Mara nyingi sana Marais wengi wanakuja, wana-*challenge* mipango ya wenzao walioiacha nyuma! Sasa mpango huu siyo wa Rais wala siyo wa mtu! Ni mpango wa maendeleo ya Wananchi wa Tanzania, lazima tuutengenezee sheria. Sheria ambayo itahakikisha Rais atakayekuja hana lingine, ni kuufuata mpango wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni nini matarajio yangu! Ninamwomba Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, kwa kuwa, haya ni mapendekezo yetu, tunategemea mwezi wa tatu atakapoleta mpango kamili, aje na sheria ya kuhakikisha mpango huu unakuwa na sheria maalum ya kuulinda na kutekelezwa, ili asije mtu katikati akabadili na akafanya yale anayoyataka yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama yetu ni *champion* wa huu mpango, nafikiri hatajisikia raha, anamaliza muda wake, anakuja mtu mwingine na ajenda zake, tofauti na mpango ambao unahakikisha kumkomboa Mtanzania! Hilo ni suala langu la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni, kwenye kilimo. Ndugu yangu, Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Mashimba, alipokuwa anawasilisha mapendekezo ya kamati yetu ameeleza kwa kirefu sana masuala ya kilimo, na ameeleza mchango wa kilimo katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleza kuhusu uchangiaji wa Pato la Taifa kwamba, kilimo kinachangia karibu 24.5% na pointi zake. Dada yangu pale, Mheshimiwa Doris amesema kwamba, kilimo hiki kinaajiri Watanzania takribani 75%, lakini wakati huohuo kilimo hiki ndiyo mkombozi wa mtu maskini. Tunazo changamoto ambazo kwa kweli, kilimo chetu kinakumbana nazo, kwanza kilimo chetu mpaka leo kwa asilimia kubwa kinategemea mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu, Mheshimiwa Profesa Kitila, wakati anawasilisha mpango wake nilipenda sana alipofungamanisha masuala ya maji na umwagiliaji. Mipango yetu mingi ukimwambia ndugu yangu, Mheshimiwa Aweso, yeye akili yake ni kuleta maji ya kunywa, Waziri wa Kilimo akili yake ni mabwawa! Kumbe watu hawa wawili wangefanya kazi pamoja, suala la maji ya kunywa tungepata, lakini pia, tungepata umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni matarajio yangu, tunayo miradi mikubwa ya kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria kuyaleta Singida, tuna mpango mkubwa wa kuvuta maji kutoka Ziwa Tanganyika kuyaleta Singida; nafikiri watakutana pale Itigi, kama sikosei, au Manyoni. Basi, mpango huu uunganishwe na kuhakikisha kwamba, mradi huu unaleta maji ya kunywa, *at the same times* unahakikisha unaleta umwagiliaji katika maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii iende sambamba na maeneo yote ambayo tunategemea maji kwa kuyavuta kutoka kwenye mito na mabwawa yetu. Mfano, kule kwangu Nanyumbu Mheshimiwa Aweso alikuja, ninamshukuru sana, ametuletea mradi mkubwa sana kutoka Mto Ruvuma kuyaleta Mji wa Mangaka, karibu kilometa 80, lakini mradi ule ukiunganishwa pamoja na umwagiliaji, tutakuwa tumemkomboa sana mwananchi. Kwa hiyo ni matarajio yangu katika mapendekezo haya, ni mapendekezo yetu, mwezi wa tatu atakapoleta mpango, hebu ajaribu kuhusisha

kuunganisha mambo haya mawili, ili kuhakikisha kwamba, miradi hii inakwenda pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo tunao mgogoro mkubwa sasahivi, wa wakulima na wafugaji; lazima mpango wetu ueleze ni jinsi gani ya kutatua mgogoro huu. Pia, tuna mgogoro mkubwa sana wa upatikanaji wa pembejeo, leo mbolea ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu, sisi ni wakulima wa korosho. Sisi tunategemea *sulphur* na viuatilifu, lakini kama hatutakuwa na mpango wa kuhakikisha kwamba, viuatilifu hivi vinakuja kwa wakati, ambavyo ndiyo vinasababisha kilimo cha korosho kuweza kuendelea, tutaweza kufeli! Kwa hiyo, nategemea sana hili jambo atalitilia mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninakumbuka, ninafikiri Bunge lililopita, tulianzisha hii *NAESA!* Nafikiri unaikumbuka, na tukaitungia sheria; huyu ni Wakala wa Taifa wa Huduma za Ugavi *National Agriculture Extension Services;* wakala huyu mpaka leo hajaanza, na ndiyo mkombozi wa wananchi wetu! Sasa Mheshimiwa Profesa Kitila hebu aje atueleze, mwezi wa tatu, ni lini wakala huyu, ambaye ndiyo mkombozi kwa wakulima wetu, ataanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala huyu hana tofauti na *TARURA*. Leo *TARURA* inatusaidia sana vijijini. Leo tuna *TANESCO,* na tunategemea, nayo hii *Agriculture Extension Service* ianzishwe, ili iweze kuleta ukombozi katika maeneo yetu. Vinginevyo katika mpango wako wote sijaisikia jambo hili!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, jambo hili nalo aliweke. Nina imani kabisa, kwa kuanzisha huyu wakala, ambaye tayari tumeanzisha bado haijaanza kufanya kazi, tutahakikisha tunakuwa na usimamizi wa karibu zaidi na kuongeza tija kwa wakulima wetu. Pia, tutakuwa tumetekeleza lile agizo la Mheshimiwa Rais la kuanzisha wakala huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo katika maelekezo yake amezungumzia sana sekta ya madini, ambayo Mwenyekiti ameielezea vizuri, na sisi tunakubaliana kwamba, sekta hii inakua kwa haraka sana. Mfano, mchango wa Pato la Taifa sasahivi umefikia 10% kwenye sekta ya madini, lakini mauzo ya nchi za nje yanafika shilingi bilioni 5.9, ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto, hasa kwa wananchi wetu. Tunayo madini ambayo ndiyo msingi mkubwa; tuna madini ya dhahabu, tuna almasi, rubi, coal, na shaba. Dhahabu ndiyo kila mahali, leo Geita huko tunaona matajiri wakubwa kwa sababu ya dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kule kwangu Nanyumbu tumegundua dhahabu, lakini kwa uchungu mkubwa wachimbaji wadogo-wadogo hawanufaiki na ile dhahabu ambayo imegundulika! Kuna ukiritimba mkubwa sana kwa wachimbaji wadogo-wadogo kuweza kufanya shughuli zao! Sasa ninaomba, Mheshimiwa Profesa Kitila, ili wachimbaji wadogo-wadogo waje kumiliki uchumi wao ni lazima tuunganishe katika mipango yetu. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo ninaamini kabisa tunaweza kuwakomboa wananchi wetu na ile dira tunayoikusudia itafanikiwa. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Mhata, ahsante sana kwa mchango wako.

Nilimwita Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao. Mheshimiwa Sigrada Wilhem Mligo, ajiandae.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mimi pia, naungana na Wabunge wenzangu kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kwa uwasilishaji mzuri wa taarifa; maana yake amewasilisha kwa niaba pia, ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninampongeza Mwenyekiti wangu wa Kamati, Mheshimiwa Mashimba Ndaki, naye kwa kuwasilisha maoni yetu sisi ambao ni Wajumbe wa Kamati kwa

ufanisi mkubwa. Mimi pia, naungana na Wabunge wenzangu waliotangulia kuishauri Serikali kwenye huu Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2027/2028, wazingatie sana maeneo yale ambayo yanaajiri Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia, eneo la kilimo linaajiri zaidi ya 75% ya Watanzania, na mchango wake kwenye Pato la Taifa ni mkubwa sana. Sasa namna pekee ya kumsaidia mkulima, na ambapo hatimaye unapomsaidia mkulima mmoja, maana yake ni unasaidia Watanzania wengi ambao wamejiajiri kwenye kilimo, uvuvi, na eneo la ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ya wakulima ni tija, masoko, na miundombinu ya barabara, hasa zile za vijijini. Ili mkulima aweze kupata hamasa ya kulima anahitaji apate bei nzuri ya mazao; mwaka huu akilipwa vizuri, maana yake ni hata mwakani atajitahidi kuongeza bidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ludewa ni wakulima, asilimia kubwa wanategemea kilimo na katika shughuli yao ambayo wamezaliwanayo hawahitaji kuhamasishwa, walimehamasika, yaani wanajua ndiyo mshahara wao kila mwezi. Kwa hiyo, jukumu ambalo Serikali ingewasaidia wakulima hawa wa Ludewa na wa maeneo mengine, ni kuhakikisha kwamba, wanapata bei nzuri ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia nitatoa mfano wa zao la mahindi. Mwaka huu, ambapo kuna mikoa kama Ruvuma, Mbeya, Katavi, Rukwa, na mingine, kutokana na jitihada za Serikali kutoa ruzuku ya mbegu na mbolea wananchi wamepata mazao mengi sana, lakini sehemu ya bei ya zao hili, la mahindi, kidogo tumewavunja moyo wakulima, na Serikali imekuwa ikitumia mazao ya chakula katika kudhibiti mfumuko wa bei. Kwa hiyo, wakulima hawa wakivunjika moyo, wasipoenda shambani, tutashindwa kuudhibiti mfumuko wa bei kwa sababu, chakula ndiyo kinachosababisha utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ukipita katika nyumba 10 utakuta nyumba nane wanakula ugali au wanakula maharage. Kwa hiyo, namna pekee ya kuwafanya wakulima waendelee

kulima, ili kuwe na utulivu, hasa kwenye eneo la mfumuko wa bei ni kuwapa bei nzuri na kuboresha miundombinu ya barabara, hasa za vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano. Kuna zao la mahindi, gharama kwa mwananchi kuzalisha ekari moja anatumia takribani shilingi 1,230,000; hiyo ni kuanzia kuandaa shamba, kulima na trekta, palizi zote, kupiga dawa za magugu na wale wadudu waharibifu wa mazao, kuweka mbolea, kuvuna, kununua vifungashio na, kusafirisha kurudisha nyumbani, anatumia zaidi ya shilingi 1,230,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaangalia hapo sasa, kwa bei ambayo mwaka huu Serikali imeenda kununua, ya shilingi 450 tunaona wakulima wanatengeneza hasara ya kati ya shilingi 110,000 hadi shilingi 150,000 kwa ekari moja! Kwa hiyo, sasa hii ni hofu kwamba, wanaweza wasiingie tena shambani kirahisi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunajua kuna majanga, kama changamoto ile ya Mfereji wa Hormuz, mbolea zilikuwa zinashindwa kuja hapa! Naipongeza Serikali imejitahidi sana; nilimsikia Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kuwa, Serikali imeweka ruzuku kubwa sana, walau mfuko utauzwa chini ya shilingi 100,000. Pia, ile bei wameipanga kulingana na umbali, kutoka mzigo unapotolewa mpaka shambani, hawajapanga bei wakiwa Dodoma! Hili ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama mbolea itapatikana kwa uhakika hili tatizo la mwaka huu lisijirudie tena, la bei ya mahindi kwa shilingi 450! Tunawapa hasara wakulima, na tunawavunja moyo! Pia, gharama za wanunuzi wengine kwenda kuyachukua mazao kule kwa sababu, gharama ni ya usafiri; miundombinu yetu bado ni changamoto, wafanyabiashara binafsi wengi wanakwepa au wanaenda kuwalalia wananchi kwa bei ya chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuangalie namna ya kutenga bajeti ya kutosha tuwape hawa watu wa *NFRA*. Bei ambayo mkulima anaweza akapata manufaa ni, angalau, shilingi 700. Hapo itawapa moyo wa kuendelea kulima mara kwa mara.

Vilevile, eneo hili Serikali iliangalie, ili kuhakikisha kwamba, tunajenga maghala kila halmashauri, na miradi mingine; tunazungumzia *PPP,* lakini kitu kama kujenga ghala siyo lazima tutegemee Mfuko Mkuu wa Serikali! Tunaweza tukatumia hata *outsourcing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu benki zimetoa mikopo mikubwa sana; nitatoa mfano wa jimboni kwangu, ambako nimetafuta taarifa, Benki ya *NMB* pekee imekopesha wakulima zaidi ya shilingi bilioni 22 kwenye zao hili la mahindi. Kwa hiyo, walikuwa na uhakika, ile bei ya nyuma ilikuwa ni uhakika kwamba, wakikopesha basi wananchi watarejesha, lakini sasahivi wakulima wengi hawana uwezo wa kurejesha kiwango hicho ambacho walikopa kwa hiyo, benki zitapata changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutafute pia, fedha za kutosha kuiwezesha *TARURA* iweze kujenga madaraja makubwa, kujenga barabara za vijijini ambazo zina upana unaotosha, ziwe na mitaro na changarawe za kutosha, na pale tunapoweza kujenga kwa kiwango cha zege itakuwa nzuri sana. Hii itasaidia wananchi kuweza kutoa mazao kule na kuyafikisha sokoni kwa walaji, na wakulima watapata mapato zaidi. Wataalamu na wachambuzi wa masuala ya kiuchumi, wengi, duniani wanasema sekta ya kilimo ikianza kukua kuanzia 10% kwenda mbele pato letu la Taifa litaongezeka kwa kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tuna eneo la mikopo. Mikopo ikitumika vizuri siyo kitu kibaya, maana inaathari hasi na chanya. Ukichukua mkopo ukawekeza kwenye maeneo ambayo yanachochea ukuaji wa uchumi, na kama miradi ukiisimamia ifanyike kwa wakati, na imalizike kwa wakati itakuja kuchangia kwenye kurejesha haya madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili ninaipongeza Serikali kwa kusimamia vizuri uchumi kwa sababu, namba zote, ukipitia kiwango cha deni la Taifa kwa *IMF* wanataka usivuke 55%, kwa Afrika Mashariki 50%; ukija kuangalia sisi hizo shilingi trilioni 117 tunacheza kwenye 49% kwa hiyo, bado tuko kwenye kiwango. Ila sasa tuwekeze kwenye miradi ile ambayo inakwenda kuchochea ukuaji wa Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Wajumbe hapa wamezungumzia miradi ya kilimo cha umwagiliaji; *GDP* yetu ina shilingi trilioni 186 sasahivi kwa hiyo, tukiongeza uwekezaji kwenye miundombinu ya barabara, hasa vijijini, na miradi ile ambayo ni viporo iliyokwama kwa muda mrefu tutakwenda kuchochea ukuaji wa uchumi. Kwa hiyo, zile barabara ambazo zina uchumi mkubwa, kama alivyotoa mfano Mheshimiwa Kakulu asubuhi, barabara hii inayoanzia Dar es Salaam, bandarini, maboresho yaliyofanyika bandarini yanahitaji yaende sambamba na Barabara ya kutoka Dar es Salaam mpaka Mbeya, kule Tunduma; hii ya kuja Dodoma mpaka Mwanza, vilevile ya kwenda hadi kule Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwenye maeneo ya miundombinu ya *SGR*. Serikali inatambua inafanya vizuri, lakini tuongeze kasi ya usimamizi, ili miradi ikamilike haraka ije kuchangia kwenye kulipa haya madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninazungumzia ni hii miradi ambayo tunaiita vielelezo; *LNG,* mradi wa Mchuchuma na Liganga, na ile sijui Engaruka kule! Miradi hii tumeizungumzia sana, ninatambua kuna jitihada, lakini bado kwenye maamuzi, dunia ya leo, tunavyozungumzia Dira 2050 twende hata kule kwenye *decision making,* tuwe tunafanya maamuzi ya haraka, tunaamua vitu vinaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua tunazungumza muda mrefu, miradi kama hii ingeweza kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa, ingechochea ajira, ingeongeza pato la mtu mmoja mmoja, na tungeweza kutimiza haya malengo ya uchumi wa dola trilioni moja ifikapo 2050, kama ambavyo dira yetu inasema. Kwa hiyo mwishoni namuomba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, kwa niaba ya Wananchi wa Ludewa, ile barabara ambayo ipo jimboni kwako, wewe umekaa hapo hauwezi kujisemea! Ile Barabara ya Itoni – Lusitu, yule mkandarasi amekuwa kama ana mapembe, yaani yeye ndiyo amekuwa Serikali, halafu Serikali sijui imekuwa mtu gani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu kinatudhalilisha sana kwa wananchi. Ninaisihi Serikali, eneo hili wafanye maamuzi magumu na ya haraka kuweza kutatua tatizo. Kama changamoto ni *source*

ya fedha, lakini ninafahamu mkandarasi amelipwa. Sasa kama amelipwa, inakuwaje tena tunaogopa kufanya maamuzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninajua wewe huwezi kujisemea hapo, lakini wananchi wa jimbo lako pale, na sisi Wananchi wa Ludewa hatuna sehemu nyingine ya kupita, lazima tutapita Itoni – Lusitu. Kwa hiyo, naiomba Serikali kwenye eneo hili, ikiwezekana Waziri afike aweze kutatua changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, ahsante sana.

Nilimwita Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, atafuatiwa na Mheshimiwa Sigrada Wilhem Mligo. Mheshimiwa Dkt. Johannes Lukumay ajiandae.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, na mimi, kuchangia huu mpango. Ni kwamba, mabadiliko yaliyopo yanakwenda kwa kasi duniani katika sekta ya uchukuzi, na ambayo yanachangia sana sasahivi kutoa ajira kwa wananchi wetu, kuanzia kwa madereva, akina mama ntilie huko, na wakulima kwa sababu, ndiyo chachu kubwa inayofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango uliowasilishwa hapa leo, ndugu yetu, profesa ni mwalimu wangu katika masuala ya siasa, lakini amenifundisha namna ya kukaba. Sasa ninashindwa sana kumkosoa, lakini naona kuna makosa mengi ambayo yako hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, lazima tufikie mahali tusiwe waoga katika kuamua, hasa katika kutengeneza miundombinu ya nchi hii. Hatuwezi kukuza sekta ya uchukuzi kupitia bandari, wakati huohuo hatujapanga mipango mizuri ya kutengeneza barabara katika nchi yetu. Tunakopa mikopo mikubwa katika nchi hii, lakini tunaogopa kukopa, kwa ajili ya Barabara, hili ni jambo ambalo linanifikirisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano reli, hii reli tunayoitengeneza sasahivi *(SGR),* tunatumia ma-trilioni ya shilingi katika kuwekeza katika reli hiyo, lakini tunasahau barabara! Kwa nini mfumo huo tunaoutumia kupata pesa, kwa ajili ya kutengeneza *SGR*, tusitumie mfumo huohuo kutengeneza barabara zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi tulizonazo katika nchi hii, kwanza zimepitwa na wakati! Madaraja yaliyopo yamepitwa na wakati! Hizi ni *structure,* zinakwenda kwa namba, hii ni sayansi. Ni kwamba, daraja likitengenezwa, kwa ajili ya miaka 50, ikifika miaka 50 lazima lijengwe daraja nyingine, hakuna siasa katika barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Wabunge wote hapa salamu walizotumwa na wananchi wao kuja hapa Bungeni, la kwanza wameambiwa nendeni mkashughulike na suala la Barabara; la pili, wameambiwa nendeni mkashughulike na suala la maji; ndiyo vitu ambavyo wavimebeba. Hapa sasahivi hatuzungumzii tena umeme baada ya kumaliza Bwawa la Mwalimu Nyerere. Tunajua mipango iko mizuri kwa *REA* na kila kitu. Sasa tunatakiwa tufikirie sana suala la barabara na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tufikie suala la kukopa, leteni hoja hapa Bungeni tukakope, hakuna kuogopa! Hatuwezi kuogopa wanaharakati kusema kwamba, Tanzania ina madeni makubwa! Twendeni tukakope, na Wabunge tukija hapa tupitishe hilo suala la kwenda kukopa; kama kuna mpango huo Profesa, nakuomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupa tu mfano; leo nchi zote zinazoendelea duniani zinajenga barabara, tena kwa kiwango cha chini ni njia nne, mbili zinapanda, mbili zinashuka. Huko duniani tunakopelekwa tunamshukuru sana Mheshimiwa Spika, mimi nimekuwemo katika *delegation* nyingi za Bunge; alikuwepo Mheshimiwa Dkt. Tulia hapa, tumekwenda sana nje. Leo hapa Mheshimiwa Zungu ndiyo kafungulia buti kabisa; ni kwamba, kwa ambaye hajapata bahati hiyo ya kusafiri bado, ajue tu jina lake linakuja, lakini tunasafiri. Huko tunakopita, Waheshimiwa Wabunge

ninyi wenyewe mnaona, barabara ni sita; sita zinakwenda, sita zinarudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari gani ambayo mnaleta mipango hapa? Nchi imepata uhuru miaka 60, sasa tunakimbilia 65, leo bado tunaanza kufikiria kutengeneza barabara ya njia moja, nani anasema maneno haya? Hizi barabara zilitengenezwa wakati huo, gari ni *Morris*, gari kubwa ilikuwa ni tani tatu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari ya tani tano yamekuja, tuko kwenye barabara moja! Magari ya tani 10 yamekuja, tuko kwenye barabara moja! Leo magari yanakuja ya tani 40, bado barabara moja! Mimi ninashindwa kuelewa jamani, hivi tunavyoondoka hapa ninyi Mawaziri huwa mkishuka *airport* mnakwenda kufungiwa hotelini au mnatembea kwenye hii miji ya nchi za watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri sana mpaka ninashindwa kuelewa! Kwa nini tusitafute hapa, tukakopa sisi hapa trilioni sita, kwa ajili ya barabara? Tuje tuzipitishe hizi barabara, siyo kisiasa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kabisa kwamba, barabara zimekwisha; Barabara ya Dar es Salaam, tusizungumzie habari ya Dar es Salaam – Morogoro, hapana! Barabara zimekwisha, tunataka barabara nne; yaani Dar es Salaam siyo kwamba, barabara nne zije zikomee Kibaha, hapana, na sisi tunalipa kodi za nchi hii! Watanzania wanalipa kodi! Tunataka barabara, kama ni njia nne, zitoke Kibaha hapo moja kwa moja mpaka Chalinze; Chalinze – Segera; Segera – Arusha; Segera – Tanga; hivyo, tunataka barabara za namna hiyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka barabara njia nne; Arusha – Babati, Babati – Singida, Babati – Kondoa – Dodoma. Tunataka njia nne kutokea Dodoma hapa kwenda Manyoni; Manyoni – Singida; Manyoni – Tabora; Manyoni – Singida – Nzega. Tunataka barabara ya Mwanza – Shinyanga – Mwanza. Tunataka Mwanza – Musoma, njia nne, Mwanza – Geita, njia nne; ndiyo tunataka maendeleo ya namna hiyo. Pia, tunataka barabara kutoka Morogoro moja kwa moja mpaka Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Iringa – Makambako; tunataka Iringa – Mbeya; tunataka Mbeya – Songwe – Tunduma. Tunataka Makambako – Njombe; tunataka Njombe – Songea; tunataka Njombe – Tunduru; tunataka Tunduru – Mtwara; tunataka Dar es Salaam – Mtwara; ndiyo tunataka njia za namna hiyo! Msituletee mipango ya kizamani kabisa, sisi hatuwezi kuikubali! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwe mkali katika jambo hili Wabunge tunasikilizwa, wananchi wanatushangaa sana! Tusiridhike na kusifiana hapa kwa barabara moja, haiwezekani! Hivi ninavyozungumza na wewe, leo unakuja unapanga foleni! Foleni iliyoko Dar es Salaam ndiyo foleni ya kutoka Morogoro kuja Dodoma, mnafuatana namna hii na ma-*traffic* sasa, kwenye ile mistari ndiyo wamekaa kutuvizia, hili litaisha tu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba sana Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, bosi wangu, mwalimu wangu katika jambo hili, hebu leta barabara za njia nne kwa chini! Tunataka barabara njia nne! Nendeni mkakope hata shilingi trilioni 10, tupitishe hapa, na mkituletea hapa tuone hizi barabara zote zimeorodheshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupa mfano; tuna barabara ya muhimu sana ambayo ingepunguza *jam*. Hii barabara ingetokea Korogwe tu, inakuja Handeni; Handeni moja kwa moja Dumila; Dumila tunakuja moja kwa moja, unanielewa vizuri…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uniongezee dakika kwa sababu, hili ninaoilizungumza ni suala la nchi. Ninaomba sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja Dumila – Mikumi. Tunatoka Mikumi tunakwenda moja kwa moja, ile barabara inapita Mlimba kule inatokezea Njombe, tupunguze *jam!* Haya, tuna barabara hapa, ya muhimu sana, inatokea hapa Mkiwa; hapa Mkiwa – Singida, hii barabara ingepunguza *jam* huku, kuja hapa Dodoma!

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Iringa sasahivi imekwisha, hakuna barabara iliyokwisha kwa muda mfupi, kama barabara ya Iringa – Dodoma. Jamani Wabunge tuwe wa kweli, jamani tuzungumzie sasa nchi, tukifika hapa tusianze kuzungumzia majimbo! Ikifikia kwenye mpango tuzungumzie nchi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii barabara ingetengenezwa, ya Mkiwa, leo miaka 60 jamani! Haki ya Mungu, miaka 60 na kitu ya uhuru, kutoka Mkiwa kwenda Makongolosi, kwenda Mbeya, unamlazimisha mtu anayetokea Singida azunguke Dodoma, aende mpaka Iringa, apandishe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ambayo ingepunguza *jam* ya nchi; hivi tunavyozungumza mtu anatoka Tunduma, unamlazimishaje huyu mtu anatoka Tunduma, aje mpaka Iringa, aje Dodoma hapa! Atoke Dodoma aende Tabora, Tabora aende Kigoma! Wakati kuna barabara pale kutoka Uvinza tu, kwenda Mpanda; Mpanda – Sumbawanga – Tunduma! Jamani hii nchi hii, sijui unajiuliza nini? Hivi ninyi wataalamu mnakuwa wapi? Watu wa ujenzi, watu wa *TANROADS,* mimi ninashindwa kuwaelewa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna barabara, mtu anatoka Bukoba unamlazimisha aje moja kwa moja mpaka Kasulu! Afike Kasulu, aje mpaka Nsimbo, aanze kuja sasa mpaka afike Uvinza; wakati kuna njia panda pale ya kutokea tu Uvinza, unatokea Kasulu! Jamani, hivi mnakuwaje? Yaani hii nchi hii!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara mtu anatoka Kahama anatokea zake Rwanda, si anatakiwa aje afike Kahama tu pale! Anakuja anakatizia nyuma nyuma anatokea moja kwa moja Tabora, kwa lami!

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, ninataka nimkumbushe tu Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kwamba, ndugu yangu, ninyi wakati huo, Profesa Kitila Mkumbo, tulikuwa wote huko upande wa pili, tulikuwa tunasema tutaibadilisha nchi. Leo umepewa rungu, badilisha nchi Profesa sasa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Sigrada Wilhem Mligo, Mheshimiwa Dkt. Johannes Lukumay, ajiandae.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nimeanza saa 11:40, ninaamini dakika zangu zitalindwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa mara ya kwanza ninapenda kumpongeza mchangiaji aliyepita; mimi sina itikadi kwa mtu ambaye anazungumza ukweli. Jambo la pili; mimi ninaamini sana katika uwezo wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, ningekuwa na maamuzi, ningetamani akae kwenye nafasi inayofanya maamuzi ya mwisho! Yaani awe mwamuzi wa mwisho kwa sababu, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ni mpangaji mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapokuja kwenye utekelezaji unaanza kujiuliza, mbona haya mambo yalipangwa vizuri! Utekelezaji kwa nini haufanyiki? Unakuja kugundua kwamba, hata yeye hawezi kwenda kutekeleza moja kwa moja, lazima kuwe na vikao mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nitawakumbusha hotuba ya Mheshimiwa Rais na mipango yake, ambayo aliizungumza siku analihutubia Bunge hili. Ninataka muone ni namna gani, sisi kama Wabunge, tumeshindwa kumsaidia Mheshimiwa Rais au kumtia moyo, na kumuongezea nguvu, ili mipango yake iweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza; Mheshimiwa Rais alizungumzia kuhusu kupambana na ugumu wa maisha ya Watanzania. Ukiangalia kwenye kitabu chake, ameanzia ukurasa wa tisa hadi ukurasa wa 10, anasema; "Hakika tulisikiliza na kuelewa matamanio ya wananchi, ya kupata Serikali inayoshughulikia changamoto zao, kama vile suala la gharama za maisha, kuongeza fursa za kazi na ajira, ili waweze kujiendeleza kiuchumi na kusimamia ustawi wa jamii zetu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Mheshimiwa Rais kuweka matamanio yake haya mbele ya Bunge hili, ninavyozungumza sasahivi, mfuko wa *cement* ni shilingi 30,000 kule Ludewa; pale kwako Njombe Mjini, leo hii mfuko wa *cement* ni shilingi 25,000. Ninatamani Bunge hili lijaribu ku-*reflect* ugumu wa maisha unaoendelea huko mtaani! Ninavyozungumza sasahivi, mafuta yanazidi kupanda bei licha ya Mheshimiwa Rais kutamani wananchi wapunguziwe mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mambo ya ujenzi; Mheshimiwa Rais alienda zaidi akazungumzia mpango wa kupunguza gharama ya vifaa vya ujenzi, ninajua huenda wengi mlitupa vitabu hivi, sasa ninataka niwakumbushe tu leo. Ukurasa namba 28 Mheshimiwa Rais alisema; "Kwa upande wa ujenzi wa makazi jitihada zetu zitajielekeza kupunguza gharama ya vifaa vya ujenzi, ili tuwezeshe wananchi kujenga makazi bora. Tutaweka mikakati maalum kwenye nyumba bora na za gharama nafuu, tutasimamia utekelezaji wa sera zinazolenga kuboresha hali ya makazi kwenye maeneo yenye makazi duni."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wabunge, tujitafakari; sisi kwa nafasi yetu tumemsaidiaje Mheshimiwa Rais na kuishauri Serikali kufikia haya matamanio ya Mheshimiwa Rais? Kuna muda huwa ninakaa ninatafakari, ninagundua Mheshimiwa Rais *sometimes* anakuwa na mawazo mazuri, lakini changamoto ni kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda ukurasa namba 29. Sasahivi kuna wimbi la wananchi kuchukuliwa maeneo yao na kulipwa fidia ndogo halafu yale maeneo yanaenda kupimwa, Serikali inauza mara nane ya bei waliyolipa kwa mkulima! Kwa mfano, watachukua ekari yako kwa shilingi 300,000 ile ekari inaenda kupimwa, Serikali inaingia ubia na kampuni binafsi inaenda kupima hiyo ekari yako, inapata viwanja nane; vile viwanja kimoja kinauzwa shilingi 10,000,000!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wameanza kulalamika huko! Mimi sijaanza, wameanza wenyewe! Tayari mmeona wengine wameandamana juzi! Mheshimiwa Rais alisema, ukurasa namba 29; "Sambamba na hilo, tutaongeza kasi ya urasimishaji wa

maeneo ya makazi, urasimishaji mmeugeuza imekuwa biashara; …na kuimarisha utatuzi wa migogoro ya ardhi." Ninyi mnaendelea kuongeza migogoro, mnanyang'anya viwanja vya watu; "...kwa kupima ardhi nzima kwa teknolojia ya kisasa na ya *satellite,*" kwa Kiingereza, *Land Geo Spatial Technology!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo siyo maneno ya Mheshimiwa Sigrada, ni matamanio ya Mheshimiwa Rais. Leo hii mnachukua maeneo ya watu, mnaungana na kampuni binafsi, mnanunua kwa bei ndogo; ninyi mnagawa viwanja, mnawaacha na hela ambazo hazina uwezo hata wa kuwajengea nyumba bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alienda zaidi; vifaa vya ujenzi, namba 28, kwa upande wa ujenzi! Hii nimesoma, ninaenda nyingine! Si hamnikumbushi sasa! Hata hivyo ninajitahidi, kupambana na ninyi, siyo *issue* ndogo! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alienda zaidi, ukurasa namba 15, akasema; "...tutaendelea kuweka nguvu zaidi kudhibiti mfumo wa bei za bidhaa." Siyo maneno ya Mheshiiwa Sigrada, ni maneno ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; "...ambayo ni hatua muhimu katika kupunguza gharama za maisha kwa wananchi. Pia, tutaweka motisha kwa viwanda vya ndani, ili viweze kuzalisha kwa gharama nafuu na kuuza kwenye soko la ndani na nje. Tutaongeza vivutio vya kikodi...

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

TAARIFA

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu, Mheshimiwa Sigrada anachangia vizuri, lakini ninapenda Kiti kimwelekeze achangie mpango, siyo Hotuba ya Rais, tafadhali! Kwa hiyo, Kiti kimwelekeze, ili achangie vizuri sawasawa na mpango ulioko Mezani. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada, unapokea Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jackson Kiswaga?

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kupokea. Ni mtu ambaye ana *stress* tu ndiyo anaweza kutenganisha Mpango wa Rais na Mpango wa leo uliowasilishwa. Ni kitu kimoja, na ndiyo maana hata Mpango wa Mheshimiwa Profesa Kitila unazungumzia hayahaya. Hapa tunachopambana ni utekelezaji, na nimeshangaa kuna watu wanampigia makofi! Nchi ngumu sana hii! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee tu. Hapa ninazungumzia, ni namna gani Mheshimiwa Rais alikuwa na ndoto ya kupunguza mfumuko wa bei, lakini ninalinganisha na hali ya sasa huko mtaani! Uhalisia wa maisha yaliyoko mtaani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada, ninaomba nitoe mwongozo kidogo; unachangia vizuri sana, na kwa kweli, unatoa maneno ya Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake. Basi tunakuomba, na mapendekezo ambayo unayatoa kwenye mpango ambao uko mbele yetu! Ninaomba uendelee.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi kuhusu wewe sina shida! Wewe ni mlezi wangu wa kisiasa, umenibeba kwenye mengi kwa hiyo, lazima nikusikilize baba yangu, endelea kunibeba hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu; niliangalia muda wangu, sasahivi ni dakika 48, nina dakika mbili tu na sitaongeza! Hoja yangu ni kwamba, tuna mipango mizuri sana, lakini inapofika kwenye utekelezaji, na ndiyo maana Rais kwenye kitabu chake alisema ata-*deal* na watendaji kuanzia ngazi ya Mawaziri mpaka ngazi ya kwenye kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa wa nyuma yangu hapa ametoka kuongea kitu kimoja, basi tuwe tunaamua; kwamba, sasahivi tuna-*deal* na jambo la barabara, labda mwaka huu tumalize hii miradi ya barabara, ambayo imeanza. Tuna barabara Njombe, ya mwaka 2014, ipo mpaka leo; tuna miradi ambayo ilikuwepo, mtu amekuwa Mbunge, labda miaka 20, anapigania

kitu hichohicho! Mpaka anamaliza ubunge, hiki kitu hakijatekelezwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyomaana Waheshimiwa Wabunge kurudi humu Bungeni, sasahivi imekuwa ni ngumu kwa sababu, unapoomba kura, unamwambia nitaleta barabara, nitaleta maji; miaka mitano imekata, unakuja unatabasamu-tabasamu! Wanakuambia biashara yako imeisha! Hapa sasahivi tunazungumza, kama tunacheka, lakini hukumu zetu zinakuja mwaka 2030, Mungu akitupa uzima, hukumu zetu zinakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kumalizia, ombi langu ni kwamba; Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, wewe ni mpangaji mzuri, tusaidie utekelezaji. Unapokwama; sasa nitasema nitakusaidia! Mimi nitasaidia nini sasa? Mimi ninachoweza kusema ni, Mungu akutangulie katika haya maono yako, usikutane na vigingi vitakavyofanya tushindwe kukamilisha huu mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalialia hapa, lakini nimeona asubuhi kuna mtu ametoa wazo, kuleta tozo nyingine tena kwa wananchi! Khaa! Tuna madini 100%, tumepima 16%, kama miradi ya barabara imeshindikana fedha hakuna, tukate vipande vyetu vya madini tuuze, lakini ni hatari kupeleka tozo sasahivi kwa wananchi! Tena kwenye mafuta! Tumeweka tozo za barabara, mnataka mlete na tozo za kutembea sasa! Baadaye mtataka na hewa tuwe tunalipia nyinyi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana. Mungu awabariki sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Sigrada, tunakushukuru kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Dkt. Johannes Lukumay.

MHE. JOHANNES L. LUKUMAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutuwezesha kuwa hapa leo kuongelea masuala muhimu ya nchi hii. Ninachukua nafasi hii kuweza kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuridhia kufanyika Mkutano wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU*) nchini Tanzania

ambao umesababisha Jimbo la Arumeru Magharibi kupata fursa ya kutembelewa na Wajumbe wa Umoja wa Mabunge Duniani, katika miradi ya kimkakati inayofadhiliwa na Umoja wa Mataifa. Tunashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninamshukuru sana Profesa wetu Kitila na timu yake, kwa kuandaa mpango mzuri. Ninamshukuru ndugu yangu, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Ndaki, kwa ushauri mzuri alioutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaona nimefilisiwa. Ninataka tu nikae, maana Mheshimiwa Tabasam ameongea, mwasilishaji wa kwanza ameongea, sasa sijui nitaongea nini, lakini nitasema kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa 2027/2028 ni sehemu tu ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano, lakini pia, ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya 2050, ambayo inalenga kuijenga Tanzania katika uchumi wa dola za Marekani trilioni moja. Ufikapo mwaka 2050 tunatarajia kuwa na Watanzania milioni 118, na kama uchumi huu utaendelezwa vizuri, tunatarajia pia, umri wa kuishi wa Mtanzania utafika miaka 75, na kipato cha kila Mtanzania kitafika dola za Marekani 700,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata nishati itaongezeka kufikia megawati 70,000. Pia, kuna kukuza kilimo cha kisasa ambacho wenzangu wameongelea; kuna madini, kuna utalii, na kuna uchumi wa bluu. Yote haya ni kukuza Pato la Taifa, lakini haya yote haiwezekani kuyafanya bila kushirikisha makundi yafuatayo; tunahitaji Bunge, tunahitaji Serikali, tunahitaji sekta binafsi, tunahitaji wananchi, na tunahitaji waandishi wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ili wote kwa pamoja, tufanye kazi kuhakikisha kwamba, uchumi ule tunaotegemewa wa Dola za Marekani trilioni moja, unafikiwa ufikapo Mwaka 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamesemwa mengi, na mimi sipendi kurudia, lakini namuomba tu Mheshimiwa Profesa Kitila, ameongea vizuri sana, amewasilisha; kuna mfumo amesema, '*e-delivery*', ambao ni wa kuhakiki na kutathmini utendaji kazi. Ninaomba sasa

ukatumike kuhakikisha kwamba, mipango iliyowekwa inatekelezwa; mipango ya barabara katika nchi hii inatekelezwa, mipango ya maji, ambayo ni mikubwa katika nchi hii inaenda kutekelezwa hivisasa. Pia, tunashukuru nishati imeenda vizuri, na mipango mingine ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la sekta binafsi. Tumeona kabisa kwamba, Mpango huu au Dira ya Taifa ya 2050, ambayo nimeelezea kwamba, ikifanyika vizuri itaenda kuipeleka nchi katika sehemu nyingine, tunategemea sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini cha kufanya kwenye sekta binafsi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji, tuwatambue hawa watu wanaowekeza; sekta binafsi wanafanya kazi nzuri sana. Nitatoa mfano mmoja tu, Wabunge wa Umoja wa Mabunge Duniani walipotembelea Jimbo la Arumeru Magharibi, walienda kukagua miradi miwili; mradi mkubwa wa uwekezaji wa afya, lakini kuna mradi wa uwekezaji wa kilimo cha umwagiliaji, wale wanafanya na sekta binafsi. Mfano mmoja tu, nisipoteze muda wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule uwekezaji wa sekta binafsi wa kilimo cha umwagiliaji na kilimo cha kisasa umeweza kuwafanya wananchi kuzalisha kutoka magunia 40 ya vitunguu kwa ekari moja, mpaka kufika magunia 120 kwa ekari moja. Vijana wamepata ajira na unakuta pia, mazao yanapelekwa kuuzwa nchi za nje; Burundi, Sudan, Zambia na Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninamuomba tu Waziri wetu wa Uwekezaji na Mipango tuweze kuwatambua hawa wawekezaji; hawahitaji chochote, ni utambuzi tu! Kwamba, "unafanya kazi vizuri, tuko na wewe," ili waweze kuisaidia nchi yetu kwa sababu, ni kweli kabisa kwamba, wanatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme tu kwamba, aliyoelezea Mheshimiwa Tabasam kuhusu ufuatiliaji wa miradi, ufanyike. Kila mtu asimamie nafasi yake afanye kazi. Tukifanya hivyo, hakika nchi yetu itaenda kufaidi uchumi ambao

tumejiwekea, na wananchi wataenda kuwa na tabasamu, kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alivyotueleza kwamba, anatarajia kuona Watanzania wakiwa wanatabasamu ifikapo 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru, na ninaunga mkono hoja. Nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Johannes Lukumay.

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza majina ya wachangiaji ambao walikuja kwenye Kiti leo. Kwa hiyo hapa ndiyo mwisho.

Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI: Bunge linarejea.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirejea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tumekamilisha shughuli ya leo, tutaendelea kesho, na tunaomba watu waendelee kujitokeza kujiandikisha, kwa ajili ya kuchangia. Mtakumbuka kwamba, wengi mnataka kuchangia siku za mwisho na mnapata muda mfupi! Kwa hiyo, tunaomba sana muendelee kujitokeza.

Ninaahirisha Bunge mpaka kesho, tarehe 29 Oktoba, saa 3.00 asubuhi.

(Saa 11.58 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 29 Oktoba, 2026 Saa Tatu Asubuhi)